Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 16 Julai, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, habari za asubuhi? Sikuwepo siku tatu hivi, tulikwenda kuhudhuria kikao cha IPU kuhusu uhusiano wa Wabunge na mambo ya usuluhishi katika matatizo yanayotokea katika nchi mbalimbali. Kwa hiyo, ulikuwa ni mkutano wa Maziwa Makuu pamoja na nchi za Afrika Mashariki na nafasi ya Bunge katika usuluhishi wa matatizo kama hayo.

Waheshimiwa Wabunge, mambo haya, wenzetu wana hali mbaya sana, walikuwa na hali mbaya sana, lakini Mabunge yao yalishiriki sana katika kuwahimiza watu wake pamoja waongee, wapate suluhu.

Kwa hiyo, nchi ya Rwanda sasa hivi inaendelea vizuri kwa sababu wamejitengenezea utaratibu wa kukubaliana pale wasipokubaliana.

Vile vile Burundi wanaenda, Congo (DRC) wanaendelea, na sisi Tanzania Mwenyezi Mungu ametujalia hali hii, Bunge lazima liwe kiini cha kudumisha amani na utulivu ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2008/2009 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzania kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hemed. Leo mmetuletea watu ambao huwa kawaida hawaji hapa mezani, inafurahisha sana! *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2009/2010**.**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Leo namwona Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Rashid Hamad, atauliza swali la kwanza.

*(Hapa Kipaza Sauti kilikuwa na matatizo)*

**NAIBU SPIKA:** Naona haisemi hiyo, unaweza kusogea hata mbele tu.

**WAZIRI MKUU:** Wameshaloga hapo! *(Kicheko)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naona ndio mambo yameharibika, sijui Waziri Mkuu amefanyaje! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Rais Barrack Hussein Obama, aliitumia ziara yake nchini Misri kwa kuzungumza na Waislamu na akatumia ziara yake ya Ghana akazungumza na Waafrika, na moja kati ya mambo ambayo ameyagusia sana kwamba nchi yake itakubali kushirikiana na nchi za Kiafrika zile ambazo zitadumisha na kutekeleza utawala bora. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu ya Tanzania tumeweka taasisi ambazo zinapaswa zitekeleze utawala

bora moja ikiwa ni Tume ya Uchaguzi ya Tanzania, Tume ambayo inalalamikiwa. Unasemaje katika suala hili Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Hamad Rashid swali lake zuri sana kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Naibu Spika, anachokisema ni kweli na na mimi nataka niamini kabisa kwamba ndiyo maana bado Tanzania ni rafiki mkubwa sana wa Serikali ya Marekani kwa sababu ya msingi mkubwa ambao tumeujenga katika eneo hili la utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, katika swali lake amejaribu kugusia suala la Tume ya Uchaguzi kama chombo muhimu sana katika usimamizi wa shughuli zetu za uchaguzi. Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema ni kwamba mfululizo sasa karibu kwa chaguzi zote Tume hii imefanya kazi nzuri sana. Imejitahidi sana kusimamia chaguzi hizi kwa kadri ilivyowezekana kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi yetu.

Kwa hiyo, mimi nataka niseme tu kwamba alichokisema Rais Obama, ni imani yangu kwamba Tanzania itaendelea kuwa ni moja kati ya nchi zile ambazo zitabakia moyoni mwake kama nchi ya mfano ambayo tumejitahidi katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja katika vigezo muhimu vya kuwa na utawala bora ni kuipa Mahakama uhuru wake kikamilifu. Katika Katiba yetu na Sheria yetu ya Uchaguzi, Uchaguzi wa Rais huwa hauhojiwi Mahakamani. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa taaluma yako ya kisheria huoni kama huu ni upungufu mkubwa katika utawala bora? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, pamoja na kwamba nitamruhusu Waziri Mkuu kujibu, la kwanza lilikuwa Tume ya Uchaguzi, la pili Mahakama. Swali la nyongeza linatakiwa liwe linaongeza pale pale katika swali lile linalohusika. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba ujibu kwa heshima ya Kiongozi wa Upinzani. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama unaniruhusu, tungeweza tukatoa maelezo kidogo lakini....

**NAIBU SPIKA:** Nakuruhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Jambo lolote ambalo linakuwa limewekwa ndani ya Katiba ambayo imepitishwa na Chombo kama Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo hilo ni halali kabisa kabisa mpaka Katiba itakapokuwa imebadilika.

Kwa hiyo, kwa namna ilivyo sasa, huo ndio mfumo tuliokubaliana na ni halali. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na pole na safari na karibu tena. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni Serikali imegatua shughuli zote za usimamizi wa shule za sekondari kutoka Wizara ya Elimu na kuzipeleka TAMISEMI.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini tunajua kwamba bado kulikuwa na matatizo makubwa sana ya walimu ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya mishahara, lakini vile vile kumekuwa na usimamizi mbovu hata katika shule za msingi, na vile vile kuna matatizo makubwa ya vitendea kazi ikiwa ni pamoja na uhaba wa walimu.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, huoni kwamba ugatuaji huu *(D by D)* kupeleka TAMISEMI ni kuongeza tatizo hasa ikizingatiwa kwamba Halmashauri zetu zina matatizo makubwa sana na majukumu mengi na kilio kikubwa cha Wabunge ni kwamba katika Halmashauri zetu hatuna watalaam wa kutosha. Je, tukipeleka tena suala la shule za sekondari, huoni ni kuongeza matatizo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Naibu Spika, na hata Waheshimiwa Wabunge wote, ningependa pengine hili jambo lieleweke vizuri kwamba uamuzi wa Serikali wa kupeleka shughuli za usimamizi wa jumla katika ngazi ya utekelezaji, inaonekana kama vile Serikali Kuu imeacha jukumu lake la msingi la kuendelea kusimamia shule hizi, tafsiri hiyo siyo sahihi. Wizara ya Elimu itaendelea kuwa na majukumu yake ya kuendelea kufundisha walimu (upatikanaji wa walimu), itaendelea kusimamia sera zinazosimamia sekta hiyo ya elimu, itaendelea kusimamia ubora wa walimu na watu wengine wote wanaohitajika katika utoaji wa elimu. Kwa hiyo, kimsingi ni kwamba masuala yote ya kimsingi yatabakia ndani ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kupeleka shule hizi karibu na watu, karibu na vyombo vyetu ni kwa sababu tungependa Halmashauri zetu zikawa zinajua kinachoendelea katika shule zile, wakajaribu kuzisaidia shule hizo kwa kadri itakavyowezekana. Na tunayo mifano dhahiri, kwa sababu ya umbali uliokuwepo, nitoe mfano tu; unaweza ukaenda shule ya sekondari moja, unakuta shule imekatiwa umeme, imekatiwa maji kwa sababu tu ankara zimepelekwa Makao Makuu ya Wizara na bado hawajalipwa fedha. Kusogeza karibu na Halmashauri ni kwamba tunataka matatizo haya madogo madogo ya kiutekelezaji yaweze kutatuliwa moja kwa moja pale pale shule ilipo.

Lakini, pili; sisi wote ni mashahidi, huu mfumo wa wa kudhani kwamba tunaweza tukaendesha shule zaidi ya 2,000 kutoka Dar es salaam, ni jambo lisilowezekana na ndio maana tumeona ugatuaji huu uteremke kwa umma kwa sababu tunaamini ufanisi utaongezeka. Lakini tunakubali, kutakuwepo na changamoto nyingi bado na jukumu letu kama Serikali ni kuendelea kutafuta kila litakalowezekana kuondoa kabisa yale matatizo ambayo yanaweza yakawa ni kikwazo. Dhamira ni njema, lakini tunajua inawezekana kukawa na changamoto ambazo tutakabiliana nazo vile vile. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN. A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri Mkuu kwa majibu yake mazuri ya ufafanuzi. Mheshimiwa Naibu Spika, lakini moja ya

tatizo kubwa sana sasa hivi ni malimbikizo ya walimu na hapo hapo tunahamishia madaraka kule TAMISEMI...

**SPIKA:** Malimbikizo ya walimu au?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Malimbikizo ya mishahara, madai ya walimu! Lakini, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapo jana au nadhani juzi, Rais wa Chama cha Walimu Tanzania ametoa tamko zito sana kwamba kama hawatalipwa basi watafanya tukio la kihistoria. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, unasemaje kuhusu tamko hilo na Serikali sasa iko tayari kulipa madai hayo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka niwaombe ndugu zangu walimu nchi nzima, migomo si suluhu ya matatizo yetu, si suluhu hata kidogo. Sana sana mnachofanya ni kuwaumiza wanafunzi tu mnaowafundisha. Jambo hili la malimbikizo wote tunalifahamu na wala si siri, tumekuwa tukilieleza sana hapa. Cha msingi ambacho walimu wanapaswa kujua ni kwamba hatujapuuza hata kidogo kushughulikia matatizo yao ya malimbikizo ya fedha. Na malimbikizo yote ambayo safari hii tulikuwa tumeyapata baada ya agizo la Rais, yote tumeyaingiza katika bajeti ya mwaka huu 2009/2010, na fedha hizo zitalipwa kwa sababu zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu.

Sasa kama CWT bado wanaona juhudi zote ambazo tumekuwa tukifanya, tumejaribu kulipa malimbikizo mengi tu, si kwamba hatujafanya kitu, na sasa tumefika mwisho wa mwaka, tumesema *okay, fine*, yale yote tuliyonayo acha tuweke kwenye bajeti ijayo, tuyashughulikie yalipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesikia juu ya tishio hilo, lakini nikasema chonde chonde haitatusaidia kama Watanzania. Ni vizuri tukaendelea kujaribu kutafuta suluhu, dhamira ya Serikali ni nzuri na ndio maana nimesema ili mradi fedha hizo ziko kwenye bajeti, tufanye subira tu, tutazilipa zote. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Aprili, 24 mwaka jana ndani ya Ukumbi huu katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, nilielezea malalamiko ya wananchi wa kata ya Mwendakulima katika Jimbo la Kahama ulipo Mgodi wa Buzwagi dhidi ya Kampuni ya Barrick kuwanyanyasa katika fidia zao, kupora maeneo yao, lakini mbaya zaidi kutumia vibaya Jeshi la Polisi dhidi ya wananchi. Kufuatia malalamiko hayo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ulitoa maagizo mawili: Moja, wale wote ambao walikuwa wamekamatwa kwa kuandamana kudai haki hizo, waachiwe huru na wafutiwe mashitaka. Nashukuru kwa jambo hilo. Lakini pili, uliagiza Waziri wa Nishati na Madini afike Kahama kufuatilia malalamiko haya ya wananchi, jambo ambalo Waziri alilifanya mwezi Mei na mwezi Agosti mwaka jana.

**NAIBU SPIKA:** Sasa, swali ni nini?

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Baada ya hapo, swali; Je, ni lini Waziri atafika tena Kahama kuwapa utekelezaji wa yale aliyoyaona ili kuwaondolea adha wananchi wa Kata hiyo na kuendelea kuishi kwa matumaini kwamba siku moja haki itatendeka? Asante!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hivi kweli kila siku atatoka Waziri, mimi ningefikiri wewe ungewaambia hakuna kilichofanyika, sasa ingekuwa ndio swali, maana hujamsaidia Waziri Mkuu kitu gani hakijafanyika tangu wakati huo. Naomba uulize hiyo, ni kitu gani hakijafanyika baada ya wakati huo? Tunaomba uulize hiyo, ni kitu gani hakijafanyika kusudi Waziri Mkuu ajibu, kwa sababu kwenda tu Waziri ni wajibu wake kila siku kwenda.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Waziri aliahidi atarudi katika kipindi kifupi kuwaelezea wananchi nini Serikali imegundua na nini haki ya wananchi wale itatendeka, ndio swali.

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**MBUNGE FULANI:** Siyo swali!

**NAIBU SPIKA:** Anayesema siyo swali ni Spika, siyo mtu mwingine yeyote! *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijaribu kumjibu ndugu yangu Lembeli swali lake kama ifuatavyo:- Kwa kuwa; hoja ni kwa Waziri wangu kurudi kwenye Jimbo lake na kwenda kutoa taarifa, basi mimi namsihi Bw. Ngeleja jitahidi uende ukatoe maelezo juu ya utekelezaji wa yale tuliyokubaliana. Na mimi nina hakika Ngeleja msikivu, atakuja tu Mheshimiwa Lembeli kuja kujaribu kukutana na wananchi wako.

**NAIBU SPIKA:** Unajua Mheshimiwa Lembeli sisi tumekupa nafasi tujibu, lakini hukuuliza kitu! Sasa, naomba uulize swali la nyongeza.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Kampuni ya Barrick imedhihirisha kwamba ina jeuri, ina kiburi, Je, Serikali inadhamiria kufanya nini dhidi ya Kampuni hii hasa pale ambapo inawanyanyasa wananchi? Asante!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lembeli, kwa nini hukuuliza swali hili kwanza, ukapoteza muda. Kwa hiyo, naendelea!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru! Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu ina Katiba mbili, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kuna Vyombo vya Bunge hili la kutunga sheria, Mahakama ya kutafsiri, *Executive* kwa maana ya Serikali na wananchi wake wanaitwa Watanzania. Lakini pia kuna katiba ya Zanzibar ambayo kuna Chombo cha Kutunga

Sheria Baraza la Wawakilishi, Mahakama na *Executive* Serikali na wananchi wake wanaitwa Wazanzibari. Je, nchi yetu ina Amiri Jeshi Wakuu wawili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, umemwelewa? *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kumbonyeza rafiki yangu nikamwambia Bwana usiulize swali gumu, eeh! Kwa sababu anachosema hapa, ameuliza swali ambalo mimi nasema gumu, kwa sababu anasema Je, nchi yetu ina Amiri Jeshi Wakuu Wawili? Sasa kwa sababu umetanguliza neno nchi yetu kwa maana ya *sovereign state*, tunaye Amiri Jeshi Mkuu mmoja tu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Eeh, wewe mwingine umemjua wapi? *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED HABIBU JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Katiba ya Zanzibar pia inatambua Vikosi vya SMZ na Vikosi hivi Rais wa Zanzibar huwa anavikagua, anapigiwa mizinga 21 na kuna Wimbo wa Taifa wa Zanzibar. Je, huyu Amiri Jeshi Mkuu mmoja ana mamlaka ya Vikosi vya Zanzibar, vya SMZ?

**WAZIRI MKUU:** Jibu ni ndiyo! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru! Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala la upimaji wa VVU kwa hiari limepokelewa kwa mafanikio makubwa, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu dawa za kurefusha maisha za ARV huwa zinatolewa na wahisani na kwa sasa hivi inasemekana kwamba zimeishaanza kupata usugu; na kwa kuwa sasa hivi kuna mtikisiko wa uchumi duniani, Je, Serikali imejiandaje iwapo wahisani watajitoa katika msaaada huu ukizingatia kwamba waathirika wakianza kutumia dawa zile inabidi watumie kipindi chote cha maisha yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan, swali zuri sana! Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba majibu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la upimaji wa hiari wa Virusi vya UKIMWI ambalo swali ameulizia dada yangu Owenya, ni kweli kabisa kwamba limefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana. Lakini lengo kuu la zoezi lile ni kuliwezesha Taifa letu kujua ni kwa kiwango gani tatizo hili ni kubwa na kuwawezesha Watanzania kila mmoja kuweza kujua hali ya afya yake kwa sababu akijua inamsaidia sana yeye mwenyewe, lakini inawasaidia vile vile na Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni kweli iko changamoto kwamba kwa kadri jambo hili linavvyoonekana kufaulu, maana yake ni kwamba tunaendlea kupata takwimu zinazoonyesha hali halisi ya wale wote ambao wameathirika na kwa hiyo kazi inakuwa ni Je, tuna uwezo wa kuwahudumia?

Jibu ni kwamba hiyo ni changamoto ambayo wote lazima tuende nayo kwa kadri muda unavyokwenda. Kuhudumia hapa ni pamoja na utoaji nasaha kwa wale waathirika

ili waweze kuishi katika hali ambayo itawawezesha kuishi miaka mingi zaidi, kwa maana ya lishe, kwa maana vile vile ya kujitunza.

Lakini upande wa pili, kwa wale ambao wamefikia hatua ambayo inabidi atumie dawa, swali lako sasa linakuwa ni zuri sana. Ninachoweza kukuhakikishia Mheshimiwa Owenya ni kwamba kwa upande wa wahisani na mhisani mkubwa hapa hasa ni Serikali ya Marekani, katika hili pamoja na kutetereka kwa uchumi, kauli ya kiongozi wa Marekani ni kwamba programu hizi zote ambazo alikuwa ameishaziweka, hazitaathirika na mtikisiko wa kichumi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hiyo inatupa faraja na inatupa nafasi nzuri zaidi ya kuendelea kutumia fursa hii iliyopo hivi sasa. Lakini, na sisi wenyewe Watanzania ni lazima tuendelee vile vile kuangalia namna tutakavyokwenda tunajipima kadri uwezo utakavyoturuhusu ili tuweze kuwa na mfumo vile vile wa kuchangia kwa kadri itakavyowezekana.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru! Kwa kuwa dawa hizi za ARV, hizi *first line* sasa hivi zimeanza kupata usugu, na nchi zilizoendelea saa hivi wanatumia *second line* ambazo zinaweza kusaidia kurefusha maisha. Je, Tanzania tuna mikakati gani ya kuhakikisha kwamba wale ambao tayari dawa zimepata usugu, wanaweza kwenda kwenye *second line?*

**NAIBU SPIKA:** Naona Waziri wa Afya atajibu zaidi ya hapo, lakini Waziri Mkuu labda jaribu jaribu.

**WAZIRI MKUU:** Sina jibu zuri sana Mheshimiwa Owenya kwa sababu kidogo ni mambo ya kitalaam talaam, lakini labda baadaye nimwombe tu Prof. Mwakyusa apate nafasi pengine ya kujaribu kulitolea ufafanuzi kama ni lazima kwa sababu ni jambo kubwa na siwezi kutaka kuingia katika eneo ambalo sina utalaam nalo sana.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 30 Desemba, 2005, Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Kikwete wakati anafungua Bunge letu hili, aliahidi kwamba Serikali ya Muungano wa Tannzania itaisaidia Zanzibar katika bajeti yake mbali na ule mgao wake wa asilimia 4.5 kutoka kwa wafadhili. Lakini, juzi tumesikia *statement* kutoka kwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais wa Zanzibar kwa masuala ya fedha akisema kwamba Serikali ya Muungano wa Tanzania haijasaidia bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa hata senti moja. Je, wewe ukiwa ni Msimamizi Mkuu wa mambo ya Serikali ya Muungano unasemaje kuhusu hili? Asante!

**NAIBU SPIKA:** Yaani nyie kila saa mnataka migongano, eeh! Haya Waziri Mkuu! Mh!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijaribu kumjibu rafiki yangu Dr. Ali Tarab Ali swali lake kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Naibu Spika, mimi tatizo langu wakati mwingine ni kauli ambazo zinajitokeza katika masuala yanayogusa

eneo hili la Muungano, wakati mwingine zinaweza zikatoa picha ambayo si nzuri sana, ikaonekana kana kwamba hiyo ndiyo hali halisi ilivyo.

Lakini, kama kweli tukikaa tukajaribu kusema hebu tuhesabu tuone nini hasa kimefanyika kati ya pande hizi mbili hata katika hili ambalo umeniuliza, wakati mwingine unaweza ukakuta picha inayojitokeza ni tofauti kidogo. Kwa hiyo, mimi nataka niheshimu sana alilolisema ndugu yangu Waziri kutoka Serikali ya Mapinduzi, lakini niombe tu kwamba mambo haya ni vuziri, kama kweli mnataka mkae chini muanze kuchukua takwimu za hali halisi ilivyo, basi tukae kwanza chini tujaribu kufanya hilo zoezi, baadaye ndiyo tunaweza tukakaa tukakosoana vizuri. Mimi nilisikiliza, lakini kidogo ilinitisha kama matamshi mengine mengi yanavyonitisha. Muungano ni jambo jema, tumelijenga vizuri sana, ni vizuri tukaendelea kuuenzi kwa kadri itakavyowezekana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Najua swali la nyongeza atauliza Hemed! *(Kicheko)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Mkutano huu wa 16 unaoendelea wakati wa kuwasilisha bajeti ya Serikali lilijitokeza tatizo la misamaha ya kodi kwa taasisi za kidini na kwa busara yako Mheshimiwa Waziri Mkuu ulikaa na wahusika na ufumbuzi ukapatikana. Katika Mkutano huu huu wa bajeti wakati wa kuwasilisha hotuba ya Wizara ya Katiba na Sheria, kulikuwa na tatizo la Mahakama ya Kadhi, tukapata taarifa kutoka vyombo vya habari kwamba umekaa na wahusika kimya kimya kwa lengo lile lile la kupata ufumbuzi wa suala hili.

Lakini vile vile tulipata taarifa kwamba mmekubaliana utoe tamko la kufuta kauli ya Serikali kwamba Mahakama ya Kadhi ipo na haitokuwa katika sheria za nchi kwa sababu haiwezi kuongozwa na wakristo na wale wasiofahamu sheria za Kiislamu. Swali langu ni kwamba Je, tamko hilo mpaka leo hujalitoa, utalitoa lini?

**NAIBU SPIKA:** Kwani wewe ulikuweko kwenye mazungumzo hayo? *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, uko ukweli kiasi fulani kwa yale anayoyasema rafiki yangu Mheshimiwa Khamis. Lakini labda nitumie fursa hii kusema kilichotokea hasa ni nini. Nilikuwa nimesita kulifanya kwa sababu jambo lile lilitamkwa na Waziri wangu Mambo ya Katiba na Sheria na kwa bahati mbaya tukawa tumemtuma kazi nyingine. Kwa hiyo, nilikuwa nasubiri arudi ili yeye aweze kusema kilichokuwa kinajaribu kusemwa hasa ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hoja ile kuwasilishwa Bungeni vyombo vya habari vilisema sasa Mahakama ya Kadhi yazikwa. Na ndio maana muda wote nimekuwa nasema sana juu ya vyombo vya habari vinapoandika visipoangalia vinaweza vikaandika vikapotosha kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, na matokeo ya *Headlines* zile zilitokeza kwenye magazeti zimepokelewa katika hisia tofauti. Tofauti kweli kweli na zilileta changamoto

kubwa sana kwa Serikali lakini wote tulikuwepo Bungeni alichojaribu kusema Mheshimiwa Waziri ilikuwa ni kwamba Serikali imeunda Kamati, tunataka twende kwa wenzetu Waislamu tuwaombe na wenyewe waunde Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitaka tukae pamoja tuwape kile ambacho baada ya kutafakari kwa muda hivi tumekuja nacho kama pengine ndio njia ya kwenda mbele. Sasa kama vyombo vingesema Serikali yaunda Kamati kuzungumza na wenzetu Waislamu ingekuwa nzuri sana, kwa sababu hoja kwamba sasa Mahakama ya Kadhi imekufa sio kweli na mimi nataka nikuambie Mheshimiwa Khamis Serikali hii wala hatusemi kwamba hakuna uhalali wa Mahakama wala Ofisi ya Kadhi kuwepo hata kidogo, hatujasema hili! Tulichoahidi tulisema, Chama kitajitahidi kupitia Serikali yake kulipatia ufumbuzi suala la Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kulipatia ufumbuzi ni kuhangaika kujaribu kutafuta njia ambayo tunaweza tukafikia kwa maelewano. Tukaona ni mfumo gani uweze kuchukuliwa katika kujaribu kujenga kitu ambacho tunadhani ni sahihi, na mimi nataka nimshukuru sana Mufti kwa sababu baada ya Mkutano ule ambao ulihudhuriwa na Maulamaa karibu watatu, wanne hivi lakini Masheikh karibu ishirini na zaidi kwa hiyo jumla walikuwa 35 baada ya pale alitoa kauli ambayo mimi nadhani ilikuwa nzuri na akawaasa wenzetu Waislamu wavute subira wakati jambo hili lina shughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam akajaribu kutoa ufafanuzi zaidi kidogo kuonyesha kwamba muda si mrefu litakuwa limepatikana lile Jopo la Masheikh ili wakae na Serikali.

Sasa tutafakari si hili tu ambalo tulikuwa tumejaribu kuja nalo lakini kujaribu kuona sasa hili ambalo nilipokwenda nikawaambia Serikali haina tatizo na jambo hili tunachowasihi ni jambo moja tu kwa kuwa mnazungumza kwamba Mahakama ya Kadhi au Ofisi ya Kadhi msingi wake ni Imani ya dini. Mimi nikasema pengine si busara chombo hicho mkakiweka katika mfumo unaotakiwa kusimamiwa na dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ukileta huku kwenye dola sisi tutaendelea kutazama chombo kile kama dola tu. Kumbe yapo mambo ya imani ambayo yanatakiwa yaangaliwe kwa umakini mkubwa. Niliwaambia Viongozi wale kwamba nimezungumza na Rais. Rais amesema nenda kajaribu kuzungumza nao waombe kama wataweza katika mjadala huo waone namna wanavyoweza kuanzisha ofisi au mahakama hiyo ya Kadhi ndani ya mfumo wao wa dini ya Kiislamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa upande wake itafanya kila itakalowezekana kusaidia mfumo huo mtakaokuwa mmekuja nao. Kuhakikisha unajengwa, unaendelezwa mpaka hapo tutakaposema sasa chombo kimeweza kusimama lakini bado ibaki ni nguzo muhimu katika imani ya dini ya Kiislamu hilo ndilo lililojitokeza na nikasema tutajaribu kurudi kwenye Bunge na kulitolea ufafanuzi ili pengine liweze kuchukua muelekeo huu au mtazamo huo. Na mimi nasema hata hili tulilopendekeza haina maana kwamba hilo ndilo suluhu ya kila kitu. Matarajio yangu ni

kwamba pengine baada ya kuzungumza nao wataboresha, watatupa mawazo ya ziada tuone nini cha kufanya lakini lengo libaki palepale kwamba tutafute njia ya kuweza kupata suluhu ya jambo hilo, ndio hasa ilikuwa madhumuni ya mazungumzo yetu.

**NAIBU SPIKA:** Asante! Tumechukua muda mrefu Hemed sikupi nafasi hata kama ni haki yako. Nitamuita Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga.

**MHE JUMA S. N'HUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika naomba kushukuru kupata nafasi hii swali langu litakuwa moja tu na linahusu TRA. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba niishukuru Serikali kwamba imekuwa ina bidii kubwa sana kuangalia TRA, lakini hivi sasa viongozi wetu wanakwenda mara nyingi pale Bandarini na wanaona ule mlundikano wa makasha yaliyoko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa wanazopewa huenda zikawa sahihi au siyo sahihi lakini la msingi ni kwamba Serikali ilijitahidi kufanya utaratibu wa makasha yale kuondoka kwa haraka na kuwafikia wananchi. Wengi wanaoagiza makasha yale wanapenda kupata haraka mizigo yao tatizo linalowakumba ni urasimu uliopo wa kupata hayo makasha kutoka kwa *TRA*, *TBS* na *TICTS.*

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inachukua utaratibu gani ama wa kufanya utafiti wa kutosha kuona urasimu uliokuwepo hivi sasa unaondoka ili tatizo hili la kulundikana makasha uondoke.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa N'hunga swali lake kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo pale bandarini kwa ujumla wake wa mlundikano wa makasha au *containers.* Hilo Serikali inalijua na ndio maana tumekuwa tunajaribu sana kulipatia ufumbuzi na kwa juhudi ya Rais na juhudi ya Serikali yetu kwa ujumla ninachoweza kuwahakikishia Watanzania ni kwamba juhudi zile zimezaa ahueni kubwa sana, hali ya mlundikano wa makasha sivyo kama ulivyokuwa wakati tumeanza kulizungumza, kumekuwepo na juhudi kubwa sana na hata mlundikano wa meli uliokuwa umejitokeza nao umepungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado nakubaliana na wewe kwamba kwa sababu hatujafika mahali tukaanza kujivuna kwamba sasa tumefikia hatua ambayo mambo yote ni asilimia 100. Bado juhudi zinahitajika na mimi nakuahidi tutaendelea, tunabanana kweli kweli na watu wa *TRA* usiku na mchana tumejaribu kuwaweka pale na wanafanya kazi sasa kwa *shift* masaa 24 katika juhudi za kuhakikisha kwamba kazi hii inakwenda kama tulivyokuwa tumetarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendeleza juhudi mpaka tufikishe jambo hili mwisho ambapo Watanzania wataridhika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali kwa Waziri Mkuu umekwisha. Tunapenda kukushukuru sana Waziri Mkuu kwa majibu yako na ndiyo maana unaitwa Waziri Mkuu! Unaweza kujibu maswali ya Kadhi, Bandarini, kila mahali na umejibu kwa ufanisi, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hoja ile kuwakilishwa Bungeni vyombo vya habari vilisema sasa Mahakama ya Kadhi yazikwa. Na ndio maana muda wote nimekuwa nasema sana juu ya vyombo vya habari vinapoandika msipoangalia mnaweza mkaandika vikapotosha kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, na matokeo ya *Headlines* zile zilitokeza kwenye magazeti zimepokelewa katiak hisia tofauti. Tofauti kweli kweli na zilileta changamoto kubwa sana kwa Serikali lakini wote tulikuwepo Bungeni alichojaribu kusema Mheshimiwa Waziri ilikuwa ni kwamba Serikali imeunda Kamati tunataka twende kwa wenzetu Waislamu tuwaombe na wenyewe waunde Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukae pamoja tuwape kile ambacho baada ya kutafakari kwa muda hivi tumekuja nacho kama pengine ndio njia ya kwenda mbele. Sasa kama vyombo vingesema Serikali yaunda Kamati kuzungumza na wenzetu Waislamu ingekuwa nzuri sana, kwa sasababu hoja kwamba sasa Mahakama ya kazi imekufa sio kweli na mimi nataka nikuambie Mheshimiwa Khamis Serikali hii wala hatusemi kwamba hakuna uhalali wa Mahakama wala Ofisi ya Kadhi kuwepo hata kidogo hatujasema hili tulichoahidi tulisema Chama kitajitahidi kupitia Serikali yake kulipatia ufumbuzi suala la Mahamakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika,sasa kulipatia ufumbuzi ni kuhangaika kujaribu kutafuta njia ambayo tunaweza tukafikia kwa maelewano. Tukaona ni mfumo gani uweze kuchuliwa katika kujaribu kujenga kitu ambacho tunadhani ni sahihi, na mimi nataka nimshukuru sana Mufti kwa sababu baada ya Mkutano ule ambao ulihudhuriwa na Maulamaa karibu watatu, wanne hivi lakini Masheikh karibu ishirini na zaidi kwa hiyo jumla walikuwa 35 baada ya pale alitoa kauli ambayo mimi nadhani ilikuwa nzuri na akawaasa wenzetu Waislamu mvute subira wakati jambo hili lina shughulikiwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Sheikh wa Mkoa wa Dar es salaam akajaribu kutoa ufafanuzi zaidi kidogo kuonyesha kwamba muda si mrefu litakuwa limepatikana lile Jopo la Masheikh ili wakae na Serikali. Sasa tutafakari si hili tu ambalo tulikuwa tumejaribu kuja nalo lakini kujaribu kuona sasa hili ambalo nilipokwenda nikawaambia Serikali haina tatizo na jambo hili tunachowasihi ni jambo moja tu kwa kuwa mnazungumza kwamba Mahakama ya Kadhi au Ofisi ya Kadhi msingi wake ni Imani ya dini.

Mimi nikasema pengine si busara chombo hicho mkakiweka katika mfumo uanaotakiwa kusimamiwa na dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu ukileta huku kwenye dola sisi tutaendelea kutazama chombo kile kama dola tu. Kumbe yapo mambo ya Imani ambayo yanatakiwa

yaangaliwe kwa umakini mkubwa niliwaambia Viongozi wale kwamba nimezungumza na Rais. Rais amesema nenda kajaribu kuzungumza nao waombe kama wataweza katika mjadala huo waone namna wanavyoweza kuanzisha ofisi au mahakama hiyo ya Kadhi ndani ya mfumo wao wa dini ya Kiislamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa upande wake itafanya kila itakalowezekana kusaidia mfumo huo mtakaokuwa mmekuja nao. Kuhakikisha unajengwa, unaendelezwa mpaka hapo tutakaposema sasa chombo kimeweza kusimama lakini bado ibaki ni nguzo.

muhimu katika imani ya dini ya kiislamu hilo ndilo lililojitokeza na nikajaribu kusema tutajaribu kurudi kwenye Bunge na kulitolea ufafanuzi ili pengine liweze kuchukua muelekeo huu au mtazamo huo. Na mimi nasema hata hili tulilopendekeza haina maana kwamba hilo ndilo suluhu ya kila kitu matarajio yangu ni kwamba pengine baada ya kuzungumza nao wataboresha, watatupa mawazo ya ziada tuone nini cha kufanya lakini lengo libaki palepale kwamba tutafute njia ya kuweza kupata suluhu ya jambo hilo ndio hasa ilikuwa madhumuni ya mazungumzo yetu.

**NAIBU SPIKA :** Ahsante tumechukua muda mrefu Hemed sikupi nafasi hata kama ni haki yako. Nitamwita Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga.

**MHE. JUMA S. N'HUNGA :** Mheshimiwa Naibu Spika naomba kushukuru kupata nafasi hii swali langu litakuwa moja tu na linahusu *TRA.* Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba niishuKUru Serikali kwamba imekuwa ina bidii kubwa sana kuangalia TRA, lakini hivi sasa viongozi wetu wanakwenda mara nyingi pale Bandarini na wanaona ule mlundikano wa makasha yaliyoko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa wanazopewa huenda zikawa sahihi au siyo sahihi lakini la msingi ni kwamba Serikali kufanya utaratibu wa makasha yale kuondoka kwa haraka na kuwafikia wananchi. Wengi wanaoagiza makasha yale wanapenda kupata haraka mizigo yao tatizo linalowakumba ni urasimu ulikuweko wa kupata hayo makasha kutoka kwa *TRA*, *TBS* na *TICTS.* Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali inachukua utaratibu gani ama wa kufanya utafiti wa kutosha kuona urasimu uliokuwepo hivi sasa unaondoka ili tatizo hili la kulundikana makasha uondoke.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Hnunga swali lake kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo pale bandarini kwa ujumla wake wa mlundikano wa makasha au *conteiners.* Hilo Serikali inalijua na ndio maana tumekuwa tunajaribu sana kulipatia ufumbuzi na kwa juhudi ya Rais na juhudi ya Serikali yetu kwa ujumla ninachoweza kuwahakikishia Watanzanaia ni kwamba juhudi zile zimezaa ahueni kubwa sana, hali ya mlundikano wa makasha sivyo kama ulivyokuwa wakati tumeanza kulizungumza, kumekuwepo na juhudi kubwa sana na hata mlundikano wa meli uliokuwa umejitokeza nao umepungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado nakubaliana na wewe kwamba kwa sababu hatujafika mahali tukaanza kujivuna kwamba sasa tumefikia hatua ambayo mambo yote ni 100%. Bado juhudi zinahitajika na mimi nakuahidi tutaendelea, tuna banana kweli kweli na watu wa TRA usiku na mchana tumejaribu kuwaweka pale na wanafanya kazi sasa kwa *shift* masaa 24 katika juhudi za kuhakikisha kwamba kazi hii inakwenda kama tulivyokuwa tumetarajia na tutaendeleza juhudi mpaka tufikishe jambo hili mwisho ambapo Watanzania wataridhika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali kwa Waziri Mkuu umekwisha tunapenda kukushukuru sana Waziri Mkuu kwa majibu yako na ndiyo maana unaitwa Waziri Mkuu. Unaanza kujibu maswali ya Kadhi, Bandarini kila mahali na umejibu kwa ufanisi nashukuru sana.

## MASWALI NA M AJIBU YA KAWAIDA

Na . 225

### Mpango wa Elimu Kwa Waliokosa – MEMKWA

**MHE. ABDUL JABIR MAROMBWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mpango wa Elimu kwa waliokosa (MEMKWA). Umesaidia sana kuwapatia Elimu watoto wetu; na kwa kuwa mahitaji ya kutoa Elimu hii bado ni makubwa hapa nchini mfano katika Wilaya ya Rufiji:-

(a) Je, mafanikio gani yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa mpango huu hapo 2003?

(b) Je, Serikali inaweza kuruhusu kuendelea na mpango huo kwa maeneo yenye mahitaji?

(c) Kwa kuwa, kiwango cha posho kwa walimu cha 20,000/= ni kidogo mno. Je, ni lini Serikali itaongeza posho hiyo walau ifike kima cha chini cha mshahara?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika,, mpango wa elimu ya msingi kwa waliokosa yaani MEMKWA Umekuwa na mafanikio makubwa kwa kuwa umetoa fursa kwa watoto wengi wenye umri mkubwa kuandikishwa na kupata Elimu ya msingi na hivyo kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Aidha idadi ya wanaoandikishwa katika madarasa ya MEMKWA imeendelea kupungua kwa kuwa wengi wamejiandikisha katika madarasa ya MEMKWA na hatimaye kuingizwa katika mfumo rasmi:-

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaweza kuruhusu Mpango huu kuendelea pale kwenye maeneo ambayo yameonyesha kuna mahitaji.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba kiwango cha shiling 20,000/= hakilingani na uzito wa kazi ya wawezeshaji wa MEMKWA. Hata hivyo, Serikali inatoa wito kwa Halmashauri kuongeza kiwango cha posho kwa kutumia vyanzo vya fedha walivyonavyo.

**MH. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyogeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza Mheshimiwa Naibu Spika ni Je, ni lini sasa Serikali itatangaza rasmi kwamba mpango huu wa MEMKWA umefikia kikomo chake. Kwasababu inavyoonyesha hakuna kikomo huku mbele.

(b) Je, ni utaratibu gani ambao Halmashauri yenye matatizo ya mahitaji ya MEMKWA ni ifuate ili Halmashauri hiyo iweze kupata kibali cha kuweza kuwaendeleza wanafunzi hawa wa MEMKWA hasa katika Wilaya ya Rufiji na hasa kwenye Jimbo langu lile la Delta.

**MHE. NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abdul Marombwa ni Mwalimu kwa taaluma. Mpango huu ulipoanzishwa madhumuni yake ilikuwa ni kuwapatia fursa wale ambao kwa sababu mbalimbali ziwe za kiuchumi, za Kijamii walikosa kupelekwa shuleni waweze kuendelea na mfumo huo, kwa hiyo kusema utakoma lini haukomi mpaka pale tutakapoona kila mwenye kustahili kwenda shule na kupata Elimu kaipata.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Utaratibu gani wa Wilaya ambao unahitaji, sasa mimi kidogo hapa Mheshimiwa Mbunge kanichanganya yeye anaulizia ukomo kumbe Rufiji bado wana mahitaji. Sasa nimuombe tu kwamba Afisa Elimu wa Wilaya ya Rufiji atasikia, tutampa maelekezo kama wapo hasa kule Delta na zifahamu Delta nimefika mwenyewe, ni kama hadith ukiziona zile Delta tutakuongezea uwezo ili na kule wote wapate hiyo Elimu na wewe mwenyewe nakuomba tusaidie.

**MHE. DR. ZAINABU A. GAMA:** Kwa kuwa**,** mpango huu wa MEMKWA unakwenda vizuri na mpango huu unafanana na mpango mwingine unaitwa MUKEJA. Wengine wananiambaia MUKEJA lakini mpango huo wa MUKEJA kwa wale walioikosa kwa ajili ya Uchumi wanashindwa kuendelea kwa sababu gharama yake kila mwanafunzi kwa kupitia Idara inayohusika nawatu wazima inawa - *charge* karibu laki mbili na arobani na kitu kwa mwaka. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutusaidia kupunguza hili ili Wananchi hao wengine nao waweze kunufaika kama MEMKWA?

**MHE. NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Naibu Spika, MUKEJA kirefu chake ni (Mpango wa Uwiano wa Kiuchumi Katika Jamii) maana yake nini?

Badala ya kuwafundisha wale wasiojua kusoma na kuandika ABCD na kujumlisha 1+1 unawapa stadi zitakazo wawezesha baada ya kisomo kile kujipatia namna ya kujikimu ndio maana tukaita Mpango wa Uwiano wa Kiuchumi Katika Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni kiasi gani cha kuanzia inategemea na vikundi vyenyewe viliazimia kutaka kupatiwa stadi zipi. Mathalani kuwa Seremala au Waashi vifaa vile ndio bei yake sasa pengine tu rai ya Mheshimiwa Mbunge nifanye utafiti na nitamuagiza Afisa Elimu anayehusika katika maeneo yake, kuona kikundi hicho anachokizungumza katika kujitafakari kwao waliazimia kufanya nini ili kujikimu na tuone.

Je, kiwango hicho walichopewa ndicho kilichokuwa kinastahili?na baada ya hapo nitaweza kutoa uamuzi lakini nitakuwa muongo sasa hivi nikikwambia wanaambia punguza maana sijui wenyewe wana kikundi waliazimia kufanya mradi gani.

Na. 226

**Watu Wanaochanganya Mafuta ya Taa na Dizeli**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Je, Serikali kupitia wakala wake wa *EWURA* Imefanikiwa kukamata watu wangapi wanaohusika na uchanganyaji wa mafuta ya taa na dizeli katika kipindi cha miaka miwili ya 2007 – 2008 , na ni hatua zipi zilichukuliwa dhidi yao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika,, naomba kujibu la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa Mbunge wa Bubu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* Pamoja na majukumu mengine iliyonayo inasimamia ubora wa bidhaa za mafuta ya dizeli zinazouzwa hapa nchini .Katika kutimiza wajibu wake, EWURA katika kipindi cha miaka miwili iliyopita 2007 na 2008 ilifanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye vituo vya kuuzia bidhaa hizo, hifadhi za bidhaa hizo na baadhi ya magari ya kusafirishia bidhaa hizo na kuchukua sampuli kutoka katika matenki ya maghala ya kuhifadhia bidhaa za mafuta ya dizeli kisha kupima ubora wa bidhaa za mafuta ya dizeli kama unakidhi viwango vilivyo thibitishwa na Shirika la Viwango la Tanzania *(TBS).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha mwaka 2007, *EWURA* ilichukua sampuli kwenye vituo vinavyouza bidhaa za mafuta ya dizeli sabini na tano (75). Matokeo ya maabara yalionyesha kuwa jumla ya vituo vinavyouza bidhaa za mafuta ya petroli ni hamsini na tisa (59) vilikuwa vinauza mafuta ambayo hayakuwa yanakidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Tanzania *(TBS).*

Vilevile katika kipindi cha mwaka  2008, EWURA ilifanikiwa kuchukua sampuli katika vituo vinayouza bidhaa za mafuta ya dizeli  tisini (90). Matokeo ya maabara yalionyesha kuwa kati ya vituo hivyo, vituo arobaini na nane (48) vilionekana kuuza bidhaa za mafuta ya dizeli zisizokidhi viwango vilivyoweka na Shirika la Viwango Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2007- 2008 EWURA ilikagua maghala ya kuhifadhia mafuta thelathini na tatu (33) na magari kumi na mawili (12). Kati ya maghala hayo, kumi na nane  (18) yalikutwa na bidhaa za mafuta zisizokidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania.

Pia kati ya magari 12 ya mafuta yaliyokaguliwa , magari (6) yalikutwa na bidhaa za mafuta ya dizeli yasiyokidhi Viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania. Kazi hii inaendelea na itaendelea kufanyika sehemu zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya dizeli  2008 kifungu 44, kifungu kidogo cha 2 (a),  na kanuni za uchukuaji na upimaji wa ubora wa mafuta, mamlaka imechukua hatua zifuatazo juu ya waliokutwa na bidhaa za mafuta ya petroli zisizokidhi viwango. *(Makofi)*

Katika kipindi cha mwaka 2007 hadi 2008, vituo 102 zilitozwa faini na kufungiwa kwa muda ;vituo 5 vilifungiwa kwa miezi 12 kila kimoja.Vituo vilivyofungiwa kwa miezi kumi na mbili  (12) ni: Abdulatif Mohamed Msamvu,Barabara ya Iringa, *Abdullatif Kobil* Msamvu, Barabara ya *Dodoma*,  *Oilcom Kihonda*, Brabara ya Dodoma;*Camel Oil Msamvu*,Barabara ya Dodoma vyote vya Manispaaa ya Morogoro na Vigwaza Petrol Station katika Mkoa wa Pwani.

**MHE. MASOLWA C MASOLWA:**  Mheshimiwa Spika kwa kuwa Takwimu za maabara zinaonyesha kwamba zaidi ya nusu ya matokeo ya mafuta hayakidhi viwango je, EWURA huwa wanachukua vipimo pia kwa mafuta yanayoingia nchini ili kuona ubora wake?

**NAIBU WAZIRI  WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, meli inapofika Bandarini pale ambapo TRA wanafanya ukaguzi wa idadi ya mafuta pia hapohapo hufanywa *sample testing* kujua mafuta yale ni mafuta yanakidhi viwango. Na mafuta huchuliwa pale na kupelekwa maabara kabla hata hayajaingia kwenye mfumo wa kuingia kwenye *Distribution* (ugawaji wa mafuta) katika mfumo huu wa kawaida kwa hiyo taarifa ni kwamba mafuta yanafanyiwa ukaguzi kabla hayajaingia kwenye mfumo wa ugawaji.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, EWURA ndicho chombo kinachopanga bei ya mafuta na  wakati mwingine bei za *EWURA* huwa juu kuliko bei za wafanyabiashara wa mafuta. Je, *EWURA* huwa inazingatia vigezo gani bei zao kuwa juu na bei za wafanyabiashara kuwa chini?

**SPIKA**: suala la msingi lilikuwa ubora wa mafuta siyo bei. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa yote unayajua basi jibu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo wanazotumia *EWURA* kupanga bei ya mafuta ni vingi. Na vinazingatia mambo mengi vinazingatia bei ya kununulia, bei ya soko huko nje, gharama za Bandarini Dar es saalm, gharama zinazokadiliwa za usafirishaji na ndio maana unatakuta labda bei za Dar es salaam zikawa tofauti na bei za Kigoma kwa sababu ya kile kipande cha usafirishaji hapo katikati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo mambo yanayozingatiwa ni mengi. Lakini *EWURA* inaweka bei ya kikomo cha juu na kikomo cha chini, kama walivyosema *EWURA* wenyewe wakati wa semina ya Wabunge juzi hiyo haimzuii mfanyabiashara kuweka bei ya kwake mwenyewe hata ikiwa chini ya bei ya hapo ya bei elekezi watakayo toa wao.

Mheshimiwa Spika, kazi ya *EWURA* ni kwamba wao wamefanya tathimini yao kwa kujua kwamba hiki ndio kiwango stahili kwa mazingira ya biashara wakati huo. Kama bei ikiwa chini pia *EWURA* wanaingia kuangalia kwanini bei iko chini labda kuna mambo mengine hapa yaliyopita yanayomfanya yule bwana kuwa na nafasi kubwa zaidi ya kupunguza bei kuliko wengine, sasa lazima tujue hapa kuna kanjanja au kama kuna kitu kingine.

**MHE. IDDI MOHAMED AZZAN:** kwa kuwa *EWURA* imekuwa ikifungia vituo vingi na kuviadhibu kwa kuuza mafuta ambayo yamechanganywa na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri hapa kwamba zipo *depot* au maghala ambayo yamegundulika yakiwa na mafuta ambayo hayakidhi viwango. Je, ni maghala mangapi ambayo yamechukuliwa hatua kwa kusambaza mafuta ambayo hayakukidhi viwango.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yangu ya msingi *EWURA* ilikagua maghala ya kuhifadhia mafuta 33. Na katika hayo maghala 18 yalikutwa na bidhaa za mafuta ya dizeli isiyokidhi viwango. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Sheria maghala 18 yatakuwa yamechukuliwa ya kuuza mafuta chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa lazima niseme kitu kimoja kwamba yanapokuwa mafuta yako chini ya kiwango kuna sababu mbalimbali zinazofanya mafuta yawe chini ya kiwango. Kwa hiyo, *EWURA* wanafanya kutoa adhabu ile kulingana na *Findings* matokeo waliyopata kulingana na utafiti waliofanya baada ya kujua kwamba haya ni mafuta yaliyochanganywa au labda yametokana na uchafu wa *matank* au kadhalika. Kwa taarifa niliyonayo ni kwamba maghala 18 haya yamechukuliwa hatua na *EWURA*. *(Makofi)*

Na 227

**Kuweka Mitambo ya Umeme Katika Mji wa Sumbawanga**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI (K.n.y. MHE. PAUL PETER KIMITI)** aliuza:-

Kwa kuwa, mwishoni mwa mwaka 2008 Serikali kupitia *TANESCO* iliahidi kununua genereta nne (4) kwa kutangaza tenda mbalimbali ili miji ya Namanyere na Mpanda iwe na uhakika wa kupata umeme.

(a) Je, mpaka sasa ni mtu, taasisi au kampuni gani iliyopatikana kwa ajili ya kuleta mitambo hiyo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kushirikiana na kumsaidia Mzalendo Bwana Kasiano Kaegele akamilishe nia yake ya kiwanda cha mkaa wa mawe Namwele, Sumbawanga ili kitoe huduma ya Nishati ya umeme kwa Mkoa mzima na kupunguza mzigo mkubwa unaobebwa na *TANESCO* Nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wizara yangu iliahidi hapa Bungeni wakati wa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge tarehe 16 Aprili, 2008, kununua Jenereta 4 zenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 1.25 kila moja ili Mji wa Sumbawanga uwe na uhakika wa kupata umeme.

Hata hivyo kama ilivyoelezwa hapa Bunge tarehe 3 mwezi huu wa julai, 2009 wakati tukijibu swali Na 154 lililoulizwa na Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko (Mb), kuwa maombi ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa jenereta 17 zenye uwezo wa kuzalisha MW 1.25 kila moja kwa ajili ya miji ya Kibondo, Kasulu, Loliondo, Sumbawanga na Kigoma mjini yaliwasilishwa Serikalini, kati ya hizo Jenereta 4 kwa ajili ya mji wa Sumbawanga. Mpaka sasa jenereta tano tu za Kigoma mjini ndizo zilizopatiwa fedha, jenereta zilizobaki zinasubiri upatikaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti ,Mbunge wa Sumbawanga mjini kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali natambua kuwa mji wa Sumbawanga kwa sasa unategemea umeme kutoka Zambia ambao siyo wa uhakika, na kiwango cha ubora wake si cha kuridhisha *(Low voltage).* Mipango ilibuniwa ya kuvunja *capacitor bank* ili kuboresha upatikanaji wa umeme kutoka Zambia umeonekana hautakuwa na tija kwa kuwa huko Zambia kwenyewe umeme hautoshi kaskazini mwa nchi hiyo. Kwa kutambua hilo Naibu Waziri wa Nishati na Madini alikwenda Zambia kuongea na Wizara ya Nishati ya Zambia ili kujadili upatikanaji wa umeme Sumbawanga .

Mheshimiwa Naibu Spika, aliongozana na wawakilishi wa wa Utawala wa Mkoa wa Rukwa na watalaamu wa *TANESCO* wa Mkoa na Makao Makuu. Kwa Muhtasari Serikali ya Zambia imekubali kuwekeza kwenye mitambo ya umeme ya Chasimba ili kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme hapo kwa kuunganisha kwa kuunganisha na kituo cha umeme cha Mbala.

Makubaliano hayo yatawezesha kuongeza kiwango cha umeme Sumbawanga, na kama umeme huo utakuwa utakuwa ni mwingi wa kutosha ,fikra za kuunganisha na Namanyere inaweza ikapitiwa utekelezaji. Ili hilo liwezekane ni lazima umeme utakaofika Sumbawanga uwe zaidi ya MW6.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine kama nilivyokwishaeleza mipango ya kununua mitambo imekamilika, italetwa na Kampuni ijulikanayo kama *Zwart Twchniek Ltd.* ya Uholanzi, na itakuwa na uwezo wa jumla ya MW 5.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TANESCO* na *REA* imekuwa ikitafuta vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwa kutoa ruzuku na misaada ya kitaalamu kwa waibuaji wa miradi ya umeme waliozingatia vigezo na vya kupata ruzuku na misaada hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo naomba Bwana Kasiano Kaegele awasilishe ofisini kwangu nia hiyo, tutaifanyia tathimini ili tubaini kama imefanyiwa upembuzi wa kutosha na pia kama amezingatia vigezo vya kupatiwa ruzuku ili mradi huo wa makaa ya mawe uweze kupatiwa msaada wa Serikali kama itakavyowezekana kulingana na uwezo wa Serkali kwa wakati huo

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** kwa kuwa ahadi ya kupeleka umeme kutoka Sumbawanga kwenda Namanyere Nkasi ilikuwa imetolewa na Serikali na kwamba wangeanza kutandika nguzo hata kabla mitambo yenyewe hiyo haijafika. Ninapenda kufahamu sasa hatua hiyo imefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jakaya Mrisho Kikwete alipokuwa anahutubia hapa Bungeni alipokuwa anahutubia Bunge hili Tukufu. Aliahidi kwamba umeme lazima utapatikana pale Namanyere hata kwa kununua jenereta, na pale alipokuwa anazindua mfuko wa Mwalimu Nyerere *Raising Fund* Dar es salaam kwa mara ya pili tena alitamka kwamba Namanyere ni lazima inapatiwa umeme na hapa Mheshimiwa Waziri amesema jenereta hazijanunuliwa. Je, ni kwanini ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais hazijapewa umuhimu wa kwanza na Wananchi wa Namanyere waelewe nini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Nyami kwamba suala la umeme wa Namanyere kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais linaendelea kupaitwa utekelezaji.

Kwa sasa katika Mkoa huo wa Rukwa umeme unaokwenda Namanyere unatokea Sumbawanga kiasi cha Kilomita 100, hapo Sumbawanga penyewe umeme uliopo ni wa megawati 3 hautoshi kwa hiyo ndio maana nikasema kwenye majibu ya msingi ili umeme uende Namanyere lazima Sumbawanga penyewe pawe na umeme usiozidi megawati 6 kutokea Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema katika majenereta hayo yananyokuja. Majenereta manne kila jenereta moja ina uwezo wa megawati 1.25 kwa sababu mahitaji ya Namanyere yanaelewka na kwa sasa hivi na kwa sasa hivi mnatumia hicho kijenereta cha dizeli kuwashia pale Halmashauri, mimi nakuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitashauriana na wenzangu kwamba ili katika jenereta tatu japo moja iende Namanyere ikakidhi mahitaji ya msingi wakati tuna kamilisha tatizo la Namanyere.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na muda tunaendelea na swali linaloelekezwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 228

**Mauaji ya Wazee Vikongwe**

**MHE. KHERI KHATIBU AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la kuwatunza wazee ni wajibu wa familia; na kwa kuwa jamii ya watanzania hivi sasa inashuhudia mauaji ya wazee vikongwe hasa katika Kanda ya Ziwa Victoria:-

(a) Je, ni vikongwe wangapi wameuawa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2005 hadi 2008?

(b) Je, kuna watu waliokamatwa kuhusiana na mauaji hayo?

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani za dharura na za makusudi kuzuia mauaji hayo?

**NAIBU WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kheri khatibu Ameir, Mbunge wa Matemwe lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, vikongwe waliouawa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2005 hadi 2008 ni vikongwe 1997.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi 2008 jumla ya watuhumiwa 1698 wa mauaji ya vikongwe wamekamatwa.(c)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali kuzuia mauaji hayo ikiwemo:-

(i) Kuvitumia vikundi vya Intelijensia ili kubaini matukio, kutambua wote wanaojihusisha na uhalifu na wanaonunua viungo ili kuwakamata na kuwafikisha mbele ya sheria.
(ii) Kushirikishirikiana na Vikundi vya Ulinzi wa Mgambo, Sungu Sungu, Ulinzi Shirikishi Jamii ili kuwalinda vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi.
(iii) Serikali imeimarisha *task force* ya kila Mkoa, Wilaya ili kuzuia na kupambana na matishio ya uhalifu ukiwemo mauaji ya albino na vikongwe
(iv) Tunahimiza familia ziongeze jitihada za kuhudumia na kulinda wazee wao.
(v) Familia ziwe mstari wa mbele kushirikiana na vyombo vya dola katika kutafuta na kubaini waovu katika jamii zetu
(vi) Jeshi la Polisi linaendelea kutoa Elimu kwa wananchi kupitia Polisi Jamii, ili waweze kuacha vitendo vya mauaji ya vikongwe na uhalifu kwa ujumla.

**MHE. KHERI KHATIBU AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa jawabu lililotolewa na Waziri, waliofariki kati ya mwaka 2005 mpaka 2008 ni watu 1997, hii inaonekana kwamba, kwa muda wa miaka mitatu kwa kila siku wanakufa vikongwe wawili, hawa ni vikongwe tu. Waliokamatwa ni 1698; Je ni wangapi wamefikishwa mahakamani na wangapi wamehukumiwa na hukumu zao ziko vipi?

**NAIBU SPIKA:** Hilo swali la *statistic* ataliweza sasa hivi, tena Waziri mwenyewe anakaimu?

**NAIBU WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huko nyuma mauaji ya vikongwe yalichangiwa na kesi za kawaida za mauaji hivyo hatuwezi kutoa takwimu halisi kati ya hawa ni wangapi na waliofikishwa mahakamani ni wangapi na wangapi walihukumiwa. Kwa sababu ilichukuliwa kwa ujumla yote ni makosa ya uhalifu wa mauaji.

**MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru sana. Kwa kuwa mauaji ya Albino na Vikongwe ni tatizo ambalo linazidi kuwa kubwa, Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba wakati umefika kuongeza nguvu ya askari kwenye maeneo yenye mauaji mengi. Mfano mzuri ni kama walivyofanya Tarime na Rorya.

**NAIBU WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI k.ny WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba upo umuhimu wa kuongeza jitihada katika kupambana na mauaji haya ya kidhalimu,

lakini mfano mzuri ni kwamba Serikali inachukua hatua na mapambano haya yakiongozwa na Waziri Mkuu, sote ni mashahidi namna ambavyo amefanya ziara ya kuhamasisha na kuhakikisha mapambano haya ni endelevu. Hivi sasa vikosi vyetu vimejipanga vizuri katika kupambana na hali hiyo na kila jitihada zitachukuliwa ili kuhakikisha mauaji haya ya kidhalimu yanaondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi ningependa nitoe wito kwamba wananchi waachane na dhana hizi za kishirikina ambayo inasababisha kwa kiasi kikubwa mauaji haya. Hasa imani za kichawi ambazo zinaleta matatizo makubwa katika nchi yetu na katika kufanikiwa ni kufanya jitihada ya kazi zaidi lakini si kwa njia za kichawi. *(Makofi)*

Na. 229

**Vigezo vya Hospitali za Kawaida kuwa Hospitali za Rufaa**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwanzoni mwa mwezi Februari,2009 Serikali ilitoa ya ridhaa kwa hospitali ya Sliani inayoendeshwa na Madhehebu ya KKKT Arusha kuwa Hospitali ya Rufaa:-

(a) Je, ni vigezo gani vinavyotumiwa na Serikali kufanya Hospitali yoyote iwe Hospitali ya Rufaa?

(b) Kwa kuwa, Hospitali ya *St. Francis* ya Mjini Ifakara ambayo inaendeshwa na madhehebu ya Kanisa katoliki ina vitanda 371 na watumishi zaidi ya 500, kituo cha utafiti cha Kimataifa (*ICH*) na chuo cha Waganga Wasaidizi (*Assistant Medical Officers*); Je, ni vigezo gani vya ziada vinahitajika kutimizwa ili Hospitali hiyo iwe ya Rufa?

(c) Je, Serikali haioni kuwa hamna uwiano wa mgawanyo wa Hospitali za Rufaa nchini hasa ikizingatiwa kuwa Mikoa ya Kusini ina Hospitali moja tu ya Rufaa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama Mbunge wa Kilombero, kwanza naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haijatoa ridhaa kwa Hospitali ya Seliani kuwa Hospitali ya Rufaa, bali imetoa ridhaa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kuitumia hospitali ya Seliani kama Hospitali yake Teule, kama ambavyo inatumika hospitali Teule ya *St. Francis* katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero. Baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a)Vigezo muhimu vinavyotumika ili kuifanya Hospitali yoyote iwe walau ya Rufaa ni:-

(i) Kuwa na wataalam wa kudumu na kutosha walau katika huduma muhimu zifuatazo:-

(a) Upasuaji (*Surgical services*);

(b) Magonjwa ya akina Mama (*obstetrics and Gynaecology*);

(c) Magonjwa ya watoto(*Paediatrics*);

(d) Huduma za uchunguzi wa magonjwa *(Diagnostic Services*);

(e)Huduma za meno; na

(f) Huduma za macho, masikio na pua (*ENT*).

(i) Kuwa na na vifaa vya kutosha kwa ajili ya huduma mbalimbali za kitalaam.

(ii) Kuwa na majengo ya kutosha kutolea huduma zote zinazotakiwa katika hospitali hiyo.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, ili hospitali ya St. Francis iweze kufikiriwa kupandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa ya kanda au Taifa inatakiwa kutimiza vigezo nilivyovitaja katika kipengele (a) hapo juu. Aidha, baada ya kujiridhisha kuwa imekidhi vigezo hivyo wahusika wanatakiwa kuwasilisha Wizarani maombi ya kupandishwa hadhi kuwa hospitali ya rufaa. Hata hivyo, kwa kuzingatia ukubwa wa gharama za kuendesha hospitali za rufaa ni vema kwanza tuhakikishe kuwa walau kila kanda inakuwa na hospitali ya rufaa badala ya kuwa na hospitali mbili za rufaa katika kanda moja.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa sasa hakuna uwiano sawa wa mgawanyo wa hospitali za Rufaa hapa nchini. Kwa kulitambua hili Serikali imeanza mchakato wa kujenga Hospitali ya Rufaa Mkoani Mtwara kwa ajili ya Kanda ya Kusini. Aidha, kuna mpango wa kujenga hospitali ya Rufaa Dodoma kwa ajili ya Kanda ya Kati. Kupitia mpango wa maendeleo ya Afya ya Msingi Serikali itaboresha hospitali zote za Mikoa ili kuwa hospitali za rufaa za mikoa. Hii ni pamoja na kuziongezea idadi na aina ya wataalam wanaotakiwa.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. namshukuru Naibu Waziri kwanza nimuarifu kwamba vipengele vyote (a) katika hospitali ya *St. Francis Ifakara* yamekidhiwa kwa hivyo tutatuma maombi.

(i)kwa kuwa hospitali ile ina vifaa karibu vinavyolingana na Hospitali ya Muhimbili. Je, Wizara itakubali sasa kuanzisha mchakato wa kuweka Chuo Kikuu Kishiriki ili tuzalishe Madaktari wengi.

(ii)Katika Hospitali ile kuna watumishi wa aina tatu, kuna wale wanaolipwa na Serikali Kuu na wale wanaolipwa na Halmashauri na wapo wanaolipwa na Dayosisi. Kwa kuwa wale wanaolipwa Dayosisi ni wengi na maslahi yao hayalingani na watumishi wanaolipwa na Serikali Je, Wizara itakuwa tayari kutoa ruzuku ya kusaidia Dayosisi ile ili mishahara ya hawa watumishi wa chini ambao ndiyo wanafanya kazi kubwa katika Hospitali ukilinganisha na wenzao katika Wizara ya Afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa kwamba Hospitali ya *St. Francis* ina watalaamu na vifaa vya kutosha, kuhusu suala la kufanya mchakato wa kuanzisha Chuo Kishiriki hili ni wazo zuri, lakini sasa hivi bado Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba tunakiboresha kile chuo kikuu kishiriki cha Muhimbili ambacho sasa hivi tunajenga nje ya Mji ili kukipanua na kuweza wanafunzi wengi zaidi. Hata hivyo hilo ni wazo zuri tunalichukua baadaye tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuna watalaamu wa aina tatu, ambayo wanalipwa na Serikali Kuu, Halmashauri ya Wilaya na Dayosisi lakini katika sera yetu ya afya Wizara katika Hospitali hizi Teule huwa tunatoa Ruzuku kwa sababu ya vitanda lakini vile vile mishahara ya Watumishi, lakini kuna wale watumishi ambao Dayosisi wanawaajiri wao. Tumekuwa tukitoa maelekezo hapa katika Halmashauri zetu na Hospitali zote ambazo ni teule kwamba wale wafanyakazi ambao wako katika Dayosisi ni vizuri nao wakawasiliana na Halmashauri husika ikaombewa ajira halafu wale watumishi wakaendelea kufanya kazi katika Hospitali zile teule.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwakumbusha Halmashauri zote ambazo wanahospitali Teule, wale wafanyakazi ambayo wanasifa za kuajiriwa wahakikishe kwamba wanawaajiri na kuwaacha pale pale kwa sababu watatusaidia kutoa zile huduma na kuboresha zile huduma katika hospitali zetu teule.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umeisha na maswali yameisha. Kwanza kabisa tuwatambulishe wageni tulionao hapa Bungeni. Tunao wageni wengi leo.

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Capt. John Chiligati, Mwenyekiti wa Bodi Ndugu Lucas Nsagazwa na Mjumbe wa Bodi Ndugu Pius Chakutanga karibuni sana, kuna wageni wa Mheshimiwa Dr. James Msekela, ambao ni Ndugu Haruna Luambo Mjumbe wa Kamati ya siasa ya CCM Wilaya ya Uyui, Ndugu Said Ntohondi, katibu wa Mbunge Tabora Kaskazini na Ndugu Alex Msekela ambaye ni mtoto wake, wote mnakaribiswa.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni 75 wa Mheshimiwa Juma Killimbah, ambao ni wanafunzi wa shule ya msingi Kiomboi wakiongozwa na Mwalimu wao Ndugu Hamis Sinda Itanda, mwalimu na wanafunzi wasimame popote walipo, nafikiri wamekosa nafasi labda wapo *basement.*

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni 12 wa Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, ambao ni Wenyeviti wa CCM wa Kata ya Musoma Mjini naomba wasimame ahsanteni karibuni sana tunawashukuru kwa kuja kutuangalia, Tuna wageni wa Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Ponsiano Nyami kutoka *D-Light design East African Limited* ambayo ni Ndugu Joseph Mutashobya, mtalaam wa masoko na mauzo na Ndugu Abbas Mohammed Meneja wa Masoko, karibuni sana. Tunao wanafunzi 40 na Walimu watatu kutoka shule ya Msingi Kizota, Dodoma karibuni sana wenyeji wetu na tunawatakia kazi njema huko.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wa Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, ambao ni Stand Kibona na Ndugu Enock Bwire, karibuni sana hakusema ni wanahusiana vipi nafikiri ni ndugu zake. Tunao wageni wa Mheshimiwa Ephraim Madeje, ambao ni Mwenyekiti wa CCM Dodoma Mjini Ndugu Denis Bendera, Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini Ndugu David Mzuri, Katibu Msaidizi CCM Wilaya ya Dodoma Mjini Ndugu Eva Degeleki karibuni sana. Pia wapo Wenyeviti 30 wa CCM Kata wa Wilaya ya Dodoma Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni wa Mheshimiwa Shally Raymond ambao ni Makatibu waenezi wa Kata zote za Manispaa za Moshi wakiongozwa na mratibu wa msafara Ndugu Bakari Mwacha, karibuni sana. Tuna wageni wa Dr. Luka Siyame Mbunge wa Mbozi Magharibi, Ndugu Bryson Simwinga na Ndugu Daniel Lameck Mwembe, kutoka Mbozi ambao ni wanafunzi kutoka *UDOM*, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wa Waziri wa Kazi Ajira na Maendeleo ya Vijana Profesa Juma Kapuya kundi la kwanza ni familia yake ikiongozwa na mtoto wake Bi. Aisha Kapuya, karibu. Tunalo kundi la pili wageni kutoka Wizarani na Taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ambaye ni Kijakazi Mtengwa na kundi lake lote wasimame mahali walipo, karibuni sana. Kundi la tatu ni mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani *ILO* Kenya, Tanzania, Uganda na Somalia, Ndugu Ausga Mushi, ahsante sana na karibu. Kundi la nne ni wafanyakazi wakiongozwa na Rais wa shirikisho la Vyama vya wafanyakazi *TUCTA* ambaye ni Ndugu Juma Omari, nadhani watakuwa *basement* kwa sababu nafasi haitoshi, karibuni sana. Kundi la tano ni Mwenyekiti wa Chama cha waajiri *(ATE)* ni Ndugu Wakili Kornelius na Katibu Mtendaji wa *ATE* Ndugu Dr. Aggrey Mlimka, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, Kundi la Sita ni ujumbe wa watu nane kutoka MakaoMakuu ya umoja wa vijana wa CCM Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Hamad Yussuf Msauni, karibuni sana, kundi la saba ni ujumbe wa watu 12 kutoka Wilaya ya Urambo wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Ndugu Adam Nkwakwi karibuni sana, naona Urambo mmeshatawala Bungeni wiki iliyopita mlikuwepo na leo tena karibuni sana(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tuna kundi la nane ni wageni 20 kutoka Umoja wa vijana wa CCM Wilaya ya Maswa, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Abel Jambo, karibuni sana kutoka Maswa. Kundi la tisana ni vijana 14 wa kutoka Korea taasisi ya *International Youth Fellowship Can you rise up please*, karibuni sana, tunao wageni wa Kimataifa sina hakika mnaongea lugha gani kwa tutaongea lugha ya kwetu, tumefurahi sana kwamba mpo hapa kushiriki na sisi, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni wa Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegir, ambao ni Ndugu Lengeli na Ndugu Laiser, karibuni sana. Tuna mgeni wa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, ambaye ni Dotto Ameir Gama, ambaye ni mdogo wake, karibu sana. Tunao viongozi wa chama cha walemavu Tanzania wamekuja kusikiliza hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, nafikiri watakuwa kule chini karibuni sana. Wapo wanafunzi 32 kutoka chuo cha biashara *CBE D*ar es Salaam na Mwanza, karibuni sana. Tunao Richard Kasesela na Abdulkarim na Salehe Reyes wako Dodoma kwa ajili ya kutembelea Bunge, Karibuni sana. Mheshimiwa Ritha Mlaki ana Baba yeke mdogo Mchungaji Shangali, kutoka Machame, karibu sana Mchungaji. Pia yupo Sangiwa Mnzava kutoka Moshi, huyu ni Shemeji yake, karibu sana. *(Makofi)*

Kwa ujumla wageni wote mnakaribishwa kwa sababu Bunge letu ni la wazi kila mwananchi ana haki ya kuja kusikiliza. Kwa hiyo, wale ambao hatukuwataja pia tunawakaribisha katika ukumbi huu.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge shughuli za kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa William Shellukindo anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 16 kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika ukumbi namba 227 saa nane mchana. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Mohamed Missanga anawatangazia wajumbe wa Kamati yake kwamba leo kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi Namba 219 saa saba mchana, wajumbe wanaombwa wawahi na kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* Mheshimiwa John Momose Cheyo, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na kikao leo tarehe 16 saa saba mchana katika ukumbi namba 231. Kwa hiyo, wajumbe wake wahudhurie bila kuchelewa.

Waheshimiwa Wabunge nimepata ombi kutoka kwa Mheshimiwa Hafidh Tahir Ali kwamba Wabunge wote wa Mkoa wa Mjini Magharibi wanatakiwa kukutana saa tano leo asubuhi ukumbi wa Pius Msekwa, kuna mambo muhimu nadhani wao wanafahamu.

Waheshimiwa Wabunge haya matangazo mengine yaliyoandikwa kwa mkono nitaya-*study* kwanza kwa sababu sijui yanasema nini, Tuendelee.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Mafua Makali ya Nguruwe

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kutoa Kauli ya Mawaziri kuhusu Mafua Makali ya Nguruwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi; mafua makali ya Nguruwe ni ugonjwa unaoathiri mfumo wa njia ya hewa ya binadamu unaosababishwa na virusi aina ya influenza A, H1,N1. Maambukizi yanaweza kutokea kati ya binadamu kwenda kwa binadamu mwingine kwa njia ya hewa iwapo mgonjwa atakohoa au kupiga chafya bila ya kujikinga au mtu kugusa kitu chenye virusi vya ugonjwa huo na kujigusa mdomoni au puani. Ugonjwa huu husababisha mlipuko kwa binadamu na kuathiri watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu mwenye ugonjwa huo anaweza kuambukiza wengine siku moja kabla ya dalili za ugonjwa kujitokeza hadi siku saba baada ya kuwa mgonjwa. Kwa hiyo, mtu anaweza kumwambukiza mtu mwingine kabla ya hata yeye mwenyewe kujijua kama anaumwa na vile vile wakati akiwa mgonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Ugonjwa; kwa sasa hivi ugonjwa huu umekwishaingia hapa nchini na tumekuwa na mgonjwa mmoja ambaye ni raia wa Uingereza. Hadi sasa hakuna mwananchi Mtanzania ambaye ameonekana kuwa na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mlipuko huu wa ugonjwa ulianza huko Mexico mwezi April mwaka 2009 na hadi sasa nchi 135 zimeathirika na ugonjwa huu zikiwa na wagonjwa wapatao 94,512 na vifo 429. Katika bara la Afrika nchi 11 zimeathirika na kuwa na jumla ya wagonjwa 116 bila ya vifo zikiwemo nchi za jirani za Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua na maandalizi yaliyokwishafanyika katika viwanja vya ndege; maandalizi yaliyokwishakufanyika katika uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere ni kama ifuatavyo:-

(i)Mafunzo kwa watumishi wa afya uwanja yametolewa, na pia kuelimisha na kuhamasisha wafanyakazi wa uwanja wa ndege.

(ii)Ufuatiliaji wa jinsi ya kutambua abiria walio na dalili za ugonjwa wanaoingia nchini umeimarishwa, fomu maalumu zimeandaliwa kwa abiria wanaoingia ili kuweza kutambua dalili za ugonjwa. Vifaa kinga vimetolewa kwa ajili ya wafanyakazi wa uwanja, gari limetolewa kwa ajili ya shughuli za usafiri endapo kutahitajika kusafirisha mgonjwa.

(iii)Chumba maalumu kwa ajili ya uchunguzi wa awali kwa abiria walio na dalili kimetengwa na chumba hicho kiko katika hatua za mwisho za ukarabati kwa ajili ya chumba maalumu cha hospitali na utaratibu wa rufaa umeandaliwa kwa ajili ya wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Kilimanjaro, Kilimanjaro *International Airport*, mafunzo yametolewa kwa wafanyakazi, fomu za utambuzi za afya zimepelekwa, vifaa kinga vimepelekwa, na ufuatiliaji wa jinsi ya kutambua abiria walio na dalili za ugonjwa wanaoingia nchini umeimarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuimarisha ufuatilia katika viwanja vingine vya ndege vya Arusha, Mwanza na Mtwara. Aidha tunaendelea kuwasiliana na Mikoa yote ya Mipakani yenye njia za kutoka na kuingia nchini kwa ajili ya ufuatiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa wadau mbalimbali kuhusu suala zima la mafua ya nguruwe; wadau ambao wameshirikishwa katika suala zima la kupambana na ugonjwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa;
(b) Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi;
(c) Wizara ya Maliasili na Utalii;
(d) Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika;
(e) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa;
(f) Wizara ya Mambo ya Ndani;
(g) Wizara ya Habari Michezo na Utamaduni;
(h) Wizara ya Miundombinu hasa mamlaka ya bandari na usafiri wa anga na barabar;a
(i) Hospitali binafsi za Aghakan na Hindu Mandal;
(j) Wadau wa maendeleo kwa mfano WHO, kituo cha Marekani cha udhibiti na Kuzuia Magonjwa *CDC n*a wananchi kwa ujumla pia wameshirikishwa kwa njia ya vyombo vya habari na vipeperushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine iliyofanyika ni kama ifuatavyo;

(i) Kuunda Kamati ya watalaam wa kupambana na ugonjwa huu;
(ii) Kutoa elimu na hamasa kwa wananchi juu ya kuwepo na jinsi ya kujiepusha kwa ugonjwa huu kupitia vyombo vya habari na vipeperushi;
(iii) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya mikoani na Wilayani;
(iv) Kuimarisha shughuli za ufuatiliaji wa ugonjwa katika vituo vya mipakani na hasa katika uwanja wa kimataifa wa Julius Nyerere na *KIA;*

(v) Kuimarisha utoaji wa taarifa za magonjwa ya milipuko kutoka vituo vya afya

(vi) Kutayarisha sehemu za kutenganisha na kulaza wagonjwa iwapo ugonjwa huo utaingia nchini, *(isolation rooms*);
(vii) Kuandaa na kusambaza vifaa kinga vya kutumia wakati wa kumhudumia mgonjwa

(viii) Kujenga uwezo wa maabara za Taifa za Influenza ya binadamu na wanyama kwani sasa vipimo vipo

(ix) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imepokea msaada wa dawa inayoitwa *tamiflu* kutoka shirika la afya duniani ambazo ni kwa ajili ya kinga na matibabu pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa zilizopatikana ni dozi 52,000. Mgawanyo wa dawa hizo umeelekezwa katika Hospitali za Mikoa nchini kote, pamoja na hospitali kubwa za binafsi. Dawa hizo zimepelekwa katika mikoa 20, hospitali tatu za Manispaa ya Jiji la Dar es Salaam, Hospitali nne za Rufaa na za binafsi tatu, ambazo ni Aghakhan, Hindumandali na Herbert Kairuki. Kila hospitali ilipatiwa dozi 1000 kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Gazeti la *The Sun* la Uingereza kuhusu idadi ya wagonjwa wa mafua ya nguruwe na msimamo wa nchi dhidi ya kauli hiyo: Gazeti la *The Sun* la Uingereza, toleo la wiki iliyopita, lilitoa taarifa ya kupotosha kuhusu idadi ya wagonjwa waliopatikana hapa nchini. Gazeti hilo liliripotiwa kuwa Tanzania inashika nafasi ya nane duniani kati ya nchi 10 zilizokumbwa na Ugonjwa wa Mafua Makali ya Nguruwe ikiwa na jumla ya wagonjwa 2076. Taarifa hiyo ilinukuliwa na moja ya magazeti yanayoandikwa kwa Lugha ya Kiswahili hapa nchini. Napenda kuwaarifu wananchi kwamba, hadi sasa ni mgonjwa mmoja tu aliyethibitishwa kuwa na mafua makali ya nguruwe, ambaye ametibiwa na kupona kama tulivyotoa taarifa hapo awali. Hivyo, naomba ieleweke kwamba, taarifa iliyotolewa na Gazeti la *The Sun* la Uingereza si sahihi na tayari tumekwishatoa taarifa rasmi kwa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi tunawaomba waendelee kufuatilia taarifa za nchini kuhusu hali ya ugonjwa duniani na nchini. Vyombo vya Habari viendelee kusambaza taarifa za ugonjwa huu na wananchi waendelee na wafuatilie mikakati ya kinga ya ugonjwa na watoe taarifa kwenye vituo vya matibabu endapo wataona wana dalili ambazo zimetajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa taarifa na mgonjwa mwenyewe si alitoka Uingereza hata hivyo? (*Kicheko*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 – Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, inayohusu Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili Mpango wa Kazi na kupitisha Makadirio ya Matumizi

ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru kwa namna ya pekee kabisa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani yake na heshima kubwa aliyoionesha ya kuendelea kunipa nafasi ya kuiongoza Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo na ustawi wa jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole za dhati kwa jamaa na familia za Wabunge wenzetu, waliofariki dunia katika kipindi hiki cha mwaka mmoja ambao ni Marehemu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Marehemu Richard Nyaulawa, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Marehemu Faustine Kabuzi Rwilomba, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Busanda na Mbunge wa zamani wa Jimbo la Biharamulo, Marehemu Phares Kabuye. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi na awajalie ndugu wa marehemu moyo wa subira. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo na Mawaziri wote walionitangulia, kwa hotuba zao nzuri zilizoelezea vyema mipango ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Haroub Masoud, Mbunge wa Koani, iliyojadili na kuyakubali Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu tarehe 1 Juni, 2009. Hotuba hii imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati hiyo, ambao tunaamini utaiwezesha Wizara kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana imepangiwa kazi na majukumu yafuatayo:- (a) uratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za Kazi.

(b) Kuzuia migogoro ya kikazi kwa kufanya kaguzi na kutoa elimu katika sehemu za kazi.

(c) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya ukuzaji wa ajira nchini, hususan upatikanaji wa ajira mpya zisizopungua milioni moja ifikapo mwaka 2010.

(d) Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi kuratibu Mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kukuza ajira, hususan mpango wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

(e) Kuratibu na kusimamia mipango ya maendeleo ya vijana kiuchumi, kisiasa na kijamii.

(f) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mbio za Mwenge wa Uhuru nchini.

(g) Kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya Waajiri.

(h) Kusimamia mipango ya usalama na afya za wafanyakazi mahali pa kazi *(Occupational Health and Safety),* kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA).

(i) Kusimamia mipango ya uboreshaji wa tija na ufanisi kazini kupitia Shirika la Tija la Taifa (*NIP*).

(j) Kuratibu na kusimamia masuala ya Hifadhi ya Jamii nchini.

(k) Kutoa miongozo ya uendeshaji na kusimamia kazi za Wakala na Taasisi zifuatazo: Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii(NSSF); Shirika la Tija la Taifa (NIP); Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA); Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA); Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA); na Ofisi ya Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia utekelezaji wa majukumu haya, Wizara inaongozwa na Sheria, Sera na Miongozo ifuatayo: Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025); Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 – 2010; Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs); Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007; Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2003; Sheria za Kazi Na. 6 ya Mwaka 2004 ya Ajira na Mahusiano Kazini na Na. 7 ya Mwaka 2004 ya Taasisi za Kazi; Sheria Na. 20 ya Mwaka 2008 ya Malipo ya Fidia kwa Wafanyakazi Wanaoumia Kazini *(Workers' Compensation Act);* na Sheria Na. 3 ya Mwaka 2008 ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa shughuli za Hifadhi ya Jamii Nchini ya Mwaka 2008 *(Social Security Regulatory Authority).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 hadi 2010 inaelekeza Wizara yangu kutekeleza maeneo muhimu yafuatayo:-

Kuendelea kuwa karibu na Wafanyakazi na kuhakikisha kuwa, Serikali inayashughulikia kwa ukamilifu na kwa wakati matatizo ya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Na. 20 ya Mwaka 2008 ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia au kupata madhara kazini, imepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kikao chake cha mwezi Oktoba, 2008 na utayarishaji wa Kanuni za Sheria hii umekwishaanza. Aidha, Kanuni za Sheria ya Hifadhi ya Jamii zimekamilika na uandaaji wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa masuala ya Hifadhi ya Jamii unaendelea.

Jumla ya kaguzi za kazi 2,305 zimefanyika katika maeneo ya kazi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara, ambapo wadau mbalimbali pia wameelimishwa juu ya haki na wajibu wao katika kutekeleza Sheria za Kazi kupitia kaguzi hizi. Aidha, wadau wa masuala ya kazi katika Mikoa ya Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Iringa, Singida, Dodoma, Kigoma, Kagera na Mara, wamepatiwa mafunzo ya Sheria mpya za kazi, zinazotumika hivi sasa na wamejengewa uelewa mzuri na uwezo wa kuzitekeleza na kuzitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga mwamko miongoni mwa wafanyakazi na waajiri kuhusu dhana ya mapatano ya pamoja na kuwawezesha wafanyakazi wengi kushirikiana vyema na waajiri katika majadiliano, maamuzi na ukuzaji tija sehemu za kazi, jumla ya vyama viwili vya wafanyakazi vimesajiliwa ambavyo ni Chama cha Wafanyakazi wa Kiwanda cha Karatasi Mufindi *(Mufindi Paper Workers Union-MPETU)* na Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu *(Tanzania Higher Learning Institutions Trade Union - THTU).*

Aidha, Shirikisho moja la Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi vya Afrika Mashariki *(East African Trade Union Confederation - EATUC)* lilisajiliwa. Vile vile Chama kimoja cha waajiri kijulikanacho kama Muungano wa Waajiri wa Kilimo, Biashara, Viwanda na Madini *(Tanzania Association of Agriculture, Commerce, Industry and Mining Employers - TAACIME)* kilisajiliwa. Jumla ya Vyama 23 vya Wafanyakazi, Vyama viwili vya Waajiri na Shirikisho moja vilisajiliwa katika rejista ya vyama. Vyama 17 vya Wafanyakazi vilikamilisha marekebisho ya Katiba zake na kuziwasilisha kwa ajili ya usajili. Aidha, vyama hivyo viliwasilisha taarifa zake za wanachama na mahesabu yaliyokaguliwa kwa ajili ya kumbukumbu na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba, ajira mpya milioni moja zinapatikana kwa wananchi ifikapo mwaka 2010; mpaka kufikia mwezi Desemba, 2008 takwimu za hali ya ajira nchini zinaonesha kwamba, jumla ya ajira mpya 1,271,923 toka sekta mbalimbali zimepatikana kama ifuatavyo: Serikali (85,571), Mashirika ya Umma (965) na Sekta Binafsi (1,185,387). Juhudi zinaendelea kuzihamasisha Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma na Sekta Binafsi, kutoa kipaumbele kwa suala la kukuza ajira katika sekta/maeneo husika na kutolea taarifa.

Aidha, utaratibu umeandaliwa wa kuunda na kuteua Wajumbe wa Baraza la Taifa la Kukuza Ajira na Kamati ya Taifa ya Wataalamu ya Kukuza Ajira. Mchakato huu utashirikisha wadau wa Sekta ya Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 imetafsiriwa kwa Lugha ya Kiswahili na kuchapishwa ili kuwapa wadau uelewa rahisi na mzuri katika kuitekeleza Sera hii. Rasimu ya awali ya Muswada wa Sheria ya Taifa ya Ajira *(Draft National Employment Bill, 2009)* imekamilika, ambapo imefanyiwa marekebisho na kujumuisha vipengele muhimu ikiwa ni pamoja na muundo mpya wa kitaasisi wa usimamizi wa masuala ya ajira nchini. Vile vile, maandalizi ya awali ya utayarishaji wa Kanuni za kutekeleza Sheria ya Taifa ya Ajira yamefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea kuwahamasisha vijana kujiunga katika vikundi mbalimbali vya ushirika ukiwemo ushirika wa kuweka na kukopa (*SACCOS*) na hivyo kuwawezesha kiuchumi na kuongeza ajira; Wizara yangu imekamilisha mchakato wa kuainisha *SACCOS* mbili kwa kila Halmashauri/Manispaa zote Tanzania Bara, ambazo zitapewa fedha za Mfuko wa Vijana na kisha ziwakopeshe vijana. Vile vile, mwongozo mpya unaozielekeza Halmashauri/Manispaa za Wilaya juu ya matumizi bora zaidi ya fedha za Mfuko wa Vijana katika Wilaya zao umekamilika na kwa sasa mchakato wa kuichapisha katika Lugha ya Kiswahili unaendelea. Uhamasishaji wa Vijana kuanzisha *SACCOS* unaendelea kwa kutumia fursa zote zinazojitokeza na Vijana wanaendelea kuhamasika na kujiunga katika *SACCOS* mbalimbali nchini.

Vile vile, vijana 40 kutoka Morogoro, Dar es Salaam na Mpwapwa walipata mafunzo kwa wakufunzi (*TOT*) ya teknolojia ya kutengeneza mkaa kwa kutumia masalia ya mazao na majani makavu chini ya uratibu wa Kituo cha Maendeleo ya Vijana cha Ilonga kwa kushirikiana na wataalamu kutoka *Appropriate Rural Technology Institute (ARTI-TZ)* ya Dar es Salaam, kwa lengo la kuwezesha ukuzaji wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa namna ya kushughulikia masuala ya watoto kisekta umeboreshwa ili kutoa ufanisi na utekelezaji mzuri zaidi na wenye mafanikio katika kushughulikia masuala ya ajira ya watoto nchini. Taarifa ya utafiti wa ajira ya mtoto ya mwaka 2008 imezinduliwa na kusambazwa na sasa inatumika kuwatambua watoto hao. Umefanyika ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu ya kukomesha utumikishaji watoto kwenye maeneo/Wilaya tano kati ya 18 zinazotekeleza programu hiyo. Wilaya hizo ni Simanjiro, Iramba, Igunga, Urambo na Ilemela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2005/06 mpaka kufikia Mei, 2009, Shirika la *NSSF* limewekeza jumla ya shilingi milioni 869,123.17 katika vitega uchumi mbalimbali, ujenzi wa majengo na kutoa mikopo katika miradi ya maendeleo ya Serikali na makampuni ili kusaidia kutatua matatizo makubwa ya kijamii kama ifuatavyo: mikopo shilingi milioni 39,175.4, miradi na dhamana za Serikali shilingi milioni 272,082.25, hisa shilingi milioni 33,235.61, amana za muda maalumu shilingi milioni 369,415.95 na majengo na ofisi shilingi milioni 155,213.95.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine, imeendelea kuratibu utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira kupitia benki na asasi ndogo ndogo za fedha. Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2009 jumla ya shilingi 5,755,698,950 zilikuwa zimetolewa kuwanufaisha wajasiriamali 64,956, ambapo wanaume ni 27,678 na wanawake 37,278 katika Wilaya 46 ambazo hazikufikiwa na zilizopata fedha chini ya kiwango katika awamu ya kwanza ya mpango. Jumla ya benki na asasi za fedha 12 zinashiriki kutoa mikopo kwa wananchi katika awamu ya pili ambazo ni Benki ya CRDB, Benki ya Akiba, Benki ya Posta, Benki ya Wakulima – Kagera, Benki ya Ushirika – Kilimanjaro, Benki ya Uchumi, Benki ya Jamii – Mwanga, Pride, Mfuko wa Dhamana wa Rais, *SCCULT*, Dunduliza na Benki ya Azania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/09, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa Sheria za Kazi, yaani Sheria Na. 6 ya mwaka 2004 ya Ajira na Mahusiano Kazini na Na. 7 ya Mwaka 2004 ya Taasisi za Kazi. Madhumuni ya Sheria hizi ni kutoa haki na wajibu kwa wafanyakazi na waajiri ili kuongeza tija, ufanisi na uhusiano mwema katika sehemu za kazi.

Hivi ni vigezo muhimu katika kukuza uchumi na ajira kwani vinavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kazi moja kubwa iliyofanywa katika kipindi hiki ni ukamilishaji wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi na Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa masuala ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine iliyofanywa na Wizara yangu katika kipindi hiki ni maandalizi ya Sera, Programu na Mikakati ya kukuza ajira nchini, ambayo itakuwa ndiyo Dira ya kuongoza mapambano dhidi ya tatizo la ukosefu wa ajira na hasa miongoni mwa vijana. Wizara ilishirikisha wadau mbalimbali zikiwemo Wizara zote, Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri, *NGOs* na Waheshimiwa Wabunge, ambao waliweza kutoa maoni kupitia fursa na nafasi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sura kamili ya kazi zilizofanywa na Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2008/09 kuhusu usimamizi kazi na huduma za ukaguzi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa mwaka 2008/2009, iliendelea kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi kwa wafanyakazi na waajiri. Hali hii imesababisha kuwepo na mahusiano mazuri katika maeneo mengi ya kazi na hivyo kuleta amani na utulivu kazini, ambayo ni moja ya vivutio muhimu kwa wawekezaji. Kwa sababu hiyo katika kipindi hiki kulitokea migogoro michache ambayo ilipatiwa ufumbuzi, ukiwemo mgogoro wa Kiwanda cha Sukari Moshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/09, Wizara ilitekeleza malengo yafuatayo kuhusu usimamizi wa kazi na huduma za ukaguzi:-

(i) Kukamilisha utafiti juu ya uwezo wa ulipaji na athari za vima vya chini vya mishahara katika sekta binafsi, ulikamilishwa.

(ii) Jumla ya kaguzi 1,211 zimefanyika katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi nzima, ambapo kaguzi 318 zilifanyika chini ya zoezi maalumu lililofanyika kuanzia mwezi Februari hadi Mei, 2009 na kaguzi 893 chini ya utaratibu wa kawaida.

(iii) Kanuni za Sheria Na. 3 ya Mwaka 2008 ya usimamizi na udhibiti wa masuala ya Hifadhi ya Jamii zimekamilika na taratibu za kuwapata Mtendaji Mkuu, Mwenyekiti wa Bodi na Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa masuala ya Hifadhi ya Jamii yamekwishatolewa na tayari watu wamewasilisha maombi na yanaendelea kuchambuliwa.

(iv) Jumla ya rufaa 119 zilitolewa uamuzi kati ya 501 zilizowasilishwa kwa utaratibu wa Sheria za Kazi za zamani.

(v) Fidia ya jumla ya Shilingi milioni 11,340,000 kwa wafanyakazi 105 walioumia au kupata madhara wakiwa kazini imelipwa.

(vi) Kuwashirikisha wadau na jamii kwa ujumla katika kupambana na ajira mbaya ya mtoto, ambapo jumla ya watoto 29,078 waliokuwa katika ajira mbaya wametolewa na kuingizwa katika elimu ya msingi na ufundi.

(vii) Kuratibu shughuli za Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Ajira ya Mtoto.

(viii) Sheria mpya ya Fidia Na. 20 ya mwaka 2008 imekamilika na kupitishwa na Bunge.

(ix) Kushiriki mikutano mbalimbali ya kikanda na kimataifa inayohusu masuala ya kazi kama vile ya Shirika la Kazi Duniani (ILO), Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika ( *SADC*), Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/10 malengo yafuatayo yatatekelezwa:-

(a) Kusimamia majadiliano baina ya wafanyakazi na waajiri.

(b) Kukamilisha Kanuni za Sheria ya Fidia Na. 20 ya mwaka 2008 kwa Wafanyakazi.

(c) Kuratibu uanzishwaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(Workers' Compensation Fund)* na Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa masuala ya Hifadhi ya Jamii *(Social Security Regulatory Authority).*

(d) Kujenga uelewa juu ya viwango bora vya kazi *(Labour Standards)* miongoni mwa Jamii.

(e) Kuratibu na kusimamia Bodi za Mishahara Kisekta.

(f) Kuratibu na kusimamia Sera na Sheria zinazopambana na Ajira Mbaya ya Mtoto.

(g) Kuratibu na kusimamia shughuli za Baraza la Ushauri wa masuala ya Kazi, Jamii na Uchumi *(Labour Economic and Social Council).*

(h) Kuratibu na kushiriki katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani *(May Day).*

(i) Kuendelea kupokea na kushughulikia malipo ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata madhara wakiwa kazini.

(j) Kukamilisha na kumalizia Rufaa zilizo mbele ya Mheshimiwa Waziri na Kamishna wa Kazi.

(k) Kukamilisha na kumalizia mashauri yaliyopo katika Mabaraza ya Usuluhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara yangu imeendelea kuratibu shughuli za ukuzaji wa ajira nchini hususan utekelezaji wa azma ya Serikali kuhakikisha upatikanaji wa ajira mpya milioni moja ifikapo mwaka 2010. Hadi kufikia mwezi Deseaba, 2008 jumla ya ajira mpya 1,271,923 zilikuwa zimezalishwa katika sekta mbalimbali na hivyo kuvuka lengo la kupata ajira milioni moja kwa asilimia 27.2. (*Makofi*)

Hata hivyo, Sekta ya Kilimo ambayo huchukua zaidi ya asilimia 70 ya watu wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka haikuhusishwa katika hesabu hizo. Takwimu hizi zinaonesha kuwa, sekta binafsi inaongoza katika ukuzaji wa ajira nchini kwa kiwango cha asilimia 93.2. Kwa kuwa suala la ukuzaji wa ajira ni mtambuka, hivyo ni jukumu la kila mdau kushiriki kikamilifu katika shughuli za ukuzaji wa ajira na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 imezinduliwa rasmi. Sera hiyo imechapwa kwa Lugha ya Kiingereza na Kiswahili na kusambazwa kwa wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Ofisi za Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Jiji, Mjini, Vyama vya Waajiri, Vyama vya Wafanyakazi, Taasisi Binafsi na za Umma.

(b) Rasimu ya awali ya Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira imekamilika. Taratibu zinaandaliwa za kuufikisha kwa wadau ili ujadiliwe.

(c) Rasimu ya awali ya Muswada wa Sheria ya Taifa ya Ajira imepitiwa na kuboreshwa kwa kuainisha vipengele vipya vinavyokidhi muundo mpya wa Wizara na Taasisi zake.

(d) Hadidu za rejea za Baraza na Kamati za kukuza ajira ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya zimeandaliwa na kuanza kusambazwa katika Ofisi za Mikoa na Wilaya.

(e) Mikoa ya Lindi, Mtwara na Morogoro tayari imeunda Kamati za Kukuza Ajira pamoja na kuteua Maafisa Waratibu wa Dawati la Ajira katika ngazi za Mikoa na baadhi ya Halmashauri na kutoa mafunzo maalum kwa Wajumbe wa Kamati hizo.

(f) Zoezi la kuhuisha Kamusi ya Kazi (Tanzania Standard Classification of Occupations) limefanyika. Rasimu ya awali ipo tayari kusambazwa kwa wadau ili kupata maoni kabla ya kuikamilisha.

(g) Jumla ya makampuni 138 yamefanyiwa ukaguzi ili kubaini wageni wenye vibali na wasio na vibali vya ajira.

(h) Jumla ya Vikao 19 vya kujadili maombi ya vibali vya kazi kwa raia wa kigeni vilifanyika. Maombi 3,762 ya vibali vya kazi yalipokelewa. Kati yake maombi 2,387 yalikuwa mapya na 913 ya kuongeza muda. Maombi 2,473 yalikubaliwa na 827 yalikataliwa. Kati ya maombi yaliyokubaliwa, 1703 ni ya mara ya kwanza na 770 ni ya kuongeza muda. Maombi 457 yalisitishwa ili kupata taarifa zaidi juu ya makampuni yaliyoomba.

(i) Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2009 mikopo yenye thamani ya Shilingi 42,845,518,950 imetolewa kwa wananchi walengwa kupitia *SACCOS*, vikundi na wajasiriamali mmoja mmoja, ambapo jumla ya wajasiriamali waliofaidika na mikopo hiyo ni 66,368 wakiwemo wanaume 42,776 na wanawake 23,592.

(j) Wajasiriamali 204 (wanawake 150 na wanaume 54) toka kwenye makundi ya vijana kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, wamewezeshwa kushiriki Maonesho ya Kumi ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya Afrika Mashariki huko Kigali, Rwanda, ambapo Tanzania ilipata ushindi wa jumla pamoja na wa bidhaa za ubunifu kuwa mshindi wa kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kukamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukuza Ajira pamoja na mpango wake ikiwa ni pamoja na kuendelea na mchakato wa uundwaji wa Kamati za Kukuza ajira za Mikoa na Wilaya.

(b) Kuratibu vikao vya utatu vya kujadili maombi ya vibali vya kazi kwa wageni.

(c) Kufanya kaguzi mara kwa mara z a vibali vya kazi kwa wageni wanaofanya kazi nchini.

(d) Kuwawezesha wananchi hususan wa maeneo ya vijijini kupata mafunzo ili waweze kujiajiri na kuboresha ajira zao kwa lengo la kuondoa umaskini.

(e) Kuwasilisha rasimu ya Muswada wa Sheria ya Ajira kwa wadau kwa ajili ya kuujadili.

(f) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kukuza Ajira.

(g) Kuratibu ushiriki wa wajasiriamali wadogo wadogo wa sekta isiyo rasmi katika maonesho ya Kumi na Moja ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya Afrika Mashariki yatakayofanyika Jijini Dar es Salaam. Maonesho haya yatakwenda sambamba na

maadhimisho ya miaka kumi tangu maonesho haya yaanzishwe mwezi Novemba, 1999.

(h) Kutekeleza hatua ya pili ya Marekebisho ya Sheria za Kazi na Ajira.

(i) Kwa kushirikiana na wadau, Wizara itaendelea na utekelezaji wa Mradi wa kujenga usawa wa jinsia na ajira bora kwa wanawake.

(j) Kuratibu Wakala wa Ajira nchini.

(k) Kuratibu mchakato wa uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Mafunzo ya Ajira *(National Centre for Employment Studies)* ambacho kitasaidia kutoa elimu, kuchambua na kutoa taarifa kuhusu masuala ya Sekta ya Ajira kwa Serikali, Taasisi za Umma na Binafsi, *NGO* na wananchi kwa ujumla.

(l) Kuendeleza mchakato wa uandaaji wa Sera ya Taifa ya Uhamaji wa Nguvu Kazi *(Labour Migration Policy).*

(m) Kuratibu miongozo, viwango na mifumo ya kukusanya, kuchambua na kutangaza takwimu na taarifa za soko la ajira kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na wadau wengine.

(n) Kukamilisha na kuratibu matumizi ya Kamusi ya Kazi kwa wadau mbalimbali kama vile waajiri, Wakala wa Huduma za Ajira, Idara ya Uhamiaji na Watafiti.

(o) Kwa kushirikiana na wadau wengine Wizara itashiriki kikamilifu katika utafiti wa nguvu kazi katika nchi za Afrika Mashariki *(East African Manpower Survery)* na kushiriki katika maandalizi ya utafiti wa Watu wenye uwezo wa kufanya kazi *(Labour Force Survey)* wa mwaka 2010/11.

(p) Kuendelea kuboresha mfumo wa upatikanaji wa taarifa na takwimu za soko la ajira kwa ngazi za Mikoa na Wilaya kwa kuanzia Mikoa ya majaribio ya Lindi, Mtwara na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Vijana, katika mwaka 2008/09, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuratibu shughuli za maendeleo ya vijana nchini, ikiwa ni pamoja na kufanya tafsiri na machapisho ya Sera ya Maendeleo ya Vijana, maandalizi ya mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana na pia kuwashirikisha vijana katika matukio na mikutano mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/09, malengo yafuatayo yalitekelezwa:-

(a) Utaratibu mpya umewekwa kwa kila Halmashauri ya Wilaya Tanzania Bara kuainisha *SACCOS* mbili za vijana ili ziweze kupatiwa fedha za Mfuko wa

Maendeleo ya Vijana na kisha *SACCOS* hizo ziwakopeshe vijana wajasiriamali nchini.

(b) Halmashauri 115 ziliwasilisha Wizarani majina 229 ya *SACCOS*, kati ya hizo 220 zimepewa fedha kwa wastani wa Shilingi 5,000,000 kwa kila *SACCOS* na hivyo kufanya jumla ya fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya mikopo ya vijana kupitia mfumo wa *SACCOS* katika kipindi cha mwaka 2008/2009 kufikia shilingi 1,100,000,000.

(c) Jumla ya miradi ya maendeleo 1,458 ilizinduliwa nchi nzima wakati wa Mbio za Mwenge wa Uhuru. Miradi hiyo ilikuwa na jumla ya thamani ya shilingi 93,209,996,810.72. Nguvu za wananchi zilikuwa na thamani ya shilingi 23,153,299,636, mchango wa Serikali ni Shilingi 33,708,750,188.72, wahisani walichangia Shilingi 32,059,904,516 na Michango ya Mwenge ilikuwa shilingi 4,288,042,470.

Aidha, Mwenge wa Uhuru ulihamasisha pia wananchi katika masuala ya kutunza mazingira hususani vyanzo vya maji, mapambano dhidi ya Ugonjwa wa UKIMWI, rushwa, dawa za kulevya na pia kuhamasisha na kuamsha ari ya wananchi katika kujitolea kupitia uanzishaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mwaka huu wa 2009, Mwenge wa Uhuru ulianza Mbio zake Jijini Mwanza tarehe 29 Mei 2009 na utafikia kilele chake Mkoani Mara tarehe 14 Oktoba, 2009.

Katika kuamsha ari ya kujitolea miongoni mwa wananchi hususan vijana, shughuli mbalimbali za kujitolea ziliandaliwa ambapo vijana wa Tanzania wakishirikiana na wenzao kutoka nchi mbalimbali Duniani, walishirikiana katika miradi mbalimbali ya kimaendeleo kupitia makambi kazi ya kujitolea ya vijana ambayo yalifanyika katika Mikoa ya Singida na Tabora na wengine nimewaona leo hapa katika *Gallery*.

(d) Kwa kushirikiana na wadau wengine, hususan UNFPA, Wizara imeendelea kuwapatia vijana stadi za maisha ili waweze kuyamudu maisha yao na kuepukana na matumizi ya madawa ya kulevya, pamoja na maambukizi ya VVU/UKIMWI. Mwongozo wa kufundishia Stadi za Maisha kwa vijana walio nje ya shule utakaotumika na wadau na Taasisi zote upo katika hatua ya kuchapishwa.

(e) Wiki ya Taifa ya Vijana iliandaliwa katika viwanja vya Tangamano Mkoani Tanga, ambapo vijana kutoka sehemu mbalimbali Tanzania kupitia Taasisi 94 walishiriki kwa siku nane. Katika maonesho hayo, Vijana walionesha kazi zao mbalimbali za ujasiriamali, huduma kwa jamii na stadi nyinginezo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu juu ya masuala mbalimbali ya kijamii na upimaji wa VVU/UKIMWI, athari za rushwa na dawa za kulevya.

Aidha, vijana wajasiriamali waliweza kutangaza na kuuza bidhaa zao mbalimbali walizotengeneza zikiwemo bidhaa za ufumaji, ushonaji, ususi, ufugaji, ufuaji

chuma, utumiaji wa takataka kuzalisha bidhaa, usindikaji wa vyakula mbalimbali, bidhaa za kilimo, uvuvi na utengenezaji mkaa kwa kutumia nyasi na mabaki mengine ya mashambani.

(f) Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya vijana katika vituo vya vijana vya Sasanda, Ilonga na Kilosa. Mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano yanatolewa katika Kituo cha Vijana Ilonga, mafunzo ya kilimo na ufugaji yanaendeshwa na Kituo cha Vijana cha Sasanda na mafunzo ya ujasiriamali kupitia Kituo cha Vijana cha Marangu.

(g) Mafunzo ya wajasiriamali katika Wilaya tatu za Mkoa wa Dar es Salaam yaliandaliwa na kuendeshwa. Mafunzo haya yalihusisha vijana 150 kutoka vikundi vya vijana wazalishaji mali na vijana wajasiriamali wanaoendesha biashara ndogo ndogo. Aidha, watendaji wa masuala ya vijana na vijana wameshiriki mikutano ya nje ya nchi na matamasha ya vijana kwa lengo la kujenga mahusiano mazuri na kutekeleza kwa pamoja mikakati ya kimataifa inayohusu maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo kuhusu maendeleo ya vijana:-

(a) Kuratibu na kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kufuatilia marejesho ya mikopo ya awali na kuzipatia *SACCOS* zitakazorejesha fedha walizokopeshwa mwaka 2008/2009.

(b) Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa kwa mwaka 2009.

(c) Kuendesha mafunzo kwa vijana wajasiriamali katika vituo vya vijana kwa lengo la kuwapatia ujuzi wa kukuza mitaji na biashara kwa ujumla.

(d) Kuchapisha mwongozo wa kufundishia stadi za maisha kwa vijana nje ya shule na kuwapatia mafunzo Waelimishaji Rika ili wawe na kiwango kizuri cha utaalamu kinachohitajika.

(e) Kuendesha warsha za uhamasishaji wa viongozi na wataalam katika ngazi ya wilaya kuhusu programu ya vijana nje ya shule.

(f) Kuratibu shughuli za kujitolea na Siku ya Kujitolea Duniani.

(g) Kushiriki na kuwawezesha Vijana kushiriki katika mikutano ya kimataifa inayohusu maendeleo ya vijana duniani.

(h) Kuendeleza ushirikiano na taasisi, mashirika ya ndani na nje ya nchi yanayofanya kazi na vijana kama vile Jumuiya ya Madola, *UNDP, UNICEF, UNFPA, ILO, FHI,* Idara za Serikali na Taasisi zisizokuwa za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri iliratibu shughuli za vyama na kushughulikia maombi ya usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Vyama mbalimbali vilifanyiwa kaguzi za kumbukumbu za wanachama na kupewa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/09, shughuli zilizotekelezwa ili kufikia malengo yaliyowekwa ni kama zifuatazo:-

(a) Jumla ya maombi tisa ya usajili wa vyama vipya yalipokelewa. Vyama hivyo ni maombi saba ya Vyama vya Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu *(Tanzania Higher Learning Insitutions Trade Union - THTU),* Kiwanda cha Karatasi Mufindi (Mufindi Paper Employees Trade Union - MPETU), Sekta Binafsi (CHASETA), Migodini *(Mining Workers Union of Tanzania - MTU),* Kiwanda cha Nguo cha NIDA *(NIDA Workers Union - NWU).*

Taasisi za Fedha, Mabenki, Viwanda, Huduma za uchakataji, uchambuzi na useketaji wa mazao ya kilimo *(Finance, Industries, Banking, Utilities, Commerce and Agro Processing Industries – FIBUCA),* Kilimo na Chama cha Wafanyakazi wa Sekta ya Afya Kinondoni (*Kinondoni Health Workers Union - KIHEWU).* Aidha, maombi mawili kutoka vyama vya waajiri ni Muungano wa Waajiri wa Kilimo, Biashara, Viwanda na Madini *(Tanzania Association of Agriculture, Commerce, Industry and Mining Employers - TAACIME)* na Shirikisho la Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi vya Afrika Mashariki *(East Africa Trade Union Confederation - EATUC).* Hawa wote waliomba.

(b) Kati ya maombi hayo, vyama viwili vya wafanyakazi vimesajiliwa ambavyo ni Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu *(Tanzania Higher Learning Institutions Trade Union - THTU)* na Chama cha Wafanyakazi wa Kiwanda cha Karatasi cha Mufindi *(Mufindi Paper Workers Union - MPETU)* na kufanya idadi ya vyama vya wafanyakazi vilivyosajiliwa kufikia 23. Aidha, chama kimoja cha waajiri cha muungano wa waajiri wa kilimo, biashara, viwanda na madini *(Tanzania Association of Agriculture, Commerce, Industry and Mining Employers - TAACIME)* nacho kimesajiliwa na kufanya idadi ya vyama vya waajiri vilivyosajiliwa kufikia viwili.

(c) Shirikisho la Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi vya Afrika Mashariki *(East Africa Trade Union Confederation - EATUC)* limepata usajili hapa nchini kwa makubaliano ya Viongozi wa Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi vya Afrika Mashariki. Mchakato kuhusiana na maombi ya usajili wa vyama vya wafanyakazi vilivyosalia unaendelea kufanyiwa kazi.

(d) Jumla ya Mikoa 11 ilitembelewa na viongozi wote wa vyama walioko katika Mikoa hiyo walishauriwa juu ya umuhimu wa kutunza rejista zao kwa mujibu wa taratibu mpya za sheria. Mikoa iliyohusika katika zoezi hili ni Tanga, Pwani, Dar

es Salaam, Lindi, Mtwara, Tabora, Kilimanjaro, Arusha, Singida, Morogoro na Dodoma.

(e) Jumla ya washiriki 119 wakiwemo waajiri kutoka Serikali za Mitaa walielimishwa juu ya Sheria za Kazi, hususan uhuru wa wafanyakazi wa kuunda ama kujiunga na vyama pamoja na haki za kichama. Mikoa iliyohusika ni Mara, Mwanza, Kagera, Tabora na Kigoma.

(f) Taarifa za wanachama na hesabu zilizokaguliwa zilifuatiliwa kutoka vyama vyote vya waajiri na wafanyakazi. Jumla ya vyama 16 vya wafanyakazi na kimoja cha waajiri wamewasilisha taarifa zao zinazoishia tarehe 31 Desemba, 2008 kwa mujibu wa Sheria.

(g) Vikao elekezi vinne kati ya Ofisi ya Msajili na viongozi mbalimbali wa vyama vilifanyika. Viongozi hao walielekezwa namna ya kufanya kazi kwa pamoja, umuhimu wa kutunza kumbukumbu za wanachama na kuzingatia katiba za vyama. Vyama vilivyohusika ni Chama cha Wafanyakazi, Watafiti na Wanazuoni *(Researchers, Academicians and Allied Workers Union - RAAWU)*, Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu *(Tanzania Higher Learning Institutions Trade Union - THTU)*, Chama cha Wafanyakazi Walinzi wa Makampuni Binafsi *(Tanzania Union of Private Security Employees - TUPSE)* na Chama cha Wanahabari *(Tanzania Union of Journalists - TUJ).*

(h) Wizara kwa kushirikiana na Taasisi na Wakala zilizo chini yake ilishiriki katika Maonesho ya Wiki ya Vijana kwenye kilele cha Mwenge wa Uhuru yaliyofanyika Jijini Tanga, Oktoba 8 hadi 14, 2008, Wiki ya Utumishi wa Umma na Saba Saba kwa lengo la kujitangaza na kuelimisha umma juu ya kazi za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri itatekeleza malengo yafuatayo katika mwaka 2009/10:-

(a) Kushughulikia maombi ya usajili wa vyama.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa sheria za kazi kwenye vyama kwa kufanya kaguzi za kumbukumbu za wanachama.

(c) Kufuatilia hesabu za mwaka za vyama ambazo zimekaguliwa.

(d) Kuwaelimisha viongozi wa vyama juu ya sheria za kazi na kanuni zake.

(e) Kutoa ushauri wa kisheria juu ya taratibu za uanzishwaji wa vyama pamoja na umuhimu wa kujiunga na vyama vilivyopo.

(f) Kushughulikia maombi na kuchukua hatua kwa vyama vinavyokiuka Sheria na kuyawasilisha Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi.

(g) Kufuatilia migogoro inayosababishwa na uanzishwaji wa matawi ya vyama katika sehemu za kazi na kutoa ushauri wa kisheria kwa wahusika.

(h) Kufanya vikao na vyama kwa lengo la kutoa maelekezo na kubainisha kwa pamoja matatizo yanayotokana na utekelezaji wa sheria za kazi na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara ilitekeleza majukumu ya kuajiri watumishi wapya, kuboresha mazingira ya kazi, kupandisha vyeo watumishi na kusimamia maadili na nidhamu mahali pa kazi.

Mheshimishiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara ilitekeleza shughuli zifuatazo:

(a) Kuimarisha mazingira ya kazi katika ofisi za kazi zilizopo Mikoani na Wilayani kwa kuzipatia vitendea kazi kama vile samani za ofisi na kompyuta na kuzifanyia matengenezo.

(b) Ofisi za kazi za Mikoa na Wilaya zilizofanyiwa ukarabati ni Ofisi za Kazi za Kagera, Tabora, Lindi, Muheza, Korogwe, Lushoto, Morogoro na Kituo cha Maendeleo ya Vijana, Ilonga.

(c) Kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ofisi za ulinzi, usafi na matengenezo madogo madogo ya vifaa vya ofisi katika kuboresha utendaji kazi.

(d) Kamati ya Maadili, Nidhamu na Kudhibiti Rushwa katika Utumishi wa Umma ilianzishwa, watumishi 370 wamepata mafunzo ya maadili katika utumishi wa umma, vita dhidi ya rushwa na utawala bora katika Mikoa yote ya Tanzania Bara.

(e) Jumla ya watumishi wapya 38 wameajiriwa, watumishi 59 wamepandishwa vyeo na wengine 26 wamethibitishwa kazini.

(f) Kwa kuzingatia umuhimu wa Michezo sehemu za kazi, Wizara ilishiriki katika Michezo ya Mawizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) iliyofanyika Mkoani Morogoro.

(g) Katika kuendeleza watumishi kielimu, watumishi 14 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 270 ya muda mfupi.

(h) Wizara kwa kushirikiana na Taasisi na Wakala zilizo chini yake ilishiriki katika Maonesho ya Wiki ya Vijana kwenye kilele cha Mwenge wa Uhuru yaliyofanyika Jijini Tanga, Oktoba 8 hadi 14, 2008, Wiki ya Utumishi wa Umma na Saba Saba kwa lengo la kujitangaza na kuelimisha umma juu ya kazi za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itatekeleza malengo yafuatayo yanayohusu maendeleo na ustawi wa watumishi kwa mwaka 2009/10:-

(a) Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi ndani na nje ya nchi.

(b) Kuendelea kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma kwa umma.

(c) Kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za michezo kwa Wafanyakazi wa Wizara.

(d) Kukamilisha kazi ya ukarabati na kuzipatia vitendea kazi ofisi za kazi za Mikoa na Wilaya kwa vituo vya Mtwara, Mbeya, Rukwa, Iringa, Kilombero, Kilosa, Mara, Singida, Moshi na Dodoma.

(e) Kuendelea kutoa mafunzo ya maadili, vita dhidi ya rushwa na utawala bora sehemu za kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Jumla ya kaguzi 3,208 za kawaida na kaguzi maalum 3,620 zilifanyika. Wafanyakazi 2,643 walipimwa afya zao.

(b) Waraka wa mapendekezo ya Sera ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ulikamilishwa na kuwasilishwa katika mamlaka zinazohusika kwa lengo la kuidhinishwa.

(c) Mchakato wa ukarabati wa ofisi ya Mkoa wa Mtwara umeanza na ununuzi wa samani kwa ajili ya Ofisi ya Dodoma unaendelea.

(d) Uhamasishaji wa umuhimu wa usalama na afya sehemu za kazi ulifanywa kwa kutumia vyombo vya habari, hususan katika maadhimisho ya wiki ya Usalama na Afya Duniani ya mwaka huu 2009 yaliyofanyika Jijini Dodoma.

(e) Mafunzo ya masuala ya usalama na afya mahali pa kazi katika vikundi vidogo vidogo vya wajasiriamali kwa sekta mbalimbali yamefanyika katika Mikoa ya Tanga, Morogoro na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2009/10 Wizara kupitia OSHA itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kufanya kaguzi 4,800 za kawaida za afya na usalama sehemu za kazi.

(b) Kufanya kaguzi 5,330 maalumu na za kisheria za usalama na afya mahali pa kazi na kupima afya za wafanyakazi 9,000 katika sehemu mbalimbali za kazi.

(c) Kuimarisha ofisi za kanda ya Kusini iliyoko Mkoani Mtwara na Kati iliyopo mjini Dodoma.

(d) Kununua magari matano kwa ajili ya kurahisisha na kupanua wigo katika zoezi zima la ukaguzi na kusajili sehemu nyingi zaidi za kazi.

(e) Kutoa mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi hususan namna ya kuunda na kuendesha kamati za afya na usalama mahali pa kazi.

(f) Kuendeleza mchakato wa kuanzisha mfumo wa kuripoti na kutoa taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi.

(g) Kuimarisha wafanyabiashara wadogo na wa kati ili waweze kuboresha mazingira ya kazi kwa kuendesha warsha katika Mikoa mitatu ya Tanzania Bara.

(h) Kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

(i) Kuridhia Mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani inayohusiana na usalama na afya mahali pa kazi.

(j) Kuunda Baraza la Kitaifa la Afya na Usalama Mahali pa Kazi.

(k) Kukamilisha Kanuni sita kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

(l) Kuanzisha Tovuti ya OSHA itakayosaidia jamii kuongeza uelewa wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa Kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Watafuta kazi 1,661 waliandikishwa, watafuta kazi 433 waliunganishwa na waajiri na 128 walithibitishwa kuajiriwa. Pia watafuta kazi 256 walipewa mbinu za kutafuta kazi na kujiajiri na jumla ya nafasi za kazi 401 zilisajiliwa.
Aidha, kwa kushirikiana na wakala binafsi uitwao J.O Trust Fund, Wakala uliwaunganisha watafuta kazi 10 na kuajiriwa nchini Saudi Arabia.

(b) Jumla ya watumishi 46 wa wakala wameajiriwa. Aidha, Maafisa wa TaESA walitembelea Wakala mbalimbali zinazotoa huduma za ajira ili kuona jinsi wenzetu walivyojipanga katika kutoa huduma za ajira kwa Watanzania

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2009/10, Wizara kupitia TaESA itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kupanua na kuboresha utoaji huduma za ajira nchini.

(b) Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za ajira nje ya nchi.

(c) Kuweka na kuimarisha mifumo ya huduma za uendeshaji katika kuwezesha utoaji bora wa huduma za ajira nchini.

(d) Kuweka na kuimarisha mifumo ya taarifa na mawasiliano juu ya soko la ajira.

(e) Kuwajengea watumishi uwezo kwa njia ya mafunzo ili kuongeza ufanisi.

(f) Kuweka na kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi.

(g) Kusimamia vyema mapato na matumizi ya fedha za Wakala.

(h) Kuhudhuria mikutano ya kitaifa na kimataifa inayohusu masuala ya huduma za ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), ambalo ni moja ya taasisi zilizo chini ya Wizara yangu, liliendelea na majukumu yake ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango, uwekezaji na kulipa mafao ya aina saba kwa wanachama.

Ili kuboresha mafao ya wanachama, Shirika limeendelea kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali kama vile dhamana za Serikali, mikopo, hisa za makampuni yaliyosajiliwa katika soko la hisa la Dar es Salaam na makampuni yasiyosajiliwa na katika ujenzi wa nyumba na ofisi za kupangisha au kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2008/2009, malengo yafuatayo yametekelezwa:-

(a) Mapato ya shilingi milioni 398,179.3 yalikusanywa, sawa na asilimia 99.15 na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipa mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali na kulipia gharama za uendeshaji.

(b) Ujenzi wa mabweni matano na madarasa katika Chuo Kikuu cha Dodoma yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 5,000 umekamilishwa. Mchakato wa awamu ya pili ya ujenzi wa majengo mengine unaendelea.

(c) Awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba za polisi katika maeneo ya barabara ya Kilwa Dar es Salaam, Ziwani Balacks Unguja na Limbani Kisiwani Pemba, umekamilishwa.

(d) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, umekamilishwa. Vilevile ujenzi wa kituo cha biashara cha wafanyabiashara ndogo ndogo *(Business Park)* katika Manispaa ya Ilala, upo katika hatua ya mwisho.

(e) Ujenzi wa ofisi katika Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Mbozi umekamilika. Aidha, Ujenzi katika Ofisi ya Wilaya ya Njombe upo kwenye hatua ya kumpata mkandarasi.

(f) Ujenzi wa nyumba 300 za bei nafuu katika maeneo ya viwanja vya Kigamboni (Mtoni Kijichi) unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, NSSF inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kukusanya jumla ya shilingi milioni 533,650.3 na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipia mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo.

(b) Kutoa elimu kwa wanachama wake, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii hasa Sheria ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Masuala ya Hifadhi ya Jamii nchini. Shirika pia litafanya upembuzi yakinifu ili kuona uwezekano wa kuangalia upya mahitaji ya wanachama wake kulingana na mahitaji ya hifadhi ya jamii kwa lengo la kuboresha maslahi yao.

(c) Kukamilisha uwekaji kompyuta katika ofisi zake za Mikoa na Wilaya na kuziunganisha katika mtandao wa Shirika.

(d) Kuendelea kuboresha uwekaji wa kumbukumbu mbalimbali za wanachama na kujenga vituo vitatu vya kuweka kumbukumbu hizo katika Mikoa ya Pwani, Ruvuma na Rukwa.

(e) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi katika Mikoa ya Arusha, Kigoma, Manyara, Morogoro na Shinyanga na ujenzi wa ofisi Wilayani Kahama na Njombe.

(f) Kuendelea na miradi ya ujenzi wa Jengo la Ubalozi wa Tanzania Jijini Nairobi, Kenya, nyumba za Polisi, ujenzi wa nyumba za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (TPDF), majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma, sehemu za wafanyabiashara wadogo *(Industrial Parks)* na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Mtoni Kijichi.

(g) Kujenga hoteli ya kisasa Jijini Mwanza, Hospitali ya Apollo Jijini Dar es Salaam, eneo la wafanyabiashara ndogo ndogo Jijini Mwanza, jengo la Shirika la Utangazaji Tanzania, Ofisi za RITA na jengo la Mzizima Jijini Dar es Salaam ambalo litakuwa na huduma za benki, hoteli, maduka, vyumba vya mikutano, sehemu za kuishi na ofisi.

(h) Kushiriki katika mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni ambapo kwa sasa taratibu zinakamilishwa za kumpata mshauri elekezi *(Transaction Advisor)* ambaye atahusika na kazi ya kukamilisha mchakato wa kumpata mbia binafsi, kuhakiki nyaraka za mradi na kuitisha zabuni za kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Taifa la Tija (Nip), lina majukumu ya kuboresha tija na ufanisi kazini katika taasisi za umma, mashirika yasiyo ya kiserikali na makampuni binafsi kwa kutoa huduma za mafunzo, ushauri, uelekezi na utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2008/2009 Shirika lilitekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kushiriki katika mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni ambapo kwa sasa taratibu zinakamilishwa za kumpata mshauri elekezi *(Transaction Advisor)* ambaye atahusika na kazi ya kukamilisha mchakato wa kumpata mbia binafsi, kuhakiki nyaraka za mradi na kuitisha zabuni za kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa daraja.Jumla ya mafunzo 80 yamefanyika sawa na asilimia 100, ambapo washiriki 1,200 kati ya 1300 walihudhuria. Hii ni sawa na asilimia 92.30 ya lengo.

(b) Huduma za uelekezi 35 zilitolewa kwa wateja mbalimbali kutoka taasisi za umma, mashirika ya umma na binafsi. Hii ni sawa na asilimia 87.50 ya lengo lililopangwa.

(c) Utafiti mmoja ulikamilika kati ya sita uliopangwa.

(d) Jumla ya shilingi 11,370,000 zimelipwa kwa Shirika kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi zikiwa ni malipo ya fidia ya mwisho ya Kiwanja Namba 906/H kilichomilikishwa kwa Chuo cha Tiba na Afya cha IMTU.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2009/10 Shirika litatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendesha mafunzo 80 ya uongozi kwa watumishi 1,300 kutoka taasisi za umma na binafsi.

(b) Kutoa huduma za ushauri kwa wateja 40 katika sekta za umma na binafsi.

(c) Kufanya tafiti nane katika maeneo yanayolenga kuboresha tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ni moja kati ya Taasisi zilizoundwa kutekeleza Sheria mpya za Kazi na inafanya kazi katika Kanda 11. Jukumu kubwa la Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(Commission for Mediation and Arbitration)* ni kusuluhisha na kufanya uamuzi wa migogoro sehemu za kazi. Aidha, upande ambao hautaridhika na maamuzi ya Tume, unaweza kupeleka shauri hilo katika Mahakama ya Kazi ambayo kwa Sheria za sasa ni kitengo chini ya Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/09 Wizara yangu kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Migogoro 6,489 ilipokelewa. Kati ya hiyo migogoro 5,212 ambayo ni sawa na asilimia 87 ilisuluhishwa na kumalizika. Migogoro 1,277 inaendelea kusuluhishwa.

(b) Migogoro 770 iliyoshindikana kusuluhishwa ilishughulikiwa katika ngazi ya uamuzi ambapo migogoro 570 ilitolewa uamuzi na migogoro 200 inaendelea katika hatua mbalimbali za uamuzi.

(c) Mabaraza ya Wafanyakazi 15 yalisimamiwa kuundwa. Semina 10 za mafunzo kuhusu sheria za kazi za mwaka 2004 zimetolewa na mikataba mitano ya uundaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi imeidhinishwa. Ilitoa ushauri kuhusu masuala ya ushirikishwaji wa wafanyakazi katika Taasisi sita. Aidha, Tume imeratibu ufasiri wa Kanuni za Sheria Mpya za Kazi za mwaka 2007 kwa Lugha ya Kiswahili kwa kushirikiana na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) ambazo uzinduzi wake ulifanyika tarehe 21 Januari, 2009.

(d) Mikataba mitano ya Chuo cha Elimu ya Biashara Tawi la Dodoma, Wakala wa Maabara na Mkemia Mkuu wa Serikali (*GCLA*), Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (*TCAA*) na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (*PPRA*) ilisajiliwa.

(e) Mafunzo ya kujenga uelewa wa Sheria za Kazi za mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2007 yaliandaliwa na kutolewa katika kanda tano.

(f) Watumishi wapya 32 wameajiriwa katika nyanja mbalimbali ili kuboresha utendaji wa Tume.

(g) Kuhudhuria mikutano ya kitaifa na kimataifa inayohusu utekelezaji wa sheria za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/10, Tume itafanya yafuatayo:-

(a) Kupokea na kusajili migogoro mipya ya Kikazi na kuandaa taarifa za migogoro hiyo.

(b) Kuendesha mafunzo ya uelewa kwa Waajiri na Wafanyakazi juu ya matumizi ya Sheria za Kazi.

(c) Kujenga uwezo wa Tume kwa kutembelea nchi zinazoendesha shughuli za utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi kwa malengo ya kujifunza.

(d) Kupeleka migogoro iliyoamuliwa na Tume kwenye Mahakama ya Kazi kwa ajili ya utekelezaji, mapitio na uamuzi.

(e) Kuandaa taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya elimu na ushirikishwaji wa wafanyakazi na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika ikiwa pamoja na Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma.

(f) Kushughulikia maslahi ya watumishi wa Tume, upandishwaji vyeo kwa watumishi, kuwaendeleza kitaaluma na kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

(g) Kuandaa na kuratibu vikao vya Kamati ya Huduma Muhimu *(Essential Services Committee).*

(h) Kukamilisha na kuzindua Mkataba wa Huduma kwa Wateja *(Client Service Charter)* na kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za michezo kwa wafanyakazi wa Tume.

(i) Kuratibu ufasiri wa Sheria Na. 6 ya mwaka 2004 ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria Na. 7 ya Taasisi ya kazi kwa kushirikiana na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu yote niliyoyaeleza, yametekelezwa kwa ushirikiano na mshikamano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Napenda nitumie nafasi hii, kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, pamoja na Masharika na Taasisi zake, kwa juhudi zao kubwa walizoonesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga (Mbunge), Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa msaada na ushauri wake wa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Hajjat Kijakazi Rajabu Mtengwa na Naibu Katibu Mkuu, Bibi Edine Mangesho, pia kwa Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara, pamoja na Bodi zao ambao wameshirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu tuliyopangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wetu wote, ambao kwa namna mbalimbali wemetuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kwa njia ya pekee, naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Ushauri wa Masuala ya Kazi, Uchumi na Jamii *(Labour, Economic and Social Council - LESCO),* Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. Naishukuru pia *TACAIDS* kwa misaada mbalimbali kwa Wizara na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo tumeshirikiana nazo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya wahisani, ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu yake. Kwa uchache, naomba shukrani za dhati ziende kwa Serikali ya nchi na Mashirika ya Kimataifa ya *Denmark, World Bank, ILO, UNDP, UNICEF, UNFPA* na *CYP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue fursa hii, kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo langu la Urambo Magharibi, kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipatia ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa. Wao ni sehemu kubwa ya ufanisi katika utendaji wangu wa kazi. Naomba nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, kwa jinsi anavyoendesha Baraza letu kwa uadilifu na uaminifu mkubwa, nawapongeza vijana wa under 17 wa Mkoa wa Tabora kwa kuingia fainali kwa kuifunga Morogoro jana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2009/2010, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 16,967,382,000 kwa Fungu 65. Kati ya fedha hizo Shilingi 9,044,591,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo Shilingi 1,937,025,800 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Shilingi 7,107,565,200 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kiasi cha Shilingi 7,922,791,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambapo Shilingi 1,978,845,000 ni fedha za hapa nchini na Shilingi 5,943,946,000/= ni fedha za nje.

Vile vile naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe kiasi cha Shilingi 3,163,657,000 chini ya Fungu 15 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, ambapo shilingi 739,157,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 1,300,000,000 ni kwa matumizi mengineyo. Aidha, kiasi cha Shilingi 1,124,500,000 ni fedha za nje kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi, namshukuru Spika na Wenyeviti wa Bunge letu, kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii au mwakilishi wake, Mheshimiwa Ameir anaendelea. Ahsante karibu.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 na Kanuni ya 114(7), nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge (2007), majukumu ya Kamati hii ni pamoja na kufikiria na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Kazi,

Ajira na Maendeleo ya Vijana. Tarehe 01 Juni, 2009, Mjini Dar es Salaam, Kamati ilikutana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Katika kikao hicho, Kamati ilipata maelekezo ya Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kuhusu utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009, Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka wa fedha 2008/2009 na Malengo yaliyomo katika Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika**,** Kamati katika kufikiria taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2008/2009 na bajeti ya mwaka 2009/2010, ilizingatia miongozo muhimu ya Wizara ikiwa ni pamoja na dira, dhima, majukumu na melengo ya Wizara. Katika kikao hicho, Kamati iliweza kuhoji kuhusu utekelezaji katika sekta mbalimbali za Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Vilevile ilihoji kuhusu Bajeti ya mwaka 2009/2010, malengo yaliyowekwa na Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, katika mwaka wa fedha uliopita wa 2008/2009, Kamati yangu ilitoa maoni na maagizo katika maeneo mbalimbali na hasa yanayohusu:-

(i) Mkakati wa Serikali wa kuibua Ajira Mpya milioni moja ifikapo mwaka 2010.

(ii) Umuhimu wa fedha za uwezeshaji kupelekwa moja kwa moja kwenye SACCOS na Asasi za kifedha.

(iii) Wizara kuwa na utaratibu wa kufuatilia matumizi na urejeshwaji wa fedha hizo ili ziweze kukopeshwa kwa wajasiriamali wengine na hivyo kukuza ajira na kuondoa umaskini.

(iv) Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha kuwa fedha hizo zinawafikia walengwa. Aidha, Wizara iweke utaratibu wa kufuatilia katika mabenki kujua kama fedha hizo zimekopeshwa kwa walengwa.

(v) Ili kuleta mafanikio katika kukuza ajira ni lazima wafanyabiashara ndogo ndogo (Wamachinga) wapewe mafunzo ya ujasiriamali.

(vi) Kuendeleza zoezi la kutambua vijiwe vya vijana na kuwawezesha kiuchumi kwa kuwasaidia fursa mbalimbali ili kupunguza watu wasio na kazi.

(vii) Wakati umefika kwa Serikali kukamilisha mkataba wa mpango wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni, kwa udhamini wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

(viii) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) uangalie uwezekano wa kujenga majengo ya wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) katika Majiji ya Mwanza na Arusha kama linalojengwa Manispaa ya Ilala Jijini Dar es Salaam.

(ix) Serikali ichunguze utaratibu uliotumika kumilikisha kiwanja 906/H kutoka Shirika la Tija ya Taifa (NIP) kwenda Chuo cha IMTU, kuna malalamiko toka Taasisi ya Umma-NIP kuwa haikutendewa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa ufafanuzi uliotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa kiasi kikubwa Serikali imefanyia kazi baadhi ya ushauri na maelekezo ya Kamati na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika itaendelea kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya shilingi 12.7 bilioni. Waziri aliifahamisha Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2008/2009. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na mafanikio yake ni kama ifuatavyo:-

(i) Ili kuondoa matatizo katika kupanga viwango vya mishahara, Bodi za Mishahara zilizinduliwa rasmi katika Sekta nane tarehe 18 Aprili, 2007 zimeanza kufanya kazi. Bodi hizo ni Bodi ya Sekta ya Kilimo, Madini, Afya, Viwanda na Biashara, Ulinzi katika Makampuni Binafsi, Huduma za Usafiri na Mawasiliano, Huduma za Usafiri Majini na Huduma za Wafanyakazi wa Majumbani na hotelini. Bodi hizo zimeanza kutekeleza majukumu yake.

(ii) Kukamilisha ukarabati wa Ofisi ya Kazi Jijini Dar es Salaam na Mwanza.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau na jamii imefanikiwa kupambana na ajira mbaya ya watoto na baadhi ya watoto kuingizwa katika mfumo wa elimu ya msingi na elimu ya ufundi (VETA).

(iv) Wizara imefanya kaguzi za kazi 893 katika Sekta Binafsi.

(v) Kituo cha Ajira cha Dar es Salaam kiliimarishwa ili kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri.

(vi) Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Huduma na Kukuza Ajira imeandaliwa na inachambuliwa na wataalam kwa lengo la kupitishwa katika vyombo vya maamuzi Serikalini.

(vii) Wizara iliendelea kuratibu ukamilishaji wa marejeo ya Sheria ya Kazi Awamu ya Pili, Sheria ya Hifadhi ya Jamii na Sheria ya Ajira ambazo zimepitishwa na Baraza la Mawaziri. Kuhusu Sheria za *Occupational Health and Safety Act, Workman's Compensation and National Employment* Service Act, Kamati ilijulishwa kuwa zipo kwenye hatua za kukamilishwa.

(viii) Serikali inaendelea kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007.

(ix) Kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na idadi ya watu (UNFPA), Wizara imeandaa mwongozo wa Stadi za Maisha ambao utatumika kufundishia vijana na wadau wanaojishughulisha na utoaji wa elimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio, changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka 2008/2009 ni pamoja na:-

(i) Namna ya kuhakikisha kuwa huduma za Hifadhi ya Jamii zinazingatia Sera na Sheria ya Hifadhi ya Jamii na njia bora ya kuwafikia walengwa katika ngazi zote hadi vijijini.

(ii) Kukabiliana na tatizo la UKIMWI sehemu za kazi ili kupunguza/kuokoa kupotea kwa nguvu kazi ya Taifa.

(iii) Uwezo mdogo wa kuwafikia vijana wote mijini na vijijini kwa lengo la kuwahamasisha, kuwaelimisha na kuwajengea uwezo wa kujiajiri.

(iv) Kuhakikisha kuwa mikopo ya wajasiriamali inawafikia walengwa kwa wakati hasa vijijini.

(v) Upatikanaji wa takwimu sahihi za ajira mpya zinazozalishwa kote nchini hasa katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kwamba, utaratibu wa kutoa mikopo kwa vijana kwa kutumia SACCOS za Vijana zilizoanzishwa kila Wilaya, ambao kila SACCOS imetengewa shilingi milioni tano kwa ajili ya kukopesha, kiasi hicho ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana wamehamasishwa na kuitikia kujiunga na SACCOS hizo, fedha zaidi zinahitajika ili kukidhi mahitaji haya. Kamati inaishauri serikali iandae Waraka maalum utakaoboresha utekelezaji wa suala hili, ikiwa ni pamoja na kuongeza fedha na kuzipeleka moja kwa moja katika SACCOS za vijana zinazoandikishwa rasmi. Hatua hii itarahisisha ufuatiliaji wa matumizi na marejesho ya fedha hizo na kuleta manufaa kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Serikali iliyo madarakani inatamka kwamba, Serikali itaongeza ajira milioni moja ifikapo mwaka 2010; na kwa kuwa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa kushirikiana na Wadau, ilitayarisha Programu ya Kukuza Ajira (*National Employment Creation Programme*), ambayo inatekelezwa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali; Kamati inaishauri Wizara kupitia kitengo chake cha Habari, kuifahamisha jamii kuhusu idadi ya ajira ambazo zimekwisha patikana na mchakato mzima uwe wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika Kamati hairidhishwi na usimamizi wa Serikali kupitia Wizara hii katika kulinda ajira kwa kazi zinazoweza kufanywa na Watanzania lakini zinafanywa na wageni toka nje ya nchi. Mfano hai ni kuwepo kwa wageni toka nchi za Mashariki ya Mbali wakifanya biashara ndogondogo za maduka *(Retail Shops*) na machinga katika miji yetu. Vivyo hivyo kuna wafanyakazi wenye asili ya nchi za Pembe ya Afrika katika hoteli wakitoa huduma za kawaida ambazo zinaweza kufanywa kwa ufanisi na vijana wazalendo wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaomba Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hasa Idara ya Uhamiaji na Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (*National Investiment Center),* kuhakikisha kwamba, ajira za Watanzania zinalindwa vilivyo. Kwa msingi huo, vibali vya wageni kufanya kazi nchini visitolewe kiholela na pia Serikali katika ujumla wake, ishirikiane na kituo cha Uwekezaji nchini kufuatilia shughuli za wawekezaji toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara hii ndiyo yenye dhamana ya kutoa vibali kwa wafanyabiashara wa ndani na nje, Kamati hairidhishwi na wafanyabiashara ndogo ndogo wa kigeni waliotapakaa nchini hivi sasa hususan Jijini Dar es Salaam, ambao wameharibu soko la bidhaa za Taifa letu kwa kuingiza bidhaa ambazo baadhi yake zimethibika kuwa bandia na za thamani ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati inapenda kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kuwa katika kipindi cha mwezi Mei na Juni 2009, aliunda Kamati Maalum ya Wataalamu ya kufanya utafiti wa maeneo ambako kuna raia wengi kutoka China na Korea. Uchunguzi huo ulitokana na hoja kwamba, kuna Wachina wanaofanya kazi za kimachinga Dar es Salaam na hivyo kuwanyima Watanzania nafasi za kazi. Matokeo ya utafiti huo uliofanywa Jijini Dar es Salaam yalibaini kwamba:-

(a) Makampuni yamekuwa yakitumia watu wa katikati (Madalali/Vishoka) kupata vibali/leseni na nyaraka mbalimbali kutoka Serikalini, jambo ambalo linapotosha taarifa sahihi kutoka pande hizo mbili (Serikali na Makampuni).

(b) Wataalam wageni wanaopata vibali vya kazi nchini huwaweka jamaa zao kama tegemezi (*Dependants*) kwenye vibali hivyo lakini baadae wanajiingiza kwenye ajira kinyume na taratibu za sheria.

(c) Baadhi ya Wataalamu wageni hawana vyeti vya taaluma husika ingawa wakati wa kuomba vibali hivyo waliwasilisha vivuli vya vyeti hivyo.

(d) Baadhi ya makampuni yanaghushi vibali/leseni za biashara na nyaraka nyingine za serikali.

(e) Wapo Wachina na Wakorea wenye uraia wa Tanzania na wanaona uhalali wao wa kufanya hizo biashara.

(f) Wageni wengi walioko maeneo ya Kariakoo ni wawekezaji waliopitia Kituo cha Uwekezaji *(Tanzania Investment Centre)*, hivyo wapo nchini kihalali kwa kuwa wamefuata taratibu zote halali za kuwafanya wawe kwenye maeneo yale.

(g) Makampuni mengi yenye wataalamu wageni yanafanya biashara tofauti na aina ya biashara iliyoidhinishwa kwenye leseni hizo.

Kimsingi, Kamati inashauri mambo yafuatayo yachukuliwe hatua ili kukabiliana na tatizo hili: Wananchi waelimishwe zaidi kuhusu maamuzi mbalimbali yanayotolewa kuhusiana na wageni wafanyakazi; Serikali iweke msisitizo katika kuainisha aina ya shughuli ambazo zinaweza kufanywa na wageni; Serikali iweke utaratibu wa kufanya kaguzi za mara kwa mara ili kubaini matatizo sehemu za kazi; na adhabu zitolewe kwa wahusika kama watabainika kufanya makosa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazidi kuiomba serikali ifanye haya yafuatayo:-

(a) Ianishe uaandaji wa sheria ya ajira ambayo itaweka bayana taratibu bora zaidi za kupendekeza utoaji vibali vya kazi kwa wageni.

(b) Ibainishe aina za kazi zinazoweza kufanywa na wageni na kuzitangaza.

(c) Iweke bayana majukumu ya wadau mbalimbali katika kushughulikia utoaji wa vibali vya wageni kwa lengo la kupunguza urasimu.

(d) Iainishe aina ya adhabu kwa watakaokiuka taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wakala wa Huduma Za Ajira Tanzania (*TAESA*) ya kusaidia wahitimu mbalimbali wa vyuo katika suala la kupata ajira, Kamati imesikitishwa na hali mbaya ya jengo la Ofisi za TAESA ambalo limechakaa na linavuja. Jengo hili halijakarabatiwa kwa muda mrefu sasa na hivyo kuathiri utendaji na ufanisi wa kazi kwa kiwango kikubwa. Kamati inaishauri serikali kutenga fungu maalum kwa ajili ya kuisaidia *TAESA* katika mambo yafuatayo:-

(i) Kukarabati jengo la ofisi ambalo linavuja na kupunguza ufanisi wa kazi, ikiwa ni pamoja vitendea kazi vilivyopo vikiwa chakavu kwa kutofanyiwa matengenezo kwa muda mrefu.

(ii) Kukagua mfumo wa umeme wa ofisi ili kuuboresha na kuondoa hitilafu za mara kwa mara na kuharibu baadhi ya vitendea kazi kama vile kompyuta.

(iii) Kuwapangia vituo vya kazi watumishi wapya (walioajiriwa) katika Ofisi za Kanda za Arusha, Mbeya, Dodoma na Mwanza na kuwalipa stahiki zao kama vile posho (*Subsistance Allowance)* na nauli ambazo zinatolewa kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ni Taasisi yenye jukumu la kutatua migogoro ya kazi ya waajiri na wafanyakazi chini ya Sheria ya

Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya Mwaka 2006. Kwa sasa Tume hii inafanya kazi katika mazingira magumu yasiyoridhisha kutokana na mambo yafuatayo:-

(a) Upungufu wa watumishi, Tume inatakiwa kuwa na uwakilishi katika Wilaya zote Tanzania Bara. Ufinyu wa bajeti unaifanya Tume kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa.

(b) Uhaba wa majengo ya ofisi za kuendeshea shughuli za Tume ni mkubwa. Tatizo hili litazidi pindi Tume itakapoajiri watumishi wapya katika mwaka mpya wa fedha wa 2009/2010.

(c) Uhaba wa vitendea kazi vinginevyo kama vile kompyuta, samani na vyombo vya usafiri ni tatizo kubwa. Tume mpaka sasa ina gari moja tu katika kutekeleza shughuli zake nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri serikali kuiongezea fedha Tume hii ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi, ikizingatiwa kuwa Elimu ya Sheria mpya za kazi inahitajika kuenezwa kwa lengo la kuzuia migogoro isiyo ya lazima. Uzoefu unaonesha kuwa, elimu ikitolewa migogoro ya kazi ambayo si ya msingi huwa haitokei.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajasiriamali wadogo nchini wanajitahidi katika nyanja za ubunifu na hili linajidhihirisha wazi kwa kuwa mwaka 2008 wajasiriamali wadogo 203 wa sekta isiyo rasmi, walishiriki Maonesho ya Nguvu Mali na Jua Kali yaliyofanyika Kigali nchini Rwanda. Katika Maonesho hayo, nchi yetu ilikuwa mshindi wa kwanza wa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Wajasiriamali wanapokuwa kwenye Maonesho ya Kimataifa kama haya, hupata tenda za biashara kutokana na ubora wa bidhaa zao, lakini wakati mwingine hushindwa kufikia malengo ya biashara kutokana na urasimu wa vibali vya ubora toka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA).

Kwa kuwa urasimu huu unawanyima wajasiriamali wetu fursa ya kufanya biashara nje na badala yake tunaishia kulaumu kuwa nchi jirani zinatuzidi kibiashara, Kamati inashauri Serikali kuhimiza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), kutoa nyaraka za ubora wa bidhaa katika muda muafaka ili kuwatia moyo wajasiriamali hawa wanaojituma kwa lengo la kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/09, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi *(The Workers Compensation Act, 2008).* Sheria hii iliyotungwa kwa lengo la kukidhi mahitaji ya jamii ya sasa, hususan wafanyakazi kufuatia malalamiko yao ya muda mrefu kuhusu upungufu uliomo katika sura 263 ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi. Sheria hii imetungwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Sheria hii inakusudiwa kutoa mwongozo, kanuni na muundo bora katika kushughulikia madai ya fidia ya wafanyakazi wanaoumia wakiwa kazini au kuugua magonjwa yatokanayo na kazi. Kamati inaishauri serikali kuiongezea Wizara kiasi cha shilingi 1,000,000,000 kilichoombwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010, lakini haikutengewa fedha hizo. Wizara ikiongezewa kiasi hicho itaweza kukamilisha kazi zifuatazo:-

Kukamilisha maandalizi ya Kanuni za Sheria ya Fidia ya Mwaka 2008; kuweka viwango vya michango ya waajiri; kusajili waajiri watakaochangia katika Mfuko wa Fidia; kuunda Bodi ya Utatu kwa ajili ya kusimamia na kuunda mfuko; kununua vitendea kazi kwa ajili ya ofisi za mfuko; kugharamia uchapishaji, usambazaji wa sheria na utoaji wa elimu kwa umma; na kugharimia uendeshaji wa mfuko ikiwa ni pamoja na kulipia pango la ofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na makadirio ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010. Jumla ya shilingi 16,967,382,000 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 65 na kiasi cha shilingi 3,163,657,000 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, naomba kukushukuru wewe binafsi, kwanza kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu na pia kumshukuru Naibu Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge.

Aidha, nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma Kapuya, (MB), Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, (MB) na Wataalam wa Wizara, wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Kijakazi Mtengwa, kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2008/09 na Bajeti ya Mwaka 2009/10. Kamati inawashukuru na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Haroub Said Masoud (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati; nawashukuru sana. Ninapenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii kwa majina:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama - Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub S. Masoud - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma O. Ally, Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Zuleikha Y. Haji, Mheshimiwa Salim A. Khalfan, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa

Dkt. Gertrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila na Mheshimiwa Mohamed A. Said.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Ofisi yake, kwa kuiwezesha Kamati yangu kufanya kazi ya kuchambua na kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Bajeti.

Aidha, napenda kuwashukuru Ndugu Elieka Saanya, Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Brown Mwangoka kwa kuratibu kazi za Kamati hadi maoni kutoka kwa wakati unaotakiwa. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza**.**

Mheshimiwa Naibu Spika**,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ameir umeisoma vizuri hotuba yako. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii.

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFANI (MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa majaliwa yake ya uzima kwetu sote. Naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha maoni juu ya Hotuba ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99 (7), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa DKT. Slaa, kwa ushauri wao na busara kwangu tokea mwanzoni mwa kipindi hiki cha mkutano wa bajeti hadi sasa ninapowasilisha Hotuba hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile natoa shukrani kwa wananchi na wanachama wote wa Jimbo langu la Tumbe, bila kusahau Viongozi wa Chama Changu cha Wananchi – CUF (Chama Kikuu Upinzani Tanzania), kwa imani waliyonayo kwangu, nami natoa ahadi kuwa nitaendelea kushirikiana nao kwa dhati katika kuhakikisha mambo yanaenda kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, natoa shukrani na pongezi kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa kazi kubwa ya kuliongoza vyema Bunge hili. Aidha, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa matayarisho mazuri ya bajeti iliyowasilishwa hapa Bungeni asubuhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za kazi na haki za wafanyakazi. Baada ya kuona kuwa sheria za kazi za zamani hazikidhi mahitaji ya soko la ajira kwa sasa, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria mpya za kazi, Namba 6 na 7 za mwaka 2004. Kuwa na mfumo wa sheria za kazi na usuluhishi wa migogoro ya kazi ni sehemu muhimu sana katika soko la ajira, ulinzi wa haki za wafanyakazi na kuongeza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa sheria ziko wazi lakini kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria hizi na waajiri, pale waajiriwa wanapodhalilishwa na kwenda katika baraza la usuluhishi na hata kufika kwa Mheshimiwa Waziri. Waziri anatoa uamuzi wake na pengine mahakama inatoa maamuzi yake dhidi ya waajiri, lakini bado uamuzi huo unashindwa kutekelezwa na waajiri hao. Kambi ya Upinzani kwa hili tunauliza Serikali kuwa wahusika wanaokataa kwa makusudi kutekeleza maamuzi halali ya vyombo vyote vinavyotoa maamuzi ni hatua gani zinachukuliwa dhidi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakala wa usalama na afya mahali pa kazi (OSHA) ni taasisi ngeni sana kwa Watanzania walio wengi. Kutofahamika vyema kwa wakala huu, kunasababisha wafanyakazi katika sekta za umma na zile za binafsi waendelee kutopata haki zao kadhaa za kisheria. Si rahisi mtu kudai usichokijua zaidi na zaidi, hasa miongoni mwa wafanyakazi na waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado makali ya OSHA hayajaonekana kikamilifu. Wapo waajiri wengi wanaopuuza matakwa ya kisheria kuhusiana na afya na usalama mahali pa kazi. Wafanyakazi katika sehemu nyingi za kazi zenye hatari na athari za kiafya, hawapatiwi zana bora za kujikinga kwa mfano, kofia, miwani za kupunguza ukali wa miali katika kazi za kuunganisha vyuma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, OSHA ni lazima iwabane na hata kuwashtaki panapohusika, waajiri na hata waajiriwa wazembe katika kuzingatia afya na usalama wa jumla kazini. OSHA ni chombo chenye jukumu la kusimamia utekelezaji (*enforcement*) wa sheria husika na ni lazima ipewe uwezo na yenyewe iwe na meno.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano mema mahali pa kazi baina ya waajiri, waajiriwa, vyama vya wafanyakazi na chama cha waajiri, pamoja na Serikali ni jambo ambalo kwa njia moja ama nyingine ni kigezo muhimu katika kuinua utendaji na kukuza pato la Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa migogoro na migongano baina ya wafanyakazi na waajiri ni suala ambalo linaileteа na kuitia hasara nchi yetu. Aidha, mbali na sheria zilizopo, mahusiano mahali pa kazi yanavurugika pale kundi moja linapoonekana kuneemeka kupitia mgongo wa kundi lingine linalozalisha. Kwa maana halisi, kundi kubwa kunyimwa au kupunjwa haki zake kwa visingizio vya aina yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasia ya kweli katika nchi yoyote ile duniani, inaanzia kwa wafanyakazi kuwa na vyama vyao vilivyokuwa huru na vinavyoweza kudai

maslahi yao ya msingi. Hivyo, mwendelezo huo wa uhuru wa vyama vya wafanyakazi huleta demokrasia ya kweli kwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia mwafaka wa kiasi gani mwajiri anatakiwa kumlipa mwajiriwa, majadiliano baina ya chama cha wafanyakazi na mwajiri wa sehemu husika ni muhimu sana. Hivyo basi, migogoro inayotokea baina ya Chama cha Walimu, Wauguzi, Wafanyakazi wa Bandari, Reli na Serikali ni matokeo ya kukosekana kwa uwazi unaostahili toka kwa Serikali kuhusiana na stahiki zao halali. Aidha, mbali na suala la maslahi, mahusiano yanakuwa mabaya sana kutokana na mazingira mabovu wanayofanyia kazi, ambayo pia yanaweza kusababisha kupungua kwa tija au kuwa hatarishi kwa wafanyakazi. Jambo hili husababisha mgogoro vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wafanyakazi ni kundi ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kulipa kodi ili kufanikisha mipango na kuendeleza nchi yetu. Kwa bahati mbaya, kundi la wafanyakazi ndilo limekuwa haliheshimiki na kuthaminiwa toka hata kabla hatujapata uhuru wetu. Kambi ya Upinzani imejaribu kuorodhesha baadhi ya matatizo ya wafanyakazi toka kabla ya uhuru hadi hivi leo, nayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kipindi cha kati ya miaka ya 1950-1960:
Kulipwa mishahara duni; ajira za kulazimishwa (forced labour) kama vile manamba kwenye mashamba ya mikonge na chai; kufukuzwa kazi kiholela bila malipo; mazigira duni ya kazi; na kuzuiwa kujiunga na vyama vya kazi na siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha miaka ya kati 1961 -1964: Mazingira ya kazi yaliendelea kuwa magumu; mishahara iliendelea kuwa duni; na baadhi ya watumishi wa serikali hawakuruhusiwa kujiunga na vyama vya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kipindi cha miaka ya kati 1964 -1977: mazingira ya kazi duni; mishahara isiyokidhi mahitaji muhimu ya maisha; Wafanyakazi kutokuwa na uhuru wa kujiunga ama kuanzisha Vyama vya Wafanyakazi wanavyovipenda; kukosa uwakilishi wa Wafanyakazi; kukosekana kwa demokrasia ya kweli ndani ya Vyama vya Wafanyakazi; kukiukwa kwa haki za msingi za Wafanyakazi za kujiunga na vyama na kuchagua viongozi wao; baadhi ya wafanyakazi kufukuzwa kazi kwa uonevu; baadhi ya ajira kutolewa kwa upendeleo bila sifa, jambo lililochangia kufa kwa baadhi ya Mashirika ya Umma na ukosefu wa kazi; na baadhi ya Wafanyakazi kunyimwa haki ya kusoma na kujiendeleza nchi za nje kwa sababu za kisiasa kwa sababu hawakuwa wanachama wa chama tawala.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kipindi cha miaka ya 1978 -1990: Mishahara duni; kupunguzwa kazini; kutokuwepo kwa uhuru na haki za wafanyakazi kuunda ama kujiunga na chama chochote cha wafanyakazi; kutokushirikishwa katika mipango na sera za uchumi na maendeleo ya nchi; kutokuwepo kwa uwakilishi wa kweli wa Wafanyakazi katika vyombo vya maamuzi; na Waajiri wageni wa sekta binafsi kuanza kuwapuuza Wafanyakazi kwa kutoheshimu sheria za kazi, kuzuia kuanzishwa kwa vyama vya Wafanyakazi sehemu zao za kazi, kuajiri vibarua zaidi, kulipa mishahara duni na kufukuzwa kazi ovyo ovyo.

Katika kipindi cha miaka ya 1990 hadi 2000 hali ilikuwa kama ifuatavyo: Mishahara duni kwa wafanyakazi; kutotekelezwa kikamilifu uhuru na haki za binadamu zikiwemo haki za Wafanyakazi kuunda ama kujiunga na chama chochote cha Wafanyakazi; kutokushirikishwa kikamilifu katika mipango na sera za uchumi na maendeleo ya nchi; uwakilishi mdogo wa Wafanyakazi katika vyombo vya maamuzi; kuwepo kwa ajira za uonevu hususan katika maeneo ya uchumi huria (EPZ) na ongezeko la ajira za vibarua zenye malipo duni; na kuongezeka kwa ajira za watoto katika mashamba ya chai, mikonge, kahawa na miwa, migodi na kazi za ndani.

Katika kipindi cha miaka 2000 – 2005 kumeshuhudiwa mazingira duni ya kazi; mishahara duni; uhuru usio makini wa Wafanyakazi; uhuru mdogo; ukiukwaji wa haki za Wafanyakazi za kuunda ama kujiunga na chama chochote cha Wafanyakazi katika baadhi ya sehemu za kazi; kutokushirikishwa kikamilifu katika mipango na sera za uchumi na maendeleo ya nchi; uwakilishi duni wa wafanyakazi katika vyombo vya maamuzi; upunguzwaji wafanyakazi katika zoezi la ubinafsishaji; kuongezeka kwa ajira za vibarua; na ukiukwaji wa Sheria za kazi na kufukuzwa kazi ovyo ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo hayo yote ambayo yameendelea kuwakumba wafanyakazi inaonesha kuwa, yamekuwa yakijirudia na mengine mapya kujitokeza kila kukicha na mbaya zaidi wale waliopewa dhamana ya kuangalia kundi hili la wafanyakazi, ndio hao hao wanawazidishia matatizo na mahali pengine hata viongozi wao wa vyama vya Wafanyakazi hasa mahali pa kazi, kuwageuka waliowachagua na kusimama upande wa waajiri. Watendaji wa Serikali nao kwa upande mwingine walionekana dhahiri kushindwa kusimamia vyema sheria na sera zilizopo, jambo ambalo miaka yote kimekuwa ni kilio kikubwa kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sas, hakuna sera ya pamoja inayotawala maendeleo ya rasilimali watu kwa sekta zote. Hata hivyo, zipo sera za hapa na pale katika sekta mbalimbali zinazohusu maendeleo ya rasilimali watu. Kambi ya Upinzani inaona kuwa huu ni upungufu mkubwa katika kadhia nzima ya mipango na maendeleo ya ajira hapa nchini. Kukosekana kwa sera hii ya pamoja nayo imepunguza sana nguvu ya Wafanyakazi *(power to negotiate* na umetumika mtindo wa *divide and rule).* Hivyo basi, ilani inayosema kuwa kwa kipindi cha miaka mitano itatoa ajira milioni moja bila kuwepo na sera inayotawala rasilimali watu, inaibua maswali mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mara tunaambiwa kuwa, zaidi ya asilimia 76.5 ya watu wetu kwa mujibu wa taarifa ya maendeleo ya Hali ya Umasikini ya Mwaka 2007 *(PHDR),* wameajiriwa katika kilimo. Ukweli kutokana na utafiti uliofanywa na *Tanzania Rural Investment Climate Survey (RICS),* unaonesha kuwa kati ya asilimia 40 - 45 ya asilimia 76.5, wanajihusisha na shughuli zisizokuwa za kilimo, yaani *non-farm wage and self-employment activities.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali kama kweli inataka kuleta mabadiliko ya kiuchumi katika nchi hii ni lazima kuachana na sera zisizokuwa na tija, badala yake ijikite katika kuweka sera ambazo zitasaidia kuwezesha

sekta hii inayojihusisha na shughuli zisizo za kilimo zitakazohamasisha kilimo ili kuleta maendeleo kwa taifa. Wenzetu wa Nchi za Mashariki ya Mbali, wamepiga hatua za haraka kutokana na kuimarisha shughuli zisizo za kilimo na kilimo katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa uamuzi uliofanywa wa kujenga *Machinga Complex* haukuangalia mustakabali mzima wa maendeleo ya nchi yetu, bali ulifanywa kwa lengo la kufurahisha kundi fulani tu au ulikuwa ni wa kisiasa mno. Hivi ni kweli kuna kijana atakayekaa kijijini na kuanzisha shughuli zake za kijasiriamali zisizokuwa za kilimo na aache kuja mjini kwenye majengo ya *Machinga Complex.* Hata hivyo, watakaopata nafasi ndani ya jengo hilo ni wachache sana, kiasi cha kuwa punje ya mchanga baharini. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inashauri mazingira yanayowekwa mijini kwa gharama kubwa, yawekezwe vijijini ili kiwe kivutio kwa vijana kubakia huko huko badala ya kukimbilia mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** nguvukazi katika Tanzania inakua kwa asilimia tatu kwa mwaka. Mwaka 1999 ilikisiwa kuwa imefikia 16,006,178. Zaidi ya nusu wako kwenye kundi la umri wa miaka 10 - 19 na asilimia kama 80 hivi wanaishi Vijijini. Karibu asilimia 8.5 ya nguvukazi ina zaidi ya elimu ya msingi au mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvukazi iliyo na elimu ni ndogo na iko zaidi mijini. Kwa ujumla inakadiriwa nguvukazi mpya 800,000 huingia kwenye soko kila mwaka, kwa mujibu wa Taarifa ya Maendeleo ya Hali ya Umasikini ya Mwaka 2007 (PHDR), wengi wa nguvukazi hiyo wakiwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizo na ile ilani inayosema kuwa itatoa ajira 1,000,000 kwa kipindi cha miaka mitano, ukilinganisha na takwimu za Taarifa ya Hali ya Maendeleo ya Umasikini, maana yake ni kwamba, kipindi cha miaka mitano kutakuwa na watu wasiokuwa na kazi 4,000,000. Ukitoa ajira 1,000,000 za ahadi tunabakiwa na watu 3,000,000 wasiokuwa na ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anaweza kutusaida kwa hili; ni lini hasa Sera ya Taifa ya Rasilimali Watu itakuwa tayari kwa mipango ya maendeleo ya sekta zote, tofauti na ilivyo sasa ambapo kila sekta inakuwa na mipango yake kulingana na utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu huu wa sera moja ya maendeleo ya rasilimali watu, inapelekea kupishana kwa matarajio ya ajira kati ya sekta na sekta. Jambo ambalo linatoa takwimu tofauti za kitaifa kuhusiana na ajira na uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyowahi kutahadharisha katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha uliopita, Serikali iliyopo madarakani, inaonekana kupalilia na kuupigia debe umachinga, miongoni mwa vijana wetu ambao wapo zaidi ya milioni 12 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kukuza ajira kwa vijana kupitia ujenzi wa kile kinachoitwa masoko ya kisasa ya wamachinga ni kuwadumaza na kuwadanganya vijana na pia kujidanganya kama Taifa. Umachinga si baraka bali ni dalili ya tatizo kubwa la kiuchumi na kijamii linalofukuta ndani ya Taifa letu. Taifa hili haiwezekani liwekeze matumaini yake kwa kazi ya uchuuzi na ulanguzi wa bidhaa za kigeni miongoni mwa vijana wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wetu wanatakiwa wasaidiwe na wawezeshwe kufanya kazi zenye mwelekeo wa uzalishaji wa bidhaa na hata huduma. Tutafute tatizo sahihi linalowafanya vijana wetu washinde vijiweni na kwenye makempu, kupiga soga siku nzima badala ya kujishughulisha na uzalishaji mali na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Watanzania tunawaandaa vijana wetu kujitegemea ndani ya dunia iliyo katika karne ya 21 kupitia ukuzaji wa shughuli za umachinga, Serikali ya Rwanda kwa taarifa sahihi, inaendesha zoezi la kutoa kompyuta ya kupakata *laptop* kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi na ambapo sisi tunahangaika na kumaliza tatizo la madawati mashuleni bila mafanikio endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanatakiwa waandaliwe mazingira ya kushiriki kwa ufanisi katika uzalishaji mali tangu wakiwa katika shule za awali. Aina ya elimu na mafunzo ya vijana wetu mashuleni na vyuoni ni kati ya mambo yanayoamua vijana hao hatima yao, wawe wazalishaji au wachuuzi tu wa bidhaa za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuzitaka shule zetu na vyuo kutoa elimu ya kiuzalishaji kwa vijana wetu, pia taasisi za JKT na JKU zijikite katika kuwaandaa vijana kwenye mwelekeo wa mafunzo ya kiufundi na kiuzalishaji mali na kamwe taasisi hizo zisigeuke kuwa kama Magereza na vyuo vya mafunzo ya itikadi na propaganda kwa faida ya chama fulani cha siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limejijengea umaarufu mkubwa sana katika jamii na huo ni ukweli ulio wazi kabisa. Pamoja na umaarufu huo, kuna mambo mengi sana ambayo sisi Kambi ya Upinzani tunaona ni udhaifu mkubwa na pengine umaarufu uliojengwa ulikuwa na lengo la makusudi ili kufanikisha udhaifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika ukaguzi wake kwenye Shirika hili, iligundua mambo mengi na matumizi ya ovyo ovyo ya fedha za wanachama. NSSF ilikopesha jumla ya shilingi 1,525,368,525 kwa kampuni ya M/S Medtech toka Aprili, 2003 na mkopo ulitakiwa kurejeshwa Disemba, 2004, hadi sasa pesa za wanachama hazijarudishwa. Aidha, Taarifa hiyo inaonesha kuwa, hakuna gawiwo lililowahi kutolewa na makampuni hayo. Kwa ujumla Ripoti imebaini kuwa, NSSF imekuwa inawekeza sehemu zisizo na tija kwa wanachama. Taarifa inasema kuwa NSSF ni miongoni mwa taasisi zenye masurufu ambayo hayajerejeshwa ya jumla ya shilingi 22,231,219.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizowekezwa na NSSF kwenye mabano ni Tanzania Oxygen Ltd (shilingi 13,200,000), Tanzania Housing Bank (shilingi 495,280,000), First Adili Bank Corp Ltd ilipewa mkopo wenye utata wa shilingi 3,152,024,742. Kampuni nyingine ambazo NSSF imewekeza bila kupata gawio kwa kipindi chote ni CDC Mbeya Cement (shilingi 1,152,024,742), Ubungo Plaza (shilingi 9,817,038,702), TANRE Share (shilingi 1,000,000,000), HEPZ (Quality Group Share) shilingi 47,156,025,113 na PPL Pension Properties (shilingi 3,500,000). Jumla ya uwekezaji usio na tija ni shilingi 62,789,093,299.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ilisema kuwa mifano hiyo ni michache, inayoashiria udhaifu mkubwa katika upangaji wa miradi na uwekezaji wa NSSF na kwamba inapaswa suala hilo kuchukuliwa kwa uzito maalumu ili kunusuru fedha za wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inadhani wakati umefika sasa mfumo wa kuwashirikisha wanachama wenyewe katika maamuzi ya namna ya kuwekeza fedha zao ubuniwe, kwani fedha hizi si za Serikali na wala NSSF au mifuko mbalimbali ya Wafanyakazi kama vile PPF, GPF, LAPF si vyombo vya fedha. Haiwezi kuingia akilini wafanyakazi watoe jasho lao, waweke fedha hizo kama akiba zao na hatimaye ziwekezwe na mamlaka ambayo wao hawaidhibiti kwenye biashara ambayo wao kama wadau wakubwa wala hawapati taarifa zake na wala haijulikani wanafaidika nazo vipi hasa. Shirika kama PPF limekuwa kwa muda mrefu hata halipeleki taarifa zake kwa wanachama wake kama vile wafanyakazi wa hoteli mbalimbali Ngorongoro na au wafanyakazi wa TANAPA (Ngorongoro), pamoja na kuahidiwa mara kadhaa na Katibu Mkuu wa Hazina. Huku ni kuwahujumu wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mbali na matatizo hayo ya udhibiti wa fedha za wanachama, NSSF imetamkwa kuwa ni miongoni mwa taasisi zenye utunzaji mbovu wa kumbukumbu za wafanyakazi, ambapo mikataba ya ajira, nakala za vyeti, barua za ajira, taarifa za kupandishwa vyeo, uhamisho na ongezeko la mishahara wakati wa ukaguzi havikuwepo. Aidha, NSSF ni miongoni mwa taasisi za serikali ambazo hazizingatii sheria ya ajira ambapo wakati wa ukaguzi iligundulika kuwepo kwa uvunjwaji wa sheria za ajira kwa kutoa ajira bila kufuata taratibu zilizowekwa. Hii ni pale inapoajiri watu bila kuwa na sifa wala uzoefu, bila kutangaza nafasi za ajira, pia kulikuwa na wafanyakazi walioajiriwa wakiwa na umri mkubwa kuliko kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la NSSF ambalo fedha zake zinatokana na fedha zinazowekezwa na Wafanyakazi, wanachama wa mfuko huo kwa ajili ya mafao yao, lilitoa Mkopo wa US $ 7,000,000 (Tshs Billioni 8.4 ) kwa Kampuni ya Makaa ya Mawe na Nguvu za Umeme – Kiwira, wakati wafanyakazi wenye kustahili mafao yao wanahangaika na kusagika soli kufuatilia mafao yao; fedha zao hizo wala hazijulikani kama zitarudi kwa kutokuwepo ushahidi wowote wa dhamana iliyowekwa iwapo mkopaji atashindwa kurejesha *(Collateral)* fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkopo huu ulitarajiwa kulipwa baada ya miezi sita lakini hadi tarehe 26 Machi, 2009 ulikuwa haujalipwa. Isitoshe, Mkataba huo, katika

kifungu cha 10.5 unasema kuwa, mkopo huo umedhaminiwa na Serikali kwa asilimia 100 pamoja na Benki ya *CRDB.* Hii inashangaza kwani fedha zenyewe ni za Wafanyakazi wa Tanzania na Serikali yao inadhamini kwa asilimia 100 ili wakopaji wakishindwa, Serikali yaani Wananchi wa Tanzania wakiwemo Wanachama wa NSSF, watalipa deni hilo kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani baada ya kuipitia taarifa hiyo kwa makini, inaonesha shirika lina udhaifu mkubwa wa kiutawala; hivyo Kambi inaitaka Serikali kuhakikisha inachukua hatua za haraka za kiutawala ili kuhakikisha shirika hili linaendeshwa kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Tija la Taifa (NIP); napenda kutoa changamoto kwa serikali kuhuisha suala zima la tija katika harakati za uzalishaji mali na huduma. Matumizi ya nguvukazi ya taifa na hasa wataalamu wachache waliopo, kwa mfano madaktari, wahandisi, marubani, watafiti wanasayansi na kadhalika ni lazima yazingatie misingi ya tija *(productivity).*

Mheshimiwa Naibu Spika, adui mkubwa wa tija ni pamoja na kuua motisha na morali ya kazi miongoni mwa wafanyakazi na matumizi yasiyo sahihi ya wataalamu *(misallocation of human resources).* Kwa mfano, si jambo linalohimiza tija kumlazimisha mtu au yeye kulazimika kuwa mwalimu pasipo na wito wowote katika kazi hiyo. Haileti tija watu kufanya kazi fulani ili wagange njaa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** NIP iishauri na kuisaidia Serikali ipasavyo ili gharama za kuzifanya kazi mbalimbali zilete busara ya kiuchumi na matokeo yanayoshabihiana na gharama (kwa maana ya rasilimali fedha, watu, muda, vitu na kadhalika). Kuzingatia kiumakini kabisa misingi ya tija, kunapunguza sana uwezekano wa kufanya kazi bila kufikia matokeo tarajiwa. Ni lazima kazi zetu mbalimbali tuzifanye kwa faida na si kwa mazoea tu. Haya yote yatawezekana endapo shirika litawezeshwa katika kutekeleza majukumu na mipango yake iliyojipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nilipokuwa Kigali, walikuwa wanasema huwa wanafuatilia sana mwenendo wa Bunge letu hili na wanaona *live* na wakasema watu wengine wanazungumza kwa haraka mpaka huwa hatuelewi wanasema nini. Ni kweli Waheshimiwa; ni afadhali uzungumze kwa taratibu ukasikika kuliko kwa haraka sana usisikike kila kitu. Kwa sababu tunazungumzia ulimwengu, tunauelezea ulimwengu. Kwa hiyo, mimi nashauri Hansard inatokea, lakini hii ya kwenda kama mashine ya kusaga basi inakuwa hata maneno hayasikiki. Sidhani kama ni nzuri sana. Afadhali useme kidogo kinachosikika kuliko vingi visivyosikika. *(Makofi)*

Sasa hivi tunalo tatizo la muda hasa wakati wa Kamati ya Matumizi; kwa hiyo, inawezekana tukawa na Wabunge wengi wanataka kuzungumza wakati wa Mshahara wa Waziri na wakawa wengi kuliko muda tunaopewa kufuatana na Kanuni ya 104(2);

kwamba ikifika dakika 10 kabla ya zile dakika 30 tunazoongeza basi tunasoma vifungu tu juu kwa juu. Sasa inawezekana Waheshimiwa Wabunge wengine hawafikiwi, isionekane kwamba Kiti kinapendelea. Sisi tunapoandika hapa, hatujui nani alichangia wakati wa mjadala au nani. Tuna-*catch the eye of the Speaker*. Tunafuata orodha, tutakapokatia ni hapo hapo. Kwa hiyo, kuna wengine wanafikiria kwamba, labda Wenyeviti wanakuwa na matatizo kwamba wanatazama labda wangempa yule mtu ambaye hakuchangia huku. Humkumbuki nani alichangia. Kwa hiyo naomba tuwe tunavumiliana kwa hili.

Kesi kama ya jana, ukiingia kile kipindi cha *guillotine* maana yake tunaamua sasa wote tunaacha, tunapitisha mafungu. Asitokee Mbunge mwingine kuhusu Mwongozo, kwa sababu pale hakuna kitu, tumeshafunga. Ilitokea jana wakati wa *guillotine*, Mheshimiwa Ole-Sendeka akataka mwongozo kuhusu jambo fulani. Pale huna nafasi, tukiingia kwenye *guillotine* tumesimamisha kazi tunapitia tu mafungu. Sasa unaangalia masuala mengine, kwa mfano, aliyoizungumza Mheshimiwa Ole-Sendeka jana angeweza kuileta kwa namna nyingine kwa sababu ilikuwa ni kubwa zaidi kuliko kile Kikao kilichokuweko pale. Lilikuwa ni suala kubwa na lilitakiwa maelezo mengi zaidi. Kwa hiyo, angeweza kuileta kama maelezo binafsi kwa mujibu wa Kanuni; wakati wa kuahirisha Bunge anaweza akajieleza jana sikuridhika kuhusu jambo fulani unampa *time*. Unaposema kuhusu Mwongozo, jambo lenyewe kubwa kabisa, mwongozo ni vile vidogo vya kuendeshana humu ndani, kama hatuendi sawa sawa. Kwa hiyo, nilipenda hili tulizingatie, baada ya *guillotine* hatuhitaji mwongozo wala utaratibu; tunatakiwa kumaliza kazi kwa sababu tunakuwa hatuna muda mwingine na kwamba, tunapokuwa kwenye mshahara wa Waziri mkiwa wengi muda ukaisha, inabidi tuishie tunapoishia. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba tuzingatie hayo.

Tunaendelea, leo tumekula muda wa Wizara hii kwa sababu tulikuwa na ile Kauli ya Mawaziri. Tunaye mchangiaji ambaye hajachangia hata mara moja; Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, atakuwa wa kwanza. Tutaingia waliochangia angalau mara mbili, kwa muda tulionao atakuja Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Dkt. Sigonda, Mheshimiwa Mushi na Mheshimiwa Masilingi wanaweza kufikiwa. Mheshimiwa Rita Mlaki.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mungu kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge hili Tukufu kwa siku hii ya leo, kuchangia hoja muhimu ambayo inawagusa Watanzania wengi; hoja ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja hii. Vile vile nawashukuru sana Wananchi wa Jimbo langu la Kawe kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kufanikisha kazi walizonituma Bungeni, kwa kuchangia maendeleo ya wananchi hasa shule, barabara, vituo vya polisi na vituo vya afya. Ninaomba nilete shukrani maalum kabisa kutoka kwa Wananchi wa Mbezi Beach, ambao tumewajengea barabara na wamefurahi sana wanasema wanashukuru lakini wanaomba tujenge na nyingine kwa mfano huo huo. Vile vile Wananchi wa Kunduchi wanashukuru kwa maji, ambayo sasa kwa muda mrefu walikuwa hawapati, sasa wanapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutazidi kuomba na mimi nawaahidi wananchi wangu wa Kawe kwamba, nitakuwa nao bega kwa bega kuhakikisha kwamba, yaliyobaki kwa kipindi kifupi yanafanikiwa. Nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi, mwalimu wangu Profesa Kapuya, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Mheshimiwa Kapuya, amebobea katika Wizara hii kwa muda mrefu na amefanya mambo mengi akisaidiwa na Watendaji wake, Katibu Mkuu na wengine. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja katika hoja hii. Nitajikita sana katika Sekta au eneo la ajira kwa vijana. Mwaka wa 1996, 1997 na 1998, iliyokuwa Tume ya Jiji la Dar es Salaam ikiongozwa na Mheshimiwa Keenja wakati huo, ilitoa *statistics* zinazoeleza vijana wasio na kazi katika Jiji la Dar es Salaam. Walisema vijana laki sita hawana ajira. Hapo hapo ilikisiwa kwa wakati huo Dar es Salaam kulikuwa kuna watu milioni tatu japo sensa ilipokuja mwanzo wa miaka ya 2000 ilisema ni milioni tatu, lakini Dar es Salaam kama mnavyojua watu wanakuja wanatoka, kwani ndiyo Jiji Kuu ambalo lina biashara za kila aina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni miaka 10 tangu tulipopata hiyo sensa ya kwamba ni vijana 600,000 hawana ajira. Miaka 10 imepita, wakati huo ilikuwa moja ya tatu ya wakazi wa Dar es Salaam, wengi wao wakiwa vijana walikuwa hawana kazi. Sasa inakadiriwa kwamba, Dar es Salaam wakazi wa kudumu ni milioni nne na laki tano. Tukifanya kwa karibu kabisa, kuna wale wanaokuja wanakaa kipindi fulani wanaondoka, tunaweza kukuta ni zaidi. Tuchukulie milioni nne na laki tano. Hapo hapo kwa mahesabu ya haraka haraka, tukichukulia moja ya tatu ya hawa tunakuta milioni moja na laki tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi hapa wanakaa kwenye majimbo yao lakini wanapita Dar es Salaam na mtakuwa mmeona hili suala la vijana wengi Dar es Salaam ambao hawana kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukichukulia Wilaya ya Kinondoni katika Mkoa wa Dar es Salaam, kila wakati ina watu wengi kuliko Wilaya ya Ilala na Wilaya ya Temeke. Kwa maana hiyo basi, hata wale vijana wengi pia wako Wilaya ya Kinondoni. Jimbo la Kinondoni na Jimbo la Kawe, kwa maana hiyo basi jimbo langu la Kawe vile vile lina vijana wengi sana ambao hawana ajira. Nilikuwa nimeandika hapa, lakini kwa sababu hizi *data* sina hakika nazo, siyo vizuri kuzitaja lakini ni kwa malaki; nikichukulia watu milioni moja na laki tano hawana ajira, nikichukulia nusu laki saba ina maana kwangu karibu laki tatu hawana ajira. Hii ni *population* kubwa sana, unaweza ukalinganisha na nchi nyingine ndogo katika Bara la Afrika. Vijana wengi wanaomaliza darasa la saba, wengine wanamaliza kidato cha nne, wengine wanatoka Mikoani kuhamia Dar es Salaam kutafuta kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa wanaishi maisha ya tabu sana. Wanakaa vijiweni kuanzia asubuhi mpaka jioni, wengine wakisubiri kupata *taxi* za kuendesha,

wengine wakisubiri kuwa wapiga debe katika madaladala, wengine wanaomba, wanashinda siku nzima bila kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwa ni tatizo kubwa sana. Tunawaonea huruma sana kwa sababu wanajiingiza wengine katika vitendo viovu bila kupenda. Wanafanya mambo mabaya, wengine wanalewa, wengine wanafanya udokozi usio wa lazima na jamii kwa ujumla inaathirika sana na matatizo kama haya. Vijana wangu hawa wamenituma na wameniomba sana; mimi naishi Mikocheni, pale Mikocheni ni katikati ya Jimbo, tukirudi Mjini napita Msasani, nikitoka pale Mikocheni nakwenda Kawe, Kunduchi, Mbweni na Bunju.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema ukweli vijana au mkipita tunaomba mtazame katika hayo maeneo, utaona kwa mfano ukipita Kawe hapa mjini, kuna eneo linaitwa Mzimuni Ukwamani, Kwa Ndobe, ukifika mpaka Tangi Bovu, utaona vijana wengi sana hawana neno wanapiga kelele wanaimba, wanacheza hawana hata mahali pa kucheza, wananiita kwa nguvu sana, nikienda maeneo yangu ya kazi mimi siku hizi huwa nafanya shughuli zangu binafsi Kunduchi. Nikipita pale lazima nipite katikati ya hawa vijana mpaka Tegeta Mjini, Mtongani, Salasala pale Njia Panda Afrikana, nadhani mnaona pale kuna bajaji, teksi, baiskeli na vijana wengine wanakuwa matrafiki wanapitisha magari huku na kule Wazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanabaki kuita Mama Rita., tunakufa njaa. Inatia huruma Mwenyekiti. Niseme ukweli kama mama, maana wengi ni watoto wetu. Kata za Mbweni na Bunju ni Kata za mashambani ambako wangeweza kulima, lakini wanaolima hawana pa kupeleka mazao yao. Vile vile hakuna biashara nyingi, kwa hiyo, wanashinda na wazazi; mnapofanya mikutano wanasema tusaidieni vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningewaomba sana tulifikirie hili suala kwa uzito mkubwa sana. Kwanza, naomba kusema vijana hawa wako tayari kufanya kazi yoyote siyo kwamba ni wavivu. Kuna siku moja nilikuwa ninapita, wakaniomba nikawaambia twendeni nikawape kazi; nikawachukua kwenye gari, nikawanunulia mapanga nikawapeleka kufyeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, walifyeka sana na walifurahi. Ndipo nikahakikisha kwamba, wapo tayari kufanya kazi na hawachagui kazi. Manispaa ya Kinondoni imejitahidi sana. Nikiwa kama Mbunge na Diwani, tumetenga maeneo kadhaa. Tumejenga masoko kwa mfano pale Kawe, Msasani, tumetoa mikopo lakini bado tuna matatizo hayo. Vijana wangu wamenituma wanaomba msaada. Mawazo ambayo ningependa kutoa kwa haraka sana, Wizara ya Kazi yenyewe imejitahidi, waliweka malengo ya watu milioni moja lakini tumepata ajira milioni moja na zaidi. Wasaidiwe na Wizara nyingine, kwa mfano, Wizara zote ziwe na kipengele katika bajeti zao au katika mpango maalum kama ule mpango wa UKIMWI waseme sisi tutachangia ajira kwa kiwango fulani. Kwa mfano, Viwanda na Biashara wanaweza wakatazama wakahamasisha viwanda ambavyo ni *labour intensive*, ambao wanaweza wakaajiri mpaka vijana 3,000. Wizara ya Kilimo kuna maeneo mengi sana ya kulima

wakawachukua hawa vijana na kuwepo mkakati wa Serikali wa kupata fedha ili vijana waweze kulima.

Wizara ya Ulinzi na JKT tuwapeleke hawa vijana kule kambini, watakuwa tayari kufanya kazi kwa bidii sana. Tuwape mafunzo kule VETA, wanashindwa kujilipia, kuna *levy* inapatikana kwa kila leseni. Ile *levy* inakwenda VETA iwasaidie vijana hawa waweze kusomeshwa bila kulipa. Wanaofuzu waandikishwe, kuna Kitengo amekiongelea pale Mheshimiwa Waziri ambapo wanaandikisha watu kwa ajili ya ajira waweze kusaidiwa. Mwekezaji anayekuja anajaza fomu anasema nitaajiri watu kiasi kadhaa, atazamwe ili waweze kusaidia kuajiri hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano India, wana Wizara ya SME hii inasaidia mafunzo, mitaji, masoko na vijana wengi sana wanaajiriwa na nchi inaendelea. La mwisho, ningependa kuongelea mazingira ya wafanyakazi. Naomba Serikali ilisimamie hili ili kulinda afya za hawa wafanyakazi. Kuna madawa mbalimbali, viwanda kama *chemicals, ledy acide hydrokcides* na mavumbi ambayo yanapatikana katika viwanda, watu angalau wavalishwe *mask* ili wanapovuta hewa zisije zikawaumiza, wavalishwe na *gloves* na Wizara au Serikali icheki na kuhakikisha kwamba, watu hawa wanapewa vifaa vinavyofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mashine za moto. Nakumbuka tulipoanzisha Kiwanda cha AGOA, Waamerika walikuja kukagua, wakasema lazima tufanye *insulation* j kuhakikisha kwamba, joto lile la kwenye mashine haliwezi kuathiri wananchi. Hebu hawa wenye viwanda watazame wafanye kitu kama hicho. Kuna sakafu nyingine unakuta zinateleza, angalau kuwe na tahadhari tuangalie hii Idara, nina hakika wana kitengo cha namna hiyo inaweza ikasimamia. Kwa sababu akiumia mfanyakazi hatujui kama analipwa au inakuwa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda unaisha. Ninaomba kusema au kurudia kwamba, suala hili la vijana na ajira Serikali nzima ilichukulie kwa makini na wamsaidie Waziri wa Kazi hizo Wizara nyingine ziko nyingi, ambazo zinafanya uchumi kuna Wizara ambazo zinazalisha, kuna Wizara za *service,* kuna Wizara ya Ulinzi na JKT, wanaweza wakasaidia sana. Huu mkakati uwe mkakati maalum, ambao unawezeshwa ama huu mkakati ambao unaweza ukasaidia kama ambavyo tumeweka mkakati wa UKIMWI na tunaona mafanikio makubwa sana, tunauita *awareness* ya Watanzania kujikinga na UKIMWI imekuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumalizia kwa kusema kwamba, vijana wa Jimbo la Kawe watakuwa tayari kufanya kazi yoyote kama watasaidiwa na ninaomba Serikali itusaidie pia katika taasisi za fedha kuhakikisha haya mabenki yanakubali kutoa mikopo. Tukishawafundisha hawa vijana, tukishawapeleka katika sekta mbalimbali za kazi, angalau wengine wajiajiri na wanaweza wakajiajiri tu kama watapata msaada wa fedha. Kwa hiyo, kama kuna hizi benki zilizoanzishwa, nakumbuka Shirika la Viwanda walipewa bilioni tano za kuanzia na …

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. RITA L. MLAKI:** Baada ya kusema hayo, naunga mkono ho Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlaki ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa DKT.Guido Sigonda pia ajiandae. Mheshimiwa Dora Mushi atafikiwa na Mheshimiwa Wilson Masilingi atafikiwa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Kwanza, niwapongeze Mawazi, kaka zangu, kwa kazi nzuri wanayofanya. Kabla sijaanza kuchangia, nilitaka tu nisome kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2008.

Ukienda pale ukurasa wa 98, tunaambiwa kuna utafiti umefanyika ambao unaonesha kwamba, kutakuwepo na upungufu wa kazi katika nchi yetu *almost* watu milioni mbili na laki tatu. Nimeamua nianze hili kwa kusema kwamba, Wizara hii ni muhimu sana na umuhimu wake *employment* duniani ndio siasa ya leo. Ukienda kwenye nchi za wenzetu walioendelea, vyama vinashindwa uchaguzi kwa sababu ya kazi, kwa hiyo, unaweza ukaona umuhimu mkubwa kwa Wizara hii. Kwa hiyo ni lazima na sisi tuanze kujipanga ili kuona kwamba na sisi suala la kazi tunalipa msukumo unaostahili. Ukiangalia leo duniani kuna mtikisiko mkubwa sana wa uchumi, lakini angalia *rescue package* zote za nchi kubwa zilizoendelea, unakuta kazi yao *number one* ni namna ya kuokoa kazi, kuokoa ajira. Ninayasema haya ili tuone umuhimu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nilitaka nianze kidogo na historia ya nchi yetu. Suala la kazi ni muhimu sana, lakini kazi hizi zinatoka wapi? Huko nyuma Viongozi wa Taifa hili waliamua kwa makusudi, wakaanzisha viwanda vikubwa, wakaanzisha biashara kubwa kubwa. Viko viwanda na makampuni makubwa ya Serikali, lakini sababu ya kuanzisha viwanda hivyo, pamoja na kuwa kwa ajili ya uchumi, ilikuwa ni pamoja na kutoa kazi. Tunafahamu Reli, Bandari, ATC, National Milling, RTC, Transport Company, viwanda vya nguo, vya sigara vya bia, kulitokea nini; viwanda hivyo tumeviuwa wenyewe? Kwa hiyo, maana yake sisi wenyewe huwa tunafanya juhudi ya kupunguza kazi za Watanzania wetu. Tumeshuhudia walikuwa hawatoi gawio serikalini, lakini humu ndani hatukulalamika sana; kisha baadaye na mageuzi ya dunia kukaja na mawazo ambayo mimi ninasema yalikuwa ni muhimu sana kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo haya ni kuleta wabia, kufanya *privatization* na kuleta *new investiments.* Ukisikia sasa Watanzania ambao leo tupo tunalalamika kweli, tumeanza kusema nchi imeuzwa. Sasa nimekuwa ninajiuliza kila siku, kwa sisi tunaokwenda Kanisani; hivi watu wameokoka lini wakati nchi hii inakufa, makampuni yetu hayaleti faida, watu wetu wanafukuzwa kazi kila siku, hatukusikia mtu analalamika; lakini leo tumeanza kufanya juhudi za kutaka kazi iwepo, kodi ziongezeke, uchumi ukue, huku lugha za kusema tunauza nchi? Jamani hatueleweki duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niwaambieni leo na nitatoa baadhi ya *statistics* chache tu. Dunia ya leo na duniani kote, nchi kubwa na nchi ambazo hazijaendelea kama za kwetu, wanashindana kupata *investiments,* maana yake ni nini? Waweze watu wao kupata kazi, waweze kupata kodi, waweze kukuza uchumi wao; sisi tunataka kucheza mchezo hapa wa kudhani tunaweza kufanya mambo ambayo yalitushinda miaka ile. Naombeni sana tuwasaidie hawa watu; kutatua matatizo sio kufukuza watu, tuwa-*engage* hawa watu tuongee nao. Mimi nitataja mifano michache, huko nyuma tulikuwa na kampuni moja ya simu *TTCL.* Historia yake inajulikana, tulikofika wenyewe tunajua, lakini tumeifikisha kwa mikono yetu wenyewe. Baada ya mageuzi makubwa kwenye hii *industry* ya *communication* leo *industry* hii peke yake imeajiri watu 10,000 na tukienda zaidi wataajiri watu wengi, hapo sijataja kodi wanazolipa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndio maendeleo; ni lazima watu hawa wanaofanya kazi hii tuwaenzi; haiwezekani watu hawa tuwaambie kila siku ndio wanatuharibia. Leo hii karibia nchi nzima inaunganishwa na mtandao. Utasikia kila mtu kwangu kijiji changu hakijapata mtandao ni kwa sababu ya mageuzi haya yaliyofanyika. Haya ndio maendeleo. Tuna kiwanda cha bia, leo kimeajiri Watanzania 1,400, hao wana *direct employment.* Ukienda wale wanaouza bia. Ukienda kwa wale *transporters,* maana yake hiyo 1400 unaizidisha karibia mara tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008, kiwanda cha bia peke yake, kimechangia kwenye uchumi bilioni 200 kwenye kodi. Wamefungua kiwanda cha Arusha, Mwanza na sasa wanafungua Mbeya. Jukumu tulilonalo kama Serikali na Waziri wa Kazi, hawa watu ni lazima tuwaoneshe na sisi tunajali mchango wao, ni lazima tuwe tayari kufanya maamuzi. Moja ya matatizo tunayoya-*face* ni kwenye kufanya maamuzi, *investors* hawatuelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuangalia Sekta ya Mabenki. Tulikuwa na benki moja ya *NBC* hapa, ilikuwa inafanya hasara; tukafanya maamuzi benki yetu tukafungua na milango, leo Tanzania tuna mabenki 38 na yote yanafanya faida. Ukitusikia hapa tunasema tumeuza nchi, nchi ipi tumeiuza? Wanaoajiriwa kwenye mabenki haya ni watoto wa nchi hii na ukiangalia sasa mchango kwa nchi hii na kwenye mabenki haya kwenye uchumi; leo hii wameajiri karibu watu 20,000, Serikali yetu yote kwa ujumla wake, imeajiri watu 3,000. Leo kuna watu wanalalamika hapa na mimi ninasema Waziri ni lazima u-*take lead,* kulinda wafanyakazi.

**NAIBU SPIKA:** Una uhakika na hizo *figure?*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio ninao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri taarifa. Naomba ukae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba afute hiyo kauli kwa sababu Serikali kwa maana ya watumishi wa umma, wako zaidi ya 300,000 sio 3,000. Mwaka jana tulitoa

vibali vya kuajiri, mwaka huu tumetoa vibali vya ajira mpya 45,000 na hata mwaka jana tumeajiri zaidi ya watu 30,000.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na maana ya 300,000 naona nimepunguza sifuri moja.

**NAIBU SPIKA:** Hata mimi nadhani ulikuwa una maana hiyo hiyo. Ahsante endelea.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kwenye hiki kitabu nilichonacho hapa, ambacho ni cha Serikali, orodha hii inasema ni 300,000.

**NAIBU SPIKA:** 3,000 saa nyingine inasomeka kama 300,000 hivi.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, ninaeleza haya ili tuone umuhimu wa hii Wizara. Nimeongea habari ya mabenki, ukienda kazi ambayo inafanyika Kilombero Sugar, kwenye Industry ya Mining na kwenye Tourism, pamoja na matatizo yaliyopo, ajira iliyopatikana huko ni nyingi sana.

Ninayasema haya ili sasa mwelekeo wetu katika kuangalia mambo yetu haya, hasa katika hii sekta ya *investment*, isiwe ni mwelekeo wenye *negativity*, wenye kudhani watu hawa nia yao ni mbaya tu. Mimi ninaamini wanao mchango mkubwa sana kwenye maendeleo yetu. Ukiangalia hata humu ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri, kuna mambo makubwa inasema *NSSF* itafanya, lakini *NSSF* hizo *pension* zinatoka wapi? Kwenye haya mashirika ya kawaida, kwa sababu ukiangalia mfumo wetu wa *pension* sio watu wote wanategemea wafanyakazi wa Serikali, maana *Pension Fund* ziko karibia tatu au nne; kuna wengine wako *Local Government*, kuna wengine wako kwenye mashirika yale ya serikali, wengine wako Serikali Kuu. Watu wa *NSSF* wanategemea kama uchumi huu utakua, kuwe kuna *investment*, watu wengi waajiriwe, ndio shirika letu hili litafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema, nataka tukubaliane, ukienda leo kuongea na *investors* kinachoonekana ni kwamba, kuna *indecision*, hatuoni mchango wao. Kwa hiyo ni muhimu sana kwa sababu *investment* maana yake ni kazi. Kwa hiyo, lazima *drive* ya ku-*invest* Tanzania iwe kubwa ili watu wengi waweze kutoa kazi. Mimi ninasema liko Shirika letu hili la Reli ni kweli wafanyakazi wanalalamika sana, wanatishia kugoma kila siku, lakini ndugu zangu pamoja na kwamba huyu aliyeletwa hafai; lakini Shirika hili la Reli limekufa wakati wetu. Watanzania wenzetu ndio wametufikisha hapo, hakuna aliyelalamika. Kwa hiyo, tunasema kama yapo matatizo kazi ifanyike ya kwenda kuyatatua, lakini haiwezekani na sisi tuache kuchukua nafasi ya uongozi wa kusema hapana, maamuzi yaliyofanyika ni sahihi. Ninachotaka kusema, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema haya, ninataka nitoe ushauri kwa marafiki zangu Mawaziri hawa, bahati nzuri Mungu amewasaidia ni weledi wazuri sana. Wizara inaongozwa na Profesa, inaongozwa na *PHD Holder*, nadhani waliowaweka pale walikuwa na maana. Wasiwaangushe waliofanya hiyo kazi. Lazima wa-*take lead* kwenye suala la *investment,* kwa sababu wanakwenda kwenye kuhakikisha kuwa Tanzania kunakuwa na mazingira mazuri ya *investment* ili kazi zipatikane. Kama mnataka tunakuja tunajadili hapa, vikoba vingapi tumefanya, *SACCOS* ngapi tumefanya; hapana, sio mazingira ya karne ya 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Rais Obama wakati anaongea Ghana alisema, jamani ni lazima mvutie uwekezaji, ndio *economic* za dunia ya leo. Hakuna muwekezaji atakayekuja kama kuna *corruption*. Siku hizi kuna lugha wawekezaji wanasema Tanzania ni nzuri kabla huja-*invest,* ukisha-*invest you are no longer important.* Kwanza, unaitwa wewe ni mwizi, wewe unakuja kutuhujumu, hapana. Niwaombe wenzangu humu ndani, lugha hii haitusaidii sana huko nje, yapo matatizo tuyatatue. Hatuwezi kutatua matatizo kwa kupiga kelele. Mimi ninasema watu wa Wizara hii mtusaidie kuhakikisha mnaweka *Task Force* ili kujua matatizo ya *investors*, kama wana matatizo wayatatue, kama sisi tuna matatizo tuyatatue. NIli nia yetu kubwa ni *employment*, kodi na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tusipowa-*engage* ni hatari. Kwa hiyo, ninachowaomba sana, ninalisema hili kwa sababu *trend* ya dunia ya leo, kipindi tunachokipita *under globalization*, kama watu hawawezi kuja kwako ku-*invest,* dunia hii utabaki nyuma tu. Hata tungesema watu wote waondoke tushike wenyewe, tutaanza kushikana mashati tu; *at the end of the day we need these people*, *they need us.* Kwa hiyo ni lazima tu-*strike a balance,* lakini nia yetu iwe ni kukuza uchumi;, hili ndilo litakalotuondoa hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hicho anachokisema Mheshimiwa ni muhimu sana. Unajua tuko katika Dunia hii ya mashindano, sasa mara nyingi sisi tunapenda sana kulaumu vile vitu vinavyofanyika, matokeo yake kweli *investors* wanatuona tuna matatizo sisi. Bunge hili pengine mtafute muda mzungumze, kwa sababu anaweza akakuta kitu kidogo tu katika eneo lake, akatoa lawama kubwa sana kuliko hali halisi. Kwa hiyo ni kweli *investors* hapa Tanzania wana matatizo kwa sababu yetu, hasa kwenye mambo yale utakuta tunalalamika mno.

Juzi tulikuwa na Mbunge mmoja wa *South Africa*, sijui alikuja kwenye Mkutano fulani katika hoteli zetu hapa, akakuta tumeajiri wahudumu hawajui hata neno moja la kizungu. Akasema jamani ninyi Watanzania, tunawapenda sana lakini sasa ndio mnatuwekea mtu ambaye hawezi ku-*communicate* na wageni, sasa inakuwaje?! Viko vitu vya namna hiyo; kwa hiyo, ninafikiri alichokisema Mheshimiwa Serukamba, tukielewe. *(Makofi)*

Tunaendelea, Mheshimiwa Dokta Guido Sigonda.

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo katika hii Wizara, ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo yetu Kitaifa. Kwanza kabisa, kabla sijaunga mkono hoja yenyewe, niliomba tu nijaribu kukumbusha kidogo kwamba, nitakayoyazungumza yatahusu zaidi Wilaya yangu ya Chunya, sitakwenda nje ya hapo. Nasema hivyo, kutokana na umuhimu wa majukumu ya Wizara hii, kwa vijana ambao wanaishi Wilayani Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbushe tu kwamba, wakati nimeingia kwenye Bunge hili mwaka 2006, nilieleza waziwazi bila kusita kwamba, Wilaya ya Chunya ni maskini. Nikaelezea sababu kubwa ambayo mimi nilikuwa nina imani kwamba, ndio inayosababisha Wilaya ya Chunya iendelee kuwa maskini mojawapo ilikuwa ni Viongozi wa Kitaifa kuonekana kana kwamba wanaisusia ile Wilaya kwa kutokuitembelea. Hilo nililieleza na ninashukuru, baadhi ya viongozi walifika mahali kusikia kile kilio changu. Ni kweli kabisa kwamba, mgeni njoo mwenyeji apone; Viongozi wa Wizara ya Elimu walifika wakaona hali halisi ya kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nimeingia kwenye Bunge, kulikuwa na shule ya sekondari moja tu mwaka 2006, Aprili. Kutokana na msukumo wa Viongozi wa Elimu, sasa hivi kuna shule za Sekondari 10 katika kipindi kifupi tu hiki. Mimi ninaamini kwamba; ni kutokana vilevile na ule msukumo, pamoja na kwamba wananchi tumejitahidi, lakini kama kiongozi anatembelea mahali, anatoa aina fulani ya msukumo. Kwa hiyo, ninaishukuru sana hiyo Wizara, lakini kuna Wizara nyingine vilevile kwa ruhusa yako, Wizara ya Miundombinu; bahati nzuri kilio changu kilisikika na Naibu Waziri wa sasa wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana; aliposikia kile kilio changu alifika aliongozana na aliyekuwa Waziri wake Mheshimiwa Chenge. Baada ya hapo ni sisi safari zetu za kwenda nje ya Jimbo langu, ilikuwa ni *pick-up* pamoja na malori. Sasa hivi tuna mabasi matatu ambayo yanazunguka katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninazungumza hivyo? Yapo mambo mengine vilevile na zipo Wizara nyingine ambazo zimefanya hivyo. Ninataka nielezee wazi wazi kwamba, hii Wizara ambayo tunaizungumzia leo, kwa kweli haijatusaidia kitu chochote katika Wilaya ya Chunya. Hilo ndilo la kwangu, kwa sababu ya majukumu ya hii Wizara; nikianza kuyasoma hapa haya majukumu, kuna neno la kusimamia, kuna neno la kutekeleza utekelezaji, kuna neno la uwezeshwaji, kuwezesha. Sasa ningeweza tu nikawauliza marafirki zangu; Mheshimiwa Profesa jinsi ulivyoiwezesha Wilaya ya Chunya katika misingi ile ya majukumu, nasema kwamba bado. Kuna mifano nitaitoa; katika kipindi cha miaka minne hii, katika upande wa mikopo kwa vijana ni shilingi milioni 10 kwa vikundi viwili tu; milioni tano tano. Kikundi kimoja cha LUPA shilingi milioni tano, ambalo ni Jimbo la mwenzangu na kikundi kingine kwangu Galula, ambayo ni milioni tano. Wilaya nzima ni milioni 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vijana ambao sasa hivi wananisikiliza, hicho kiasi kweli kinaweza kikawasaidia namna gani? Kkuna matatizo ambayo yanajitokeza, ambayo Wizara yenyewe nafikiri kutokana na mipango yake tunashawishiwa sisi

viongozi kwamba, tuhamasishe vikundi ambavyo ndivyo vinaweza vikawa ngao ya kupata mikopo kwa urahisi. Urasimu ambao upo wa kusajili tu hivi vikundi, unakatisha tamaa. Kwanza kabisa, tulikuwa tunaambiwa kwamba, ili usajili kikundi basi inatakiwa mpaka upeleke maombi kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani. Wakalegeza wakasema hapana, hata Mkoani kuna msajili pale, anaweza akafanya hivi, wakaenda mpaka Wilayani, lakini mpaka hivi sasa hali ni ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwangu nimehamasisha vikundi zaidi ya 22, tatizo ni jinsi gani tunaweza tukavisajili hivyo vikundi. Nilikuwa ninaomba tu kwamba, labda Wizara ijaribu kufikiria namna inavyoweza kuwasaidia vijana kama Vijana wa Wilaya ya Chunya, ambao matatizo ya ile Wilaya yanajulikana. Nimeelezea hapa kwamba, Wilaya ya Chunya kwanza ni vigumu kuitembelea;, ni vigumu kufika na vigumu kwa kila aina ya msaada kupatikana. Sasa mimi nilikuwa naiomba hii Wizara, ijaribu kufikiria ni jinsi gani inavyoweza kutusaidia sisi Wananchi wa Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mfano mmoja ambao ni wa masikitiko sana; kuna hizi fedha za JK; miongozo ilitolewa na fedha zikatoka, lakini Mheshimiwa ninakuthibitishia kwamba, Jimbo langu la Songwe, fedha zile zilipotoka hakuna hata kijana mmoja, hata mjasiriamali mmoja aliyepata hata shilingi moja ya hela hizi za JK. Sasa sababu ni nini? Nilijaribu wakati ule Waziri alikuwa ndugu yangu Mheshimiwa Chiligati, nilipomwambia hili, alijitahidi sana kuchukua hatua. Akaja mpaka pale Wilayani, akakuta kuna ujanja ujanja tu uliofanyika, wale ambao wako karibu ya Benki, wanaozunguka Benki wakati ikijulikana kabisa kwamba, lile Jimbo lenye Kata 10, benki ni hii moja tu. Unatoka kilometa 160, 170, unakwenda benki moja; sasa wale wa karibu pale ndio walioanza kupata hizi na sio zaidi ya 200 ni 126 tu ndio waliopata, kwangu hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linanitia uchungu sana na ndio maana nilisema kwamba, pengine niiunge mkono hii hoja baada ya hii hasira yangu kutoka. Nitaiunga mkono tu, lakini naomba ieleweke tu kwamba, ililinipa uchungu sana. Wakati inajulikana kabisa kwamba, Wilaya ya Chunya nako kuna vijana, nako kuna wajasiriamali, hata shilingi moja! Halafu hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa, baada ya hapo wakanieleza kwamba, awamu ya pili fedha zitatoka, kwa masharti kwamba sasa tunapitisha *TASAF*. *TASAF* kwenyewe ndio hivyo tena na sharti lingine ni lazima kuwe na kikundi, ambacho kinapata matatizo namna ya kusajiliwa. Sasa hivi uimekuja mtindo mwingine kwamba hapana ni lazima hizi hela zitapitia *SACCOS*. *SACCOS* kwenyewe ndio huko, yaani inatia uchungu. Sisi tunakubali kwamba, tutafuata masharti yote, lakini vilevile tusaidiwe, Wizara itusaidie na moja ya msaada ni wao wenyewe angalau kupita kuja kuzungumza na sisi, sisi tunajitahidi sana lakini na wao wakipata nafasi ya kuja kututembelea nafikiri wanaweza wakapata picha nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yangu huwa yanakwenda moja kwa moja kwenye *point*. Nikishaona kwamba, lile linalonisumbua nimeshalitoa, basi huwa nina kitu kingine cha kukieleza. Ninaomba tu, pamoja na matatizo yote ambayo Wilaya ya Chunya tunayo, naomba vijana walioko huko wasife moyo. Serikali ni sikivu sana na mimi bahati nzuri nimeyasema na sijayasema leo tu. Hata Mheshimiwa Waziri Mkuu,

anajua hali ya Wilaya ya Chunya, kuna wakati mwingine nilifikia mahali nikaanza kumlaumu Waziri Mkuu kwamba, wewe ndiye unayesababisha; Wilaya ya Chunya ukubwa wake ni 46% ya Mkoa wa Mbeya. Sasa hivi kutuweka mpaka tuwe na Wilaya moja maana yake ni nini? Huwa nafika mahali hapo na yeye ananielewa, lakini nilikuwa naomba tu kwamba, vijana mnaonisikia hivi sasa msife moyo Serikali ni sikivu, nina uhakika kabisa kwamba, baada ya kuzungumza hii kero yangu, basi Serikali na hii Wizara itanisikia na bila ya shaka nina imani kwamba, itachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DORA H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima hata nikaweza kuwepo hapa Bungeni leo, nami niweze kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu. Pili, niwapongeze Mawaziri wote wawili; Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Naibu Waziri, Wataalamu wote kwa hotuba yao nzuri waliyoiwasilisha hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa uamuzi wake mzuri wa kuendeleza zoezi la kuvitambua vijiwe vya vijana wote nchini ambao hawana kazi. Kwanza kabisa, niipongeze Serikali kwa sababu imelenga kuwasaidia na kuwainua kiuchumi na pia kuwapa fursa mbalimbali ili waweze kujiajiri na zaidi ya hapo Serikali iweze kupunguza idadi ya watu wasiokuwa na kazi nchini. Vilevile naipongeza pia Serikali kwa sababu imeweza kuanzisha *SACCOS* za vijana wasiokuwa na kazi nchini katika wilaya zote. Vilevile Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuwapatia mikopo na hivyo basi, vijana wengi wamehamasika na kukubali kujiunga na *SACCOS* hizi. Naona fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuwasaidia vijana hawa kuwapa mikopo, hazitaweza kutosha kabisa ni chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika kila Wilaya shilingi milioni tano hazitawatosha na kwa kuwa, Serikali imelenga kuwainua vijana hawa ili waondokane na umaskini, mimi ningeishauri Serikali iweze kuongeza fedha hizi angalau zifikie milioni 20 au 30 na kuendelea, kwa sababu vijana hawa ndio nguzo na ndio nguvu kazi ya nchi yetu. Tunaiomba sana Serikali na Wizara husika iweze kufikiria hilo na kama imeamua kuwasaidia vijana iwasaidie. Zaidi sana iweze kutoa pia elimu kwa vijana hawa, waweze kuchukua mikopo hii na kuweza kujifunza namna ya kurejesha mikopo yao ili pia zile fedha zitakaporudishwa, ziweze kuwazungukia kuwakopesha vijana wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nizungumzie suala la *TBS.* Kumekuwa na urasimu mkubwa katika Shirika la Viwango Tanzania. Kuna wajasiriamali wengi wana bidhaa nzuri sana, mwaka 2008, walifanikiwa kwenda Nchini Rwanda (Kigali) kushiriki Maonesho ya Kimataifa. Wajasiriamali hawa walishiriki na wakapata nafasi ya kwanza; hivyo basi, waliweza kupata tenda nyingi ili waweze kusafirisha hizi bidhaa zao katika nchi mbalimbali. Wanapofika hapa sasa wakija kwenye Shirika la Viwango Tanzania wanawasumbua, hawataki kukubaliana nao kuwapa nembo kwa ajili ya zile bidhaa zao, hawataki kuwasaidia ili nao wapate moyo waone kwamba na bidhaa zao ni nzuri, zimependwa nchi za nje na hapa nchini pia zinapendwa. Sioni sababu kwa nini *TBS*

wasiwape vibali vya kuweza kusafirishia bidhaa zao? Inaonekana basi kuna urasimu, ningeiomba Serikali ishughulikie hilo, iangalie uwezekano wa kuweza kuwasaidia hao wajasiriamali wetu ili nao waweze kuinua uchumi wao pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja kwenye vibali vya wageni; hii ni kero. Kila mtu anayesimama anazungumzia suala la wageni wanaoingia kinyemela nchini, wengine wana vibali. Utakuta vile vibali ni vya kughushi, vingine vimetengenezwa na Watanzania wenyewe halafu wanawaleta wale watu hapa nchini. Utakuta kule Kariakoo na sehemu nyingi za Dar es Salaam, ukikuta fremu ukiuliza utaambiwa ni shilingi milioni moja. Hivi mtu wa chini, watoto wetu wafanyabiashara wadogo wadogo, watauza kitu gani pale kwenye lile duka hadi waweze kulipia kodi ya shilingi milioni moja kwa mwezi? Utakuta yale maduka yote yana Waarabu, Wachina na watu ambao sio Wananchi wa Tanzania; hivi kweli tutafika wapi? Ukienda kwenye madini utakuta watu wana vibali vimetolewa, wachimbaji wadogo wadogo hawana fursa; wachimbaji wakubwa wa uwekezaji ndio hao wanaoangaliwa na ndio wanaotegemewa. Hivi vijana wetu watakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kule Dar es Salaam, zile biashara ndogo ndogo sana kama vile saluni, kupamba harusi, Wachina nao siku hizi wanapamba harusi; hivi inawezekana kweli? Watanzania wamefikia kiasi hicho kila kazi tunawapa wageni? Hivi sisi tutalia umaskini mpaka wapi? Tunaomba basi Serikali yetu iangalie pia hizi fursa za ajira za wananchi wetu, iweze kuzilinda, sio kutoa vibali tu kwa wageni, hata watoto wetu wanakosa nafasi za kufanyia biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hilo la vibali liangaliwe, wengi wamezungumza kwamba, kuna watu wana-*forge* vibali wanawapa watu, utakuta ile biashara hailingani na iliyopo kwenye kibali chake. Kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine limeikumba nchi yetu, yaani mambo ya DECI. DECI imeingia hapa nchini, wananchi wametoa fedha zao na mwisho kabisa utakuta wale watu wamepata hasara kumbe walikuwa ni matapeli. Sasa mimi binafsi nimeshakutana na watu kama hao na nilikutana nao hapa Bungeni, wakawa wanaelezea habari za kutoa mikopo midogo midogo na mikubwa na kuwaelimisha wananchi juu ya ujasiriamali. Mimi nikaona ni watu wazuri, nikawakaribisha katika Mkoa wangu wa Manyara. Walifika Manyara wakafungua Ofisi katika kila Wilaya, sasa wamezunguka Mkoa mzima wamechukua shilingi 15,000 kwa kila mwananchi, zaidi ya wananchi 10,000 walipata hasara hiyo na ikaonekana kwamba, mimi ndiyo niliwapeleka nikijua kwamba ni wazuri kumbe matapeli. Jina la kampuni hiyo ni Good Opportunity Co. Ltd.

Ninachotaka kusema, vyombo vyetu vya usalama vinafanya nini? Watu kama hao matapeli wanaweza wakawaingilia wananchi wetu na kuchukua fedha na kujinufaisha wao wenyewe; *at the end of the day* utakuta wale watu kumbe walikuwa ni matapeli! Wanafungua ofisi kubwa kubwa, wanaweka *computer* na vyombo mbalimbali, lakini

baadaye wanafunga zile ofisi kisha hawaonekani tena na vyombo vya usalama vimekaa kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba Serikali na vyombo vinavyohusika, viweze kuangalia watu ambao si wema wanaoingia katika nchi yetu na kuwadanganya wananchi wakijitia kwamba, wao wana kampuni ya kutoa mikopo. Naomba hili liangaliwe sana. Pia namshukuru Mungu kwamba, wale watu wamekamatwa na sasa hivi wako ndani. Ninachofanya tu ni kwamba, nachukua nafasi hii kuwaomba Wananchi wa Manyara kwamba, watu hawa mimi niliwakuta na nilidhani kwamba ni watu wema nikawakaribisha kwetu, nikijua watakwenda kuleta maendeleo lakini baadaye walifanya sivyo. Hivyo, nawaomba Wananchi wangu wa Mkoa wa Manyara, wanisamehe sana na tuendelee kufanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia tena suala la Shirila la Tija la Taifa. Toka mwaka 2006 tumekuwa tunasikia kilio chao kwamba, Serikali haikuwatendea haki. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia haki Shirila la Tija la Taifa ili waweze kurejeshewa kiwanja chao. Serikali imeamua kuwalipa milioni 11 wakati wao walishatumia fedha zaidi ya milioni 200. Naomba Serikali iangalie uwezekano kama ikiwezekana, warejeshewe kile kiwanja kwa sababu kama shida ilikuwa hawajakiendeleza, milioni 11 hailingani; inawezekana mmewaonea. Ninaomba Serikali iangalie upya namna ya kuwasaidia, ikiwa ni kuwarejeshea kiwanja chao warejeshewe, ikiwa ni kuwalipa fedha zao basi walipwe kutokana na fedha ambazo walikuwa wamezitumia pale ni zaidi ya shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo inapambana na ajira mbaya ya watoto katika nchi yetu. Kwa kweli tatizo hili lilikuwa kubwa, lakini sasa Serikali imeingilia kati na vijana karibu 2978 wameondolewa katika utumikishwaji wa ajira mbaya, wameingizwa kwenye Elimu ya VETA ili waweze kupata stadi za kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo mimi sina mengi, naomba niishie hapo na ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na pole kwa kupambana na matapeli.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitamwita Mheshimiwa Wilson Masilingi.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii nzuri.

Kwanza, napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara na pia Watumishi wote wa Mashirika mazito kama hili la NSSF, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii na mengineyo

yaliyo chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwa kuanzia. Nasema kwa kuanzia kwa sababu bado wana kazi nzito ya kufanya.

Pili, napenda kumpongeza ndugu yetu Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge mpya wa Biharamuro, kwa ushindi wa kishindo. Tofauti ya ushindi ni kubwa mno, kwa sababu walioshindwa hawakufika Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa sababu katika taarifa yao wametueleza kwamba, ajira imeongezeka kwa watu 1,271,923 hadi Desemba 2008. Bila shaka mwaka huu itaongezeka zaidi, kwa sababu kwa mujibu wa taarifa tulizozipata hususan kutoka kwa Wizara ambazo tayari zimeshawasilisha bajeti zao; wengi wataajiriwa. Hongera sana kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Eneo lingine ninalopenda kuchangia baada ya pongezi ni vijana au maendeleo ya vijana na kaulimbiu yetu ya mwaka huu wa fedha ya Kilimo Kwanza. Nilikuwa nasoma hotuba nikakuta maelekezo ya Wizara hii zaidi ni kuratibu, kuelekeza sera, miongozo ya Sheria, Kanuni na Taratibu. Sasa kipengele cha kuendeleza vijana hakipati uzito unaostahili na ni lazima tutafakari ni kwa namna gani tutawezesha Wizara yetu hii ili pamoja na kuratibu au kuandaa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na kusimamia miongozo inayotoa iwezeshwe ili ijikite zaidi kuwalenga vijana. Kwa mfano, nataka mwaka huu wa fedha waanze na Muleba Kusini na ni mapendekezo ya ushauri. Kwa kuwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji imekuja na mpango mzuri wa kilimo cha umwagiliaji katika Jimbo la Muleba Kusini hususan kata ya Ikondo, Vijiji vya Buyaga na Buhangaza hekta 480, skimu hiyo ya umwagiliaji itakamilishwa mwaka huu wa fedha. Vijana wapo wa kutosha, ambao wakiwezeshwa na mashirika mazito kama NSSF, wanaweza wakahakikisha mwaka huu wa fedha hekta 480 zinaanza uzalishaji mara moja na fedha zitarudi chini ya usimamizi wa NSSF, Wataalamu waelekezi kutoka Kilimo na Wizara ya Maji na Uwagiliaji ili tuweze kuwa na matunda ya harakaharaka kutokana na mpango mzuri huu wa umwagiliaji, ambao najua sambamba utaendana na kujenga Barabara ya Kamishango, Buyaga, Buhangaza hadi Luhanga.

Hili ni pendekezo ambalo nalileta kwako Mheshimiwa Waziri, kwa sababu wewe ni mdau wangu muhimu sana, kwani unawapenda vijana na una malengo mazuri lakini huna fedha. Nimekuwa naangalia bajeti yako; bilioni tisa hii ndiyo inakusaidia kuendesha mambo yako. NSSF bajeti ya utekelezaji wa mambo yao ni bilioni 40. Wamenivutia sana hawa NSSF, kwa sababu mchango wao katika Jamii ni mkubwa sana, wanastahili pongezi za dhati. Chuo Kikuu cha Dodoma, kazi waliyoifanya pale hatutaisahau kwani wamejenga Makao Makuu ya PCCB, nimeona kwenye magazeti jengo linavutia sana, nadhani nitapata fursa ya kulitembelea na siyo kwenda kuhojiwa bali kwenda kuliangalia linavyovutia.

Kitu kingine kilichonivutia ni kwamba, mafao ya wafanyakazi mwaka huu wamepanga kuwalipa bilioni 83.456.9, hayo ni malipo ya mafao tu. Kwa hiyo, siyo kwamba NSSF inawekeza tu katika vitega uchumi, lakini inajali hata wanaochangia katika mfuko huo. Kwa hiyo, kazi ya NSSF na uwazi wao hasa ukiangalia katika

kiambatanisho cha 7 katika ukurasa wa 82 na 83, inaonesha NSSF wamekuwa wawazi, wametuonesha wanatarajia kukusanya shilingi bilioni 533.650.3.

Kilichovutia zaidi, watawekeza katika vitega uchumi shilingi 401,764,000,000. Hawa NSSF wanazo pesa, ndiyo maana ninaendelea kusisitiza kwamba, tafadhali sana, kupitia kwako naiomba sana Wizara iangalie hili pendekezo nililolitoa la kuangalia hii skimu ya umwagiliaji ya Kata ya Ikondo katika Vijiji vya Buyaga na Buhangaza, tusije tukaingiza fedha katika kutengeneza mradi wa umwagiliaji halafu baadaye usizae matunda na baadaye vitafutwe visingizio vya kuuza huu mradi kwa watu wanaoitwa wawekezaji, ambao pindi wanaposhindwa kuzalisha huwa wanakimbilia kuomba msaada wa Serikali.

Naishukuru Serikali imeweza kuwadhamini wafanyabiashara na hili si jambo baya, lakini tuelekeze sasa hata kuwadhamini vijana wetu kwa sababu vijana wetu hawakopesheki na kila mtu anajua. Tunasema tutahamasisha benki ziwakopeshe vijana katika kulima na kuvua samaki kama katika Kata ya Mazinga kule kwangu Muleba Kusini na Chato, Mheshimiwa John P Magufuli ananikumbusha ni jirani yangu huyu. Hawa vijana wana nyenzo na wako kwenye biashara, lakini hawana mitaji, yale majengo yanayojengwa Dar es Salaam ni jambo jema hata wamachinga wajengeeni katika miji yote, maana vijana wako kila mahali, yaani mijini na vijijini lakini sasa vijijini njooni haraka sana. Anzieni Muleba, Wavuvi wa Kata ya Mazinga wapewe mitumbwi, nyavu za kisasa ili waweze kushiriki katika uvuvi wa kisasa.

Umwagiliaji Kata ya Ikondo, tuanzie Tarafa ya Shamba iwe awamu ya pili, yaani kuanzia mwezi wa nne mwaka kesho. Tufanye umwagiliaji kwani migomba yetu inahitaji maji kwa umwagiliaji. Haya mashamba yetu madogo katika Wilaya ya Muleba Kusini bila msaada wa fedha tutakuwa tunazaa vijana maskini na tukifa tutakuwa tumewaacha vijana katika hali mbaya sana ya umaskini na ndiyo maana nimeanza mkakati wa kuomba Pori la Burigi lifutwe. Mkandarasi wa kujenga Barabara ya Kagoma, Muleba, Kyamiorwa, Biharamulo na Lusahunga ameshaanza kazi. Tukiwa na lami inapita kwenye pori la wanyama si vizuri. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naona anatabasamu bila shaka atakuwa mdau wangu katika kufuta pori hilo kwani ni kapori kadogo kana Ziwa Burigi, ambalo linaweza likatumika katika umwagiliaji, vijana 500,000 wa Muleba wapate mahali pa kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu umefika unapajua sana, mwenye hekta moja ndiye tajiri mkubwa, hekta moja tu. Mimi narudia kusema kwamba, mimi namiliki hekta hazizidi kumi sijui na mimi nihamie Mikoa mingine kwenye ardhi kubwa na mimi nichukue hekta 200, lakini kulima sijui lazima niwe mkweli labda nihodhi tu ili nije kuuza baadaye. Mimi najua kulima vidogo vidogo tu hivi, labda watoto wangu waje kulima baadaye sasa hivi mimi siwezi kuhodhi ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalosisitiza ni kwamba, Muleba Kusini mtutazame kwa jicho la pekee. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakutegemea sana, kwani hujatutembelea ila naomba uje utuone kama Waziri Mkuu. Ulitutembelea kama Waziri, lakini sasa uje kama Waziri Mkuu, uone mashamba yetu, uone vijana ambao wana ari ya kazi, wana

moyo wa kujitolea na wanafanya kazi kwa bidii. Sisi kwetu hatuiti vijiwe, tunayaita maeneo ya kujiburudisha. Hivi kwa nini kijana akienda kutembea jioni mnasema amekwenda kijiweni? Amekwenda kujiburudisha hamjamburudisha, mnasema amekwenda kijiweni. Mimi naomba msiseme wamekwenda vijiweni ni kwamba tuwatafutie maeneo ya kwenda kujiburudisha, lakini kazi wanafanya isipokuwa haina tija kutokana na uwekezaji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia picha hapa ya kava ya Mheshimiwa Waziri wetu aliyeleta hoja, yaani Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, nimeweka miwani kuiangalia vizuri sana. Mimi nimeishi Tabora miaka 25 iliyopita, nilikuwa Hakimu wa Mkoa wa Tabora. Kwa hiyo, huo Mkoa naujua mpaka Urambo. Ule Mkoa ni mzuri sana, una raslimali nyingi pamoja na mawe. Sasa wanachimba msingi hawa vijana kwa kujitolea, wakishirikiana na vijana rafiki zetu kutoka nchi za nje, wanaanza kujenga msingi kwa kutumia matofali ya kuchoma. Mheshimiwa Waziri ni lazima atueleze; hii sekondari iko katika Kata gani ili Wahandisi waifuatilie?

Likitokea tetemeko kidogo tu tutaua watoto wa shule, kwani huwezi kuanza msingi wa shule yoyote hata ya *kindergarten* kwa matofali ya kuchoma; ni lazima uwe wa mawe au matofali ya *cement on a serious note.* Huu siyo utani ni shule gani na kwa nini umeiweka kwenye kava hii kuleta aibu? Tuna shule nzuri tu mfano mimi kwenye Kijiji cha Bunyagongo tumefika mpaka kwenye Mtambapanya na kuzidi pale tukakosa mabati mwaka mzima kwa sababu ya umaskini tu. Ingewekwa hiyo hapa na yenyewe ni ya vijana walichimba msingi siku moja tu, wameanza chini kwa mawe na *cement*, matofali ya kuchoma juu, lakini hawa wanaanza na matofali ya kuchoma ndani ya udongo? Hii lazima Wahandisi waangalie na ifutwe mara moja waanze upya, hilo lazima nieleze. *(Makofi/Kicheko)*

Huu ni mfano wa kuonesha kwamba, vijana wana moyo wa kufanya kazi tunawaangalia tu hatuwasaidii, lazima twende kuwawezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamuita Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya.

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, lakini umenishtukiza kwani mimi nilitegemea nitapata nafasi jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nizungumzie namna gani tunaweza tukawatayarisha vijana wetu wakajiajiri zaidi wao wenyewe bila kungoja Serikali kuwapa ajira.

Ajira kuna namna tatu; kuna ajira ambazo Serikali inakuwa nazo na inaweza ikatoa ajira hizo kutokana na wawekezaji au Serikali yenyewe kuwahitaji vijana katika Wizara, Idara au Mashirika Mbalimbali; kuna ajira ile ambayo hutegemea wawekezaji

wanaokuja katika nchi na kutoa ajira kwa wananchi wa nchi ile ambapo kipo kitega uchumi kile; na ajira ya mwisho ni ile ajira ya vijana wenyewe kutafuta njia ambazo zitamfanya apate maendeleo yake, kula yake au kuendesha familia yake.

Sasa tuanze na hii ajira ambayo inatolewa na Serikali. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alipotoa kauli kwamba, atatengeneza ajira kiasi fulani kwa kila mwaka kwa nchi yetu, watu wengi walikuwa wana mwamko wa kufikiri kwamba, ajira zile ni lazima zitokane na Serikali yenyewe, hapana! Ni ajira ambazo mazingira yatakayoweza kumfanya kijana akapata kazi ndiyo ajira yenyewe. Sasa mazingira hayo ndiyo kitu cha kuzingatia, nafikiri hatujajipanga tu tukawa makini, lakini ajira katika nchi hii zinaweza zikaongezeka mara mbili au mara tatu kila mwaka kwa vijana wetu.

Tuchukulie mfano, kama alivyosema Mheshimiwa Peter Serukamba kwamba, mara nyingi wawekezaji wanapokuja katika nchi yetu wakawekeza kunakuwa na mambo madogo madogo au hata makubwa yanayofanywa na wawekezaji yanayorejesha nyuma ajira au haki za wanaoajiriwa wananchi wenyewe wa Tanzania. Kukurupuka tu tukasema kwamba kila mtu afukuzwe, kila mwajiri apewe *conditions* ambazo hazipo, tutakuwa tunawavunja moyo wawekezaji hawa na tunapunguza ajira katika nchi yetu, lakini ni kipi kinachofanya hata wao wakawekeza halafu wananchi wakapiga kelele? Ni mikataba! Inakuwa namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, anapokuja mwekezaji akaweka rasilimali yake, yaani *capital* angalia namna gani wewe unaweza ukamu-*accommodate* raia kufanya kazi pale na ukaisimamia mikataba ya raia yule ili alindwe katika kazi anayoajiriwa na mwajiri yule aliyewekeza katika nchi yako. Hicho ni kitu kinachoshindikana! *A very good example* ambayo siku zote inapigiwa kelele katika nchi hii kwamba, tulipofungua milango hatukufungua milango tu bali tumefungua na madirisha na kila kitu, wanaingia nyuki kutupa asali, lakini humo humo wanaingia nzi kutupa maradhi na mambo mengine mengi tu na nitawapa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawalaumu Wachina kuwepo Kariakoo au kuwepo Tanzania, Mchina yeyote anayekuja kuwekeza, Mhindi yeyote, Mzungu yeyote au hata Mwafrika anayetoka katika nchi nyingine za Kiafrika kuja kuwekeza, lazima apewe masharti ya kuwekeza. Moja katika masharti muhimu kwa mwekezaji ni kwamba, je, anayo *capital* ya kufanyia kazi katika nchi anayoingia? *Capital* hiyo mmeangalia *feasibility study* zake alizozifanya kwa *project* ambayo anataka kuifanya katika nchi ile? Hiyo *project* anayowekeza katika hiyo nchi itakuwa na manufaa kwa wananchi; itazalisha kuweza kupata *commodities* kwa ajili ya *local consumption* na nyingine kusafirisha? Atatoa ajira kiasi gani kwa Wananchi wa Tanzania? Ukishaangalia hayo ndiyo unampa kibali cha kuweza kuwekeza katika nchi yako, huwezi kumwacha Mwananchi wa Tanzania, ambaye ndiye anatakiwa kuuza matunda, juice ya ndani, kuuza maji ya kunywa, nguo na viatu, halafu ukamleta mtu kutoka nchi za nje akaja akachukua nafasi ambazo kazi zile zingefanywa na Watanzania na hicho ndicho kinachofanyika.

Leo unawakuta ndugu zetu wa Kichina wanauza maua ya plastic Kariakoo, la kusikitisha hata kama wanakuwa na maghala ya kuweka bidhaa basi hata bidhaa zile

wanakwenda wakibeba wenyewe kwa mkokoteni badala ya kuwatumia vijana wetu. Halafu wanaleta mali *in containers, containers* mia au mia mbili zinakuwa bandarini, sisi hatuna haja ya kuuziwa bidhaa ambazo zimeshatengenezwa, haja yetu ni kuweka viwanda vitengeneze bidhaa na sisi tusafirishe na kisha tutoe ajira kwa vijana wetu.

Sasa vijana hawa kama tutawajengea mazingira mazuri, Wachina wakawekeza hayo maua wakayatengeneza hapa tukasafirisha nchi jirani, wakatengeneza hizo pafume tukasafirisha nchi za nje, wakatengeneza nguo kutokana na pamba yetu ambayo sasa hivi imeshuka bei tukasafirisha vitambaa na nguo nchi za nje, hapo tutasema kwamba, ndugu zetu Wachina wametusaidia. Mimi sikatai uhusiano uliopo baina yetu na Nchi ya China, wala tusiyavamie haya mambo tukawafukuza kwa saa 24 tukavunja uhusiano mzuri wa historia uliokuwepo baina ya Tanzania na China, ila tuangalie ni mazingira gani Wachina waweze kufanya kazi katika nchi yetu, watatoa ajira kiasi gani ili vijana wetu waweze kufaidika na ajira zinazotolewa na Wachina. Vivyo hivyo, kwa watu wengine ambao wana dhamira nzuri na nchi yetu.

Kuna vijana wanaamka hawajui wafanye nini, wanajiajiri hata kwa kupika chakula tunawaona akina mama ntilie, lakini nenda kaangalie magezeti ya leo yote, *front pages* utaona namna gani Jeshi la Mgambo linavyowafukuza hawa vijana kwa kuwapiga, kuwasukuma na kuwamwagia chakula na kadhalika. Jamani *investment* yake haizidi 50,000/= anapika chakula, chakula kama wali na mchuzi wa maji, anatuhudumia sisi Watanzania ili jioni akalishe watoto wake katika kaya yake, lakini wewe unamvurugia chakula chake, unachukua na masufuria yake na yeye unambeba unakwenda kumuweka kituoni. Nyuma kaacha kaya inataka kula na kuangaliwa. Badala ya kwamba, yeye umemwona na sufuria bovu wewe ukamtafutia sufuria jipya, ukamtafutia mwiko wa kisasa, ukampa jiko ambalo litahimili moto kwa muda mrefu asitumie mkaa mwingi; wewe unamfukuza barabarani aende wapi Mtanzania huyu? (*Makofi*)

Hawa vijana ndiyo tunawahitaji kesho kwa ajili ya uchaguzi hawa, tunawafanya kama kofia za misikitini, kuna baadhi ya misikiti kunakuwa na kofia ndani unapoingia na unapotaka kuswali unaivaa unaiweka, unatoka wewe huna kofia. Ndiyo tunavyowageuza! Mwakani hawa hawa ooh! mtapata kazi, mtapata ajira tupigieni kura, tukimaliza kura haya Jeshi la Mgambo wachukueni wapelekeni. Hatuwezi kufika, tuwajengeeni mazingira hawa waweze kujua kwamba, nchi yao inawatumikia na inawajali.

Nenda mpakani Tunduma, pale kuna vijana wanachukua sukari kutoka Zambia mpakani wanaingiza Mbeya, jinsi wanavyofukuzana na Polisi utastaajabu utafikiri siyo Watanzania. Wana unafuu kwa watu wa Mbeya, kwani sukari inayotoka Zambia kuingiza Mbeya inakuwa ni rahisi zaidi kuliko sukari ambayo inatoka Dar es Salaam kuisafirisha kuipeleka Mbeya. Ninaweza kuthubutu hata Mkuu wa Mkoa wa Mbeya anakula sukari inayotoka Zambia, lakini yeye ndiye anayekaa na Kamati ya Ulinzi ya Mkoa kuwafukuza hawa eti wanapita njia za panya, si njia ya za panya, tuwajengeeni mazingira wale vijana wapewe mikopo, wawe *encouraged* waingize sukari na wapewe hata maeneo ya kujijengea nyumba za kuishi baadaye. Hii ndiyo namna ya kuwahifadhi hawa vijana wakapata ajira; ajira sio lazima kupelekwa Jeshini wala Polisi, hapana! Ikiwa

hatutamjengea mazingira akawa anapata mkate wake asubuhi, mchana na usiku itakuwa umeshampa ajira huyu.

Tumeanzisha JKT, mimi ninachoomba kifanyike katika JKT ni kwamba, tuwachukue vijana tuwasomeshe uselemara, tupate *Electricians, Electronics* tuwapate, mafundi mbao, mafundi wa kujenga na kila anapotoka mpe *tool box* yake, mwambie hii hapa ndiyo zawadi ya leo umemaliza wewe ni *electrician*, *electronics*, *carpenter*, atarejea kijijini kutafuta riziki yake kutokana na ile *tool box* uliyompa. Badala yake, tutawachukua JKT tukawapigishe kwata tu, hili ndilo Jeshi la Tanzania tunakwenda nao. Tuwafunze sasa namna ya kutafuta mkate wao, watakaokubalika kubaki kutokana na nidhamu za kijeshi wataingizwa Jeshini, Polisi na *Immigration* na hata Magereza, lakini wale ambao watatoka na ujuzi watakwenda vijijini kufanya kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Kilimo Kwanza kimetengewa mabilioni, haya mabilioni ilikuwa ichukuliwe angalau 20% tufungue viwanda japo vitatu vya kusindika juice kutokana na matunda yetu. Tazama Mkoa wa Pwani, mananasi yanavyooza, nenda Mbeya katazame ndizi kule, nenda Muheza katazame machungwa pale. Sasa Kilimo Kwanza tuzalishe nini? Tuanze na *irrigation* mwaka huu kwa kutegemea kwamba mwakani tutazalisha; hapana. Hiki tulichokuwa nacho kwanza tukitunze, *we have to produce* ambacho tunacho. Tuna maziwa kwani tuna ng’ombe milioni 19.8, lakini Maziwa tunaagiza Kenya, nyama tunaagiza toka Australia na Brazil. Hoteli zetu zinaagiza mpaka mayai; *it is real shame*, tujenge misingi ya kujenga viwanda vidogo vidogo vya kusindika ili *juice* yetu itokane na matunda yetu, nyama zetu tuweze kuzisafirisha, kadhalika na ngozi zetu tutengenezee viatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninategemea kwamba, Serikali itachukua busara zangu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ila sikukuruhusu uimbe humu ndani, umeanza kuimba hujapewa hurusa. (*Kicheko*)

Ahsante sana kwa mchango wako mzuri na ilikuwa vizuri umeweza kumalizia mchana huu.

Sasa tukirudi Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Halima Mdee, wawe wamejiandaa halafu nitawaita watoa hoja tupate muda mwingi pengine wa mshahara wa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wale niliowatangaza asubuhi walikuwa ni wageni wa Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Ponsiano Nyami, nimeambiwa kwamba wanafanya maonesho ya *solar lights,* yaani zile taa za *solar* kwenye eneo letu la maonesho pale. Kwa hiyo, mnakaribishwa kwenda kuona na mfanye maamuzi yenu huko huko mkiona yanafaa.

Baada ya hapo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11 .00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia kiti*

**HOJA ZA SERIKALI**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge kipindi cha kwanza nilitamka wafuatao ndiyo watapewa nafasi ya kuchangia, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Halima Mdee, halafu nitamwita Naibu Waziri, halafu atafuatia mtoa hoja mwenyewe ambaye ni Waziri. Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mawazo yangu katika Wizara hii ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, ambayo tumeanza kuijadili toka asubuhi. Vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa nguvu, afya na uwezo wa kutoa mawazo yangu kwa jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nianze kuwapongeza Mheshimiwa Waziri mtani wangu Prof. Kapuya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, bila kumsahau Alhaji Ramadhani Dau, pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuleta kasi ya maendeleo pamoja na kupunguza kero za wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, basi naomba nianze kuchangia kama ifuatavyo, nikianzia na ajira kwa vijana. Ni kweli Serikali inajitahidi sana kuongeza ajira kwa vijana, vijana wengi wameajiriwa, wamekuwa Walimu, Wauguzi, Madaktari, Wahandisi na kada zingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado hiyo haitoshi kwani Vijana wengi walio mitaani wanaadhirika, hawana ajira. Naomba sana Serikali ijitahidi kufikiria namna ya kuwakwamua hawa vijana. Nashukuru pia kuwa Serikali inajitahidi kuwapeleka vijana hawa kwenye vyuo vya ufundi, *VETA* na Taasisi mbalimbali za ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba, vijana hawa wanapotoka kule wanakuwa hawana vitendea kazi, hawana mitaji, sasa hawa vijana hata kama kapata fani ya aina yoyote, hiyo fani ataifanyia nini? Ndiyo maana wengi wao wanasahau fani walizosomea, unakuta wanajiingiza kwenye fani ambazo hazina sifa hata kwenye jamii, vijana wanakuwa wezi, vibaka na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuwasaidia hawa vijana, hasa hawa wanaochukua fani za ufundi wanapomaliza mafunzo yao basi waondoke chuoni wakiwa na vitendea kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wakipata vitendea kazi hapo tutakuwa tumewasaidia vya kutosha maana hata kama atafanya jambo baya mtaani, atakuwa hana lawama kwa Serikali, atakuwa hana lawama hata kwa wazazi wake kwa sababu atakuwa ameichezea fani yake yeye mwenyewe. Naomba sana Serikali iwajali vijana, iwape vitendea kazi, hata kama ni kwa kuwakopesha. Pale kijana anapohitimu tu basi aondoke na vifaa vyake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado niko kwenye vijana. Vilevile vijana hawa hawapati mikopo. Mkopo wa JK unapita pembeni kwa vijana, mikopo hii iko mbali sana na vijana. Mikopo hii iliyodhaminiwa na Benki Kuu, imepelekwa kwenye mabenki yetu *CRDB*, *NMB* na mabenki mengine, sasa vijana hawa wana uwezo wa kwenda kukopa kwenye mabenki hayo? Wana dhamana gani, watoto wadogo hawana nyumba hawana chochote cha kudhaminisha katika mabenki haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuwasaidia hawa vijana, naomba hizi fedha za JK zisogezwe Wilayani. Nashukuru sana, sasa hivi Mfuko wa JK, umefika katika *SACCOS* za Wilaya na zinapelekwa shilingi milioni tano kwa kila Wilaya. Lakini hizo bado hazitoshi, ni ndogo naomba fedha ziongezwe na sio kuongezwa tu, waangalie na taasisi zingine nazo zipewe fedha hizi ili vijana waweze kukopa kwa urahisi. Kuna taasisi kama vile *SIDO, PRIDE, VIKOBA* na nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali izingatie hili, endapo itapeleka pesa kwenye taasisi hizi nilizozitaja, vijana hawa wataweza kukopesheka. Lakini kwenye mabenki hawakopesheki, kwani hawana dhamana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Profesa Kapuya, mtani wangu kwa vijana hana ujanja, kwani wanamtegemea, dhamana yao anayo yeye, uwezo wa kuwakomboa anao na nguvu anazo na namfahamu akiamua kuchacharika, unachacharika kweli, naamini utafanya hayo kwa ajili ya vijana ambao ni Taifa la kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Hili ni Shirika ambalo linafanya kazi nzuri sana, limewekeza kwenye majengo, limesaidia Serikali kujenga majengo mbalimbali. Kwa mfano, jengo hili la Bunge, *NSSF* imetoa pesa, Chuo Kikuu cha Dodoma, *NSSF* imetoa pesa, sasa hivi nasikia Wamachinga wanajengewa soko la kisasa pale Dar es Salaam na TANESCO wamekopa *NSSF* na maeneo mengine mbalimbali *NSSF* inasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba Serikali kupitia Wizara hii na pia namwomba Alhaji Ramadhani Dau, sasa awakumbuke wadau wake na wadau wake ni

wafanyakazi, apeleke uwekezaji wa majengo Wilayani na Mikoani waliko wadau wake, naomba sasa awajengee nyumba za kuishi, wafanyakazi wengi wanastaafu bila ya kuwa na nyumba za kuishi kwa sababu hatujawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini *NSSF* ikienda huko Wilayani na Mikoani na ikajenga nyumba za kuishi, wafanyakazi watapanga hizo nyumba kwa bei nafuu na wafanyakazi wataweza kukopa zile nyumba kwa bei nafuu. Nakuomba sasa Dau uwakumbuke wadau wako ambao ndio wanaowezesha hata mikopo hii mikubwa mikubwa ya Serikali pamoja na wafanyabishara wakubwa wapate pesa za kukopa. Naamini kabisa wafanyakazi mkiwajengea nyumba watafurahi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile *NSSF* inaikopesha Serikali, lakini Serikali inakuwa nzito kurudisha mikopo hiyo. Naiomba Serikali ielewe kwamba, pesa hizi ni za mzunguko zinatakiwa na wengi, hebu Serikali tuwe mfano kwa wengine, tunapokopa pesa tukumbuke kurudisha pesa hizo kulingana na mikataba tunayoisaini. Tunapochelewa kurudisha hiyo mikopo tunawanyima haki wawekezaji wengine wanaohitaji kutumia zile pesa na vilevile Serikali huwa inawapa *guarantee* wafanyabiashara wakubwa wanapokopa. Sasa hawa wafanyabiashara wakubwa mnaowapa *guarantee* ya kukopa, kwanini hamuisaidii *NSSF* ili warudishe hiyo mikopo? Wako ambao hawarudishi. Naiomba Serikali kwa hili haiwezi kukwepa, haina ujanja, ishirikiane na *NSSF* kuhakikisha kwamba, hawa wafanyabiashara waliodhaminiwa na Serikali wanarudisha mikopo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika hawa wafanyabishara wakihimizwa na Serikali watarudisha mikopo yao. Ninao mfano hai, katika Kamati yangu ya *POAC* tulitembelea Kagera *Sugar* ambao walishindwa kabisa kurejesha mkopo wao waliokopeshwa na *NSSF*, lakini baada ya kwenda kule na kuwa wakali kidogo, Shirika hili la Kagera *Sugar* liliweza kuanza kurejesha mkopo wake. Kwa hiyo, nina uhakika Serikali ikijikita kuhimiza wale iliowadhamini kukopa, watarejesha hizi pesa ili na wengine wakope hasa wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea hilo, naomba nimalizie kuhusu Mfuko wa JK. Mfuko huu wa JK kweli unasaidia sana lakini bado vijana hawajautumia vilivyo. Hivyo, naomba sana vijana hao wathaminiwe, wapewe hii mikopo ili waweze kujikwamua kimaisha. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao hawa vijana wanaotumia madawa ya kulevya na bangi. Vijana hawa wanadhalilisha Taifa, vijana hawa wanadhalilisha jamii, Mheshimiwa Prof. Kapuya wanusuru hawa vijana ni wako, wengi wamezagaa mijini na hata wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa ni Taifa la kesho, vijana hawa ni nguvu ya Taifa, tutakapowaacha waendelee na mwenendo walio nao, hatujawakwamua hawa vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara hii ishirikiane na Halmashauri za Wilaya na Miji, Manispaa na Majiji, kutafuta namna ya kuwalea hawa vijana. Vijana hawa hatuna ujanja, ni wa kwetu, tukiwaacha wataendelea kututia aibu, wataendelea kutuletea hasara, wataendelea kuwaumiza watu huko mitaani, ngwara kila siku na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hawa vijana tuwathamini, tutafute maeneo ya kuwatunza katika kila Halmashauri au angalau kwa mkoa, tutafute eneo moja na vijana hawa tuwakusanye hapo ili tuweze kunusuru maisha yao. Bila kufanya hivyo wataendelea kudhalilika na wataendelea kuisumbua jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee migogoro ya wafanyakazi. Migogoro hii inatokana na wafanyakazi kutopata maslahi yanayokidhi haja, naomba sana Serikali ihakikishe kuwa, inapopanga mkakati wa kuangalia maslahi ya wafanyakazi iwe inawashirikisha. Wafanyakazi wana wadhamini wao na wadhamini wao ni vyama vyao vya Wafanyakazi, angalau Serikali ifike mahali iandae ratiba ya kukutana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi, kujadiliana nao, kuangalia kero zao ni nini? Wanahitaji nini? Wanapungukiwa nini? Serikali inawasahau katika kitu gani? Wakifanya hivyo nina hakika migogoro ya wafanyakazi na Serikali itaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Kapuya uwezo wa kukutana na wafanyakazi anao, uwezo wa kujadiliana nao anao kwa sababu maslahi wanayopata wafanyakazi hayaendani kabisa na hali halisi ya uchumi wa nchi na uchumi wa dunia, ndiyo maana unakuta migogoro kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta wafanyakazi wanadai pesa zao, mapunjo yao, pesa za matibabu, uhamisho na kadhalika, wanapocheleweshewa ndipo hapo mgogoro unapoanza. Lakini kama tutakuwa na muda maalum wa kukaa na kuzungumza nao, nina hakika migogoro hii itakwisha. Tukumbuke kuwa, wafanyakazi ni tegemeo la Taifa kwani ni watu wanaofanyakazi za kuleta maendeleo ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu vijana ambao huwa wanakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa. Vijana hawa wanafanyakazi nzuri sana na vilevile Mwenge wa Uhuru kukimbizwa kwake umeleta manufaa makubwa sana katika nchi yetu kwa sababu kila Halmashauri hujitahidi kuibua miradi ya maendeleo ambayo ina maslahi na wananchi wake ili mwenge wa uhuru unapopita iifungue ama kuweka jiwe la msingi, jambo ambalo ni jema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la kusikitisha hapa ni kwamba, vijana hawa wanaokimbiza Mwenge wa Uhuru ambao huwa ni vijana sita tu, tunasahau maslahi yao. Pesa wanazopewa hazifanani kabisa na uzito wa kazi yao. Kazi yao ni nzito, wanabeba chombo chenye heshima na dhamana kubwa kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, lakini viposho wanavyopata ni vidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri alitazame jambo hili upya kabisa ili vijana hawa wapate heshima wanayostahili na kupata maslahi wanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia vijana wanaokimbiza Mwenge wa Uhuru, naomba nizungumzie juu ya Chama cha Wafanyakazi kinachojulikana kwa jina la *FIBUCA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, chama hiki kimetokana na chama cha *TWICO*, wamejiengua huko wakaamua kuanzisha chama chao na wafanyakazi hawa wanatoka kwenye taasisi za fedha, mabenki, viwanda na maeneo mengine mbalimbali na hata *DAWASCO, NSSF,* nao wako kwenye chama hiki cha *FIBUCA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, chama hiki bado hakijasajiliwa na kama chama hakijasajiliwa unategemea nini? Maslahi ya wafanyakazi hawa si yanakwenda bure? Maana wanajiendesha bila utaratibu. Nafahamu sasa hivi wana usajili wa muda, lakini usajili huu wa muda watafika nao wapi? Naomba sana Serikali ikae, itafakari ione namna ya kukisajili chombo hiki ambacho kimebeba wafanyakazi wengi, maana chama hiki kikijiendea hovyo hovyo ndiyo matokeo yake itafika mahali mgogoro unaanza, pesa zitaliwa, wataanza kudhulumiana, wataanza kudaiana, nidhamu ya kazi itapotea kwa sababu chama bado hakina msimamo mzuri na msimamo mzuri wa chama hiki ni kuwa na usajili wa kudumu. Kwa hiyo, chama hiki kikisajiliwa kitawasaidia sana, hawa wafanyakazi kujiona na wao wana chombo kizuri, chombo ambacho kinatetea maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nimwombe Mheshimiwa Dau aje Singida, nimeshamsikia sana kwenye Mikoa ya wenzetu, Mwanza, Kagera, tena Kagera ambako ni mbali, ndugu yangu Dau umeshafika, Singida ambayo iko karibu hapa hapa unairuka tu. Tunaomba aje sasa awekeze Singida, maendeleo ya mahali popote ni pamoja na majengo, Singida tunahitaji maendeleo. Mkuu wa Mkoa amejipanga vizuri, anahitaji majengo ya kisasa, tunahitaji soko la kisasa, karibu Singida, aje awekeze tutampa ushirikiano, wala hatapata shida na ardhi iko tele Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutamshukuru sana akija Singida kwa sababu na sisi Wanasingida ni wadau wako, kama ni wafanyakazi Singida wako, aje awekeze Singida na akifanya hivyo atakuwa ametusaidia sana ndugu yangu kama alivyofanya Mwanza, kama alivyofanya Mbeya, kama alivyofanya Dar es Salaam na maeneo mengine. Singida katika mikoa yote unaambiwa ni mkoa wa kwanza kwa umaskini, tunajisikia vibaya kutajwa hivyo lakini akifika na yeye huko, atakuwa ametunusuru ndugu yetu. Hivyo, tunamwomba aje Singida ajenge nyumba za kuishi za kupanga wafanyakazi kwa gharama nafuu pamoja na kukopeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana, naomba nitumie nafasi ya mwisho kwa kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sasa nitamwita msemaji wa mwisho katika orodha yangu, Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwa uchache hotuba ya Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze tu kwa kuzungumzia suala zima la elimu kwa sababu imekuwa ni kama ada, Waheshimiwa wenzetu wakisimama na kujivunia ujenzi mzima wa madarasa kitu ambacho ni kizuri kabisa. Lakini nilikuwa nadhani kwamba ni muhimu kwenda zaidi ya madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ripoti kadhaa na ukiangalia ripoti ya MKUKUTA hasa katika suala zima la elimu unaona kwamba *enrolment* siyo mbaya, wanafunzi wanaoingia darasa la saba ni asilimia 97.3, ukija kwa watu ambao wanamaliza darasa la saba inashuka mpaka asilimia sabini na nane, ukija kuangalia vijana wetu ambao wanafaulu darasa la saba ni asilimia sabini, watu ambao wanaingia sekondari kwa sababu tunapozungumzia suala zima la elimu sitegemei kwamba, tunazungumzia watu ambao wameishia darasa la saba au la pili au darasa la kwanza. Tunazungumzia elimu katika *level* ya sekondari mpaka Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *enrolment* ya shule za sekondari ni asilimia ishirini tu, watu ambao wanafaulu *form four* ni asilimia thelathini na tano ya ile asilimia ishirini, watu ambao wanaingia Chuo Kikuu ni robo ya ile asilimia thelathini na tano. Kwa hiyo, nadhani badala ya ndugu zangu kukaa na kujisifu kwa dhati kwa madarasa, ni muhimu pia tuangalie ni *mechanism* gani tutatumia ili tuweze kuhakikisha kwamba watu ambao wanaingia sekondari na watu ambao wanaingia Vyuo Vikuu idadi yao inaongezeka, kwa sababu katika *generation* ya sasa hivi hatuangalii mtu wa darasa la saba wala hatuangalii majengo yasiyokuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika suala zima la sera ya vijana, nakumbuka nilivyoingia Bungeni mwanzoni kabisa, niliuliza swali na nakumbuka Mheshimiwa Nsanzugwanko ndiye aliyenijibu na swali lilikuwa linahusu Baraza la Vijana, nikaambiwa mchakato unaendelea Baraza la Vijana litaundwa. Baraza la Vijana limekuwa historia mpaka sasa hivi hakuna baraza la vijana na hatujui hali ikoje. *Actually experience* inaonesha kwamba, hata kukiwa kuna michakato mizima ya kuanzisha hili baraza watu wanafikiria kwamba vijana wanapatikana Chama cha Mapinduzi peke yake *which is very wrong.* Vijana ni watu ambao wapo kwenye vyama na wengine hawako kwenye vyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kama kuna mchakato wowote ambao utapelekea kuundwa baraza la vijana, hasa ukizingatia kwamba kuna sera mpya ya maendeleo ya vijana ambayo ilizinduliwa na Mheshimiwa Chiligati, ni muhimu kuwepo na ujumuisho wa vijana kutoka katika sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo hiki cha kuchagua baadhi ya vijana inapelekea kwamba, vile vitu ambavyo hiki kikundi cha vijana kimechaguliwa kwa ajili ya kufanya utafiti wanavielezea kama matatizo ya vijana, vinakuwa haviendani na uhalisia kule chini. Kwa mfano, ukiangalia kwenye sera mpya ya vijana ya mwaka 2008, unaona

kwamba vitu ambavyo wanavielezea kama ni matatizo ya vijana, ni masuala ya afya, kutumia madawa ya kulevya na kadhalika.  Lakini hii sera haizungumzii kabisa kwa takwimu ni kwa kiasi gani vijana hali zao kiuchumi zikoje na nina uhakika hata leo nikimuuliza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya vijana aniambie *status* ya vijana wa Kitanzania ikoje kiuchumi, sijui kama jibu lake linaweza likawa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia taarifa ya maoni ya watu ambayo ilitolewa na Serikali mwaka jana, ina tofauti na kilichobainishwa katika sera ya vijana.  *Policy* ya vijana inaonesha kwamba, matatizo ya msingi ya vijana ni afya na vitu kadhaa vinavyoendana na hayo.  Vijana katika utafiti wao ambao ulifanywa kwa kuwahoji vijana wa kawaida mtaani unaonesha kwamba, tatizo lao la msingi ni kutafuta kazi ama kupata kazi na tatizo la msingi hasa kwa vijana ambao wametoka vijijini ni suala zima la maji hasa ukizingatia kwamba, usambazaji wa maji haujafanikiwa kama ambavyo ilitakiwa iwe.  (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sera ya vijana haijazungumzia maji kabisa kama sehemu ya tatizo la vijana ambalo Serikali inatakiwa ilizungumzie ili kuweza kutatuliwa.  Kwa hiyo, kuna matatizo ya msingi ambayo tunatakiwa tukiwa tunafanya hizi tafiti zetu ambazo zina malengo ya kuunda vyombo maalum kwa ajili ya vijana, tuhusishe makundi yote pasipo kujali itikadi wala mambo mengine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la ajira kwa vijana ni nyeti sana na ukiangalia kwenye malengo ya MKUKUTA ambayo pia yameingizwa kwenye ilani ya CCM inaonesha kabisa kwamba, lengo la mwaka 2010 ni kupunguza asilimia ya ukosefu wa ajira kutoka kumi na mbili mpaka asilimia sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Waziri ametueleza jinsi ambavyo alifanikiwa kutengeneza hizo ajira ambazo amesema milioni moja na pointi kadhaa na amevuka lengo.  Lakini nadhani ni muhimu pia angetuambia haya malengo ya MKUKUTA ambayo yamekuwa *incorporated* ndani ya Ilani ya CCM ya kushusha upungufu wa ajira kutoka asilimia kumi na mbili mpaka asilimia sita kwa mwaka 2010 yatatekelezeka ama hayatekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalizungumza hili kwa sababu ukiangalia kwa mfano, ile ripoti ya nguvu kazi ambayo ya mwisho ni ya mwaka 2006, inaonesha bayana kwamba, katika watu milioni 18.8 ambao wana uwezo wa kufanya kazi katika *population* nzima ya Tanzania ambayo sasa hivi nadhani inakaribia milioni arobaini asilimia sitini na tano ni vijana. Sasa unapokuwa na asilimia sitini na tano ya vijana katika watu ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa, halafu unakuta hao hao vijana asilimia kubwa hawana ajira *then* kuna masuala ambayo ni muhimu kuyaangalia. Hali kadhalika ukiangalia ripoti hii unakuta kwamba, asilimia themanini ya hiyo asilimia sitini na tano ya vijana ni wafanyabiashara wadogo wadogo, watu waliojiajiri au watu ambao wanafanyakazi ambazo hazina ujira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani ni muhimu wakati tunapotoa takwimu zetu za suala zima la ajira, tuweze kuchanganua ili ijulikane waliojiajiri ni wangapi ili Serikali ijue itatoa *support* kiasi gani. Watu ambao wako nyumbani wanafanyakazi hawalipwi, ambao inakuwa *termed* kama ajira ni kiasi gani na watu waliojiajiri wenyewe ni kiasi gani ili hata wakati tunapangilia mipango yetu tuweze kujua ni kwa kiasi gani tunaelekeza nguvu katika hayo maeneo hasa ukizingatia kwamba, wanatengeneza asilimia themanini ya watu ambao hawana ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye *NSSF*. Mama Chilolo amezungumzia kwa uchache na kumwomba Mkurugenzi Dau aende Singida, labda amjengee na yeye vitega uchumi ili maendeleo yaweze kupatikana Singida. Hali kadhalika nitoe pongezi kwa Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii kwa kazi inayofanya hasa ukizingatia hiki Chuo chetu Kikuu cha Dodoma na bila Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, hiki Chuo tunachokiona kinamea kama uyoga kisingekuwepo hapo. Lakini vilevile lazima ieleweke kwamba, tunapochukua fedha kutoka kwenye mifuko hii ya hifadhi ya jamii ambayo mama zetu, baba zetu, kaka zetu wanaweka akiba zao pale, tuna jukumu la kurudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonesha kwamba madeni mengi yanayokopwa *NSSF*, *PSPF* yanakuwa ni magumu sana kurudishwa. Nitatoa mifano, kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* inaonesha kwamba karibia shilingi bilioni hamsini na nane ambazo wamekopeshwa watu binafsi hazijarudishwa. Natarajia Waziri akija hapa atueleze kuna mikakati gani ya hizi fedha kurudi kwa sababu *observation* ya *CAG* inaonesha kabisa kwamba, menejimenti imejitahidi haiwezi kurudishwa. Kwa hiyo, pia inanifanya nijihoji juu ya uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji sasa kama Mkurugenzi Mtendaji anashindwa kukusanya madeni na pesa zinaendelea kutolewa *then* hapo kunakuwa kuna tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, ni muhimu tujiangalie ili tujue tunaweza kufanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 127 wa ripoti ya *CAG*, inazungumzia juu ya suala zima la ununuzi wenye kutia shaka wa huduma za ulinzi. Kama utaniruhusu naomba kunukuu, inaonesha kwamba, taarifa za uchunguzi zilizofanywa na idara ya ulinzi na kusainiwa na Mkuu wa Idara hiyo *Chief Security Manager*, ilitoa maoni ambayo ni tofauti na yaliyotolewa na Kamati ya kutathmini. Inasema, zabuni za kutumia vigezo tofauti na kuteua kampuni ya ulinzi ya *alliance day and nights security guard limited*, yenye Sanduku la Posta 305, Tabora, kutoa huduma za ulinzi katika maeneo ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Mwanga, Same na Tarakea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Kazi anatokea Tabora, ukiangalia hii taarifa sijasema kwamba hii kampuni ni ya kwake, inaweza ikawa ni ya kwake ama si ya kwake, ama ni ya jamaa yake, ama ni ya wapiga kura wake. Lakini unapokuwa na Waziri mwenye dhamana na wakati huo huo unakuta amepewa kazi za ulinzi Arusha ofisi mbili, Kilimanjaro ofisi tano, Tabora maeneo mawili afadhali hata ingekuwa Tabora peke yake, Dodoma maeneo mawili, Singida maeneo mawili, sasa unajiuliza hapa kwa namna moja ama nyingine kunaweza kukawa kuna mgongano wa maslahi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana asiwepo moja kwa moja lakini kwa tafsiri ya kawaida Waziri mwenye dhamana ya chombo hiki, kampuni kutoka Tabora Mkoa wake inapata tenda kwenye maeneo mengine siyo ndani ya Mkoa wake na tathmini za *CAG* zinaonesha kwanza *performance* ya hiyo kampuni ni *very poor,* inafanya watu tujiulize maswali kwamba hiki ni kitu halali au siyo kitu halali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ripoti ya *CAG* inazungumzia suala zima la....

**NAIBU SPIKA:** Kampuni jina lake hukusema, hatukusikia sisi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kampuni jina lake inaitwa *Alliance Day and Night Security Guard Limited* yenye Sanduku la Posta 305, Tabora kutoa huduma za ulinzi maeneo ya Arusha, Kilimanjaro, Tabora, Dodoma, Mwanga, Same na Tarakea. Kwa hiyo, hili nadhani Mheshimiwa Waziri tu anisaidie ili ku-*clear doubt* kwamba *how come* Tabora na *how come* inapata na maeneo mengine wakati ukizingatia *capacity* yake ya ku-*perform* ni mbovu na kama hakuna suala zima la *conflict of interests.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija tena kwenye ukurasa wa 154, kuna mauzo ya majengo yaliyokuwa ya *NSSF*. Hapa tunaambiwa kwenye ukurasa 154 kwamba kuna Kampuni ya *MS Tiles Fresh* iliuziwa jengo ambalo liko *Club Oasis*. Sasa unaambiwa Kampuni ya *MS Tiles Fresh* ilisajiliwa tarehe 22 Desemba, 2004 siku ambayo Bodi ya Wakurugenzi iliidhinisha kuuzwa kwa majengo hayo. Tuliona kwenye kesi za *EPA* mambo yalivyokuwa, kampuni zilikuwa zinatengenezwa *faster faster* kwa malengo ya ku-*achieve* kitu fulani. Sasa unapokuwa na Kampuni kama hii mpya imeundwa siku ambayo mkataba umesainiwa kwa ajili ya kuidhinisha mauzo halafu Kampuni hiyo hiyo inasajiliwa siku hiyo hiyo, halafu inakwenda inapewa hiyo kazi hapo kuna maswali ambayo nadhani Waziri wa Kazi anatakiwa aje atujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye ukurasa wa 149 wa ripoti ya *CAG*. Inaonyesha kwamba kulikuwa kuna zabuni zilizopewa kwa ajili ya mauzo ya majengo ya *NSSF* yaliyokuwepo Ada *Estate*. Ukiangalia kwa makini unakuta kwamba baada ya watu kuanza kuchunguza walipokwenda kwa madhumuni ya kudai nyaraka wakaambiwa kwamba nyaraka zote za zabuni zilizowasilishwa hazikuweza kusomeka kwa sababu zimeharibiwa na maji, hivyo taarifa muhimu kama vile majina ya zabuni na bei zao hazikupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika kama *NSSF* kweli hakuna makabati ya kuweza kuhifadhi *documents*, hadi *documents* zinalowana. Watu wa *CAG* wanakwenda kutaka kukagua hawazioni. Sasa unakuta kuna vitu kama hivi ambavyo vinatakiwa viangaliwe. Nashauri badala ya kukaa hapa na kusifiasifia ni kweli kwamba *NSSF* wamefanya kazi nzuri lakini kuna vitu vidogo vidogo ambavyo inabidi tuviangalie kwa sababu hili Shirika letu linaweza likageuka *DECI*. Hatuwezi kuwa tunaingiza fedha au tunatoa fedha zinapotea au tunafanya vitu vya ajabu ajabu matokeo yake mababa zetu, babu zetu na wajukuu zetu watakuja kushindwa kupata…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa*

*kuzungumza Mheshimiwa Mbunge)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana - Mheshimiwa Profesa J. Kapuya, Naibu wake - Mheshimiwa Dr. Miltoni Makongoro, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara na Taasisi zake kwa hotuba nzuri na kazi nzuri kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo sugu la machinga wa kigeni wanaokosesha ajira vijana wetu likomeshwe kwa utafiti na mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kuna umuhimu mkubwa kuwa na mpango kamambe sio tu wa kutotoa vibali vya kazi kwa wasiostahili bali kuwa na utaratibu rasmi wa kuwabaini na kuwa na ratiba rasmi za kuwaondoa *(Phase out)* wafanyakazi wasiostahili ikiandamana na programu ya mafunzo kwa wafanyakazi na wajasiriamali wa Tanzania wanatarajiwa kuchukua nafasi za wageni wanaotazamiwa kuondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezashaji wa wajasiriamali bado haujawa katika kiwango kinachotarajiwa. Kwanza walengwa wengi hususan vijijini hawafikiwi na badala yake wajanja wachache mijini ndio wamekuwa wakifaidika. Pili, benki ambazo zimekabidhiwa jukumu hili (*NMB* na *CRDB*) na pia *SCULT* bado zinafanya kazi hii kwa urasimu mkubwa na kuwasumbua sana wananchi wanaohitaji mikopo hata kwa wale walio na ufahamu mzuri na kufuata masharti yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja kubwa ya kupunguza urasimu, kulegeza zaidi masharti pamoja na kuikubali hati ya kimila kama dhamana. Aidha, zaidi ya Benki ya Akina Mama na Benki ya Kilimo kutarajiwa kuhudumia wajasiriamali wadogo na wa kati, ipo haja ya kupanua mfuko na wigo wa mikopo kwa kuhusisha taasisi nyingine zenye uzoefu mkubwa na mtandao mpana kama vile *SIDO* kushiriki katika mfuko wa mabilioni ya Mheshimiwa Rais (mabilion ya JK) na mifuko mingine. Aidha, kwa kushirikiana na HAZINA na VIWANDA, utazamwe uwezekano wa kuanzisha *Venture Capital Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja ya kulitumia ipasavyo Shirika la Taifa la Tija *(NIP)* katika kutoa mafunzo na mbinu za kuongeza tija ili uzalishaji nchini Tanzania uwe wa tija na ufanisi zaidi kuiwezesha nchi yetu kuzalisha bidhaa bora na kuhimili ushindani mkali katika zama hizi za utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ARCH. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana - Prof. Kapuya, Mheshimiwa Naibu Waziri - Dr. Miltoni Makongoro, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote hapo Wizarani kwa kutuletea hotuba nzuri na yenye mwelekeo wa kutia matumaini. Hongereni sana. Pia niwapongeze kwa kuitekeleza Ilani ya CCM kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Tunaishauri Serikali kupitia Wizara hii kukomesha ajira kwa watoto na badala yake wapewe fursa ya kuendelea na masomo. Inasikitisha sana kuona hata ajira ambazo Watanzania (wazawa) wanaziweza sana zinachukuliwa na wageni kwa njia mbalimbali za udanganyifu. Ninapendekeza hali hii ikomeshwe mara moja na kuweka udhibiti mkubwa zaidi na wa kudumu.

Ninashauri Serikali kutoa mwongozo kuhusu kima cha chini cha mishahara kwa wafanyakazi hasa wa Viwandani kwa mfano Kiwanda cha Nguo cha Urafiki.

Shirika la Taifa la Tija (*NIP*) halijatumika vya kutosha katika kuongeza tija hapa nchini kwenye kutoa mafunzo, ushauri, uelekezi na utafiti jambo linalofanya maendeleo ya nchi kuwa kidogo. Ninashauri hili shirika liboreshwe zaidi ili liweze kufahamika vizuri na ikiwezekana iwe ni lazima wafanyakazi wa Serikali kupata mafunzo kupitia shirika hili.

Ni muhimu sana kuyaangalia mashirika yetu ya hifadhi za jamii hasa kwa malalamiko mengi yaliyopo, mfano malipo kwa wanachama, uwekezaji ulio makini, matumizi bora ya rasilimali zake na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWAJUMA H. KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kuamka nikiwa mzima. Pia nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika, pamoja na wenyeviti wote kwa jitihada zenu kwa kutuongoza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba nielekee kutoa mchango wangu katika Wizara husika. Kwa kuanzia, natoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri Kapuya na Naibu wake Mheshimiwa Makongoro kwa hotuba yao iliojaa busara, hekima ili wafanikishe azma yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, neno ajira liko katika maeneo matatu katika nchi yetu. Kuna ajira ya Serikali, ajira binafsi na ajira za sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, iliahidi ajira milioni moja kwa Watanzania wetu. Ni vyema basi Serikali inijulishe katika ajira hizo ni wanawake wangapi walioajiriwa katika ahadi hizo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira binafsi, vijana wetu walio wengi wanajiajiri wenyewe. Kwa nini vijana wetu pale wanapojiajiri wapelekewe mgambo kuwanyanyasa na kuwapiga, kuwachukulia mali zao na mara nyingine huwatia ndani. Hivyo, Serikali haioni huruma kwa vijana wetu hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira za watoto majumbani, ongezeko la ajira za watoto majumbani zinasababisha watoto wetu kukosa elimu. Hivyo, Serikali ina mikakati gani kwa watoto hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa katika nchi yetu. Sekta binafsi hasa zile za wageni zinawakosesha vijana wetu ajira. Walio wengi huja na watu wao mikononi na kuwapa ajira katika kazi zao, kwa nini Serikali haina sheria kuzuia utaratibu huo? Hivyo, ni kweli Serikali inawahurumia vijana wetu. Natumai Serikali itakuwa sikivu kwa kuweza kuwapatia ajira Watanzania wetu. Ahsante.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Juma Kapuya pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mahanga. Pili, napenda kusema kuwa wafanyakazi wa Tanzania ni watu wenye kujituma sana na hata nchi jirani kupenda kuajiri wafanyakazi toka Tanzania.

Mfano, madereva kutoka Tanzania kufanya kazi Burundi, huu ni ukweli kwamba Watanzania wanao uwezo, nguvu na ari ya kufanya kazi kwa bidii. Hivyo basi, naiomba Serikali kufuatilia hasa makampuni binafsi. Kwani katika bajeti yako ya mwaka 2008/2009 nilichangia kuhusu vijana wa *Vicfish* jinsi ambavyo walinyanyaswa na aliniahidi atapita na tutatue hili.

Pia, aliniahidi atanijulisha ni lini angekuwa Mwanza ili tutembelee kiwandani na kuwasikiliza wadhulumiwa wa kiwanda hicho, lakini hakuniarifu na sikujua ni nini kiliendelea. Hivyo basi, wakati wa majumuisho unifahamishe haki za wafanyakazi ambao niliwaongelea na ahadi aliyonipa ilifikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia makampuni ya ulinzi ni mengi ambayo hutoa mshahara mdogo na mingi iko chini ya mshahara kima cha chini. Hivyo basi, Wizara hii ni muhimu ikatoa kauli kuhusu mishahara na isiwe chini ya kima cha chini na pia kuliwekea mkazo na kuwachukulia hatua wale wote ambao wakikiuka sheria hiyo. Itakuwa vizuri na wafanyakazi hao tukawajali kama nao ni Watanzania wenye familia ambazo zinahitaji kuhudumiwa.

Pia ni vizuri tukajua Watanzania hawana nafasi katika nchi za wenzetu kama wanaweza kufanya kazi za umachinga. Cha ajabu, hapa Tanzania tumekuwa na kasumba ya kuwathamini sana watu kutoka nchi za nje na hata kuwaachia kufanya kazi kama za

umachinga, tunaona hapo Kariakoo, Wachina wanauza mitumba na maua ya reja reja au huu ndiyo uwekezaji, tuwekeze viwanda hata umachinga nao.

Ni vizuri kazi za kimachinga zifanywe na Watanzania na zifanywe bila kusumbuliwa, kwani hawa Wachina ambavyo hawasumbuliwi. Pia Waziri kaongelea mikopo ya *SACCOS*, ni ukweli usiopingika kuwa mikopo hiyo inatolewa kisiasa, kwani kijana kujiunga naambiwa mpaka awe mwanachama wa chama fulani. Kwa sababu ukisema utatoa kwa vijana, ni vijana wapi? Sababu hatuna vijana wa kitaifa katika Wilaya, ila tuna vijana wa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tazama vijana ambao hukimbiza Mwenge huwa ni vijana kutoka kitengo gani? Kwani hatujawahi kuona vyama kushirikishwa katika kupelekwa vijana katika kukimbiza Mwenge huo. Husikia ni kijana wa chama Fulani! Ni wazi kuwa baadhi ya vijana wanakwazwa na itikadi zao za vyama. Tuwe wakweli, pia tuwe na kutambua vijana na kuona vijana wote ni sawa na kutojali itikadi zao. Naiomba sana Wizara hii ipitie sana makampuni binafsi hasa ya ulinzi katika mishahara yao, kwani maisha yao ni tata na mishahara yao hairidhishi kabisa. Ahsante.

**MHE. FATMA OTHMANI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia kuhusu vijana. Mpaka hivi sasa vijana wetu wengi bado wapo mitaani wakikaa kwenye vigenge na kuvuta unga na mabangi na kubwa ni kwamba hawana kazi wala biashara za kufanya, kwani biashara nyingi ndogo ndogo ambazo zilikuwa zifanywe na hawa vijana wetu leo, nyingi tu zinafanywa na wafanyabiashara kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

Natumaini Wizara italiingilia kati suala hili kwa kupanga mpango mzuri tu ili hawa vijana wetu wafanye biashara na hawa ndugu zetu wa Kichina na wao wangeuza kwa jumla sio kama vile wanavyouza pale Kariakoo. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri: Je, lile jumba la wamachinga ni mpaka lini watakabidhiwa wamachinga wenyewe? Kwani ni muda umeshakuwa mrefu. Naomba hebu ufanywe utaratibu kabla ya mwaka 2010 liwe tayari washapatiwa hawa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, daraja la Kigamboni limekwama wapi? Mbona kimya kikubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNA R. LEPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana wengi wamehamasishwa katika maeneo yao kujiunga na *SACCOS*, lakini hakuna matunda yoyote katika maeneo yao. Mabenki kama *NMB*, *CRDB* hawakopeshi kijana mmoja mmoja, inakuwa shida sana. Tunaomba Serikali ichukue hatua ya haraka ili vijana wafaidike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanawake wengi hawajawahi kupata mkopo hususani wajasiriamali wadogo wadogo, tunaomba Serikali iwasaidie wanawake hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze *NSSF* kwa kazi nzuri ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Ni kazi nzuri sana, pia nyumba za Polisi barabara ya *Kilwa Road*. Pia tunaomba jitihada za Daraja la Kigamboni ziongezeke zaidi.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Naibu Waziri Mheshimiwa Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya kutekeleza Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nchi yetu imeingiliwa na wageni wengi wakifanya kazi katika mahoteli makubwa na madogo, ujenzi wa majengo, barabara na kadhalika: Je, Serikali imeshafuatilia na kubaini kama wageni hao wana vibali halali kuwaruhusu kufanya kazi nchini? Je, kazi wanazozifanya Watanzania hawana ujuzi nazo? Serikali haioni ni kuwanyima Watanzania fursa ya kupata ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, wageni hao wanauza maua, vyombo vya nyumbani: Je, huu ndio uwekezaji tunaouhitaji Watanzania? Watanzania wanataka kuelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya mwisho vibali vya wageni wanaofanya kazi nchini vilikaguliwa lini au wanaishi wanavyotaka? Naomba kujua kama biashara wanazofanya ndio walizoombea leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuathirika kwa uchumi duniani, Watanzania tutaguswa na kuyumba kwa uchumi duniani wakulima, wafanyabiashara na wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfanyakazi amefikiriwa vipi na Serikali yetu ili aweze kumudu maisha yake ya kila siku? Maisha yamepanda kwa kiasi kikubwa, mshahara wa mfanyakazi uko pale pale. Je, tunawatakia mema wafanyakazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza sana Shirika la *NSSF* kwa kazi kubwa sana ya kuendeleza nchi yetu. Nawapongeza kwa kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi wa nyumba za Polisi, ujenzi wa jengo la Ofisi ya *PCCB* – Dar es Salaam, ujenzi wa nyumba za bei nafuu Kigamboni na kadhalika. Kwa kweli *NSSF* ni Shirika la mfano kwa uendelezaji wa nchi yetu. Nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu Dr. Ramadhani Dau pamoja na watendaji wote wa Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwawezesha vijana wanaoishi mijini na kuwasahau waishio vijijini sio suluhisho la tatizo la vijana. Nashauri vijana wawezeshwe vijijini huko huko waliko kwa kuwasaidia kupata vifaa vya kazi, kilimo na kadhalika, hawatakimbilia mijini tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wanakimbilia mijini kwa sababu hakuna miundombinu vijijini, hakuna vitendea kazi, wakiwezeshwa huko waliko hatutawaona mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na tukaweza kujadili hotuba hii ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru na kuwapongeza wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuleta tija kwa wafanyakazi wa Taifa letu

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifuko ya jamii, naipongeza sana mifuko ya Hifadhi kwa kazi nzuri wanazofanya za kuiokoa nchi kwa miradi mingi iliyowekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ni ya kimaendeleo inayotumia fedha za ndani. Naiomba Serikali kuongeza miradi zaidi kwa kutumia mifuko hii ya kizalendo na kuipa kila misaada mifuko hii ili kufanya kazi zake kwa uhakika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Kigamboni limetajwa katika Ilani ya Chama Tawala (CCM), lakini utekelezaji wake unakwenda taratibu sana na ujenzi wake uko kwenye maofisi na makabrasha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafsi yangu nina wasi wasi na utekelezaji wake. Naona unapigwa dana dana na kusababisha kejeli na dharau kwa wapinzani wetu mitaani na kujitapa jimbo hilo watalichukua mwaka 2010 kwa kutotekeleza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kuchukua hatua za mwanzo za ujenzi ili wananchi wajue kuwa suala hilo lipo, kabla ya uchaguzi mkuu mwaka 2010. Pia ninamwomba Waziri kulitolea ufanunuzi suala hilo kupitia Bunge lako Tukufu ili wananchi waelewe ni lini ujenzi utaanza na kikwazo gani kilichocheleweshа ujenzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kuwasilisha mchango huu katika Bunge hili. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa hotuba yake iliyolenga utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji pamoja na wataalamu wa Wizara kutokana na juhudi zao za kazi ikiwa ni mwendelezo wa kulipatia maendeleo Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya vijana, katika jamii mbalimbali hasa zile zilizopo vijijini, vijana wengi wapo katika hali ngumu sana ya kimapato

kutokuwa na miradi inayoeleweka, matokeo yake kuwepo na kundi kubwa la vijana kukimbilia mijini na kujiingiza katika masuala ya ujambazi, uhalifu, wavuta unga na wabakaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali hii kuiwezesha kimapato Wizara hii katika kutekeleza jukumu la kuwafikia vijana walio wengi vijijini na kuwapa elimu na kuwahamasisha kujiunga na vikundi mbalimbali vya ujasiriamali na kuwapatia mikopo yenye uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yametokana na uwezo mdogo wa Wizara kuwafikia vijana kwa wale waliopo mijini na vijijini. Serikali iangalie kwa kina namna ya kuongeza fedha za kutosha katika kipengele cha kuwafikia vijana wasiokuwa na kazi kwa madhumuni ya kuwapatia elimu na kuwapatia maendeleo mema katika Taifa letu kwani vijana ndio tegemeo la baadaye lazima uamsho uwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Serikali huwa inajitahidi kutoa fedha za mikopo kwa lengo la kuwaendeleza wananchi katika masuala ya ujasiriamali. Pia kuna baadhi ya wajasiriamali huamua kufanya biashara kwa kuangalia namna ya kuweza kurudisha fedha hizo kwa wakati ili wafaidike na wengine ambao kipindi walichopata wao walikuwepo wengine nyuma yao wanasubiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na urasimu mkubwa unaofanywa na mashirika yetu ya viwango *TBS* katika kutoa vibali kwa wajasiriamali pale wanapotaka kwenda kufanya biashara nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iweze kuliona kwa makini suala hili, pale inapothibitika tu kuwa biashara inayofanywa ni ya kiwango kinachohitajika bila kuwepo madhara kwa binadamu waweze kuwaona mapema wafanyabiashara hao kwani wakati mwingine biashara zinakuwa za msimu, kufanya haraka kutoa nyaraka za ubora wa bidhaa muda muafaka, ni kuondoa malalamiko mengi yanayotokea kwa wafanyabiashara walio wengi na kuendelea kuwapa moyo katika biashara wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu waajiri wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao kisheria. Yapo baadhi ya makampuni ambayo wameajiri watumishi katika masharti ya muda na yale ya kudumu. Lakini inapotokea athari ya kuumia kazini mwajiriwa, wanakuwa wanawasumbua sana hata kukata tama na mwisho kuamua kurudi nyumbani.

Naiomba Serikali iwaangalie sana waajiri hawa ambao hawawatendei haki wafanyakazi walionao, malalamiko yamekuwa ni mengi mno tunayoletewa kama Wabunge wakiwa na matumaini ya kutaka kupatiwa msaada wa kuona kuwa mwajiri huyo atachukuliwa hatua gani kutokana na udhalilishaji anaoufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sheria zitumike za kuwawajibisha waajiri wasiotimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya usuluhishi na maamuzi nchini, naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza fedha za kutosha katika fungu hili. Ili iweze kuwa na watumishi wa kutosha katika Taasisi ya Tume hii na kuweze kutatua migogoro inayotokea kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchache wa watumishi unachangia kuwepo na mlundikano wa migogoro kazini inatakiwa kila Wilaya kuwa na mwakilishi anayeshughulikia masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa Ofisi pia unachangia uwasilishaji wa malalamiko ya wafanyakazi na waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukosefu wa vitendea kazi vya kutosha inaathiri juhudi za kutatua migogoro inayotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakapoongeza fungu la kutosha katika Tume hii pia elimu ya sheria mpya za kazi zinazotakiwa kutendeka kwa waajiri na waajiriwa itaweza kufikiwa kwa waajiri wote kutokana na kuwepo uhakika wa usafiri wa zana bora za kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uchelewashwaji wa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kutokufika kwa wakati. Serikali ifuatilie kwa makini sana suala hili kwani huwa inaathiri utendaji kazi ndani ya Wizara kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wasiotimiza wajibu wao kisheria ni hatua zipi zinaweza kuchukuliwa dhidi ya wafanyakazi wa aina hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la UKIMWI sehemu za kazi katika hatua tuliyofikia sasa, tunaipongeza Serikali na Wizara kwa kuweza kuwatunza waathirika na UKIMWI sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuwangalia waathirika walioko vijijini ili nao tuweze kuwatunza kwa kuwapatia chakula, dawa na virutubisho, hasa wale wasiokuwa na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ni kazi tu bora imewezesha anayeifanya apate kipato cha haki kutokana na kazi hiyo, lakini swali la kumwuliza Mheshimiwa Waziri, hao wanaozifanya kazi hizi wanaandaliwa vipi? Hapo awali vijana wengi waliokuwa wakisoma shule za msingi walikuwa na somo la ufundi kwa vitendo na hivyo shule iliyokuwa ya ufundi ilikuwa na vifaa ambavyo vilisaidia kuwafundisha vijana wetu mazoezi ya vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya vijana hawa kumaliza masomo yao ya elimu ya msingi, wanajikuta wamejifunza aina mbalimbali za kazi za mikono kutokana na

elimu yao waliyopata shuleni.  Muda huu tulionao sasa hivi, shule za ufundi zimefutwa, hazipo kabisa na vifaa pia vilivyokuwepo vimekwishapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana ambao wanajisaidia kwa biashara zao ndogo ndogo, lakini cha kushangaza vijana hao wenye biashara zao wanapata wakati mgumu toka kwa mgambo hususani Jiji la Dar es Salaam.  Mgambo hawa wanawanyanyasa sana hawa vijana, wanawanyang'anya bidhaa zao, lakini huko zinakopelekwa hazijulikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze, hivi hawa mgambo shughuli zao ni kuwashughulikia tu vijana wafanyabiashara ndogo ndogo badala ya angalau kupitia Mitaani ambako kuna matatizo mbalimbali yanayojitokeza ambayo mgambo hao wangelisaidia Jeshi la Polisi mfano mwizi amekamatwa na akapata kipigo, basi mgambo angeweza kumhami mtu huyo wakati taratibu za kutafuta Polisi zikiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu nyingine wananchi wanaamua kujipangia maeneo kwa ajili ya biashara lakini mgambo hao hao huwanyanyasa kwa kuwafukuza sehemu hizo na wakati mwingine eneo lile wala halifanyiwi shughuli yoyote, panabakia yanaota majani.  Hii ni njia mbaya ya kuwapunguzia wananchi ajira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hawa wafanyakazi wanaoajiriwa katika sekta za watu binafsi, hawa nao wanadhalilika.  Utakuta mshahara wake anaoupata ni mdogo ukilinganisha na uzito wa kazi anayoifanya.  Natoa mfano, dereva anayeendesha lori la mizigo kwa Mhindi anapata Sh.48,000/=  na Mlinzi wa usiku anapata Sh.30,000/= - 45,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kumpa dereva wa lori lenye mzigo wa thamani ya Sh. 15,000,000/= au zaidi na akufikisha mzigo ule salama lakini unamlipa Sh. 48,000/= kwa mwezi.  Namwomba Mheshimiwa Waziri hili alitolee ufafanuzi ni lini hawa watapata mshahara angalau ukawasaidia kujikimu?  Hawa wanaoajiri wanalalamikia kuwa hawawezi kulipa mishahara ya kima cha chini kwa vile biashara zao hazilipi na ambapo sio ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mlinzi anayelinda ghala lenye mali ya Shilingi bilioni tano mpaka 20, lakini analipwa Sh. 45,000/= kwa mwezi na anafanya kazi hiyo katika mazingira magumu sana. Tunaiomba Wizara iwasaidie hawa watu wanaofanya kazi hususan kwa hawa jamaa zetu wenye asili ya Kiasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana ambao wanakaa tu katika maskani, vijana hawa kama wataandaliwa vizuri katika vikundi mbalimbali wakapewa mafunzo na baadaye wakawezeshwa kwa kupewa mikopo. Ni imani yangu kuwa vijana watafaidika na hatimaye wizi au ujambazi utapungua.

Namwomba Mheshimiwa Waziri hebu tuwasaidie vijana hawa kuwaandalia mpango mzuri wa kupatiwa mafunzo ambayo yatawawezesha kujiari wenyewe.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nashukuru kwa *Allah Subbhanah Waltaallah* kunijalia na kupata fursa kuchangia kwa maandishi hotuba hii ya bajeti ya Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Prof. Juma Athumani Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Makongoro Miltoni Mahanga, Katibu Mkuu wa Wizara hii na Watendaji wote wa Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa kutoa maoni kwa mambo yafuatayo ili kuzidisha ufanisi wa utendaji kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Nianzie na suala la ajira kwa vijana. Namwomba Waziri atoe maelezo kati ya zile ajira milioni moja zilizoahidiwa na Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005/2010, hadi sasa ni ajira ngapi zimepatikana na ajira hizi zimegusa sekta zipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira ni suala la Mtambuka katika hali ya sasa ya dunia hasa kulingana na hali ya mfumo wa uchumi wa maisha. Katika hili, Serikali ama taasisi zake peke yake haziwezi kukidhi na kuwezesha jamii yote kwa ujumla kupata kazi, hivyo suala la sekta binafsi ni mdau muhimu sana katika kutanua wigo wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri na faraja Waziri kwa niaba ya Serikali anatambua sekta binafsi ambazo kwa namna moja ama nyingine zimechangia sana katika sekta hii. Naomba nitambue na Mheshimiwa Waziri anatambua juhudi za makampuni kama *Mohamed Tanzania Enterprises Limited (METL), Said Salum Bhekressa Company Limited (SSB)* na mengine mengi ambayo yanachukua nafasi kubwa ya kutoa ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kuhusu wageni, ni muhimu Wizara ikazingatia uholela au namna ya sekta ya ajira binafsi iliyovamiwa na wageni wengi toka nje hasa wa jamii ya Kichina na kadhalika. Ni vyema Wizara ikaangalia namna ya utoaji ajira ama vibali kwa wageni vinavyohusu ajira ili kuondoa uholela uliopo sasa ambapo shughuli nyingi za kijasiriamali zimevamiwa na wageni hasa wa kijasiriamali, naomba zifanywe na wazawa wa nchi yetu na sio vyema kubinafsisha shughuli hizi kwa wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru Serikali hasa kwa juhudi ambazo imewezesha kuanzisha sekondari kila Kata, hivyo ni dhahiri vijana wengi sasa hawakimbilii mijini mara baada ya elimu ya msingi, naomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa mara nyingi vijana hawa hukosa shughuli maalum ya kufanya mara wamalizapo masomo ya sekondari *(form four)* zianzishwe *Youth Resource Centres* ambazo zitatoa mafunzo mbalimbali ili kuwajengea vijana maadili mema na kufanya kazi na hata kuipenda nchi yao kwa shughuli za kimaendeleo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kukipongeza Chama changu cha CCM hasa kwa utaratibu mzuri wa kutumia Jumuiya ya Vijana (UVCCM) kwa shughuli mbalimbali za kimaendeleo. Nampongeza sana Mwenyekiti wa UVCCM Taifa *Comrade* Masauni na Katibu Mkuu Martine Shigella kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kuwaunganisha vijana na naomba Waziri kupitia Serikali! Kutambua juhudi za UVCCM na wengine waige juhudi za UVCCM badala ya kujengea chuki miongoni mwa vijana na kuleta mifarakano kuchukia Taifa lao, kuchukia nchi yetu, kuchukia viongozi wao na kadhalika.

Naomba Wizara iwe macho na mtu ama vyama vya aina hii na kama upo uwezekano lazima Wizara ichunguze kwa ukaribu wa kanuni za Jumuiya hasa za vijana za vyama mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za ujasiriamali, maarufu kama mabilioni ya JK naomba takwimu juu ya vikundi vya ujasiariamali ama *SACCOS* zilizokopeshwe kwa Wilaya ya Iramba na ni mikopo ya jumla ya shilingi ngapi tangu kuanza kwa zoezi hili la uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenge wa Uhuru, shughuli hizi bado ni muhimu sana kujenga mshikamano Kitaifa, lakini shughuli hizi sasa zinaonekana ni za kulipwalipwa sana kwa kuwa Mwenge ni kuhamasisha shughuli za kimaendeleo sio vibaya kama Mwenge wa Uhuru uguse kila Jimbo na wala isiwe Kiwilaya jambo ambalo ni la jumla jumla sana, hii itabainisha miradi na kutoa hongera kijimbo na wala haitakuwa Kiwilaya, changamoto itakuwa kubwa sana na ari ya utendaji au ushiriki wa shughuli za kimaendeleo utakuwa mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote katika Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa suala la ajira katika nchi hii kwa ujumla, hasa ajira inayowagusa kundi kubwa la vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *'rate'* ya vijana kuja mijini ni kubwa sana na baada ya mwaka mmoja au miwili ijayo idadi ya vijana kuja mijini itaongezeka mara dufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itatokana na idadi kubwa ya wahitimu wa shule za sekondari za Kata ambazo zitafika kidato cha nne katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Wizara ikaanza kuainisha mipango mkakati wa kuanza kujiandaa na tatizo hilo linalokuja mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kilimo kimeanza kuwa cha kuvutia kwa maana matumizi ya jembe la mkono nafasi yake inachukuliwa na *“power tillers.”* Tukiunda vikundi vya vijana na kuwapatia nyenzo hizi za kilimo, vijana wengi watapenda kukaa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tunaomba ishirikiane na Wizara kama ya Kilimo, ili kuainisha maeneo ya kilimo kwa kila Mkoa, Wizara ya Ardhi pia ikihusishwa kwa ajili ya upimaji ardhi ili tuunde *‘Economic Groups’* za hao vijana kila Kijiji, Kata na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, pafanyike sensa ya idadi ya vijana ambao hawana kazi na idadi hii ijumlishwe na idadi ya wanafunzi watakaomaliza *Form IV* kwa ‘*assumption*’ kwamba asilimia 20 mpaka 30 tu ndiyo watakaoendelea na masomo.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mawazo yangu kuhusu hotuba ya Waziri mwenye dhamana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kusema kuwa baada ya kuagizwa katika Bunge kwenda kuhamasisha, vikundi ili kupata ajira, kazi hiyo ilifanyika. Tatizo kubwa lililojitokeza ni kwamba katika mgao wa fedha za JK kwa kuongeza ajira kwa vijana, hakuna hata senti moja iliyopelekwa Wilayani Kibondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimehamasisha vikundi 37 hadi sasa. Ninaomba kupata maelezo kamili, nini hatima ya vikundi hivi ambavyo ni vya vijana? Kiasi kilichopungua cha milioni tano cha kuwakopesha vijana hakitoshi. Ninashauri kiwango kiongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa vibali kwa wageni havizingatii sheria. Utaratibu wa kuwa na vibali kwa wageni na kuwaruhusu kufanya kazi kudhibitiwe kwa nchi nzima ili kuondoa wimbi la wageni haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja nikiwa nategemea kuwa wakati Waziri anahitimisha, atawapatia majibu ya kueleweka vijana ambao wamejiunga na vikundi kwa kutegemea mkopo kutoka Serikalini.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara kwa kufanya kazi nzuri hasa ya kukabiliana na migogoro ya kazi katika maeneo mbalimbali ili kudumisha amani na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia machache kama ifuatavyo:- Nimefarijika, kusikia kwamba ajira zimeongezeka kwa zaidi ya asilimia 27.2. Lakini la ziada ni mchakato wa Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Taifa ya Ajira kwa mategemeo kwamba sheria hii ijayo itafafanua mengi kupitia kanuni za jinsi ya kuzalisha ajira. Hivyo basi,

naomba sana kiwekwe wazi kipengele cha jinsi gani watu wenye ulemavu wataweza kupata ajira rasmi na isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa bado watu wenye ulemavu wanashindwa kupata ajira rasmi na isiyo rasmi hata kama wana elimu na vigezo. Ingawa katika sheria ya kazi 2004 imeweka mstari mmoja kwamba mtu asibaguliwe kwa sababu ya ulemavu wake, lakini hakuna kinachofanyika na waajiri na hata mifuko ya uwezeshaji tulionayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 10 wa hotuba, imeelezea juu ya kuhamasisha vijana kujiunga katika vikundi vya uzalishaji ili waweze kuwezeshwa kiuchumi. Katika hili nalo vijana wenye ulemavu wanaume na wanawake bado hatua za makusudi za kuwahamasisha hazijafanyika. Imekuwa ni kawaida kuwa katika ziara nilizofanya malalamiko ni kwamba kundi hili halikopeshwi. Hivyo, nashauri Wizara ikishirikiana na TAMISEMI watoe mwongozo mahsusi kwa Halmashauri ili wenye ulemavu nao waweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuwa iliwawezesha wajasiriamali 204 kushiriki Maonesho ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya Afrika Mashariki Kigali na kati ya hao washiriki kulikuwa na Mjasiriamali Fundi Kushoni, asiyeona ambaye ushiriki wake huo ulimsaidia kujitangaza na umempa ari zaidi ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 23, pongezi kwa Wizara kudhamiria kuwawezesha wananchi katika maeneo ya vijijini kupata mafunzo ili waweze kujiajiri na kuboresha ajira zao. Ninaloshauri tena ni kushirikiana na Halmashauri, ili wenye ulemavu nao wasisahauliwe katika mafunzo hayo kwani wao ndio maskini wa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA M. JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa hotuba hii ambayo imebeba dhima kubwa kwa nchi yetu ya kutengeneza mazingira mazuri na ya wazi ya kuwapatia vijana ajira endelevu na kulinda usalama na afya zao kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vita dhidi ya ajira ya mtoto, kulinda haki zao na kuwakinga na mazingira hatarishi ya kazi, naipongeza Wizara kwa kuendesha programu hiyo katika maeneo/Wilaya tano kati ya 18 naitakia mafanikio mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Wizara imekuwa na mkakati gani kwa watoto wadogo wanaotumikishwa majumbani na kunyimwa haki yao muhimu ya kupatiwa elimu na baya zaidi pengine katika nyumba hiyo yumo mtoto mdogo wa mwenye nyumba, lakini yeye anasoma skuli lakini wa mwenziwe kumfanya mtumishi na anamnyima haki

ya elimu? Je, hatua gani zinachukuliwa za kisheria kwa wanaowatumikisha watoto na kuwanyima haki zao, pamoja na wazazi wa watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usalama na afya sehemu za kazi ni muhimu sana, lakini taasisi iliyowekwa (OSHA) kusimamia ni vyema kutimiza wajibu wao kwa waajiri na waajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko kwa wafanyakazi wengi kutopatiwa haki yao muhimu kazini ya usalama wa afya zao na wanapowasilisha malalamiko yao, hakuna hatua yoyote ya haraka inayochukuliwa na wakati mwingine mwajiri analindwa na taasisi ya *(OSHA).*

Mfano Mgodi wa *TANZANITE* Mererani, wafanyakazi wa mgodi huo walifika mbele ya Kamati ya Nishati na Madini na kuelezea kilio chao cha jinsi gani ya udhalilishaji unaofanywa na mwajiri huyo kwa kutumia "mashine"yenye mionzi ya kuwachunguza kila siku na tayari wafanyakazi hao afya zao zimeanza kuathirika kwa kupoteza nguvu za kiume na wakaiomba Wizara iwasaidie. Pia walieleza wafanyakazi hao mashine hiyo hata wanapokwenda kutembelewa *(OSHA),* basi eneo hilo linafichwa halitembelewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, taasisi hii *(OSHA)* imejipanga vipi kuwakomboa wafanyakazi na unyanyasaji wa aina mbalimbali ili afya zao zisiathirike kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati wanafanya kazi nzuri na kweli wanakabiliana na changamoto nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Wizara ina mikakati gani kuwapunguzia gharama zisizo na ulazima? Mfano, malipo kwenye Halmashauri zao, malipo kwa Maafisa Misitu na kadhalika. Mfano huu ni wajasiriamali wa Mtwara kinamama wanaoshughulika na kusuka vikapu. (Malipo yanayotolewa kwa kikapu kimoja zaidi ya aina tatu). Ahsante.

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Kwanza kabisa, nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa hotuba yao nzuri ya bajeti iliyosomwa, ni nzuri na yenye ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Kituo cha Uwekezaji kwa kweli kituo hicho ni cha thamani sana, kinahitaji kupatiwa wataalamu zaidi na kuboreshwa na kufanyiwa utafiti na tathmini kwani ndio dira ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Baraza la Usuluhishi la Wafanyakazi nalo lipewe kipaumbele kupatiwa fedha zaidi za kujiendesha kwani linafanya kazi nzuri ya kutatua migogoro ya wafanayakazi kwani likiwezeshwa litaweza kujiwezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kazi nzuri wanazofanya katika kusaidia jamii hasa *NSSF* kwa kujenga makazi, Ofisi za

Serikali, kujenga jengo la Chuo Kikuu na kadhalika. Pia wazidi kubuni mbinu mbalimbali na hasa kusaidia vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iangalie suala la kuajiri maafisa vijana ngazi ya Wilaya ambapo itasaidia kujulikana na kuwa na mipango mizuri ya kupata ajira na mfuko wao wa vijana ukuzwe uweze kuteremka mpaka kwenye Kata na Vijiji. Vijana wenye ulemavu nao washirikishwe kikamilifu katika nyanja zote kwani na wao wakiwezeshwa wanaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya migomo kwa wafanyakazi kupitia vyama vyao kwani Wizara iwaelimishe viongozi wa vyama hivyo na wao watapata kuwaelimisha watu wao kwani migomo sio suluhisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitakia Wizara kila la kheri.

**MHE. ALHAJ DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma Kapuya, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana - Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga - Naibu Waziri, Bi. Kijakazi Mlengwa - Katibu Mkuu wa Wizara na wataalam wao wote kwa kazi nzuri ya kuandaa na kuwasilisha Bungeni kwa ufanisi hotuba ya makadirio ya 2009/2010.

Aidha, nawapongeza viongozi hawa na wataalam wote kwa kazi nzuri ya kutekeleza majukumu ya Wizara kwa mafanikio na kukabili changamoto ipasavyo. Naunga Mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika mambo mawili tu. Suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi na Matumizi ya *NSSF* katika fursa za kiuchumi na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 suala hili ni moja ya mambo makubwa mawili yanayozungumzwa mle. Lingine ni lile la kujenga uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Sina haja ya kulizungumzia suala hili la pili kwa ukosefu wa muda. Utekelezaji wa sera hii ya msingi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi hauridhishi, kwani utekelezaji wa kizima moto *(adhoc).* Hata mpango wetu wa mabilioni ya JK ni *'adhoc'*, maana tangu zitengwe zile Shilingi bilioni 21 katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 hazijatengwa tena fedha nyingine katika bajeti ya Serikali hadi leo mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Ni dhahiri kuwa mpango huu sio endelevu, umekuwa ukiendelea hadi leo kutokana na mkakati ule wa mwanzo wa kuwataka *CRDB* na *NMB* wachangie mara mbili hadi mara nne fedha zao zaidi ya zile zilizotolewa na Serikali. Maoni ingawa mwaka 2006/2007 Serikali ilizikabidhi zile benki mbili (*CRDB* na *NMB*) Shilingi bilioni 105, zenyewe kwa pamoja zikatoa fedha za mkopo zaidi ya Shilingi bilioni 33. Mabadiliko ya sera ya kuzipa Shilingi bilioni 10.5 Taasisi nyingine za kifedha *(ACB Pride,* Benki ya

Wananchi za Mbinga, Mwanga, Dar es Salaam na kadhalika) ni uamuzi mzuri kisiasa lakini kiuchumi siyo sahihi au ovyo maana tumetoa fursa ya Shilingi bilioni 10.5 tu badala ya zaidi ya Shilingi bilioni 10.5 kama zilivyofanya *CRDB* na *NMB*.

Hata hivyo, suala la kuwawezesha wananchi ni kubwa na ni muhimu sana kwa kuwaendeleza wananchi kiuchumi. Shilingi bilioni 21 ni kiasi kidogo sana kwamba hakiendani na umuhimu wa sera yenyewe. Kwa msingi huu nahimiza utekelezaji wa sera hii kama sera ya Taifa na Uwezeshaji Wananchi *(National Economic Empowerment Fund)* na vyombo hivi vipo lakini havipewi fedha inavyostahili.

Jifunzeni kutoka sera na utekelezaji wa *'Black Economic Empowerment Progamme'* ya Afrika Kusini. Mafunzo mengine *'Bramaputra Policy'* ya Malaysia. Dhana ya kuongeza ajira inaendana na uwezo wa mitaji, hasa kwa wananchi wazawa wenu. Hili linafanyika duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa uwezeshaji utawezesha kupunguza tofauti za uwezo wa kiuchumi wenye msingi wa rangi kama zilivyo sasa katika jamii yetu. Uchumi unaoshikwa kwa kiasi kikubwa na wageni ni uchumi uliojengwa kwenye msingi wa mchanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, suala la kutumia rasilimali za *NSSF* katika shughuli za kiuchumi. Hili ni zuri sana, isipokuwa tukubali kutumia dhana ya 'kupanga ni kuchagua'. *NSSF* ielekeze shughuli zake katika aina fulani za kiuchumi, kama vile *industrial parks* za wafanyabiashara wadogo wadogo, nyumba zenye bei au gharama nafuu *(low cost hoursing schemes)* zinazonufaisha wananchi wenye uwezo mdogo kiuchumi. Tusiitumie *NSSF* kama chombo kingine cha Serikali cha kutimiza malengo yake ya bajeti, kama vile ujenzi wa madaraja, ofisi za Serikali au hospitali.

Kupanga ni kuchagua. Hizi ni shughuli za Serikali, zitengewe fedha za Serikali kutekeleza mipango hiyo. *NSSF* kushiriki katika ujenzi wa majengo ya biashara ni sahihi. Kwa sababu, hatimaye *NSSF* ipate fedha zake tena maana kama mfuko wa pensheni, wastaafu lazima waendelee kupata huduma zao za msingi na ziongezeke kuwa bora zaidi kila wakati. Haifai kushika fedha za *NSSF* au wastaafu katika miradi isiyo na tija kwao, kwa *NSSF* au kwa Taifa zima.

**MHE. COL. FETEH S. MGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri inayofanywa katika Wizara hiyo pamoja na hotuba nzuri iliowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudi iliyofikiwa kwa ajira ya zaidi ya milioni moja. Lakini bado ajira hizi ziko baadhi tu ya Mkoa. Naomba sana ajira hizi nazo zifike kule Zanzibar, hasa katika Jimbo langu la Bumbwini, kwani bado kuna idadi kubwa ya vijana bado hawajapata ajira zozote, fedha ziitwazo mamilioni ya Mheshimiwa Kikwete bado hazijafika ipasavyo Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya *VETA*, viimarishwe nchini kote kwani vitaendelea kuleta wataalam wazuri ambao wapo watakaoajiri na wale wengine watakuwa na uwezo wa kujiajiri wao wenyewe mradi wapatiwe fedha za mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kurejeshwa sheria ya JKT ili kuwadhibiti na kupanda vijana wetu katika kuwa vijana wazuri kwa Taifa letu, badala ya kusambaa nchini ovyo. Ninachokuomba, vijana hawa ni vyema wakapewa upendeleo wa mwanzo pale panapochukuliwa ajira katika majeshi yetu na hata mawizara na viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Wizara iwe karibu sana na vyama vya wafanyazi. Aidha, elimu kupitia njia mbalimbali zitolewe kama vile, *workshop*, semina na elimu kadhaa ziwapo ili kupunguza au kuondoa kabisa vurugu makazini pamoja na maandamano, mara nyingi matatizo ya mishahara na stahili za wafanyakazi, na nidhamu ya viongozi na wafanyakazi wao lazima iwapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini kwetu viwanda vingi vimekufa, ninapenda kushauri, nadhani sasa ni vyema tukafufua viwanda vyetu vidogo vidogo pamoja na kujenga viwanda vipya kwa njia ya kuja kuwekezwa na hata mambo ya ubia mradi twende kitaalamu na mikataba mizuri kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu mdogo, kwa heshima kubwa ninaomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuchangia katika hotuba hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii kwa hotuba yao nzuri sana, inatia matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira mpya milioni moja, naipongeza Serikali kwa kuvuka lengo lake kama ilivyoahidi katika kipindi cha Uchaguzi, na ninashauri ajira ziendelee zaidi. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza sasa kuja na jedwali linaloonyesha jinsi ajira hizo zilivyopatikana Kiwilaya au Kimkoa? Sijui kama itakuwa na maana zaidi iwapo ajira milioni moja na zaidi zote zitakuwa za watu wa Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, au Mbeya peke yake.

Jedwali lingeonyesha wapi juhudi ziwekwe zaidi, nini kifanyike ili mizania ya ajira ikae sawa ili tusisababishe vijana wengi wasihamie kuliko na nafasi kubwa zaidi ya ajira bila maelezo. Aidha, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ajira nyingi zilizopatikana ni za aina gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wanakosa elimu ya uhusiano kati ya *SACCOS* na mikopo. Aidha, kuiungo muhimu kati ya *SACCOS* na mikopo hawaelewi. Hivyo ninaipongeza Serikali na kuiomba kwa dhati kuja na programu ya kutoa elimu ya umuhimu wa *SACCOS.* Mimi ninafikiri ni vyema elimu ya umuhimu wa kuundwa kwa *SACCOA* ingeanza kufundishwa mashuleni ili iwe rahisi kuelewa nguvu na uhalali wa *SACCOS* kupatiwa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa kuwa watu wengi wanafanya kwa makosa, kwa kuamini kuwa kujiunga katika *SACCOS* ni kigezo tosha cha kupata mikopo bila kufanya tathimini ya uwezo wa *SACCOS* kushiriki kikamilifu katika mkopo unatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuongeza ajira, nimeangalia kiambatisho I ninashukuru sana Wilaya ya Kwimba imepata mgao wa Sh.50,000,000/=. Aidha, katika jedwali hilo zipo Halmashauri zilizopata zaidi ya Shilingi milioni 100. Je, vigezo vipi vinavyowezesha Halmashauri nyingine zipate zaidi kuliko Halmashauri nyingine? Naomba ufafanuzi.

Mfuko wa Maendeleo ya vijana: nimeona kwa Halmashauri ya Kwimba kiasi cha Sh. 5,000,000/= kimetolewa. Je, fedha hii kwa kuwa ilitegemewa kutolewa kwa *SACCOS*, kwa Kwimba fedha hiyo imepelekwa kwa *SACCOS* zipi kwa mujibu wa taarifa zitokazo Halmashauri ya Kwimba? Naomba nipewe taarifa hiyo nikajiridhishe. Kitabu cha hotuba kiko wazi kwa nini, wakati taarifa za Mikoa mingine zimo?

Wakala wa Usalama na Afya mahali pa kazi, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Naipongeza sana wakala kwa kazi nzuri wazifanyazo katika viwanda vyetu hapa nchini kwa usalama na manufaa ya wafanyakazi katika viwanda hivyo.

Ajira mpya ipatikane kuwezesha kufungua ofisi kila Mkoa ni kwani ni muhimu sana kwa usalama katika viwanda hivyo, wakiwa wengi wataweza kuwa na ratiba za kuwatembelea viwanda hivyo mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza sana shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa kazi mbali mbali za maendeleo linalozifanya katika nchi hii. Inasikitisha shirika hili linapowekewa mizengwe katika utekelezaji wa miradi mingine, mfano Daraja la Kigamboni, Jengo la *TBC*. Miradi yote hii ni ya Kitaifa – mradi wa daraja umo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika uchaguzi wa mwaka 2005. Mradi wa jengo la *TBC* ni kwa manufaa ya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua kuna nini HAZINA? Kuna nani HAZINA? Kuna kitu gani HAZINA kinachosababisha kusita kutoa vibali kwa shirika hilo kutekeleza miradi hiyo? Je, kuna siasa gani ndani ya HAZINA inayopingana na siasa ya Chama Tawala? Naomba HAZINA itakiwe kujitokeza iseme wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninauliza kumetokea nini kuhusiana na ombi la Kwimba kuiomba *NSSF* kuja kujenga nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya wafanyakazi ? Je, kwa nini *NSSF* inakuwa na mashaka, haiamini Halmashauri ya Kwimba ? Nina ombi la siku nyingi, leo ninaomba maelezo. Kama Halmashauri haiaminiki, basi waje wajenge nyumba kwa ajili ya Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema,

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yao ya Wizara hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya wananchi wanaoamini kuwa ajira ni ile inayotokana na Serikali tu. Je, Serikali inatoa ufafanuzi gani kuhusu suala zima la ajira ili wananchi wote waweze kuelewa kwa kina dhana nzima ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, *OSHA* ni taasisi ambayo haieleweki kwa wafanyakazi wengi katika sekta binafsi pamoja na sekta za umma. Hivyo ni vyema hatua za kisheria zikachukuliwa dhidi ya waajiri wanaopuuza afya na usalama mahali pa kazi kwa wafanyakazi katika sekta hizi za ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu inapaswa itolewe kwa wafanyakazi katika sekta mbalimbali za ajira ili wajue wajibu wao pamoja na haki zao ili panapotokea maonevu au ukiukwaji wa haki zao kutoka kwa waajiri wajue nini la kufanya au waende wapi kudai haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo muhimu sana kuwepo kwa mahusiano mema baina ya waajiri, waajiriwa na Serikali ili utendaji kazi uwe unafanyika kwa kufuata misingi ya sheria baina ya waajiri na waajiriwa. Hii itasaidia kupunguza au kuondoa kabisa migogoro na migongano baina ya wafanyakazi na waajiri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana ndio nguvu kazi kubwa ya Taifa letu, lakini nguvu kazi hii bado haijatumika ipasavyo. Ni vyema Serikali ikaandaa mipango na mikakati itakayosaidia vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo katika maeneo mbalimbali badala ya vijana wengi kukimbilia mijini bila ya shughuli maalum zinazoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna asilimia kubwa ya vijana wanaishi vijijini, hivyo ni vyema miundombinu mbalimbali ikaanzishwa na kuimarishwa huko vijijini ili vijana waendelee kubakia vijijini wakifanya shughuli za maendeleo na kuweza kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana waandaliwe ili waweze kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea Serikali iwaajiri. Ajira zitokane na mazingira wanayoishi kwa mfano kwenye maeneo ya kilimo, maeneo ya samaki waweze kuvua samaki na kadhalika. Katika maeneo kama haya kukijengwa viwanda kutasaidia kupatikana kwa ajira za uhakika na zenye tija.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma vizuri hotuba ya bajeti ya Wizara hii, ni nzuri, hata hivyo napenda kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shamba la Sasanda – Mbozi lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 800 liko chini ya Wizara hii na limekuwa likitumika kama moja ya maeneo ambako vijana hufanya kambi yao. Hata hivyo, eneo hilo ni kubwa sana kwa matumizi ya vijana. Mwaka jana nilikwenda sehemu ya eneo hilo kwa matumizi ya Serikali ya kijiji (kwa ajili ya kujenga shule). Wizara ilisema kwamba ina mpango kabambe wa kuliendeleza shamba hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana kwamba tangu Serikali itoe ahadi ya kuendeleza eneo hilo, hakuna kitu au kazi iliyofanyika. Hii ni dalili tosha kabisa kwamba Wizara imeshindwa kabisa kuliendeleza eneo. Kulikoni? Je, sasa si wakati mwafaka kwa Wizara kutenga/kutoa angalau hata ekari kati ya 50 na 100 kwa ajili ya matumizi ya kijiji? Ni lini sasa Serikali itakuja na mpango mkakati wa namna ya kuliendeleza eneo hilo ili wananchi wasione kama Serikali yao inawanyima ardhi bure pasipo kuitumia?

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo kwa vijana na wanawake kwa kiwango cha asilimia 10 kinachotolewa na Halmashauri za Wilaya ni kiasi kidogo. Mathalani kikundi cha watu watano hadi kumi wanakopeshwa kati ya Sh. 500,000/= hadi Sh. 1,000,000/= mgawanyo kwa kila mtu ni kidogo sana! Naomba Serikali kupitia Wizara ione uwezekano wa kuongeza mikopo hiyo ili iwe na tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kujua ni lini sasa Wilaya ya Mbozi ambayo ilipata mkopo huo awamu ya kwanza, itapata mkopo wa awamu ya pili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikiri kwamba mbio za mwenge zinachochea sana maendeleo. Hata hivyo, kuna jambo moja ambalo napenda niiombe sana Serikali, kupitia Wizara hii ifuatilie kwa karibu sana kuhakikisha kwamba miradi yote inayowekewa mawe na mbio za mwenge inakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembea maeneo mengi sana katika nchi hii, katika safari hizo nimewahi kuona baadhi ya majengo yaliyowekewa mawe na viongozi wa mbio za mwenge katika miaka tofauti, yakiwa hayajakamilika. Hili ni jambo la kusikitisha sana. Nashauri kuwe na utaratibu wa kufanya ufuatiliaji ili lengo la mbio hizo liweze kukamilika au kuwa na maana zaidi. Ahsante,

Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkono hoja.

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wamekuwa hawana ajira, wanazurura ovyo na kujiingiza katika makundi mabaya ya kihuni. Tunaiomba Serikali ibuni mkakati wa kudumu wa kupunguza tatizo la ajira kwa vijana nchini na kupunguza uzururaji wa vijana na umaskini. Mkakati uliopo sasa hautoshi kupunguza tatizo la ajira. Vyuo vya *VETA* viwekwe kila Wilaya ili visaidie kuleta ajira binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikuwa wapi wakati viongozi wa DESI wanakusanya pesa kwa njia zilizo kinyume na sheria na kusababisha adha kubwa katika nchi? Wananchi wamekuwa wanatapeliwa pesa zao na viongozi wa DESI na khatima yake hakuna mafanikio kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwe na tabia ya kuziba ufa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kuhusu maendeleo ya vijana katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo ni kuhusu suala au tatizo lililopo nchini mwetu la ukosefu wa uaminifu kwa vijana katika maeneo mbalimbali ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni masikini na kutokana na hali hiyo kumekuwepo na changamoto nyingi ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi, suala la ukosefu wa ajira ni mojawapo ya changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana ni kundi ambao linaathirika sana na changamoto hiyo ambapo licha ya kutokuwepo na ajira za kutosha, hata idadi ya vijana inaongezeka kwa kasi, hivyo kufanya tatizo hili kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa hali ya ajira ni mbaya, idadi ya vijana ambao wapo katika ajira wamekuwa hawaonyeshi nidhamu ya kutosha katika maeneo ya kazi ambayo wamepata bahati ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana huko kwa nidhamu kunatokana na idadi kubwa ya vijana kufukuzwa kazi kutokana na ukosefu wa uaminifu katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limekuwa ni tatizo kubwa kwa jamii yetu, hivyo kufanya Watanzania wengi hasa vijana kuonekana kuwa ni watu ambao hawawajibiki, kukosekana huko kwa uaminifu kumekuwepo si tu katika sekta ya umma bali hata sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inafanya ongezeko la ukosefu wa ajira kuwa kubwa, kwani kila anayetaka kuajiri anahofia kuchukua wafanyakazi kutoka hapa nchini na badala yake kuajiri wafanyakazi kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali haioni umuhimu wa kueleza wazi tatizo hili ili kutoa onyo au funzo kwa vijana walioko mashuleni/vyuoni ili waone ubaya wa tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili likiachwa bila kuelezekwa kama ni tatizo la Kitaifa litaendelea na kuharibu nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe maelezo bayana kuhusu ukubwa wa tatizo hili hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa fursa hii ya kutoa mchango wangu. Awali ya yote naomba kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, rejea Ukurasa wa 28 aya 28(b): Je, ni vigezo gani vinavyotumika kuwateua/kuwachagua wakimbiza Mwenge Kitaifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema kabisa tukajenga misingi bora ya ajira kwa vijana. Hivyo basi, tunaomba JKT, iwachukue vijana kwa dhamira nzuri ya kuwapatia mafunzo mbalimbali kama vile mafunzo ya umeme, ujenzi, useremala na hata ufundi makanika. Inaweza kuleta manufaa zaidi iwapo vijana hawa watamaliza salama na kupatiwa *"toll box"* kwa kila mmoja wao kutokana na mafunzo aliyomaliza kujifunza. Hii itawasaidia vijana hawa mara tu watakapotoka Jeshini huko, kuweza kujiajiri sehemu mbalimbali hasa vijijini. Lengo kubwa ni kuwafanya vijana wajitegemee mbali na kuongoja ajira toka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wapewe nafasi zote za ajira ya ndani na sio vinginevyo. Leo tunashuhudia jinsi Wachina wanavyopora ajira za vijana. Tulichokitarajia ni Wachina hawa kama ni wawekezaji wa kweli kuja na (i) *Capital* (ii) kujenga viwanda (iii) kutoa ajira (iv) na kuleta teknolojia na mwisho kupata soko la ndani na la nje kwa bidhaa zitakazotengenezwa. Hivyo basi, Wachina ambao wameingia kiholela kwa kisingizio cha uwekezaji wafanyiwe udadisi ili wajulikane, wale wanaoishi kinyume na utaratibu waweze kurejeshwa kwao. Ila tu naomba zoezi hili liende vema na kwa busara ili tusije tukaathiri uhusiano mzuri uliopo baina ya Jamhuri ya watu wa China na watu wa nchi yetu ya Tanzania. Vijana wajengewe mazingira mazuri vijijini ili tupunguze vijana kukimbilia katika miji mikuu na kuleta msongomano mkubwa na hata vijana kujiingiza katika mambo yanayokwenda kinyume na maadili yetu sisi Watanzania.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza kwa hotuba yao nzuri, vile vile niunge hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na vijana wengi sana ambao wanamaliza masomo yao na kwa kuwa vijana waliomaliza mwaka 2000, 2001, 2002, 2003, 2004 na 2005, 2006, 2007, 2008 huwa wakati mwingine hawapati nafasi za kwenda vyuoni, Jeshi la Polisi na Jeshi la Ulinzi na Wizara zingine ambazo wanapotaka wanafunzi waliomaliza masomo yao vigezo wanavyochukua huwa ni kuanzia wale waliomaliza miaka ya karibuni tu kama 2007 – 2008. Je, hawa wa miaka ya nyumba wawapeleke wapi na kwa nini wamewanyima haki zao? Ninaomba Serikali iwasaidie vijana hao nao wapate kwenda vyuoni kigezo kisiwe miaka hii ya kumaliza masomo ya karibuni.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Kazi, Naibu Waziri wake pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nichangie machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wananchi wanasubiri Serikali itoe ufafanuzi wa kima cha chini cha mshahara hasa kwa sekta mbalimbali ili kuondoa utata uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa kwa wananchi kuajiriwa kama vibarua kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja pasipo kuwa na ajira ya kudumu. Namwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa suala hili na suluhu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ajira kwa vijana bado ni kubwa sana kutokana na vijana wanaomaliza masomo kuwa wengi. Napenda kujua Wizara yako imejipangaje kupunguza tatizo hili kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa ushirikiano mzuri, napenda kuunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira kwa vijana, napenda kuipongeza Serikali kwa kufikia lengo lake ililojinadi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005 – 2010, kufikia lengo la ziada kufikia ajira milioni moja. Ajira sio lazima mtu aajiriwe na Serikali, kuna ajira binafsi nyingi za vijana kujiajiri wenyewe endapo Serikali yetu inasaidia kuwapatia mikopo na misaada mbalimbali hata kuwawekea sehemu maalum na nzuri za kufanyia biashara zao. Naiomba tu Serikali izidi kuwasaidia vijana wetu katika kuwaongezea ujuzi wa kazi (biashara) kwa kuwapatia elimu ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhalilishaji wa vijana wanaofanya kazi viwandani na hotelini, naiomba Serikali ifanye utafiti katika viwanda na hoteli hapa nchini ili kugundua athari zinazowapata vijana wanaofanya kazi katika maeneo hayo. Waajiri wengi wa

viwandani na hoteli nyingi hasa katika Jiji la Dar es Salaam hawawatendei haki waajiriwa hasa vijana wa kike kwa kutofungiana mikataba ya kazi na kwa hivyo kuwakosesha haki zao za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wanadhalilishwa sana na waajiri kufikia hatua ya kuwafukuza kazi bila sababu maalum tu endapo wanakataa matakwa ya mwajiri hasa kama si ya halali (kisheria). Naiomba Serikali kuliona hilo na zaidi tatizo la kutokuwalipa mshahara stahiki pamoja na kuwafanyisha kazi bila hata mapumziko siku zote. Vijana wetu wa Kitanzania wengi sana wanapata manyanyaso na hawana watu wa kuwatetea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuishauri Serikali kwa hili, napenda kuunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Kapuya, Naibu Waziri na Watendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda kupata maelezo juu ya hatua iliyofikiwa juu ya mkataba wa hiari kati ya wafanyakazi na Kampuni ya *TRL*. Aidha, pale mikataba ya hiari inapovunjwa na kupuuzwa na waajiri, ni hatua zipi zinachukuliwa kwa waajiri? Pia ningependa kujua ni kwa nini pale mishahara ya kima cha chini inapopangwa na waajiri kukataa, Serikali haioni inapokubali kuwasilikiliza waajiri hawawatendei haki wafanyakazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi sioni tofauti kati ya mfanyakazi na mtumishi na hasa kada ya chini ya Utumishi wa Umma haipewi mtazamo unaostahili mfano Madereva wanapolipwa sawa na Mhudumu bila kujali uzito wa kazi zao na dhamana walizonazo. Dereva anayemwendesha Waziri, Mkuu wa Mkoa, RAS na viongozi wengine wanalipwa sawa na Mhudumu wa ofisi. Ni vema sana Serikali kupitia kwako kurekebisha dosari hii na kuwapa Madereva wa Serikali mafao yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Vijana, kwa kutangaza kuwepo Mfuko huu, umewapa tamaa na matumaini vijana kwamba watawezeshwa na kupata mikopo toka mfuko huo jambo ambalo limeshindikana kuweza kuwakopesha vijana wote na hasa pale kiasi kidogo cha fedha ambacho kinapelekwa Wilayani. Kama dhamira hiyo bado ipo na nia ni njema na kuwapa matumaini vijana, ninapenda kujua bajeti hii imetenga kiasi gani kwa ajili ya Mfuko huu wa Wilaya ya Mpanda, nitapenda kupata maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina jukumu kubwa la kuwapatia maendeleo vijana hususan ajira, kama lilivyo jina la Wizara yenyewe. Ni wazi kuwa vijana ni Taifa la leo na kesho na kwamba idadi yao imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa na hivyo kuwa tishio kwa usalama wa nchi. Wote tunajua vijana ndio nguvu ya Taifa na kama hawatasaidiwa kujiari wenyewe au kuajiriwa.

Pamoja na juhudi za Wizara kuwapatia ajira vijana, bado kuna tatizo kubwa la ongezeko la vijana kutoka vijijini kwenda mjini.

Moja ya sababu ya wimbi hili, ni kukosekana kwa huduma za jamii kama hospitali, masoko, shule, *social clubs* na kadhalika. Serikali inabidi ihakikishe kuwa huduma za jamii zinaendelezwa vijijini ili kupunguza idadi kubwa ya vijana mijini. Athari kubwa za ongezeko la vijana mjini ni pamoja na ujambazi, vitendo vya kihuni ikiwa ni pamoja na ulevi, umalaya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana ni wengi sana hapa nchini na ni wenye nguvu za kuweza kujenga Taifa letu, kuna haja ya kupatiwa mikopo ili waweze kujiajiri wenyewe. Kama Serikali inavyotoa mikopo kwa vikundi vya kinamama na kadhalika. Naamini kabisa vijana hawa wakiwezeshwa, wataweza kulikomboa Taifa kwani watakuwa wa msaada mkubwa katika familia zao. Kutokuwasaidia vijana hawa, ni kuwafanya waingie kwenye vitendo viovu hasa ikizingatiwa kuwa janga la Ukimwi limekuwa likiwakumba sana vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imepewa fedha ndogo sana shilingi bilioni 16 tu za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni tatu tu kwa shughuli za maendeleo. Kama nilivyosema, vijana nchini ndio nguvu kazi ya Taifa lolote. Kwa bajeti ndogo hivi, napata hisia kwamba vijana wetu hawataweza kupiga hatua yoyote ya maendeleo, fedha hizi ni ndogo mno hata kasma ya utawala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya shilingi bilioni 20.6 ni wazi kuwa Wizara hii haitaweza kusaidia tatizo kubwa linalowakabili vijana wetu.

**MHE. EUSTACE OSLER KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri, lakini hasa kwa kuendesha vema shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wengi ambao hawana stahili ya kuajiriwa wameendelea kuchukua nafasi za Watanzania. Nashauri juhudi zifanyke kurekebisha hali hii. Jitihada zifanywe kuzuia vibali vya ajira visitolewe ila pale tu ambapo ni lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika wa kukagua na kuhakiki uhalali wa wafanyakazi katika sehemu za kazi. Vijana wetu wanasoma, lazima tulinde ajira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kupata nafasi ili nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pia Wakurugenzi wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa ya JK. Pesa hizi kuna baadhi ya Wilaya hazikufaidika kutokana na kutopewa mgao wao, ahadi ilikuwa shilingi milioni 100 lakini tumepewa shilingi milioni 50 tu. Sisi viongozi wa Wilaya tulipoahidiwa shilingi milioni

100, tulifanya mgao kusubiri pesa, hivyo kupewa shilingi milioni 50 imetupa wakati mgumu kwa vikundi vilivyobaki. Tunaiomba Serikali ione umuhimu wa kuongeza pesa hizo mapema ili kuweka mambo sawa kwa vikundi vilivyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshwaji wa wajasiriamali uwe na usimamizi wa wazi, vikundi watakavyounda viwezeshwe kupitia *SACCOS*, Vyama vya Ushirika wahakikishe vyama vinasajiliwa na wavitembelee na kuvipa elimu juu ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado lipo tatizo la ajira. Kazi zinapotangazwa tayari utaratibu usio rasmi huwa umetumika na hivyo kuitwa kwenye usaili ni ushahidi tu. Chombo chetu cha kusimamia ajira ili haki itendeke, kinafanya nini? Wapo vijana wenye *CV* nzuri lakini hawajaajiriwa isipokuwa wale wenye kufahamiana hupeana kazi, hivyo naomba Serikali ilione hilo. Wizara hii bado ni muhimu kwa kusimamia haki za wananchi. Hivyo watendaji wa Serikali wajielekeze kuingilia waajiri wanaopinda Sheria na matakwa ya mwelekeo wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze kazi nzuri zinazofanywa na Wizara kusimamia na kuratibu Mbio za Mwenge. Timu zinazokabidhiwa Mwenge tangu nishiriki nao nimeridhika kuwa ni vijana wanaokuwa wamechujwa vizuri. Nawapongeza viongozi wote walioshiriki mbio hizo na wale wanaoendelea na mbio. Mungu awalinde wamalize vyema na yote waliyoyaona wahusika wayafanyie kazi kama Wilaya zilivyoainisha kama risala ya utii kwa Rais tunavyoisoma toka maeneo yetu. Mwisho niwatake kazi njema.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii, kwa kusimamia kazi, ajira na maendeleo ya vijana vizuri ingawa bado kuna maeneo bado yana malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi ya kusimamia ajira haina ufanisi mzuri, kuna urasimu mkubwa na wananchi au vijana hawajui ziko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipendekeze au nishauri kuwa kwa kuwa tuna vyuo vingi ambapo wanafunzi wengi wanahitimu, ofisi hii iwasiliane moja kwa moja na vyuo hivyo ili kusiwe na rushwa katika kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndio tegemeo kubwa kwa vijana wa Taifa la leo, wanaotegemewa kuwa watendaji wakuu katika nchi hii. Vijana wanahangaika sana na vyeti vyao kutafuta kazi wakati Serikali yao ipo. Nashauri Wizara hii iwasaidie sana vijana hawa sionekane wazururaji, ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kutambua kutoa mikopo ya vijana, kupitia Halmashauri ya Wilaya, lakini vijana wengi wanalalamika hawapati mikopo hiyo. Baya zaidi, marejesho ya mikopo hiyo haifuatiliwi vizuri na Halmashauri za Wilaya ili mzunguko ufanyike kwa vijana kukopeshwa wengi. Nashauri pawe na mkataba wa kuwabana wasiorudisha mikopo hiyo, wasifikiri ni zawadi, ni mkopo. Naomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hoja yake, nipate orodha ya vikundi vya vijana waliokopeshwa toka Mkoa wa Mwanza toka mwaka 2005 – 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii, kwa utendaji wao nzuri. Napenda kuwasilisha malalamiko ya vijana wangu wa Jimbo la Kinondoni ambao hujiajiri na kupata kipato chao pale *Leaders Club* kwa kuuza vitu vidogo vidogo, kusafisha magari na kadhalika siku ya Jumapili ambapo kunakuwa na Bonanza la Michezo na baadaye muziki kuanzia saa 8 mchana hadi saa 12 jioni. Lakini cha kusikitisha Bonanza hilo limesitishwa na Ofisi ya Utumishi. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri uwasaidie vijana hawa ili waweze kupata kipato kutokana na Bonanza hilo. Naomba wahusika hasa Waziri Hawa Ghasia na Katibu wa Wizara hiyo waruhusu Bonanza hilo ambalo liko hapo tangu mwaka 1996. Madhumuni ya Serikali yetu ni kuhakikisisha vijana wanawezeshwa ili wajikwamue kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana *NSSF* waangalie uwezekano wa kuwekeza/kujenga majumba ya kibiashara eneo la Magomeni Kota (eneo Kongwe) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kinondoni, ili kuboresha eneo hilo ambalo ni kubwa sana na pia kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. Nawapongeza sana pia kwa ongezeko la ajira zilizo endelevu, ajira ambazo zinachangia sana maendeleo ya vijana. Lakini pia nimpongeze Waziri kwa namna ambavyo Wizara yake imeendelea kupata suluhu za migogoro ya kazi kwa walalamikaji wengi wa pande zote yaani waajiriwa na waajiri pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kumekuwa na migogoro ambayo mbali ya kutolewa suluhu na ofisi yako, baadhi ya waajiri wamekuwa wagumu kuheshimu maamuzi hayo, hasa ambapo mwajiriwa anapokuwa amepewa ushindi. Hii ni dosari kubwa inafanya baadhi ya waajiriwa wakate tamaa ya kupata haki zao kutokana na ushindi walioupata kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa. Je, Mheshimiwa Waziri na wataalam wake wanalijua hili? Kama jibu ni ndiyo, basi utaratibu ni upi hivi sasa ili kuona pia kunakuwa na utekelezaji wa maamuzi yao? Kama Wizara haijihusishi na kuona kuwa maamuzi yao halali yanatekelezwa, je, ni nani basi au idara gani basi inaweza kufanya kazi hiyo ili kuendelea kujenga imani kwa utawala wa sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaweza nikaelewa kwamba, kama malalamiko yaliyopatiwa suluhu na ofisi yao huko Dar es Salaam yalitokea sehemu au Mkoa ulio mbali, mahali ambako hawana msimamizi wa moja kwa moja wa ofisi yako, je, haitakuwa vema basi usimamizi wa maamuzi yao ukafanywa na ofisi za Mikoa, Wilaya na hata zile za Tarafa baada ya kuwa pia ofisi hizo zimepelekewa nakala ya maamuzi yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupeleka nakala za maamuzi au suluhu alizofikia Mheshimiwa Waziri katika migogoro mbalimbali ni muhimu tu hata kama haitakuwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji. Umuhimu wake ni pamoja na kuokoa muda wa watendaji hawa wa Serikali kuanzia Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya hadi Afisa Tarafa ambao hujikuta wanashughulishwa na baadhi ya waaajiriwa na waajiri wanaopenda kuendeleza migogoro kwa maslahi yao binafsi hata kama Sheria imejielekeza na imetumiwa kwa mikondo yote na kikamilifu katika kupata suluhu ya malalamiko yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam, kwa maandalizi mazuri ya hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uzoefu wangu kazini, napenda kusifu mchango uliotolewa na *ILO* miaka ya 1970 kwa kutekeleza programu iliyoitwa "*Special Labour Intensive Public Works Programme*". Programu ilihusu "*small scale irrigation and food control, rural water supply, rural housing*" na *Tsetse fly eradication*. Programu ilitekelezwa na ofisi ya Waziri Mkuu na *ILO* katika Mikoa ya Dodoma, Arusha na Ruvuma. Naamini kwa filosofia ya *ILO* ya kutumia nguvu kazi, wananchi walinufaika na ajira zilizotokana na programu hiyo kwa kuwa katika kila shilingi moja iliyolipwa, senti 60 – 80 zilitumika kuwalipa wananchi waliotekeleza programu hiyo. Nashauri Wizara iangalie uwezekano wa kushirikiana na sekta nyingine kubuni miradi ya aina hiyo inayolenga kutoa ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana katika Jimbo la Buyungu, wamebuni mradi wa kuzalisha chokaa. Naomba miradi maalum, mafunzo na uwezeshaji, kwa vijana hao ili waweze kuzalisha mali na kutengeneza ajira. Matumizi ya chokaa ni pamoja na kujenga nyumba, kutengeneza mbolea, kutengeneza *Pluster of Paris (POP)* za hospitali, kusafisha ngozi, kutengeneza chaki na kadhalika. Naomba ushauri juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, *Subhana Wattaalla*, namshukuru kwa kuniwezesha kuamka na pumzi na kufika hapa Bungeni nami nikaweza kutoa mchango wangu wa mada ilioko hapa mbele yetu ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri, Naibu na Watendaji wake wote, kwa jinsi walivyoandaa hotuba ya bajeti yao. Mwenyezi Mungu awawezeshe waweze kuitekeleza kwa vitendo, Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho na kwa umuhimu mkubwa, napenda kukupongeza wewe, Naibu Spika na wenyeviti wako wote, kwa kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa, nasema hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia Wizara hii kwa masikitiko makubwa kwa vijana wetu wa Dar es Salaam ambao wanajitahidi kujiajiri lakini dola linawaadhibu sana kwa kuwanyang'anya mali zao na kuwapiga na mwisho kuwatia ndani. Kwa kweli Serikali haiwatendei haki kwani Serikali iliahidi ajira 1,000,000/= na vijana wanajiajiri sasa kwa nini Serikali inawanyanyasa vijana hao? Naiomba Serikali kwa vile wako katika mchakato wa kuwapatia jengo la kufanyia biashara basi wawaandalie mpango maalum wa kuweza kupata nafasi ili kipindi hiki wafanye kazi kwa utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mataifa ya wenzetu wanathamini sana wananchi wao katika kuwapa kipaumbele katika ajira lakini nchi yetu hasa sekta binafsi zinawajali sana vijana kutoka nje ya nchi na kuwaajiri katika mahoteli na makampuni mengi nchini. Naiomba Serikali ihakikishe kipaumbele wanapewa Tanzania ili kuweza kuwaleta maisha bora kwa kila Mtanzania isiwe kwa ngonjera tu iwe kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukatai uwezo wa watu wetu kuwa mdogo, lakini naamini vijana sasa wana mwamko na wamesoma sana lakini hawapewi kazi. Serikali iyakazania mahoteli pamoja na makapuni kuwapa *priority* vijana wetu. Sambamba na hayo, waajiri wengi wanapenda kunyanyasa waajiriwa hasa wanawake kwa kupenda kuwadhalilisha kijinsia na kama hawakubali hupata taabu sana maofisini, wanashindwa kufanya kazi kwa utulivu. Naiomba Serikali kwa hili wawe wakali sana ili wanawake wawe na uhuru wa kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna waajiri wanapenda kuwaajiri watoto wadogo ili wawe wanawalipa pesa kidogo sana na vile vile kuwakatisha masomo yao. Watu hawa hawawatendei haki watoto hawa. Mtoto hasa maskini ni dhaifu sana, anashindwa kukataa kwani maisha kwake yanakuwa magumu sana kwa kukosa hata chakula na akikosa mtu wa kumtetea, mambo yanazidi kuwa magumu. Naiomba Serikali itoe elimu kwa kuwaelimisha wananchi wasiokuwa na huruma kwa watoto hawa na asiyesikia hatua kali zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pesa alizotoa Mheshimiwa Kikwete, hazikuwafikia walengwa, pesa zinaishia mifukoni kwa wajanja wa mjini kwa sababu hazikuwa na usimamizi madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NSSF* naipongeza sana kwa jitihada zake za kujenga majengo ambayo yanawasaidia wananchi lakini wamelenga watu wenye kipato cha juu tu! Je, wenye kipato cha chini wamewafikiriaje? Naiomba Serikali iangalie sana hali hii kwani mwananchi mwenye kipato cha chini hawawezi kukodi nyumba kwa shilingi laki nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumaini Wizara hii italiangalia jambo hili kwa kina. Nakushukuru sana.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kuiunga mkono hotuba ya Waziri, pia nitumie nafasi hii kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa kazi zao nzuri za kuwahudumia Watanzania. Ni ombi langu kuwa mtaendelea kuchapa kazi kwa bidii kwa faida ya mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nikujulishe mgogoro wa kikazi kati ya Wafanyakazi wa Kampuni ya Ujenzi ya Kundan Singh waliokuwa wanajenga barabara ya Mbeya – Lwanjilo – Makongorosi mjini Mbeya. Mpaka sasa, baada ya Kampuni kusitisha ujenzi wa barabara hiyo, Ofisi ya Kazi ya Mkoa wa Mbeya, hawajatoa msaada halisi wa kuwatetea wafanyakazi hawa wanyonge. Msimamo wa ofisi ya kazi unaegemea kumsaidia mjezi, Kundan Singh, hii ni hatari kuwapuuza wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi, mjenzi Kundan Singh, hata rekodi za watumishi hao wamefuta kwenye kumbukumbu zake kama sehemu ya hujuma. Naomba wafanyakazi hawa wapewe haki ya kusikilizwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu wako bila kusahau wale wote walio chini kwenye Wizara yako kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote mazuri bado mimi nimeona nichangie moja ambalo ninafikiri linaweza likafanywa na Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine taasisi, mashirika ya ndani na nje ya nchi ili kutoa ajira pia maendeleo ya vijana. Mimi bado naamini Kambi ya Vijana za Kilimo zingeweza kusaidia vijana na nchi kwa ujumla. Nafikiri kama tungewaweka baadhi ya vijana kwenye kambi tukawapa maeneo, nyenzo, mikopo na posho ya kujikimu kwa muda maalum, wapate wataalam wa kilimo kuwasimamia kwenye shughuli hii na hatimaye vijana hawa kumilikishwa maeneo hayo angalau eka tatu kila mtu, naamini vijana hawa wataweza kupata ajira ya kudumu. Naomba sana tena sana hebu tujaribu. Nilijaribu kuyasema hayo mwaka jana na nikasema hebu tujaribu angalau Mkoa mmoja halafu tupime matokeo. Utashangaa nilipata *message* kutoka kwa vijana wakiomba, naomba hilo lifanyike na lisiwe kwa Mkoa mmoja tu bali Mikoa yote. Vijana wako tayari na ardhi tunayo, naamini wengi watatuunga mkono kwenye hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo napenda kusema hili ni wazo langu na ndoto yangu imara kwa vijana. Naamini ndio ukombozi mkubwa kwa vijana wa nchi hii. Kilimo kwanza kwa kutumia nguvu za vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kuamka nikiwa mzima pamoja na wenzangu nasema “*Alhamdulillah.*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wako wote, kwa uvumilivu wenu pale ambapo tunateleza. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenye macho haambiwi tazama. Kwa kuzingatia hotuba ya Waziri Mheshimiwa Kapuya, utafahamu nia ya Serikali, ya kutaka Watanzania walio wengi wawe na ajira ili waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira ni maeneo matatu. Kuna ajira ya Serikali, ajira ya sekta binafsi na ajira ya mtu binafsi. Kwa kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, iliainisha ajira milioni moja ifikapo mwaka 2010. Nadhani Serikali ya CCM imeweza kufanikisha. Ni vema Wizara inieleweshe katika ajira hizo imeangalia jinsia? Kama ndio au sio ni vema nijulishwe ni wanawake wangapi waliofanikiwa katika ajira hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuweza kuwahamasisha vijana kwa kuitikia wito wa kujiunga na *SACCOS*. Kwa kuwa vijana walio wengi wameitika wito, kinachoonekana fedha zilizotengwa hazitoshelezi. Hivyo basi, ni vizuri mfuko huo uboreshwe ili uweze kukidhi mahitaji yake kwani kufanya hivi tutaweza kuwaondoa vijiweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvu kazi iliyo na elimu katika nchi yetu ni ndogo sana na ukiitazama iko vijijini zaidi, pia ndio eneo kubwa lililobebeshwa umaskini. Ni lini hasa Sera ya Taifa ya Raslimali watu itakuwa tayari kwa mipango ya maendeleo kulinganisha na hali ya sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro na migomo kazini imejitokeza mara nyingi hapa nchini. Naiomba Serikali inieleze ni kitu gani hasa kinasababisha matatizo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingaita ajira binafsi, ni vema niipongeze Wizara ya Elimu kwa kuweza kutoa Chuo ambacho kwa kweli kinazalisha ajira binafsi kwa vijana wetu. Chuo hiki ni chuo cha *VETA*. Chuo hiki ni soko kubwa linalozalisha ajira binafsi. Nakipongeza Chuo cha *VETA* kilicho chini ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna udhaifu mkubwa katika Serikali yetu, masikitiko na aibu inayowafika vijana wetu hasa Dar es Salaam pale wanapojiajiri utaona vijana wa mgambo huwavamia vijana katika kazi zao za kujitafutia riziki. Ni makosa gani vijana wetu wamekosea Serikali yao? Kwani Serikali haiwezi kuwaandalia vijana maeneo mahususi ya biashara zao? Kama kweli vijana tunawajali basi tuwapatie lile jengo lililoandaliwa kwa Wamanchinga lililopo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni Sheria gani waliopewa wajasiariamali wa kigeni hapa nchini, kuwa na wafanyakazi wao mfukoni? Kuna baadhi ya mahoteli makubwa yana wafanyakazi wa kigeni, jambo ambalo linasababisha ukosefu wa ajira wa vijana wetu. Naiomba Serikali iande Sheria ili nafasi za ajira ziwafikie vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Kapuya na Naibu wake Mheshimiwa Makongoro.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Makongoro Mahanga (Mb), Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la *NSSF*, Alhaji Ramadhani Dau pamoja na watendaji walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuinua uchumi wa Taifa pamoja na kuwaandaa vijana na kupunguza migogoro ya wafanyakazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi nyingi nilizomiminia, Wizara hii, napenda kuchangia hoja hii pamoja na kutoa ushauri wangu kama ifuatavyo, nikitegemea kuwa hoja zangu zitapatiwa majibu na Mheshimiwa Kapuya pamoja na Mheshimiwa Mahanga wakati wanajibu hoja mbalimbali kipindi cha kuhitimisha hoja hii. Ninawaombea Mwenyezi Mungu awape afya, nguvu, maisha marefu pamoja na mshikamano ili waweze kutekeleza vema malengo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukiri kwamba natambua jitihada za Serikali katika kuwapatia ajira vijana kupitia Idara au taasisi mbalimbali za Serikali yakiwemo Mashirika ya Umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa ajira kila mwaka Walimu, Wauguzi, Madaktari, Mahakimu, Wahandisi na kadhalika hali ambayo inapunguza sana wimbi la vijana wengi wanaohitimu kutoka vyuo mbalimbali nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua pia juhudi za Serikali kusomesha vijana kwenye vyuo vya *VETA*, Vyuo vya Maendeleo, Vyuo vya Ufundi hapa nchini lakini Serikali huwatelekeza vijana hawa mara wanapohitimu elimu hizo. Ninaiomba Serikali iweke mipango mizuri ya kuwapatia vitendea kazi hata kwa kuwakopesha ili wanaporudi kijijini waende kujiajiri na sio kuwa tegemezi tena ama kujihusisha kwenye uhalifu kwa kutafuta riziki kwa njia mbaya. Ninasubiri majibu ya Serikali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile sina budi kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uamuzi wake wa busara kutoa mabilioni kwa ajili ya kukopesha wanawake na vijana kupitia mabenki ya *CRDB* na *NMB* ambazo zimeaminiwa na Benki kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuifahamisha Serikali kuwa mikopo hii kupitia benki hizi imekuwa migumu kwa sababu ya masharti magumu kama vile dhamana ni hati ya nyumba ama mali yoyote yenye kukidhi gharama ya ukopaji. Ikumbukwe kuwa vijana wetu hawana dhamana hizo pia mabenki haya yako mbali na vijana hasa walioko vijijini. Hivyo ninaishauri Serikali mikopo hii ya JK kuipeleka kwenye *SACCOS*, *VIROBA*, *SIDO*, *PRIDE* na kadhalika ili vijana wengi waweze kunufaika kwani wapo karibu na taasisi hizi. Nasubiri majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza sana kijana wa zamani, mpenzi wangu, Alhaji Ramadhani Dau, pamoja na timu yake yote kwa juhudi zake kubwa za kuinua mfuko huu kwa nyanja mbalimbali pamoja na kuwekeza kwenye majengo mfano hai Chuo Kikuu cha Dodoma. Pamoja na juhudi hizi, pia hutoa mikopo kwa mashirika ya Serikali na watu binafsi ambao hupata dhamana ya Serikali (Benki Kuu) mfano wamekopesha *TANESCO, KAGERA SUGAR* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la Serikali kutokutoa ushirikiano wa karibu kwa shirika hili la *NSSF* wakati wanapohitaji kusaini mikataba mbalimbali ya ujenzi kwenye taasisi za Serikali pamoja na Kampuni binafsi zilizodhaminiwa na Serikali. Ninaiomba Serikali kuwa na utaratibu wenye tija kwa *NSSF* ili shughuli zao za uzalishaji ziende na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Serikali kwa kuwa hutoa dhamana kwa mashirika mbalimbali yanayokopeshwa na *NSSF*, ni vema basi iwe inatoa msukumo kwenye mashirika hayo kurejesha mikopo kwa wakati. Hii imejitokeza kwa baadhi ya Makapuni yaliyokopeshwa kuchelewa kuanza kurejesha mikopo wakati huwa wamekopeshwa kwa dhamana ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitumia Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma *(POAC)*, kutegemea fedha kufuatilia mashirika yaliyokopa na kuchelewa kulipa. Ninahakika Kamati itasaidia sana kama ilivyotembelea *KAGERA SUGAR* ambayo ilishindwa kulipa lakini sasa imeanza kulipa vizuri kwa msukumo wa Kamati hii ya *POAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kazi yake nzuri ya kuwakabidhi vijana jukumu kubwa lenye tija la kukimbiza Mwenge wa Uhuru ambao umekuwa ni janga moto kwa maendeleo ya nchi yetu. Ninayo taarifa kuwa vijana hawa hawapati marupurupu yenye tija kulingana na uzito wa jukumu au dhamana wanayopewa. Ninaomba Serikali ipitie upya marupurupu hayo ili yawe na tija kwa vijana. Nasubiri maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukumbusha Serikali kuwa dhamana ya vijana ipo mikononi mwa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana. Hivyo basi, Serikali itambue wimbi kubwa la vijana ambao wamezagaa Mikoani wakiwa wameishaathirika na madawa ya kulevya pamoja na bangi. Ninaiomba Serikali iangalie njia nzuri ya kuwanusuru hawa vijana ambao ni tegemeo la familia, jamii na Taifa kwa ujumla na nguvu kazi ya leo na kesho. Ninaishauri Serikali kupitia Wizara hii kushirikiana na Halmashauri zote nchini kutafuta njia ya kuwalea ili wasiendelee kudhalilisha Taifa letu lenye sifa nzuri duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuikumbusha Serikali juu ya Chama cha Wafanyakazi *FIBUCA* ambao walijiengua kutoka *TUICO* kwa kuwa Serikali tayari ilikwishatoa usajili wa muda sasa itoe usajili wa kudumu kwani kujiunga na Chama chochote, ni uamuzi wa wafanyakazi wenyewe hakuna sababu ya kuwanyima haki

wafanyakazi hao walioamua kuanzisha Chama chao cha *FIBUCA*. Nitashukuru kupata maelezo ya Serikali kutoka kwa Naibu Waziri au Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Serikali inatambua migogoro ambayo imekuwa inakusudiwa na wafanyakazi mara kwa mara wakiwemo Walimu kwa kutaka kuishinikiza Serikali kuwalipa madai yao au kutaka maslahi yanayolingana na uzito wa kazi zao na kuendana na wakati uliopo kiuchumi. Ninaishauri Serikali kuwa na ratiba ya kudumu ya kukutana na viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi na Serikali. Hii itaondoa migogoro inayotangazwa na wafanyakazi mara kwa mara. Nasubiri majibu ya Serikali.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naishauri Serikali iweke nguvu na msisitizo juu ya fedha za *SACCOS* za vijana. *SACCOS* za vijana na hata vijana kwa ujumla waliojiunga pamoja kuzalisha mali kwa kufanya kazi za kujitegemea hawapati ipasavyo mikopo ya fedha. Mfano hai ni Wilaya ya Muleba, hawatoi fedha kwa vijana hii inatudhoofisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, vijana wengi katika Jimbo langu bado wanashiriki katika kazi za kilimo. Vijana wanazalisha sana nanasi na pasheni. Hata hivyo, hawana soko kwa mazao hayo. Kwa hiyo, wanafanya kazi kubwa, lakini wanapata pato dogo sana. Hali hii inachochea vijana kukaa katika vijiwe vya karata na kahawa badala ya kuzalisha mali. Ninaishauri Serikali itusaidie kuwainua vijana kama hawa wapate walau mashine ndogo ndogo ambazo zinaweza kuwasaidia kukamua matunda na kutunza maji ya matunda ili kuyauza kwa bei kubwa kidogo ambayo itawapatia fedha nzuri zitakazokidhi maisha yao na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye kazi kwa karibu kuboresha mazingira ya kazi zikiwemo nyumba mahali pa kazi, mfano mashuleni. Hivi sasa tumeeneza shule za sekondari nchi nzima, lakini bado tuna tatizo kubwa la nyumba za Walimu na wafanyakazi wengine kama Waratibu Elimu Kata, watendaji wa vijiji na Kata, Mahakimu bado hawana nyumba zilizojengwa na Serikali. Hii inaua moyo wa kupenda kazi za umma na kutamani kuajiriwa kibinafsi hali inayo *frustrate* zoezi la Serikali ku-*train*, kumbe mazingira hayafai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kila ilipo au inapojitokeza ajira ya zaidi ya watu watatu ni bora Serikali ikajua hali ya mazingira ya wafanyakazi wake wengi. Mathalani kwa sasa mizani ya barabarani imejengwa kila tunapopata barabara ya lami. Huwezi kuamini ile kazi ilivyo nzito ya masaa mengi kazini, inayotaka uaminifu, uadilifu na uhodari wa kazi wafanyakazi wake ni vibarua! Hufanya kazi kwa mkataba wa miezi mitatu. Hii ni hatari! Nashauri kwenye eneo kama hili mkataba uwe walau wa miaka mitatu. Itamfanya mfanyakazi kuwa mwaminifu na atajua kuwa akikosea atafukuzwa, atapoteza haki zake nyingi kuliko ilivyo sasa. Watumishi hao wanajijua kuwa si wa kudumu, wanaiba wanavyotaka na hawana cha kupoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. MCHUNGAJI DR. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wao wote kwa hotuba yao nzuri inayokidhi mahitaji ya watu wote. Pongezi kwa Machinga Complex, Kutengeneza Ajira zaidi ya milioni moja, mitaji kwa *SACCOS* na kutatua migogoro ya Kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, JKT na JKU wajikite katika kufundisha vijana ujuzi wa kiufundi. Kuongeza juhudi ya kuendelea kutengeneza ajira kwa sababu wanaomaliza shule, vyuo, ni wengi kuliko ajira zilizopo. *Machinga Complex* zijengwe kwenye miji yote ya Tanzania. Mishahara duni tufanyeje? Wachina wabanwe ili wasifanye kazi za Wamachinga. *PPF* na *NSSF* pia wajenge nyumba za bei nafuu kwa wanachama wao. Kupunguza migogoro kazini kwa njia ya kutoa elimu. Mitaji ipelekwe *SACCOS (direct)* na sio kupitia Benki.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafutayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la *NSSF*. Katika Jedwali VII, mapato toka uwekezaji yanaonyesha yaliyokusanywa kwa mwaka 2008/2009. Je, Waziri anatoa kauli gani kwa fedha zilizokopeshwa/wekezwa katika *Kiwira Coal Mine*, kiasi cha $7 milioni ambazo zilipaswa kurejeshwa ndani ya miezi 18 na sasa ni zaidi ya miaka miwili baada ya miezi 18. Je, hii siyo kudhulumu mfuko huo na kuwanyima wanachama mafao yao kutokana na fedha hizo ambazo hadi sasa hazijulikani zitalipwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Kiwira wameshindwa kulipa, Wizara inachukua hatua gani kuidai Serikali iliyokuwa imeweka mdhamana wa 100%? Serikali itakapolipa, itatoa wapi fedha hizo za kulipa au itatokana na kodi za wananchi, ambayo ni pamoja na wanachama hao hao, jambo ambalo ni kuwapa hasara/gharama mara mbili?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za wanachama zinapowekezwa kwenye miradi mbalimbali mikubwa uamuzi hufanywa na Serikali na Bodi ya Mfuko, ambao wote wameteuliwa na Serikali. Je, isingelikuwa wakati mwafaka sasa kuunda chombo, angalau cha ushauri kitakachoshirikisha vyama mbalimbali (wawakilishi watakaochaguliwa na wanachama kupitia vyama vyao) ili kuleta uwazi na uwajibikaji zaidi katika matumizi ya fedha za wanachama na hasa kupata pia ridhaa yao kuliko ilivyo sasa ambapo maamuzi kuhusu hatima ya matumizi ya mafao yao yanafanywa na watu ambao au hawahusiki kabisa (siyo wanachama) au waajiriwa wa mfuko tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kiambatanisho Na. I, kinaonyesha kuwa hadi 31 Mei, 2009 fedha zote zilizotolewa jumla ni Sh. 5,755,698,950 tu wakati ahadi ya Serikali ni shilingi bilioni 21 yaani wastani wa shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa. Waziri anaweza kueleza tofauti hii kubwa kati ya ahadi ya Serikali na kiasi halisi kilichotolewa na kugawiwa kwa maeneo husika kimesababishwa na nini hasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sababu ipi ya msingi iliyofanya *CRDB* iliyotegemewa kutoa mkopo wa shilingi bilioni 6.2 kutoa tu shilingi 2.04 bilioni na hivyo kuwafikia tu wajasiriamali 1,505; wakati benki ndiyo iliyodhaminiwa kuwa na utaratibu mzuri zaidi wa usimamizi? Kuwa na utaratibu na takwimu hizi kuna haja ya kutumia tena Benki?

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi *(NGO)* ya *SCULT* (1992) Ltd peke yake ilifikia jumla ya wajasiriamali 17,775 na *PRIDE* iliwafikia 43,000. Je, Serikali iko tayari kufanya tathmini na ufanisi wa Taasisi hizi mbili zinazoonyesha mafanikio ya kweli ziimarishwe, ziongezewe nguvu kwa lengo la kutumia uzoefu wao ili kufikia wananchi wengi zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu wa fedha wa 2009/2010, Serikali imetenga fedha kiasi gani katika mfuko huu? Kwa kuwa Mfuko huu ni *Revolving*, hadi sasa una fedha kiasi gani zilizo tayari kutawanywa kwa wajasiriamali wadogo wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kaguzi Maeneo ya kazi, Wizara imefanya jumla ya kaguzi 1,211 nchi nzima, je, katika Wilaya ya Karatu yenye mashamba makubwa ya mkataba 45 ya Kata ya Oldeani na Ganako. Kaguzi ngapi zimefanyika? Mashamba hayo yana matatizo makubwa katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na ajira za watoto kwenye mashamba ya kahawa, kulipa wafanyakazi chini ya kima cha chini cha mishahara, mazingara na hasa nyumba za kuishi wafanyakazi ambazo hazifai kwa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, taarifa ya ukaguzi huo inaweza kupatikana angalau kwa Mbunge ili kuweza kusimamia matokeo ya ukaguzi huo? Je, hoteli za kitalii nazo zinapekuliwa? Kuna malalamiko mengi ya unyanyasaji watumishi, ningependa kujua pia mafanikio gani yamepatikana tokana na kaguzi hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko kesi mbalimbali zinazofika kwa Waziri zinachelewa sana kupata ufumbuzi, kiasi cha kesi zingine kukaa zaidi ya miaka mitano wakati wahusika wa rufaa hizi waliendelea kusota kwa maisha magumu bila kujua hatima yao. Je, tatizo la ucheleweshaji huu ni nini au ni Waziri kutokuwa na muda wa kutosha kupitia makabrasha? Iwapo hivyo ndivyo, si busara kuanzisha chombo rasmi cha kisheria kumshauri Waziri ili kufikia maamuzi mapema? Je, kama ilivyo kwa Mahakama si vema kuweka ukomo wa muda ambapo Waziri atatakiwa kutoa uamuzi wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, *PTA*. Shirika hili lilitangaza ajira mwaka jana na usaili ulifanyika mwezi Agosti na majina ya walioshinda kubandikwa kwenye mbao za matangazo. Watu hao, pamoja na majina yao kubandikwa hawajaitwa hadi leo. Je, kumetokea nini kama kuna tatizo kwa nini wahusika hawajajulishwa au kuna mizengwe gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kima cha chini cha mshahara Serikalini ni shilingi laki moja (Shs.100,000/=) ni kidogo mno, kwani ni wastani Sh. 3,340 kwa siku. Ninaishauri Serikali kulipa wafanyakazi kima cha chini angalu shilingi laki tatu (Shs.300,000/=) kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kufahamu Serikali inamkakati gani endelevu wa kuwatambua na kuwasaidia wafanyakazi wasio rasmi katika maeneo ya Mahotelini, wafanyakazi majumbani, kwenye *bar*, nyumba za wageni kwa lengo la kuwabana waajiri wao kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa aina hiyo. Ninapenda kupata ufafanuzi Serikali ina mpango fani wa kuwasaidia wafanyakazi wanaofukuzwa kazi kiholela hasa katika Mashirika ya Umma yanapobinafsishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufafanuzi, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wajasiriamali wadogo wadogo, wale wanaotembea na jua/mvua na wengine wakiwa wamebeba watoto, kwani imegundulika wanapochukua mikopo hiyo muda wa kurejesha ni mdogo na inapelekea usumbufu kweli, wengine wanaamriwa kuuza hata vitanda vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mheshimiwa Rais au mabilioni ya JK, ni kiasi gani yameweza kuwasaidia wananchi wajasiriamali wadogo wadogo kwani inaonekana tija yake kwa wajasiliamali wadogo wadogo hasa wanawake bado hazijawasaidia ipasavyo. Ushauri wangu ni kwamba zinapotolewa fedha kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa kawaida wasio na ajira kwa lengo la MKUKUTA, ni vema mkaandaa kongamano la kutafuta maoni ya wadau ili lengo lililokusudiwa lipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kunipatia nafasi hii ili nami nichangie. Kwanza nimshukuru Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mrefu vijana wamekuwa na kilio cha ajira na wakati wote vijana wanaamini kuwa ajira ni ile ya Serikali. Kwa vile ajira ya Serikali ina mikataba ambayo humwakikishia mwajiriwa kuwa ajira yake inatambuliwa kisheria. Ni vema vijana wapate stadi mbalimbali za kazi ili vijana waweze kujiajiri wenyewe na Serikali iwe na mpango madhubuti wa kuwakopesha vifaa vya kutendea kazi pamoja na kupewa mahitaji ya kuanzisha miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana washirikishwe katika michezo mbalimbali kwa vile mchezo wa miguu, mchezo wa *netball, volleyball,* riadha, ngumi na michezo mingine mingi. Michezo ni ajira, wafanyabiashara wadogo wapewe mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha biashara zao, ni kweli kwamba vijana wana mitaji mikubwa lakini hawana elimu ya biashara, vile vile mabenki yawe tayari kuwakopesha vijana (wafanyabiashara ndogo ndogo). Vijana wengi wameathirika na ugonjwa wa UKIMWI, Serikali iwe na mpango mahsusi kwa kupitia mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali *(NGO's, CBO's),*

taasisi za dini kutoa elimu ya Ukimwi kwa makundi mbalimbali na maeneo yote ya mjini na vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa vijana, hasa maeneo ya migodi hasa Mgodi wa North Mara katika Wilaya ya Tarime. Wageni wamepewa ajira ambazo zingewezwa kufanywa na vijana wazalendo, kupewa ajira wageni husababisha ugomvi baina ya mwekezaji na wananchi. Naishauri Serikali kuhakikisha kuwa ajira mbazo zinaweza kufanywa na Watanzania wawe wamepewa fursa ya kwanza kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kujenga ofisi ya kudumu ya *NSSF* katika Wilaya ya Tarime, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na uwezo wa kujenga ofisi nzuri, kulingana na mapato yanayopatikana katika ofisi hii ya *NSSF* ya Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitaka Serikali iangalie ajira katika mgodi wa Nyamongo na nipate majibu wakati Waziri anatoa majumuisho, ni wageni wangapi wanafanya kazi ambazo zingefanywa na Watanzania hasa vijana ambao wanatoka katika vijiji vya Mnto, Kewanja, Matongo, Kerende, Nyangoto, Nyamwaga, Genkuru na Nyakunguru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Nashukuru sana.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira na uwekezaji; pamoja na kukubali wawekezaji kuja kuwekeza hapa hapa nchini lakini lazima wapewe mwongozo wa idadi ya wafanyakazi, idadi ya wataalamu watakaohitajika. Kwa mfano, katika *garage* ambazo zinasimamiwa na Wachina, zimekuwa na wafanyakazi kutoka China ambao wanafanya kazi ambazo Watanzania wangeweza kuzifanya. Unakuta kuna Mchina anakwangua gari rangi, ananyoosha magari, kuosha magari na kadhalika hivi kazi hizi haziwezi kufanywa na Watanzania? Je, vijana wetu wanaomaliza *VETA* watafanya wapi kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya Wizara hii kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani, Kitengo cha Uhamiaji na kukagua vibali vya wageni hawa wanapewa vingapi kwa kila mwekezaji? Je, nini tamko la Serikali kuhusu uvamizi wa ajira unaochukuliwa na wageni kwa kazi ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya? Hivi kuna mwekezaji wa Kitanzania anaweza kwenda kuwekeza China, akauza maua ya *plastic* na kupata kibali cha wafanyakazi watano kuuza katika kiduka kimoja tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa mara nyingi Serikali yetu ikiajiri wataalam mbalimbali kutoka nje ya nchi. Lakini hapa Tanzania Serikali imesomesha wataalam wengi tu kwa fedha za walipa kodi kama kwa mfano wataalam wa afya, Walimu, watafiti na kadhalika. Ni wataalamu wangapi ambao walikuwa Watumishi wa Umma waliopo nje ya nchi na ni wa kada gani waliokuwa wanawajibika kwa Serikali na walisomeshwa na Serikali ambao wanakimbilia nje? Serikali inatueleza nini kuhusu rasilimali hii iliyokimbilia nje baada ya kupata elimu kutokana na walipa kodi wetu wa Kitanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa angalizo, kuna wawekezaji wanaomba vibali vya kufanya kazi mfano Mhasibu lakini akishaingia nchini anafanya kazi tofauti kabisa na aliyoombewa nayo kibali. Sio hilo tu, hawa wawekezaji wa ASIA, wanawalipa raia wa kwao mshahara mara kumi ya Mtanzania wakati wanafanya kazi moja. Utakuta Mhasibu ana *CPA* na mgeni anayo hiyo hiyo lakini ukija kwenye mshahara mgeni analipwa zaidi. Je, Serikali inawasaidiaje hawa wazawa wanaonyanyaswa na wageni?

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Prof. Juma Kapuya (Mb), Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga na watendaji wake wote wa Wizara hii pamoja na Mfuko wa Jamii *(NSSF)* kwa juhudi mbalimbali za kusaidia nchi yetu. Napenda pia kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tandahimba ina Benki ya Wananchi yaani *The Tandahimba Community Bank* ambayo imeonyesa kumudu vema shughuli za kifedha. Naishauri Wizara kuipa fedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira ili iweze kusaidia kutoa mkopo kwa wananchi na kujijengea uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inahudumia vijana wengi ambao wasipowezeshwa kiuchumi na kijamii wanaweza kufanya mambo mengi ya ovyo ovyo. Ni vema basi Serikali ikaongeza bajeti ya Wizara hii kwa nia nzuri ya kuijenga nchi yetu vema. Kwa mfano, Wilaya ya Tandahimba kupewa mikopo kwa *SACCOS* mbili tu kati ya nyingi zilizopo ni kama kuongeza manung'uniko kwa wasiopata.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mtwara mjini, lipo eneo la Kiyangu ambalo lilikuwa na nyumba za zamani sana za Shirika la Nyumba. Nyumba hizo zimebomolewa na Halmashauri ilitoa maelezo kuwa *NSSF* wangejenga nyumba mpya za kisasa. Tungependa kuelezwa mpango huu umefikia wapi kwani upole wa utekelezaji wa mpango huo unaleta wasiwasi kwa wananchi wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mwaka jana kulitolewa maelezo ya kujengwa kwa *complex centre* mjini Mtwara na viongozi wa *NSSF*, je, mpango huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uwekwe ili kuhakikisha miradi yote inayozinduliwa na Mbio za Mwenge inaendelezwa. Kwa sasa ipo miradi ilizinduliwa au kuwekewa jiwe la msingi na mwenge lakini baada ya hapo, miradi hiyo haisongi mbele imebaki imesimama. Nashauri kuwe na utaratibu utakaohakikisha mradi ukiwekewa jiwe la msingi au kuzinduliwa na Mbio za Mwenge lazima miradi hiyo iendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri naona tutakupa dakika zako 15 uweze kujibu baadhi ya hoja.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutoa shukrani zangu kwako kwa kunipa

nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ya hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Alhaj Professa Juma Athumani Kapuya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Ukonga wanaokaribia laki nane kwa kuendelea kuniunga mkono katika kusukuma na kuhamasisha maendeleo katika Jimbo la Ukonga. Ukonga niliyoikuta mwaka 2000 wakati nachaguliwa kwa mara ya kwanza si Ukonga ya sasa. Maendeleo makubwa yamekuwepo katika sekta zote za barabara, elimu, maji, afya, ardhi na makazi, michezo na kuondoa umaskini. Hata kero iliyokuwa ikininyima usingizi ya fidia kwa wananchi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila sasa inaelekea kufika mwisho. Naomba wananchi wa Ukonga waendelee kunipa ushirikiano nami kama kawaida yangu sitawaangusha *Inshallah*. Naishukuru sana familia yangu na hasa mke wangu mpendwa Florence a.k.a. Mkandarasi kwa kuendelea kunipa moyo, ushirikiano na msaada mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu ya kifamilia ya Ubunge na ya Serikali kwa ufanisi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo ningependa sasa nichangie mambo machache ambayo yamejitokeza katika Wizara yetu na mengine mengi, Mheshimiwa Waziri atakuja ayatolee ufafanuzi. Nianze na suala la vijana na ajira ya vijana kwa sababu yamejitokeza mengi sana yaliyozungumzwa kwenye suala hili la vijana. Labda nitoe tu ya ujumla ili hata nikikosa nafasi ya kuzungumza kujibu hoja moja moja ya Wabunge niwe nimezungumza la ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wa sasa wa ajira kwa vijana ni kuondoka katika mtazamo wa kutafuta kuajiriwa na kwenda kwenye kujiajiri au kuibua kazi, badala ya kutafuta kazi au kuomba kazi vijana waibue kazi. Kwa Kiingereza tunasema *"We are now changing the youth paradigm from job seekers to job creators*", hili ndio litatusaidia. Lakini niseme kwamba kwa nini ajira kwa vijana bado ni tatizo kubwa. Tukielewa sababu ambazo zinapelekea suala la ajira kwa vijana kuwa kubwa, sisi wote kama Serikali na wadau wakiwemo na Wabunge tutaweza kusaidia sana katika kusaidia vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sababu kama tano au sita ambazo unaweza kusema zinapelekea vijana kukosa ajira. La kwanza kabisa ni kwa sababu ukuaji wa uchumi wetu hauendi sambamba na ongezeko la nguvu kazi. Ongezeko la nguvu kazi ni kubwa kuliko ukuaji uchumi. Kwa hiyo, njia ya kufanya hapa ni kupeleka sasa ukuaji wa uchumi na uwekezaji katika maeneo yanayokuza zaidi ajira, yaani tujielekeze kwenye *Pro-employment investment*. Lakini tukifanya hivyo tunajua kwamba sekta hizo kama za kilimo, viwanda, miundombinu, madini, biashara, usafirishaji, huduma za jamii kama elimu na afya zenyewe zitaongeza ajira kama tujielekeza uwekezaji kwenye sekta hizo. Tunafanya hivyo kama Serikali na wadau wengine.

Lakini pia vijana kutokuwa na elimu hasa ya ujasiriamali, vijana wengi hawana elimu hiyo na wengi wamezungumza hayo. Kwa hiyo, wanashindwa kukabiliana na mahitaji ya soko la ajira, cha kufanya nini? Sisi kama Wizara tunatoa mafunzo lakini wenzetu wa Wizara ya Elimu shule za *VETA*, wadau wengine wanatoa elimu, tunasaidiwa hasa na nchi za nje lakini Makambi ya vijana tuliyoanzisha kutoa elimu ya

ujasiriamali na mafunzo mengine kwa vijana na Makambi ya Jeshi uanzishwaji wa JKT utasaidia sana kwenye suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, vijana kukosa mitaji na hili limezungumziwa sana, tunafanya nini? Kama Serikali ndio maana tumeanzisha *SACCOS*, hizi Benki za Wananchi na Asasi zingine za kutoa mikopo kama vile Vikoba na kadhalika, lakini kuna Mifuko vile vile ambayo inatoa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni vijana kutothubutu au kutokuwa wabunifu katika kuibua miradi inayoweza kusaidia, lazima hii itusaidie. Sasa kwenye suala hili kuna mambo ya mafunzo ya uhamasishaji ili vijana waweze kuthubutu, waweze kuibua kazi mbalimbali na wawe wabunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tano, vile vile kuna tatizo la kutopata taarifa kuhusu soko la ajira au nafasi za kazi ambazo zinajitokeza. Sasa ndio maana sisi kama Serikali tuna *TAESA*, kuna Vyuo Vikuu vinatoa taarifa za kazi na matangazo kama hayo. Lakini vile vile katika hii sekta ya ajira rasmi kuna suala la kukosa uzoefu wa kazi kulingana na mahitaji ya waajiri. Kwa hiyo hili nalo linaweza kuondolewa kwa mafunzo vyuoni, kwenye *VETA* na hata mafunzo kazini ili kuwa na uzoefu wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua waliochangia suala hili ni wengi lakini kwa ujumla nataka niyaseme hayo, lakini kuna mambo mengi sana yaliyozungumzwa kwenye sekta ya vijana. Nikianza na Mheshimiwa Idd Azzan yeye alizungumzia kwa kweli vijana kukosa ajira pale *Leader's Club* baada ya Bonanza kufutwa na Ofisi ya Rais Utumishi. Tumezungumza na Waziri, Mheshimiwa Hawa Ghasia amesema hilo litarekebishwea ili Bonanza ile iendelee na vijana wale waendelee kupata ajira pale *Leader's Club. (Makofi)*

Mheshimiwa Chiza yeye alizungumzia kuwasaidia vijana wa Buyungu Jimboni kwake, ombi limepokelewa, lakini vile vile ushauri kuhusu chokaa inavyotumika kujengea nyumba na vifaa vingine vya nyumba tutaliwasilisha kwa wataalam husika. Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe naye alizungumzia kuandaa vijana ili waweze kujiajiri. Lakini sisi kwa kweli tunaliunga mkono na sisi tunaendelea kutoa mafunzo haya ambayo umeyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Felix Kijiko naye alizungumzia shilingi 5,000,000 kutotosha vijana wake. Kwa kweli kiwango hiki ndio kipo lakini tutaendelea kukiboresha kila ambapo fedha za Serikali zinazokuja katika fungu hili zinatosheleza. Lakini tukumbuke kwamba katika Mfuko wa Vijana tulianza na shilingi 1,000,000 tukaenda shilingi 3,000,000 kwa Wilaya, sasa hivi tuko shilingi 5,000,000 kwa *SACCOS* na shilingi 10,000,000 kwa Wilaya. Kwa hiyo ni maendeleo mazuri lakini tukipata fedha zaidi tutaendelea kuimarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo amezungumzia Mwenge wa Uhuru tuwakumbuke wale vijana. Walikuwa wanapata posho ya shilingi 20,000, imeongezeka sasa hivi ni shilingi 45,000 kwa siku na wakimaliza wanapata *bonus* au

*honorarium* ya shilingi 500,000, kwa hiyo tunaendelea kuthamini mchango wao. Pia mambo ya Vyuo vya *VETA* tumeyazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Godfrey Zambi amezungumzia mbio za mwenge vile vile nimelijibu. Lakini pia amezungumzia suala la zile ekari 800. Bado tuna mkakati mkubwa sana wa kutumia pale Sasandu na kwa sasa maandalizi yako tayari. Mheshimiwa Zambi kama tulivyoahidi bado mpango huo upo na kwa sasa hatutaweza kurudisha baadhi ya hilo eneo katika shamba lile la Sasamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba naye amezungumzia kuhusu wale waliomaliza zamani vyuoni kupata nafasi. Hii ingawaje haifanyiki na Wizara yetu lakini tutawafikishia wale ambao wanahusika ili waangalie kwamba hata wale waliomaliza zamani waweze kupata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sakila amezungumzia masuala ya *SACCOS* kwa umahiri mkubwa na sisi tunamuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Col. Feteh naye amezungumzia kuhusu vyuo vya *VETA* na mafunzo ya JKT. Sisi tunadhani JKT itasaidia sana tunakubaliana na yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed naye amezungumza kuhusu vijana kujiunga na *SACCOS* na suala zima la Sera ya Taifa ya Serikali ya Rasilimali Watu. Hii ya *SACCOS* tunaikubali na hii Sera ya Taifa ya Rasilimali Watu tutashirikiana na Wizara au sekta zingine zinazohusika tuone uandaaji wa sera hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Rwakatare amezungumzia JKU na JKT na sisi tunakubaliana naye. Vile vile Mheshimiwa Sanya amezungumzia suala hilo la JKT ambalo na sisi tunakubaliana naye. Mheshimiwa Susan Lyimo anazungumzia vijana waweze kupewa mikopo ili waweze kujiajiri, huu ndio ufumbuzi na nimetaja kweli tunahitaji mikopo, tunahitaji mafunzo ili vijana waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga amezungumzia kwamba fedha hizi za *SACCOS* na JK zinatolewa kisiasa, hapana. Hizi hazitolewi kisiasa na ndiyo maana zinatolewa kwa *SACCOS* kwa sababu *SACCOS* zinaanzishwa bila ya kuangalia itikadi na wanachama wa *SACCOS* hakuna cha itikadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Raymond amezungumzia suala la mwenge na vigezo vyake ni vingi lakini sifa ni Kidato cha Nne na kuna sifa nyingine nyingi tu ambazo zinahitajika na nitakufikishia ili uweze kuziona hizi sifa.

Mheshimiwa Ligallama amezungumzia ukosefu wa ajira kwa vijana na hili nimelizungumzia hivi vikundi vya vijana havipati nyenzo. Ni tatizo kubwa, tunakubaliana naye. Lakini juhudi zinazofanywa ni kama hizi ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Njwayo naye amezungumzia kuhusu *SACCOS* mbili tu zinapata fedha za vijana. Tatizo bado ni fedha lakini tunadhani tutaendelea kidogo kidogo kuongeza hizo shilingi 5,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, amezungumzia unyanyasaji wa Wamachinga pale Dar es Salaam, tunasema kwamba kweli sio unyanyasaji. Dar es Salaam tumejitahidi sana na bahati nzuri mimi ni Mbunge wa pale Dar es Salaam kujaribu kutenga maeneo ili vijana hawa wafanye kazi kwa kulingana na taratibu. Lakini kwa kweli kila kitu lazima kiende na sheria. Unakuta kwamba unarudi maeneo yale ambayo tumesema sio ya biashara na wanakuwa wakaidi. Lakini ukweli kwamba tumejaribu sana kuboresha mazingira yao ya maeneo ya kufanyia kazi ikiwepo pamoja na hili la Machinga *Complex* ambalo hivi karibuni watagawiwa waanze kufanya kazi.

Mheshimiwa Dorah Mushi amezungumzia *SACCOS* za vijana na sisi tunasema zitaongezwa fedha, yeye anasema ziwe shilingi 20,000,000, tungefurahi kama tungepata fedha kutoka Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji naye amezungumzia kuajiri Maafisa wa Vijana katika ngazi ya Wilaya. Nichukue nafasi hii kueleza kwamba Halmashauri zile ambazo hazijaajiri Maafisa Vijana tafadhali fanyeni hivyo ili tuwe na utaratibu mzuri wa Wizara kufikia vijana katika maeneo yenu kwani kuna Wilaya nyingi hazijaanzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwera amezungumzia suala la ajira na wale vijana wenye virusi vya UKIMWI wasaidiwe, nakubaliana naye. Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Wilson Masilingi tunakubaliana na ushauri wake kuhusu kuhusisha vijana kwenye kilimo kwanza na mambo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa *Youth Resource Centre* Mheshimiwa Juma Killimbah tunakubaliana na wewe. Sasa hivi tuna Sasanda, Ilonga, Marangu na tutaendelea kuanzisha vituo vingine tunapopata fedha. Mheshimiwa Rwakatare nimeshazungumzia suala lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim amezungumzia kwamba, wajasiriamali wadogo wadogo wanaotembea na mali zao wasibughudhiwe. Nimesema hali ilivyo hawabughudhiwi lakini na wenyewe wafuate sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sigonda tumekupata Chunya tutakuja, lakini hizo shilingi 10,000,000 umezipata kama Wilaya zingine zote zilizopata. Kwa hiyo katika hili fedha tu hazitoshi, lakini kuja tutakuja. Kwa Mheshimiwa Sigonda nilikwenda nikiwa Miundombinu, sasa nitakwenda nikiwa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shibiliti amezungumzia kuratibu mbio za mwenge, nakubaliana naye, tutafuata ushauri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mkanga pamoja na Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir wamezungumzia ajira kwa walemavu. Hili linazingatiwa na tutaendelea kuliwekea mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Maida Abdallah amezungumza kwamba, tuwafikie vijana walioko vijijini na ndiyo nia yetu, ndiyo maana tunasema hata hizi fedha katika awamu ya pili za JK zielekezwe vijijini ili vijana na akinamama wa vijijini wazipate zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nuru Bafadhili amezungumzia kuhusu unyanyasaji Dar es Salaam, nimelielezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na ushauri wa Mheshimiwa Ritha Mlaki kuhusu maeneo ya kukuza ajira kwenye maeneo yetu. Suala la vijana limezungumziwa vile vile na Mheshimiwa Paschael Nakei pamoja na Mheshimiwa Chilolo na Mheshimiwa Halima Mdee. Ushauri wenu ni mzuri sana na tumeuzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mikopo ya wajasiriamali kwa kweli Wabunge wengi sana wamezungumzia na hili nadhani Mheshimiwa Waziri atawataja. Lakini niseme tu awamu ya kwanza tumeizungumza hapa mara nyingi kwamba haikwenda vizuri kwa sababu Benki tulizokuwa tunazitegemea zile mbili ni ambazo haziendi sana vijijini, lakini awamu inayofuata sasa tunategemea hizi fedha kwa sababu zinashughulikiwa na vyombo vile ambavyo vinafika mpaka vijijini basi wengi zaidi watapata. Umuhimu wa utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali nimelisema. Mheshimiwa Kimbita, Mheshimiwa Faida Bakar tunakubaliana na tumezingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Savelina Mwijage amezungumzia kero ya fedha hizi kwamba ni za kisiasa nimelijibu sio kisiasa, *SACCOS* ni kwa ajili ya wote. Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa kwa kweli tunazingatia sana maoni yake, fedha hizi ni msingi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Maida Abdallah amezungumzia kuhusu fedha Zanzibar. Tumepeleka shilingi 600,000,000, kwa hiyo sasa kazi kwa wajasiriamali wa kule Zanzibar wakiongeza na zile fedha zilizotolewa na Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dorah Mushi amezungumzia kuhusu Vikoba. Kwa kweli tunakubaliana na tuwaombe Wabunge basi mwendelee kuhamasisha Vikoba vianzishwe kwenye maeneo yenu. Kazi zinazofanywa na wageni atajibu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kidogo nijibu masuala yanayohusu OSHA kwamba haifahamiki. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri na sasa hivi wanajitangaza kwa njia mbalimbali, nina hakika wataweza kufika kwenye maeneo mengi kwa njia ambazo wanatumia sasa ambazo ni redio, magazeti, Siku ya Utumishi wa Umma, Saba Saba na

Nane Nane. Nadhani wengi mliozungumza mtaona OSHA sasa hivi ikiendelea na wamejizatiti sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Asha Jecha, Rita Mlaki wamezungumzia hatua gani zinazochukuliwa kwa wanaovunja sheria pamoja na Mheshimiwa Juma Ali Said. Kwa kweli sheria zetu za kazi tunahakikisha kwamba zinazingatiwa na OSHA wameshapeleka na watu Mahakamani na kuna mfano ambao upo ambao tayari nimewekewa hapa lakini kuna mifano mingine na wakatozwa shilingi milioni tatu. kwa hiyo hatua zinachukuliwa. Kujengewa uwezo OSHA tunakubaliana na wewe, fedha zilikuwa hazitoshi na mpaka sasa hazitoshi lakini kadri inavyoongezeka tutaendelea kuimarisha OSHA na Mheshimiwa Rita Mlaki naye amelizungumzia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TAESA* Mheshimiwa Esther Nyawazwa amezungumzia urasimu uliokuwepo na inawezekana kuona kwamba kuna uwezekano wa rushwa. Niseme kwamba kweli sidhani kama kuna rushwa kwa sababu kwa kweli *TAESA* sana sana katika usaili wao wanaandaa tu kuwapa mbinu za usaili baadae wanakwenda kusailiwa na hao wenye kazi. Kwa hiyo kusema kwamba kunakuwepo na rushwa katika ngazi ya *TAESA* sio rahisi sana, lakini tumezingatia ushauri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NIP*, kuhusu kile kiwanja tuseme kwamba *NIP* na sisi kama Wizara tumesharidhika na fedha ambazo Serikali imefidia na tumesema kwamba hili sasa liishe pamoja na kwamba labda thamani ambayo *NIP* walikuwa wanafikiria jengo lililokuwepo ni kubwa zaidi lakini baada ya malumbano haya tunaona kwamba tumalize hili suala fedha ambazo zimelipwa hizo shilingi 26,000,000 tunaona kwamba sasa tulimalize hili. Namna ya *NIP* kuendelea tunasema tunakubaliana na ushauri wa Msemaji wa Upinzani. Vile vile Shirika liwezeshwe, kwa kweli linafanya kazi nzuri sasa na tutaendelea kuliwezesha. Haja ya kulitumia Shirika la Tija la Taifa sisi Wabunge tusaidie vile vile kuitangaza NIP ili iweze kufanya kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua mengi yamezungumzwa na nisingeweza kumaliza yote kwa kipindi hiki, niseme tu yaliyobaki Mheshimiwa Waziri na kwa sababu wanavyosema “mzigo mzito mwachie Mnyamwezi” na ninaye hapa basi nitamwachia Mnyamwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya Mnyamwezi, basi Mnyamwezi mtoa hoja Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Muda wako utahesabiwa baada ya kutaja majina, Yakitajwa majina ndiyo tunakuhesabia.

**WAZIRI WA KAZI AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Unasemaje Mheshimiwa?

**NAIBU SPIKA:** Ukitaja majina ya Waheshimiwa waliochangia ndio tunaanza kuhesabiwa ule muda.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Sawa sawa.

**WABUNGE FULANI:** Baada?

**NAIBU SPIKA:** Ndio baada ya kusoma majina, akishasoma majina ndiyo tunaanza kuhesabu muda

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kufafanua baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa. Nilidhani vile vile utaniambia kwamba ile akiba alioachia Mheshimiwa Naibu Waziri ya dakika 2 utaniongezea ili niweze kufafanua vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia. Unapofika wakati huu ndipo ambapo unajua kwamba Wizara hii ni muhimu kweli kweli. Kwa sababu pamoja na kwamba ni muda mfupi sana ambao Waheshimiwa Wabunge wamepewa kuweza kutoa hoja zao kuchangia Wizara hii, lakini wengi sana wamejitokeza na kwa kweli mawazo yao ni mengi, yote ni mazuri na tutayafanyia kazi. Katika kujibu hoja inawezekana tusipate nafasi ya kujibu hoja zote, lakini zote ninawahakikishia tumezichukua, tutakwenda kuzifanyia kazi kwa dhati kabisa na tutakuwa tunatoa taarifa mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niwataje kwa maana ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata nafasi ya kuchangia katika Wizara yetu hii ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Waheshimiwa Wabunge waliochangia wakati wa bajeti ya Serikali ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Haroub Masoud, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Mwajuma Khamis, Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Zuleikha Haji, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Ibrahim Sanya na Mheshimiwa Maida Abdallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza leo hapa waliopata nafasi ni Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Salim Khalfani, Msemaji wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Guido Sigonda, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Halima Mdee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Dr. James M. Msekela, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy**,** Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Mch. Dr. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Lucy Owenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Asha Mchimba Jecha, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Col. Feteh Mgeni, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhan, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud. Lakini vile vile bila ya kumsahau Mheshimiwa sana Dr. Milton Makongoro Mahanga ambaye alichangia kwa kuzungumza. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naanza kujibu au kufafanua baadhi ya hoja ambazo muda utaniruhusu. Kwanza naomba nimshukuru sana aliyewasilisha ripoti kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Hoja zake kwa kweli zilikuwa za msingi sana na tumelizingatia katika ufafanuzi ambao tutaendelea nao huko mbele kama itakavyodhihirika. Lakini vile vile nimpongeze na kumshukuru rafiki yangu ambaye naendelea kutumainia kivuli kwa jinsi alivyochangia hapa leo. Inaelekea ni mtaalam sana wa kusoma historia lakini si mtaalam wa kusoma *current affairs*, kwa hiyo ni habari za sasa. Kwa hiyo mtu anaweza akawa naishi kwa kuangalia historia, historia bila ya kuangalia yale ambayo yaliyopo ya sasa hivi. Kuna mabadiliko makubwa sana katika sekta hii ya utoaji haki kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, anaposema kwamba kuna watu ambao wanazuiwa kupata kazi au kufukuzwa kazi kwa misingi ya kisiasa katika nchi hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nashangaa kiongozi ambaye yuko Bungeni hapa anaweza akatoa kauli hiyo. Kama anao ushahidi atuletee ili tuweze kufuatilia na tutoe majibu hapa Bungeni. Nina hakika katika sekta hii ya kazi hakuna mtu anaonewa kwa misingi ya itikadi yake ya chama, hakuna mtu anaonewa kwa misingi ya itikadi yake ya rangi, wala ya kabila wala ya jinsia, lakini kama upo ushahidi atuletee. Kuimarisha shughuli zisizo za viwandani sawa sawa. Machinga *complex*, anasema ni porojo tupu. Hivi kweli Waheshimiwa Wabunge hatuoni adha wanaopata Machinga hawa wanapokuwa

barabarani. Tunataka kuwatoa barabarani na kuwapa mahali pa kufanyia kazi unasema hizi ni porojo za kisiasa. Hivi kweli Waheshimiwa Wabunge ndio tumefikia hapo. Lakini nataka niseme kwamba tutaendelea, lakini kubwa zaidi inaelekea Mheshimiwa aliiamulia *NSSF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nifafanue suala la *NSSF*. Katika hotuba yake ya leo asubuhi Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani aliwasilisha hoja kadhaa akidai kuwa ni vielelezo vya utendaji mbaya katika Shirika la Taifa la Hifadhi la *NSSF*. Kabla sijajibu hoja za Mheshimiwa Salim Khalfani nataka kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa tarehe 22 Juni 2009, Mheshimiwa Samuel Sitta, Spika wa Bunge letu wakati anamkaribisha Dr. Wilbrod Slaa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, alitoa mwongozo kuwa kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Mbunge yeyote haruhusiwi kuzungumzia suala lolote ambalo lipo kwenye Kamati husika ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia mwongozo huo wa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa hoja zote zilizowasilishwa na Mheshimiwa Salim Khalifani dhidi ya *NSSF* na hoja ya maandishi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Slaa kuhusu mkopo wa Kiwira zinatokana na hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaani *CAG* ambayo ripoti yake itajadiliwa na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma yaani *POAC* katika Bunge hili. Hivyo basi Mheshimiwa Khalfani na Mheshimiwa Dr. Slaa hawakupaswa kuzungumzia hoja hizo. Lakini cha kushangaza zaidi jioni hii amejitokeza naye Mheshimiwa Halima Mdee ambaye ni Mjumbe wa *POAC* anayajua haya. Sasa nashangaa yeye amesimama hapa kusema yale yale, lakini tuendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Khalfani amewasilisha hoja hizo hapa Bungeni na ambazo zimeingia kwenye *hansard* na kwa kuzingatia uzito wa madai yake ni vema nikazitolea maelezo hoja hizo ili kuweka kumbukumbu sahihi kwani baadhi ya hoja alizozitoa Mheshimiwa Salim Khalfani si za kweli. Katika mchango wake, amedai kuwa *NSSF* ni shirika maarufu sana na kwamba umaarufu huo umejengwa kwa lengo la makusudi ili kufunika udhaifu wa Shirika hilo. Nadhani Mheshimiwa Mdee karudia hayo hayo, yeye akaenda mbele zaidi akasema hata uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji lazima tuuwekee alama za kuuliza. Kauli hizi ni nzito sana na ingekuwa vema Mheshimiwa Mbunge alitolee ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wake Mheshimiwa Khalfan ameeleza matatizo ya *NSSF* katika maeneo ya utoaji wa mikopo, uwekezaji unaofanywa bila kupata gawio na kutowashirikisha wanachama katika uwekezaji wa michango yao. Kama nilivyogusia hapo awali masuala aliyoyataja Mheshimiwa Khalfan yamo katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali yaani *CAG*, hata hivyo napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa ripoti hiyo bado haijakamilika. Mnano tarehe 27/5/2009, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma (*POAC*) ilikutana Dar es Salaam ili kujadili ripoti ya *CAG*. Hata hivyo, kabla ya kikao hicho mnamo tarehe 20 Mei, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Bwana Ludovick Uttoh kwa barua yake Kumb Na. DF 37/641/19/12 alimwandikia Katibu wa Bunge kumwomba

aahirishe mjadala kuhusu hesabu za *NSSF* za mwaka 2007/2008 kwa kuwa utaratibu za ukaguzi haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako naomba niisome nusu ya sehemu ya barua hiyo ambayo inahusu ripoti hii.

*"Tarehe 20 Mei, 2009 Katibu wa Bunge, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, S.L.P. 9133, Dar es Salaam.*

*Ratiba ya Vikao vya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kuanzia tarehe 25 Mei hadi tarehe 4 Juni. Nakiri kupokea barua yako pamoja na ratiba yenye Kumb…….ya tarehe 11 Mei, 2009 iliyonakiliwa kwangu inayohusu somo tajwa hapo juu. Napenda kukujulisha kuwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imepokea ratiba ya Vikao vya Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma na itatoa ushirikiano wa kutosha katika kuhakikisha vikao hivyo vinafanyika kwa ufanisi unaotakiwa.*

*Sambamba na hili, napendekeza mabadiliko ya tarehe ya vikao vya kujadili hesabu za PPRA, TCRA, NSSF na TBC zisogezwe mbele kutokana na taratibu za kaguzi kutokamilika. Kwa hiyo, ripoti hizo ziko katika hatua za kupelekwa kwenye bodi husika kwa ajili ya kusainiwa."*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya Mheshimiwa Mdee anayajua lakini nashangaa karudia hapa kaja kusema kwamba tuhukumu kabisa. Sasa pamoja na hayo na ushauri wa *CAG*, Kamati iliona vema kikao kiendelee siku iliyopangwa. Katika kikao cha siku hiyo Mei, 27/2009, Kamati ilibaini na kuridhika kuwa ripoti iliyowasilishwa na *CAG* ilikuwa haijakamilika na kumwagiza *CAG* akamilishe taratibu za ukaguzi na kuwasilisha ripoti mbele ya Kamati haraka iwezekanavyo. Haya ni maagizo yoliyotolewa katika Kamati ambayo Mheshimiwa Halima Mdee alikuwemo. Leo ananukuu ripoti ile ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 22 Juni, 2009. *NSSF* ilimwandikia *CAG* kuomba kufanyike *exit meeting* ili kuwezesha ripoti iwasilishwe katika vikao vya Bodi na hatimaye kwenye *POAC*. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa *exit meeting* ni sehemu muhimu sana ya taratibu ya ukaguzi na kwamba wakati *CAG* alipowasilisha ripoti ya mwanzo kikao hicho hakikufanyika kama ilivyokuwa inatakiwa. *Exit meeting* ni kikao ambacho wewe ukishanikagua unakaa na mimi na kuniambia bwana katika ukaguzi huu nimekugundua wewe una udhaifu huu, huu na huu. Wewe unasemaje? Nakusingizia? Nami nakwambia hapana, katika hayo mzee ushahidi wake huu hapa, mengine ulikuwa hujayaona. Hii haikufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 1 Julai, 2009, Maafisa wa *CAG* walikutana na wale wa *NSSF* ili kupitia hoja na vielelezo mbalimbali ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya *exit meeting.* Katika vikao hivyo hoja nyingi zikiwemo zile ambazo Mheshimiwa Khalfan amezitaja leo asubuhi ziliondolewa baada ya Wakaguzi kuridhishwa na majibu ya *NSSF*. Kwa mfano, hoja ya uwekezaji katika *Pension Properties Ltd*. Kampuni ambayo inamilikiwa na *NSSF, PPF, PSPF* na *LAPF*. Kupitia kampuni hii Mashirika haya ya pensheni yaliweza kujenga jengo hili la Bunge katika uwekezaji huo. Hadi sasa *NSSF* imeshalipwa na Serikali Sh.5.26bn/= kati ya sh.

11.8bn/= zilizowekezwa na shirika.  Hoja nyingine zilizofutwa ni pamoja na Ubungo *Plaza*, *EPZ, First Adil* na nyingine nyingi. Lakini hapa si mahali pake watawasilisha ripoti hiyo baada ya kupitia taratibu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 9 Julai, 2009. Kikao cha *exit meeting* kilifanyika baina ya Maafisa wa *CAG* na *NSSF*, katika kikao hicho Wakaguzi wa *CAG* waliliridhika na majibu ya *NSSF*. Hivyo kukubali kufuta kwenye ripoti yao hoja nyingine nyingi zaidi.  Kwa mujibu wa ratiba waliyokubaliana baina ya *NSSF*, *CAG* na Ofisi ya Bunge, ripoti ya mwisho ya Mkaguzi Mkuu kuhusu hesabu za *NSSF* kwa mwaka 2007/2008 itatolewa kesho Ijumaa tarehe 17 Julai, 2009 kesho.  Baada ya hapo itafuatiwa na kuwasilishwa na kuripotiwa kwenye Kamati ya *NSSF* inayoshughulikia mahesabu. Kikao hicho kimepangwa kufanyika tarehe 20 Julai, 2009 na kikafuatiwa na kikao cha Bodi ya Wadhamini ya *NSSF* ambacho kitafanyika tarehe 23 Julai, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanyika vikao hivyo ndipo ripoti ya *CAG* itakapowasilishwa kwenye Kamati ya *POAC* itakayokutana hapa Dodoma tarehe 1 Agosti, 2009.  Sasa kama ni tarehe moja haraka ya nini.  Nimeona nilizungumze suala hili kwa kirefu sana kwani taarifa aliyoitoa Msemaji wa Upinzani akiungwa mkono na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ni potofu na inapotosha ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, dai kwamba *NSSF* haiwashirikishi wanachama wake katika kuwekeza katika michango yao.  Dai hili nalo si kweli.  Maamuzi yote ya uwekezaji mkubwa kama vile mikopo, majengo na kadhalika yanafanywa na Bodi ya Wadhamini ya *NSSF*.  Uwakilishi wa Bodi hiyo ni ya utatu yaani Serikali, Wafanyakazi na Chama cha Waajiri Tanzania.  Haiwezekani wanapotaka kufanya maamuzi ya uwekezaji waite wanachama wote, sasa jamani tunataka kujenga jengo la Ubalozi, Nairobi mnasemaje wanachama?  Ni kama sisi Waheshimiwa Wabunge hapa tupo 300 lakini tunaamua maslahi na tunatunga sheria kwa niaba ya Watanzania milioni arobaini. Hivi ndivyo sera ya uwakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini wa *NSSF*, hupendekezwa na taasisi husika yaani vyama huru vya wafanyakazi na chama cha waajiri Tanzania.  Waziri mwenye dhamana na masuala ya wafanyakazi huteua wajumbe kwa kuzingatia mapendekezo hayo.  Hivyo basi si kweli kudai kuwa maamuzi ya uwekezaji yanafanywa bila kuwashirikisha wanachama ambao ni waajiri na wafanyakazi.  Ninapoletewa majina yale naangalia tu katika yale matano wamepanga moja, mbili, tatu, sina sababu ya kusema watano awe watatu. Nateua kwa jinsi walivyoniletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya *NSSF* kuwa inaajiri watumishi bila kufuata utaratibu, napenda kulifahamisha Bunge lako milioni arobaini.  Hivi ndivyo sera ya uwakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini wa *NSSF* hupendekezwa na taasisi husika yaani vyama huru vya wafanyakazi na chama cha waajiri Tanzania.  Waziri mwenye dhamana na masuala ya

wafanyakazi huteua wajumbe kwa kuzingatia mapendekezo hayo.  Hivyo basi si kweli kudai kuwa maamuzi ya uwekezaji yanafanywa bila kuwashirikisha wanachama ambao ni waajiri na wafanyakazi.  Ninapoletewa majina yale naangalia tu katika yale matano wamepanga moja mbili tatu, sina sababu ya kusema watano awe watatu.  Nateua kwa jinsi walivyoniletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya *NSSF* kuwa inaajiri watumishi bila kufuata utaratibu, napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa ajira zote za *NSSF* zinafuata utaratibu ambao umeainishwa katika Kanuni za Utumishi za Shirika.  Ajira za watumishi wa kada ya chini yaani ngazi ya mshahara wa *NSSF* yaani moja mpaka nane zinafanywa na Kamati ya Ajira na Nidhamu.  Ajira za kuanzia ngazi za NSSF 9 -12 zinafanywa na Bodi ya Wadhamini.  Nafasi hizo za ajira hutangazwa ndani ya Shirika kwanza endapo hakuna mtumishi anayekidhi vigezo vilivyowekwa.  Nafasi hizo hutangazwa katika magazeti.  Hii kutangaza ndani ya Shirika kwanza inawapa motisha wafanyakazi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuendelee na hoja zingine.  Kamati ya Maendeleo ya Jamii inasema *NSSF* iendeleze mradi wa daraja la Kigamboni.  Shirika linaendelea na hatua za kutekeleza mradi wa daraja la Kigamboni na linahusisha hatua kubwa zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kwanza kumpata mshauri mwelekezi wa kuliongoza Shirika katika kumpata mbia katika uwekezaji, Julai 2009.  Pili kumpata mbia mmoja kati ya Makampuni sita ambayo yametambuliwa Septemba 2009, kufanya mapitio ya pamoja ya mradi wa *NSSF* na mbia binafsi na kufanya usanifu wa kina Novemba, 2009.  Kufanya hatua za kumpata mkandarasi wa kujenga daraja, *procurement of contractors* Januari 2010.  Kujenga daraja lenyewe na barabara za pembezoni Machi, 2010 ujenzi wa daraja unatakiwa kuanza. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge *progress* ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiumbwa, Makame Mbarouk, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Daina Chilolo, Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Bujiku Sakila, wametoa pongezi nyingi kwa Shirika la *NSSF*. Nazipokea pongezi hizo kwa niaba ya Shirika na nawashukuruni. Mheshimiwa Masilingi anasema *NSSF* iwawezeshe vijana Kata ya Ikondo Nshamba, Jimbo la Muleba Kusini katika mradi wa umwagiliaji.  *NSSF* iwasaidie wavuvi Kata ya Mazunga, wapewe mitumbwi na nyavu.  Tunasema *NSSF* itatuma wataalam wake kufanya upembuzi yakinifu na miradi iliyotajwa ili kuona namna ya kuwasaidia wajasiriamali wa Muleba Kusini.

Mheshimiwa Charles Mwera wa Tarime anasema *NSSF* ijenge ofisi nzuri katika Wilaya ya Tarime inayolingana na mapato yatokayo Tarime.  *NSSF* iko mbioni kujenga ofisi katika Wilaya ya Tarime.  Sasa hivi Shirika hilo katika mchakato wa kupata kiwanja kujenga ofisi hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Charles Mwera wasaidie kupata kiwanja kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fatma Othman Ally ametoa pongezi kwa kuendeleza mradi wa daraja. *NSSF* inaendelea na mchakato wa uendelezaji mradi wa daraja la Kigamboni tumeshaeleza. Mheshimiwa Kiumbwa Makame anasema utekelezaji wa mradi wa daraja la Kigamboni nao tayari nimeshaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo anasema Serikali isaidie *NSSF* kurejeshewa mikopo wanayoitoa kwa taasisi mbalimbali. Ushauri utazingatiwa lakini nataka nikuhakikishie kwamba Serikali yenyewe ni mlipaji mzuri sana na hili vilevile nataka nimhakikishie Mheshimiwa Halima Mdee kwamba katika watu wanaolipa vizuri katika Shirika la *NSSF* anayeongoza ni Serikali. Kwa sababu madeni yao wanalipa kabla hata hayajaiva. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali litumie Bunge Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kufuatilia madeni ya *NSSF*, suala hili limezungumzwa na Mheshimiwa Sakila. Ushauri huu ni mzuri, hata hivyo suala la kufuatilia mikopo ni suala la utendaji zaidi, hivyo basi ni vema likaachiwa watendaji. Kamati ya *POAC* ifuatilie kwa karibu kwa kudai taarifa za utekelezaji. Mheshimiwa Bujiku Sakila anauliza ni lini *NSSF* itakwenda kujenga nyumba za bei nafuu Wilayani Kwimba kwa ajili ya wafanyakazi au kama mradi huu hauwezekani basi *NSSF* ijenge nyumba za Polisi. Uongozi wa *NSSF* utapeleka wataalam kufanya upembuzi yakinifu kuona namna ya kutekeleza miradi hii. Kuna tatizo gani Hazina kuhusiana na jengo la TBC 1? Uchambuzi wa mradi huu na wataalam wa Hazina uko ukingoni utamalizika hivi karibuni.

Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy anauliza *NSSF* inawafikiriaje wananchi wa kipato cha chini? Kwanza kabisa Shirika linawashauri wananchi wote wanaopata mapato kujiandikisha na kuchangia vizuri katika Mfuko wa NSSF, kwa kufanya hivyo watakuwa wamepiga vita umaskini. Kwa upande mwingine *NSSF* inafanya miradi yenye manufaa kwa jamii ili kuwasaidia watu wenye kipato cha chini. Miradi hii ni kama ujenzi wa Jengo la Machinga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Idd Azan anasema *NSSF* ijenge majumba ya kibiashara eneo la Magomeni *Quarter* Wilaya ya Kinondoni. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya *Pension Properties Limited* iliyoundwa kwa pamoja na Mifuko ya Pensheni kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, *NSSF* imefikia wapi katika ujenzi wa nyumba za kisasa katika eneo la Kiyangu, Mtwara Mjini? *NSSF* iko katika mpango wa kuendeleza eneo lililotajwa tayari mazungumzo yamefanywa na uongozi wa Mkoa pamoja na Kampuni ya Artmus kwa ajili ya upangaji wa nyumba hizo.

Mheshimiwa Fuya Kimbita anasema Mashirika ya Hifadhi ya Jamii yaongeze ufanisi ili kuboresha matumizi ya fedha, huduma nzuri na uwekezaji. Ushauri umepokelewa na utazingatiwa katika shughuli za Shirika

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Slaa amesema mkopo wa Kiwila ulitakiwa kurejeshwa ndani ya miezi 18. Naomba nimfahamishe Mheshimiwa Slaa

kwamba hili limo katika ile ripoti ya *CAG* lakini kwa kukudokeza ni kwamba *default notice* imeshapelekwa kwa mdhamini wa mkopo huu ili iweze kulipa mkopo wake. *NSSF* hawakopeshi bila kuwa na kinga ya kutosha kweli kweli.

Mheshimiwa Juma Ngasongwa, *NSSF* isitumiwe kama chombo cha kutimiza malengo ya bajeti ya Serikali kama vile kujenga madaraja, ofisi za Serikali na hospitali. *NSSF* inafanya miradi mbalimbali kama sehemu ya uwekezaji, maamuzi yote yanafanyika katika misingi ya kibiashara na si maagizo ya Serikali. *NSSF* kwa kweli hapa Tanzania mpaka sasa ina maamuzi mengi sana ambayo inafanya yenyewe kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi au faida ya miradi ile. Hivi ndivyo ambavyo nchi nyingine nyingi zimetumia sana mashirika haya ya hifadhi ya jamii kujenga maeneo yao. Ukienda Geneva utakuta mji ule sehemu kubwa sana umejengwa na mashirika ya hifadhi ya jamii. Kwa hiyo, hili si tukio la hapa Tanzania tu Mheshimiwa Ngasongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mdee anauliza huduma ya ulinzi. Kampuni ya *Alliance*. Hivi anaiunganishaje na mimi? Mbona simwelewi? Kwamba kampuni iliyopo Tabora ikipata kazi basi ni makosa. *That is not fair, is not fair at all*. Lakini nataka nimwambie kampuni hii ya ulinzi ya *Alliance* imepata zabuni ya ulinzi kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kampuni hii si ya Mheshimiwa Kapuya na hakuna mgongano wa maslahi, kampuni hiyo ina uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni hii imepewa kazi ya ulinzi kama vile *TTCL, NHC* na kwamba imepata *tender* Moshi na Arusha. Ngoja nikwambie mimi natoka Urambo, kuna kampuni ya wakandarasi kutoka Mara inajenga barabara Urambo tena katika kijiji cha Kaliuwa. Kwa hiyo kama ame-*win tender* unamkataza tu kwa sababu hatoki Kaliuwa? Haiwezekani, nchi hii ni huru, kila mtu atafanya kazi kutokana atakavyotimiza vigezo. Ndiyo leo nasikia kama kuna hii kampuni, sasa nashangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuzaji wa *Club* ya *Oasis*. Mwenye kampuni ya *tiles* ambaye ndiye alikuwa mteja wao aliliarifu Shirika kwamba ununuzi huu urtafanywa na kampuni ambapo ulikuwa mbioni kuisajili. Kwa hiyo ilikuwa ni kampuni ya *tiles* badae ikajibadilisha jina kuitwa kampuni ya *Club* ya *Mesh*. Kwa hiyo taratibu zingine kama ulivyoshauri tutazifuata na hasa katika uuzaji wa nyumba za Ada *Estate, tender* zilitangazwa

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Diana Chilolo, *NSSF* iwajengee nyumba wafanyakazi mikoani. Ushauri umepokelewa, hata hivyo wakaguzi wa *NSSF* unategemea uchambuzi yakinifu ya miradi husika kama inaonekana na faida watafanya hiyo kazi. Serikali ilipe madeni ya *NSSF* nilishalizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sanya, anasema Wachina kupora ajira za vijana. Walete mitaji na teknolojia pamoja na kujenga viwanda. Waheshimiwa Wabunge suala la Wachina nadhani tunalikuza sana. Lazima tufahamu kwamba hawa wachina ni rafiki zetu, ni wenzetu. Ukienda ukahesabu wachina walioko pale Kariakoo, hawafiki 50 ila kwa sababu ni wachina basi inaonekana kama wamefanya dhambi. Wapo

wachina wameingia kihalali nchi hii wana vyeti vyao, wapo wachina ambapo wameoa dada zetu, kwa hiyo dada zetu wanawawezesha wanafanya biashara hizo. Lakini nakubali wapo wachina ambao wameingia si kihalali. Hao tutawashughulikia na tunawashughulikia kwa taratibu za kawaida kabisa. Lakini tukianza kuli-*dramatise* hili suala la wachina hapa tunaweza tukazua mambo ambayo ni makubwa zaidi. Mfahamu nchi hii inao marafiki wa kutegemewa na katika marafiki hao hakuna kama China. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sanya amezungumzia suala la *strategic investors*, nakubaliana naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shibiliti anasema kazi ambazo zinatangazwa huwa tayari zina watu wake tayari. Kwa hiyo, hata vijana wanapojiandikisha kule *TAESA* ni kutimiza wajibu kwa sababu kazi ile imeshachukuliwa. Nataka nikufahamishe Mheshimiwa Shibiliti kazi zinazoletwa *TAESA* Wakala wa Ajira, hazina wenyewe. Anakuja mwajiri mwenyewe anasema jamani nina tatizo, natafuta wafanyakazi wa aina hii. *TAESA* inamwambia kama ni mfanyakazi wa aina hiyo hawa hapa. Anachukua sita, saba, nane anakwenda kuwasili mwenyewe. Kwa hiyo anayeamua nani anamchukua pale ni yeye mwenyewe mwajiri si kwa utaratibu wa nyuma ya milango, si kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafanyakazi wageni wanafanya kazi katika sekta mbalimbali je, tumewafuatilia kuona kwamba wana nyaraka halali? Nimeshazungumza jinsi ambavyo tunawafuatilia. Nimesema wapo ambapo wana nyaraka za kugushi, tukiwakamata tunawachukulia hatua na kuwarudisha makwao. Wapo ambao wanashitakiwa. Vilevile kaguzi mara ya mwisho imefanyika Juni, 2009. Baadhi ya kazi zinazofanywa na wageni zinaweza kufanywa na wazawa. Je, utaratibu kwa sasa ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mpendazoe, Mheshimiwa Zulekha, Yunus Khaji, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Lucy Owenya, lakini tuna matazo. Tuna matatizo matatu. Katika *Hotel Industry* tuna matatizo ya *hospitality* ili mgeni anapofika ajisikie. Tuna tatizo hilo. Mfanyakazi anakwenda Hotelini amekasirika utafikiri umegombana naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kama ulilolitaja wewe mwenyewe mawasiliano na watu mmekazana tufute kabisa Kiingereza. Hili ni tatizo katika *hotel industry*. Lingine kubwa zaidi ni la uaminifu. Tuna tatizo kubwa sana na uaminifu na limeshakuwa tatizo la Kitaifa. Mgeni akisahau simu tu imeshanyakuliwa. Sasa mwekezaji anakuja anataka kujenga *five star hotel* anakwambia Kapuya nina tatizo hili, ama nafunga *hotel* au unanipa kibali naleta wasaidizi kutika sehemu fulani. Wewe ungekuwa Waziri wa Kazi ungefanyaje? Nimeshaanza kuzungumza hata na Mkurugenzi wa *VETA* naomba nisaidie kuweka culture ya uaminifu katika mtaala wako. Ameliona hilo na wameanza kulifanyia kazi. Nisaidie kuwafundisha watu wajue Kiingereza wajue kuwasiliana, tumeliona hilo na tumeanza kazi kwa kubadilisha hata sifa za kujiunga na *VETA* unapotaka kuingia katika masuala ya *hotel*. Lingine ni *mind set* ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Tabora *Textile* tuna matatizo kule. Watu wanaambiwa kiwanda hiki bado kichanga. Kiwanda hiki hakiwezi kufanya kazi kwa siku sita na kufunga siku ya Jumapili. Tubadilishe ratiba tufanye shift tatu baadae Jumapili tuwe tukifanya kazi hawataki. Wanasema tunafanya kwa mtindo huu Jumapili hatufanyi kazi. Sasa haiwezekani. Sisi hapa Wabunge tunajitolea kufanya kazi Jumamosi wengine hawataki. Mind set haijabadilika, tunalo tatizo na hili lazima mlijue.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni la Mheshimiwa Serukamba, amezungumza suala zuri sana ambalo anasema wawekezaji wanaanza kuonekana kama vile hawahitajiki nchi hii. Waheshimiwa Wabunge humu sisi ndiyo wa kwanza kuwatukana wawekezaji na kuwakashifu wawekezaji na vyombo vya habari navyo vinadaka, kazi yake kila siku ni kumtafuta mwekezaji kumpaka matope. Hatuwezi kwenda namna hiyo. Ajira haiwezi kutengenezwa nchini kama wawekezaji wanaanza kujisikia nchini kwamba haiwezekani. *Barrick Gold* wame-*cut down* uwekezaji kule North Mara. Walikuwa wawekeze Dola milioni 150, kwa sababu ya kauli zinazotoka katika magazeti na kauli zinazotoka Bungeni wanaanza kujisikia hawatakiwi, wamepunguza mpaka kufikia Dola milioni 40, ni hasara kwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo makosa yanayofanywa na tuviache vyombo vya Sheria vifanye kazi tusiwahukumu sisi kisiasa. Sisi kazi yetu ni kutekeleza Sera ya Serikali. Kwa hiyo namuunga mkono Mheshimiwa Serukamba kwa sababu *really* tulikuwa na Mashirika ya Umma tuliyafikisha wapi? Hivi tumebadilika kiasi gani? Nawaambia tuna matatizo hapa, nenda kwa *Vice Chancellor* wa *UDOM* hapo. Amelalamika mpaka kwenye vyombo vya habari wachina wanavyoibiwa *material* pale *stores*. Kwa hiyo, Mchina akija na kusema kwamba Mheshimiwa *stores* nataka *Material Manager* awe Mchina unamkatalia vipi na wakati kila siku anaibiwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la migogoro ya vyama vya wafanyakazi nadhani tumelizungumza sana katika ripoti yangu. Naomba kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge tunajitahidi sana kutoa elimu kwa kuzungumza na waajiri na Vyama vya Wafanyakazi kwamba hatukutani navyo si kweli na aliyeongoza jahazi la kukutana navyo ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Alishatumia karibu siku saba kukutana na Vyama vya Wafanyakazi mbalimbali na hatimaye Mheshimiwa Rais kakutana nao tena Ikulu na akala nao na chakula cha mchana. Tumezungumza mengi. Kwa hiyo ukiuliza Vyama vya Wafanyakazi kwa mawasiliano kati ya wao na Serikali mpaka viongozi wa ngazi za juu wanaridhika kwelikweli. Sasa Waziri wa Kazi ndiyo mwenzao kabisa, kila siku anacheza nao mpira tu. Nataka kuwahakikishia kwamba sisi hatuna tatizo na Vyama vya Wafanyakazi. Yapo matatizo ambayo lazima tuendelee kuyashughulikia, kama malimbikizo ya madai ya Walimu ni kweli lakini na wao wajue kwamba fedha hizi tunazikusanya polepole, kitu muhimu ni kwamba sisi tumeshakubali kwamba madeni hayo yapo tunayalipa, uhakiki umekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume wengi wamesema inafanya kazi nzuri iongezewe fedha. Nashukuru sana kwa hilo kwa sababu kwa kweli Tume inajitahidi na imepunguza kesi nyingi sana. Zile kesi ambazo zilikuwa zinachukua miaka mitano kama

Mheshimiwa Slaa alivyosema, sasa hazichukui miaka mitano, tumeweka muda maalum kwamba ni siku thelathini lazima kesi ziishe na ndiyo maana utakuta katika ripoti niliyoitoa hapa kulikuwa na kesi zaidi ya 5,000, zimebaki kesi 1000 na kidogo. Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba kumaliza kesi 4000 kwa mwaka mmoja si kazi ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, waajiri kutoheshimu maamuzi yanayotolewa kwa mujibu wa Sheria. Hii ilikuwa zamani kwa sasa hivi *CMA* na Mahakama ya Kazi ambayo ni Kitengo cha Mahakama Kuu hawana mchezo tena. Kwa hiyo, sasa hivi kila hukumu inayotolewa inatekelezwa. Kwa hiyo, iliyokuwepo hapo ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kukomesha ajira kwa watoto tunapokea ushauri huu na kwamba tutaendelea kulifanyia kazi. Wafanyakazi wanaofanya kazi kwa mkataba wa miezi mitatu wanakosa uaminifu na uadilifu. Hili kuna Mheshimiwa Mbunge amesaidia kulisema na wanashauri kwamba wapewe mikataba ya miaka mitatu ili wawe waaminifu zaidi. Ukipewa miezi mitatu ndipo unapopimwa, wewe unaiba, nitakupa miaka mitatu kweli? Haiwezekani! Unapopewa miezi mitatu mitatu ndiyo kwa kujionesha kwamba wewe ni malaika ili uweze kuajiriwa kwa muda mrefu zaidi. Msimamo wa Ofisi ya Kazi Mbeya unalenga kumtetea Mjenzi wa Barabara Mbeya. Mgogoro huu umepokelewa na utafanyiwa kazi kwa sababu ni mgogoro mpya ambao tumeupokea sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mengine nasema tutaendelea kuyafanyia kazi na tutawasilisha ripoti kama nilivyosema. Naomba….

**NAIBU SPIKA:** Hawakusikia kama unatoa hoja au vipi.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema baada ya kusema haya, hoja zilizosalia tutaendelea kuzifanyia kazi na tunazipokea zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru usipotoa hoja wenzako hawakuungi mkono na sisi tunaikataa. Mnyamwezi ameamua kusema taratibu sijui vipi. (*Kicheko*)

## KAMATI YA MATUMIZI

### Matumizi ya Kawaida

### Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

Kif. 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ... ... ... shs 2,039,157,000/-

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sijawaona nyie wote warefu. Mheshimiwa Mongella na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Wambura. (*Kicheko*)

**MHE. DR. GETRUDE I. MONGELLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona pamoja na urefu nilionao. Hii inatokana na *donation* niliyofanya kwa wale warefu. Napenda niseme jambo moja la msingi ambalo Waziri atanisaidia kwa kutambua kwamba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kwenye kifungu gani?

**MHE. DR. GETRUDE I. MONGELLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Bado kabisa na Waheshimiwa wengine Mshahara wa Waziri bado. (*Kicheko*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 – Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana**

Kif. 1001 - *Administration and General...* ... …. …. …. …. ….Shs.2,055,620,400/-

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ningependa kwanza niseme sina haja ya kuchukua shilingi ya Waziri, nadhani atanielewa kuwa kutokana na kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii katika hali ngumu ya uchumi, ningependa tu nisisitize jambo moja Mheshimiwa Waziri anisaidie. Tumeweka kwamba kilimo kwanza na watakaolima wengi ni vijana, hatuwezi tukawa na kilimo kama vijana hawajawezeshwa na kuwezeshwa kwa vijana ni katika taaluma na tekinolojia. Katika bajeti hii sikuona uzito wa pesa zilizotengwa kuwawezesha vijana hawa kujenga huo uwezo ambao utawawezesha kuchangia katika sehemu kubwa ya kilimo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, sikuona kabisa jinsi tulivyokuwa *committed* kama nchi kuwawezesha vijana kwa sababu hata ukienda sekta ile ya *development,* pesa nyingi zimetoka katika nchi za nje bila *local component*, sasa inakuwa kama mtu unayetegemea jirani kumlisha mwanao badala ya wewe kuchangia na hili linasikitisha sana. Kama tunasema vijana ni muhimu, basi tuone hata katika tafsiri ya bajeti yetu kwamba kuna uwezeshaji katika *development* ambao unawasaidia vijana wetu katika nchi hii. Haya nayasema pia nikiwa ni Kamanda wa Vijana Mkoa wa Mwanza.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa niaba ya Waziri kwamba, Mheshimiwa Dr. Mongella amesema suala la muhimu sana. Lakini niseme kwamba katika suala zima la

kilimo kwanza, imani yangu ni kwamba, katika zile programu zote za kilimo tunazozungumzia kwenye Wizara ya Kilimo, ni muhimu sana kule sasa kwenye utekelezaji tukahusisha vijana kwenye hizi programu, ziwe za *irrigation*, ziwe za kilimo, *ASDP* pamoja na programu zote ambazo hata zile za kutumia sasa teknolojia kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini vijana wakitumika vizuri, kilimo kwanza kitaweza kuonekana. Sasa kuona hiyo dhana ya kilimo kwanza kwenye Wizara ya Kazi unaweza usiione sana kwa sababu programu zote za kilimo zinakwenda kwenye Wizara Mama na naamini kule ndiko sasa vijana wanatakiwa wahusishwe na waweze kutekeleza hii dhana nzima ya kilimo kwanza.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la nyongeza tu ni kwamba hii Serikali ni moja. Kilimo kwanza tunachokusudia kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Rais ni vitu vitatu:- Moja, kuelekeza *resources* nyingi zaidi katika kilimo. Pili, kusimamia suala zima la *transfer of technology* na la tatu ni kuongeza tija katika kilimo ili kiweze kuvutia vijana. Kwa hiyo, naamini kwa kuwa Serikali ni moja na wenzetu wakiwa wanajua kwamba tunacho Kituo cha Malangu ambacho ndicho chenye kutoa teknolojia ya kilimo kwa vijana, kwa hiyo tutaendelea kushirikiana chini ya *umbrella* hiyo kuweza kuhakikisha kwamba zile fedha ambazo Serikali imetenga kupitia Wizara ya Kilimo na kupitia kilimo kwanza, vijana wananufaika na vituo vya vijana ambavyo tunavyo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru sana kwa majumuisho mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini naomba nipate ufafanuzi. Kwa kuwa nchi yetu imekuwa ikijibadilisha kutokana na hali ya maendeleo na mabadiliko ya mtazamo wetu kiutendaji na hivyo kusababisha kuwa na vyuo vya kutosha katika mitaala mbalimbali na vile vile watu wengi sasa hivi wamekuwa wakijisomea katika umri mkubwa na kwa kuwa matangazo mengi ambayo yanatoka kwa ajili ya kazi utakuta yanazungumzia umri usizidi miaka 45, lakini muda wa kustaafu kwa ulazima ni miaka 60 na kwa hiari miaka 55. Je, kwa kufanya hivyo, hatuoni kama tunapunguza idadi ya watalaam ambao wamepata utalaam katika umri wa miaka kati ya 45 mpaka 50 kuweza kutumika katika soko letu la ajira?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali, hatukatai kuajiri mtu kuanzia miaka 45, isipokuwa ajira kuanzia miaka 45 inakuwa ni kwa mkataba kwa sababu ukiajiriwa kuanzia miaka 15, haikuwezeshi ku-*qualify* kufikia miaka ya kukuwezesha kupata pensheni kama watumishi wengine. Ili mtumishi uweze kupata pensheni, ni lazima uwe umeuchangia ule Mfuko zaidi ya miaka 15. Sasa ukiajiriwa zaidi ya miaka 45, utakuwa ni chini ya pale. Kwa hiyo utakuwa unaajiriwa lakini kwa masharti ya mkataba ambao hauna pensheni, ni kiinua mgongo tu.

**MWENYEKITI:** Lakini, *concept* aliyoeleza, mtu kuajiriwa siyo lazima Serikali. Hiyo aliyosema Waziri wa Utumishi ni Serikalini, sivyo? Sasa yule anayesoma lazima aajiriwe Serikalini?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo lazima anayesoma ajiriwe Serikalini, anapokuja kuajiriwa nje ya Serikali, taratibu hizi hazimhusu. Utakuta kuna watu wanaajiriwa katika makampuni makubwa, wanaajiriwa hata wazee wenye miaka 55 mpaka 60 mradi tu wameona kwamba una uzoefu wanaohitaji. Kwa hiyo, ndani ya Serikali, *yes*, kwa sababu kuna hilo suala la pensheni, lakini nje ya Serikali, taratibu ni zingine, kinachohitajika pale ni uzoefu wako na uwezo wako na jinsi unavyoweza ku-*negotiate*.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja na mshahara wa Waziri, lakini naomba ufafanuzi kidogo. Kutokana na mtikisiko wa hali mbaya wa uchumi duniani, Serikali inawasaidia kuwanusuru kiuchumi wakulima na wafanyabiashara na hasa mabenki yale ambayo yananunua mazao ya wakulima na inawezekana wakapata hasara na Serikali imeamua kuongezea pesa mabenki yale ambayo yananunua mazao kwa wakulima. Sasa, swali langu ni kwamba, mfanyakazi ambaye mtikisiko wa uchumi umempata, yeye anasaidiwaje na Serikali yetu?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mfanyakazi hagusiwi moja kwa moja na mtikisiko wa uchumi, isipokuwa mpaka kampuni anayoifanyia kazi ikiguswa na mtikisiko huo. Kinachotokea, kampuni kama ikiguswa na mtikisiko huo, inapunguza wafanyakazi au inafunga viwanda. Lakini wakati mwingine wanachukua njia za kuweza kushauriana na kujadiliana na wafanyakazi hawa namna ambavyo wanaweza wakanusuru ajira. Nitakupa mfano, *New Mwanza Hotel* baada ya mtikisiko huu na baada ya ile *minimum wage* mpya kutangazwa, walikaa na mwajiri wakasema, tuchague, ama tufunge Hoteli au tukubaliane kubaki na mashahara huu tulionao ambao si mbaya sana ili kuweza kunusuru ajira. Wakakubaliana, wamenusuru ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la kiwanda Camel Apelel. Camel Apalel pale umetokea mtikisiko, kwa bahati mbaya imebidi yule Bwana afunge kiwanda kabisa. Sasa pale kilichotokea ni kwamba imebidi wafanyakazi wale walipwe haki zao zote pamoja na haki za kuachishwa kazi kama mkataba wa hiari unavyosema. Sasa mkataba wa hiari ndio ambao unaweza kumnusuru mfanyakazi. Sasa ninachosema ni kwamba, ndio maana tunasema kwa sasa hivi jamani wafanyakazi na sisi Serikali na Wabunge, kazi yetu ya kwanza iwe kulea kazi tulizonazo. Tunapowatishia hawa tulionao, matokeo yake ndio haya. Hii *rescue packages* mnayosikia katika nchi mbalimbali kwa mfano Ujerumani, Serikali ya Ujerumani ilichofanya, imeingia mpaka mkataba na waajiri jinsi ambavyo wanaweza wakafidia ule upungufu wa mapato ya kampuni zile ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawafukuzwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkisoma habari za *British Airways (BA)* mpaka wafanyakazi wamechelea kufanya kazi kwa saa za ziada bila kulipwa mshahara. Sasa mfanyakazi wetu, hii *altitude* ya *mind set* bado, ndio maana unaweza ukakuta kwamba mwajiri anapokabiliwa na hali hii, *option* aliyonayo ni kumfukuza mfanyakazi au kupunguza wafanyakazi au kufunga kiwanda. Tushirikiane katika majadiliano ya pamoja tuweze kufikia muafaka ili kuweza kunusuru ajira.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nazungumzia ajira na wageni kutoka nje. Mara nyingi wawekezaji wanavyoajiri watalaam kutoa nje watu wa *profession* mbalimbali kama madaktari, mainjinia, manesi na kadhalika wakiwaleta kutoka nje huwa wanawalipa mishahara mikubwa sana kuliko wale waajiriwa wa hapa nchini na hii inawapelekea wataalam wetu wengi kukimbilia nchi za nje kwenda kutafuta ajira. Ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, je, Wizara yake ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba watalaam wetu wa ndani wanapata mishahara ambayo kidogo inafanana na wale wa nje ili tusiwapoteze watalaam hao kwa kukimbilia nje?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaokimbia kutoka nchini mwetu kwenda nchi za nje, siyo wale walioajiriwa na makampuni ya wawekezaji, nataka nikuhakikishie kwamba walioajiriwa na makampuni haya wanaendelea kutumikia makampuni haya ndani ya nchi. Lakini, tunawasaidiaje? Moja ya kazi kubwa ya Wakala wa Ajira Tanzania *(Tanzania Employment Services Agent – TAESA)* ni kuwafundisha watu wetu stadi za usaili. Hapo ndipo ambapo tunapozidiwa. Kijana amemaliza Digrii yake Chuo Kikuu, wakati mwingine hata na *Masters*, wakati mwingine hata ana *PhD*, anapopeleka *application* yake kuomba kazi, akiitwa kwenye *interview*, wanamwambia sasa wewe Bwana tunafikiria tunaweza tukakuchukua, unafikiria tukupe mshahara gani? Anasema mzee nipe mshahara wowote tu, kule nje kuna jua kule, wewe ni wowote tu utakaonipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu mwingine anapoulizwa, je, tukupe mshahara gani, anasema ili unitoe hapa nilipo mpaka nije katika kampuni yako, nipe shilingi kadhaa. Yule mwenye kampuni anasema hizi siwezi kukupa, atamweleza, wata-*negotiate* mpaka watafikia mahali. Wa kwetu anasema nipe kazi yoyote, mshahara wowote. Sasa hiyo ndiyo kazi ya *TAESA* wanajaribu kuwasaidia vijana hawa namna ya kuweza kuzungumza vizuri ili kuweza ku-*benefit*. Unatikisa kichwa Mheshimiwa Lucy Owenya nakuona, lakini ni kweli kabisa, mimi mwenyewe wamekuja Ofisini, Mheshimiwa Waziri naomba unisaidie kupata kazi, kazi gani? Wanasema yeyote! Wanakuja Ofisini kwangu, kama unataka nitakuwa nawarekodi! *(Kicheko)*

**MHE. IDD M. AZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi nilimwomba Waziri wa Kazi anisaidie wale vijana ambao siku ya Jumapili huwa wanakuwa pale *Leaders* kwenye *Bonanza*, wanafanya biashara zao ndogo ndogo, wengine wanacheza mpira pale, wakimaliza, kuanzia saa 09.00 mpaka saa 12.00 wanacheza muziki na huku biashara zinaendelea. Lakini wamefungiwa na Ofisi ya Rais – Utumishi kwamba wasiendelee na shughuli zile na nimekuomba kwamba suala langu angalau ulifikishe basi kwa wahusika tuone tunawasaidiaje vijana wale. Nataka kufahamu tu Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa suala hili utalifikisha kwa wahusika ili vijana wale waweze kuendelea na shughuli zao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hilo lilishafika kwetu siku nyingi hata

kabla ya hapo. Isipokuwa kabla yeye hajaleta, kuna wenzake ambao walileta wakilalamika kwamba katika lile eneo la *Leaders Club* watu wanapiga muziki mpaka saa 08.00 za usiku. Kwa hiyo, Ofisi yangu ilichofanya ni kwamba tulikataza zile shughuli zinazoendelea mpaka zaidi ya saa 06.00 za usiku. Kwa hiyo, tumeruhusu. Huo muda anaosema yeye tulishawaandikia kwamba wanaruhusiwa kufanya shughuli zao zote zinazoishia saa 12.00. Kwa hiyo, Mheshimiwa amesikia kama wanauza mpaka saa 12.00 waendelee. Lakini tulichokataza kutoka katika ofisi yangu ni zile shughuli ambazo zinakwenda mpaka usiku wa manane na watu wanaokaa maeneo ya karibu wanashindwa kulala. Kwa hiyo, tunawaruhusu mwendelee kupitia hii na kupitia barua ya Katibu Mkuu wangu. Mwisho, 12.00 au saa 02.00 kwa kibali maalum.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nikichangia kwa kuzungumza, nilidokeza zile fedha za JK kwa wajasiriamali. Bahati nzuri katika Jimbo langu wale wajasiriamali walihamasishwa na wakaenda kujaza fomu, lakini hawakuweza kupata hizo fedha. Kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri, sijui anaweza kutamka vipi kuhusu wale wajasiriamali ambao walitumia muda wao, walitumia fedha zao kwa kwenda kufuata hizo fedha kule kwenye Tawi la Benki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru!

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyokuwa tukijibu hapa mara nyingi na leo tumejibu, ni kweli kwamba awamu ya kwanza wengi sana wakiwemo vijana hawakupata zile fedha za Mfuko wa JK kutokana na *CRDB* na *NMB* kutofika maeneo hasa vijijini. Tumesema kwamba katika awamu ya pili, vyombo ambavyo vitatumika ni vile ambavyo vina mtandao mpaka vijijini. Lakini vile vile tumesema kwamba, hili tunaendelea kuzungumza sasa na wenzetu wa *CRDB* ambao wanaendelea na kutoa awamu ya pili, fedha zile zinazozunguka, zinazorudishwa ziende sasa kwenye maeneo au kwenye *SACCOS* ambazo hazikupata mara ya kwanza ili ile *concept* ya *revolving* iweze kuonekana, zisirudi kwenye *SACCOS* zile zile au watu wale wale ambao wamesharudisha ili na wengine waweze kuzipata. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba hili la Wilaya ya Chunya na kwenye Jimbo lake, nadhani litaweza kushughulikiwa kwa namna hiyo.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na taasisi anazozisimamia zote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Lakini pia naomba niipongeze Serikali kwa kuwawezesha wananchi wa Tandahimba na Newala karibu bilioni 1.1 awamu ya pili. Wananchi wa Wilaya ya Tandahimba kwa kushirikiana na Mbunge wao, wamejenga Benki ya Wananchi pale Tandahimba. Ili kujenga uwezo na kurahisisha huduma za pesa hizi za kuwawezesha wananchi, nadhani wakati umefika sasa Wizara au Waziri kuzitaka taasisi zilizo chini yake kupeleka pesa kwenye Benki hiyo kama inavyofanya kwa Mwanga *Community Bank*. Hii itasaidia sana kwa sababu Tandahimba iko katikati ya Newala na Mtwara pamoja na Mtwara Vijijini. Ningependa kupata *commitment* ya Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana fedha hizo ziweze kufika kule bila matatizo. Lakini kama tunavyofahamu, fedha hizi za Mfuko wa JK zinashughulikiwa na Benki Kuu wakishirikiana na Baraza la Uwezeshaji. Kinachoangaliwa ni kwamba, je, vyombo hivi vya fedha vinakuwa na Benki Kuu kwa sababu kuna masharti ambayo Benki Kuu ili ichukulie kwamba Mfuko wao au Chombo hiki ni *Micro-Finance* kuna vigezo vyake. Sasa Mwanga *Community Bank* tayari inakuwa *regulated* na Benki Kuu. Sasa hii ya Tandahimba kama iko tayari basi ni suala ambalo linaweza likazungumzika kwa sababu wao vile vile wamo katika ile *Micro-Finance Institutions* ambazo zinatambuliwa. Kwa hiyo, nadhani walete maombi ili katika hatua zinazofuata, basi Benki Kuu washauriwe kuweza kupitisha hela katika Benki hiyo. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kuuliza swali moja. Nataka kuzungumzia Mfuko wa JK. Kwa kuwa Jimbo langu la Kilwa Kaskazini si mmoja aliyefaidika na huu Mfuko kwa sababu ya umbali wa kuwa na hizo Benki na Benki kwa kweli kule kwangu hakuna. Sasa sijui vyombo gani hivyo ambavyo atavifanya vitafika kule kwangu Kilwa Kaskazini? Ningeshauri ingekuwepo labda *Mobile Bank*, labda hapo tungeelewana! Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilwa kwa mujibu wa taarifa ni kwamba ilipata milioni 91. Lakini inawezekana kabisa kwamba katika upande wa Jimbo lake, fedha hizi hazikufika. Ni kama tulivyokuwa tunazungumzia suala la Geita. Kwa hiyo, kitu muhimu kwa kweli hapa ni kuangalia katika awamu zinazokuja, je, tumejipangaje katika kuwafikia huko. Ambacho tutashauri vyombo hivi ambavyo sasa vitashughulikia kusambaza awamu hii ya pili, vijaribu kwenda kwenye maeneo ambayo hayakupata. Naamini tukifanya hivyo, awamu ya pili, basi Kilwa Kaskazini itaweza kupata mgao kwa wajasiriamali wake na Wana-*SACCOS*.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Sina lengo lamkutoa shilingi ya mshahara wowote, lakini ningeomba tu ufafanuzi. Pamoja na pongezi ambazo nimezitoa kwenye maandishi, lakini kwa muda nimekuwa nikizungumzia hata kushauri kivipi watu wenye ulemavu ambao wengine wamebahatika kusoma na wengi wao hawajasoma, lakini Mungu amewajalia kuwa na vipaji vya kuweza kutafuta chakula na wengine hawawezi kabisa, lakini, mara zote bado ninatukutia kwamba sijaona dhamira iliyo sawa sawa. Sasa, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza kwamba mwaka huu kutakuwa na jitihada ya kurekebisha awamu ya pili ya sheria za kazi na ajira. Katika hilo ndilo ninaloliuliza, sheria basi za awamu ya kwanza, namshukuru Mungu nilishuhudia kuwepo humu Bungeni na tulizipitisha. Kulikuwa na kijisentensi tu kimoja, "ajira haitabagua kutokana na ulemavu". Kanuni zake sijui zimeenda wapi au utekelezaji ukoje? Utekelezaji wa ile haukuwa makini, yaani bado sijaelewa kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa naomba kuuliza je, katika haya marekebisho yaliyosomwa hapo awali, kuna mikakati gani mahususi jamani, yaani ya dhamira ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu waliosoma angalau wanapata ajira

rasmi? Pia wale wa vijijini ambao wengi hawajasoma, lakini wana vipaji wanawezeshwa vipi kuweza kujiajiri kwa kukopeshwa? Mikopo hii yote mnayoisema hawapati. Kwa sababu kama wazima hawapati, uniambie mwenye ulemavu ambaye hata darasa hajaliona, je, katika sheria hizi kutawekwa nini ambacho kweli kitatekelezeka? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zimekuwa katika matumizi tangu 2004 mpaka leo 2009, karibuni miaka mitano, zimeonekana zina upungufu fulani fulani katika utendaji kazi, ndiyo maana tumesema tuzirejee. Kama kawaida ya zinazotungwa na Serikali, huwa kipindi kikifika wadau wote husika wanashirikishwa. Kwa hiyo, namkaribisha Mheshimiwa Mkanga na wengine, tutakapokuwa tunarejea sheria hizo, waje tukae nao ili waone bado kuna upungufu au hakuna upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu mikopo. Mikopo hii kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, fedha inaratibiwa na Benki Kuu na ile Kamati ya Taifa ya Uwezeshaji, sisi tunafanya kusimamia. Lakini zinapokwenda kule kuna Kamati ya Kijiji kama ni mtu mmoja mmoja, zinaanzia vijijini. Pale kijijini wanasema, huyu tunamfahamu, ana biashara, anaweza. Ikitoka pale inakwenda kwenye Baraza la Kata, Kata inasema huyu tunamfahamu, anaweza na biashara anayo. Ikitoka pale inakwenda moja kwa moja Benki. Kwa hiyo, kazi yako kule ndio kwenye kusimamia, sisi na Madiwani tusimamie kule. Lakini kama ni suala la *SACCOS, SACCOS* yenyewe inaanzia katika ngazi ya Wilaya, Wilaya ndiyo inasema kwamba hawa tunawafahamu wanaweza. Sasa nasema ndugu zangu, haya mengine, tukiwa wakali kule katika ngazi ya Halmashauri, katika ngazi ya Vijiji na Kata ndipo ambapo tutawawezesha hawa watu wenye ulemavu kupata. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Vile vile nimshukuru Waziri kwa majibu yake ambayo yalikuwa na hisia kidogo. Nilitaka tu nitoe ufafanuzi kidogo kwamba sidhani kama Spika alisema ripoti ya *CAG* isijadiliwe, Spika, *ruling* yake ya kipindi kile aliitoa akielekeza masuala maalum ambayo alikuwa ameipa Kamati ifanyie kazi. Kwa hiyo, sidhani kama ni vizuri kupotosha kwa sababu tunafahamu Kamati zinatoa taarifa mara moja kwa mwaka na ripoti ya *CAG* inatoka mara moja kwa mwaka. Sasa kama hatutakuwa hatuijadili *the whole year*, halafu tunasema kwamba tusubiri kwa kuwa iko kwenye Kamati, itakuwa *wrong*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika kwenye barua ambayo Mheshimiwa Waziri amei-*refer*, haizungumzii yale masuala ambayo nimeyazungumza, yale *CAG* hayajafanya marekebisho, kwa hiyo alitakiwa ayajibu, *unless* useme kwamba kuna mabadiliko ambayo wewe unayaona kwako binafsi kutoka kwenye hii ripoti ambayo siyo sahihi, kwa hiyo ameyarekebisha kwa maono yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza kwenye suala langu kuhusiana na Baraza la Vijana. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie mchakato wa uundwaji wa Baraza la Vijana umefikia wapi na wanahusishwa kiasi gani vijana katika mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Naomba ujibu hilo la mwisho.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ee maana hata mimi nilishangaa umemruhusu maswali matatu yote! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Vijana. Baraza la Vijana ingekuwa kama ni kweli wanaohusika ni CCM peke yao na Serikali iliyoko madarakani ni CCM, tungeliunda jana. Tungeliunda jana kwa sababu ingelikuwa ni makubaliano ya ndani tu. Lakini tunachotaka uwakilishi ulio mpana zaidi na kama utakumbuka katika vikao vya awali, watu maarufu waliokuwa wakishiriki katika vikao vile ni Mheshimiwa Zitto Kabwe. Mheshimiwa Zitto Kabwe siyo CCM, ni CHADEMA, unafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni Baraza ambalo litakuwa na uwakilishi wa watu wote. Hatuwezi kusema tutagawana kwamba huyu asilimia 10, asilimia ngapi, itategemea kuchangamka tu. Sasa tumefikia wapi? Karibu tunamaliza sasa muundo wa *structure*, ushauri tumekwisha kamilisha, tunaingia sasa katika utaratibu wa kutengeneza muundo. Huo muundo itabidi wadau wenyewe waujadili tena waone kama tunakubaliana. Baada ya hapo sasa ndiyo Baraza litaundwa. Hatutajali nani anatoka wapi, tutakachotoa ni mwongozo wa namna ambavyo mtu anaweza kuwa kiongozi katika Baraza lile. Inawezekana wapo watu ambao wameanza kuhamasisha vijana katika maeneo yao, hilo sisi halitupi hofu sana, kwa sababu tunajua wakati utakapofika, vijana wenyewe watajichuja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nataka kupata ufafanuzi zaidi juu ya shamba la Sasanda ambalo liko Mbozi, Kata ya Nyimbili na Vijiji vya Masangula na Nyimbili

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukru pia Naibu Waziri alipokuwa anajibu hoja amelielezea suala hili, akasema kwamba tusiombe ardhi kwa sababu wana mkakati wa matumizi juu ya eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti niseme kwamba nimekuwa nalizungumza hili jambo kwa muda wa miaka miwili au mitatu hivi na kama wiki moja hivi nimelizungumza pia na Mheshimiwa Waziri Kapuya. Lakini ninachoshangaa tunaelezwa kwamba tusiombe eneo hili kwamba mkakati wa matumizi upo. Sasa tunaposoma kitabu cha Waziri cha bajeti sioni chochote kinachotajwa kwa ajili ya kuendeleza eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapopitia kwenye kitabu cha maendeleo sioni pesa zozote za kuendeleza eneo lile. *Then* naambiwa kwamba kuna mkakati wa matumizi ya eneo lile ndipo nashindwa kuelewa. Sasa hapo ndipo tunapofikiri pengine majibu haya ni majibu ya kisiasa zaidi kuliko ukweli wenyewe wananchi wanatuelewa vipi? Namwomba Waziri anipe mkakati walio nao nikirudi kule Mbozi nizungumze na

wenzangu kwamba jamani Wizara ina mkakati wa kulitumia eneo hili ili wasindelee kunituma hapa Bungeni.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Zambi kwamba Wizara ina mkakati wa kuendeleza eneo hili. Ni kweli tumechelewa na sisi tunaelewa *sentiments* zake lakini kwa sasa mikakati ambayo tunayo na kama ambavyo tumeamua kwa kweli ni kwamba tutumie yale mashamba kama mashamba darasa ambayo yatatumika kwa ajili ya kuleta ufanisi na elimu zaidi ya kilimo kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya msukumo huu sasa wa kilimo kwanza ndiyo tunaona umuhimu mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba kweli yale mashamba tunayatumia vizuri ili kuboresha hali ya kilimo hususan katika kuwapatia vijana stadi za kilimo na kuwa kama nilivyosema mashamba darasa. Sasa hili tunaendelea kulifanya, inawezekana, usilione lakini kadri tunavyoendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo hasa katika huu mpango wa kilimo kwanza yeye ataona baada ya muda mfupi jinsi ambavyo tutaanza kuendeleza maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoanza sasa hivi tumeomba fedha za nyongeza kwa ajili ya kuboresha vituo hivi vya vijana ikiwepo na Sasanda. Hazina pamoja na Benki Kuu wanaendelea kuangalia maombi yetu, nina hakika haya maombi yakipita ambayo yanalenga katika kukuza kilimo katika nchi yetu na kuwapa ajira vijana na stadi za kilimo tutafika mahali tutaona jinsi ambavyo tutatumia eneo hili vizuri. Kwa hiyo, yeye aamini kwamba tuko katika mikakati hiyo na tutawasiliana naye kwa sababu ni kwenye Jimbo lake, tunapofanya uendelezaji huu au kuendelea kuboresha eneo hili.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa kuzungumza hapa Bungeni pamoja na wa maandishi nilizungumzia mambo mengi sana. Lakini napenda nipate maelezo kwenye jambo moja tu, niliongelea juu ya vijana hawa wanaoathirika na madawa ya kulevya pamoja na bangi, kwamba vijana hawa sasa ni wengi na wanasumbua familia na jamii hata Taifa pia linadhalilika. Nikashauri kwamba, Serikali ifike mahali ione uwezekano wa kutenga maeneo kwa angalau kila Mkoa au hata baadhi ya Mikoa vijana hawa waanze kutunzwa pale wanasumbua sana lakini Mheshimiwa Waziri hajanipa maelezo.

**MWENYEKITI:** Alikosa muda, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli katika mkakati wa kushughulikia vijana wala hatuwezi kutenga kwamba sasa hawa ni wavuta bangi kwa sasa au hawa ni wazururaji au hawa wanafanya nini ili tuweke mikakati ya kuwasaidia vijana. Kwa kweli tunaweka mikakati ambayo itasaidia vijana ambao wako tayari lakini tunajua kwamba suala la kuvuta bangi na madawa ya kulevya ni suala ambalo linashughulikiwa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kikosi maalum cha kupambana na suala hili. Sisi tuko tayari pale ambapo hawa vijana wamekubali kuacha tabia hiyo ya kuvuta bangi na

kutumia madawa ya kulevya tuweze kushirikiana nao. Tuone wako tayari namna gani tuweze kuwasaidia katika kutoa Elimu ya Ujasiriamali, katika kuwapa mitaji kama wako tayari kwa sababu kama tusipoangalia ile athari ambayo wanayo tayari unaweza kuwapa mtaji kwa ajili ya kujiajiri wakaenda kuvuta bangi zaidi ikawa kwamba hatukusaidia katika suala zima la kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo twende na suala vilevile la elimu na sisi Wabunge tusaidie. Mheshimiwa Chilolo nimemweleza kwamba mimi Mke wangu Florence anajaribu kuwalea hawa vijana wavuta bangi pale Segerea kwa maana kwanza ya kuwashawishi waache bangi halafu awasaidie na kama anawapa mradi anasimamia ili zile hela anazotoa kidogo wasiendelee kuvuta nazo bangi au madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani na sisi wengine wote tukishirikiana tuondoe kwanza ugonjwa huo wa kuvuta bangi na madawa ya kulevya halafu sasa sisi tuje na mikakati ya kuwasaidia vijana. Lakini wazo lake ni zuri tu namshukuru.

**WAZIRI WA AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Kwa nyongeza tu kidogo katika majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri sisi Wizara ni sehemu ya Tume ya kuzuia Utumiaji wa Madawa ya Kulevya. Katika Tume ile ili kukabiliana na tatizo hili kwa wale ambao wameathirika tunachofanya kutokana na mpangilio wa Kitaifa tunapo mahali ambapo tunawapeleka ili wakapate matibabu, wapate kurejeshwa katika hali ya kawaida ambapo ni hapa Hospitali ya Mirembe Dodoma, kuna kitengo kabisa kinachoshughulikia wagonjwa wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge kama kwake hili ni tatizo tuwasiliane tumwelekeze vizuri namna ambayo anaweza akatumia fursa zilizopo kuhakikisha kuwa wale vijana wanakarabatiwa kwa utaratibu uliopo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif 1002 - *Finance and Accounts*... ... ... Shs. 286,176,000/=
Kif 1003 - *Policy anad planning*... ... ... Shs. 474, 599, 100/=
Kif 1004 - *Internal Audit Unit*... ... ... ... ...Shs.108, 959,600/=
Kif 1005 - *Procurement Management Unit*... ... ... ... ...Shs.172, 887, 900/=
Kif 1006 - *Infor, Education an Communication Unit*... ... ... ... ... ... ... Shs. 141,645, 200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif 2001 - Labour... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 2,175,686,300/=

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kujua kwenye ile *title ya Programme* 20 inasema ni *Labour and Workers Participation,* lakini ukija kwenye ile *subvote* 2001 inaonyesha *labour* peke yake. Nilikuwa naomba kuuliza kama pia ni pamoja na *workers participation,* lakini nilikuwa naomba kujua ile *sub-item* 221100 ya *travel out of the country* ukiangalia utaona kwamba katika mwaka huu fedha hizo zimeongezeka zaidi ya shilingi milioni mia moja thelathini na tano, nilikuwa naomba kupata ufafanuzi, je, ni watu wengi zaidi wanaosafiri au ni kitu gani?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo fedha zimeongezeka, kwanza viwango vya safari vimeongezeka na kwa sababu sasa hivi tunasafiri kwa *activity* tumeweka kwa zile safari ambazo ni muhimu na tumeona kwamba zitagharamiwa kwa kiasi hicho kwa kuzingatia taratibu. Kwa hiyo, gharama zimepanda, nauli zimepanda na posho zimezidi.

**MWENYEKITI:** Ile ya kwanza programm 20 inasema *Labour and Workers Participation, Subvote* 2001 inasema *Labour,* 2002 inasema *Employment Division,* 2003 inasema *Registration of Trade Unions,* kwa hiyo *Programm* hiyo inahusika .

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif 2002 - *Employment Division... ...* ...Shs2,517, 780, 800/=

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho cha 2002, kifungu kidogo cha 270600 kinachosema *Current Grand to Non Financial Public Units Agencies,* napenda nijue hizi ni *Agencies* zipi na zinafanya kitu gani?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *Agency* ambayo iko pale ni *CMA* ambayo inapata *Grand* kutoka kwenye Serikali kwa ajili ya shughuli zake ambazo zinafanyika kwenye Wizara.

**MWENYEKITI:** Ni nini hiyo inaitwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Comission for Mediation and Abitiration* (Tume ya Usuluhishi na Uamuzi).

**MWENYEKITI:** Kule tulikopitisha ile *vote* 15?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA**: Ndiyo *grant*.

**MWENYEKITI:** Yaani inatoka kwenye vote 15?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA**: Inakuwa sasa na *subvote* zake.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, nilizungumzia kuhusiana na malengo ya MKUKUTA ambayo pia ni sehehemu ya....

**MWENYEKITI:** Kifungu gani? Tunaongea sasa kwenye *specific.*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** *Subvote* 2002, *Employment Division,* kifungu 221200 *Communication and Information*. Katika mchango wangu, nilizungumzia suala zima la ajira na malengo ya MKUKUTA VS ILANI YA CCM ambapo kwa mujibu wa *target* ya MKUKUTA kuanzia mwaka 2001 hadi mwaka 2010, malengo yalikuwa ni kupunguza ukosefu wa ajira kutoka 12.5% hadi 6.5%. Nilitaka tu Mheshimiwa Waziri anifafanulie katika zile ajira mpya alizozitangaza ni asilimia ngapi imepungua toka ile ya kwanza ya malengo ya MKUKUTA mpaka sasa hivi mwaka 2009 kuelekea mwaka 2010 ambapo *target* ilikuwa ni 6.5%.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, hii hapa ni shilingi milioni ishirini na moja na laki sita, sasa hii unayozungumza wewe ni sera ndio maana pale kwa mshahara wa Waziri tunazungumza zote, hizi hapa ni shilingi milioni ishirini na moja hauwezi kuzungumza unayosema. Kwa hiyo, kifungu unachozungumzia siyo?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ni *Employment.*

**MWENYEKITI:** Hata kama ni *Employment*, hapa inahusu mishahara yao, *stationary* zao *nothing else*. Sera anazisimamia huyu Mheshimiwa Waziri siyo hapa. Tunaendelea, hakuna kujibu Mheshimiwa Waziri, hiyo nimekwishajibu mimi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu hicho hicho, *sub-item* 221200, *Communication and Information*. Ninavyoelewa katika *Employment Division*, sasa hivi tuna tatizo kubwa la ajira na nilikuwa nategemea kitengo hiki cha *Communication and Information* kingekuwa kinatoa taarifa nyingi kwa vijana kuhusu ajira, lakini ukiangalia utaona kwamba katika fungu hili kimepungua kwa kiasi cha shilingi milioni 58. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutufafanulia ni kwa nini hasa tukizingatia kwamba vijana wanahitaji sana taarifa hasa za ajira?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niombe radhi, niseme katika kujibu hilo, kwa sababu *Information* zote za kazi zinatolewa sana na TAESA, ndio maana kwenye ngazi ya Wizara imebaki masuala ya sera zaidi na jukumu hili sasa liko TAESA. Nirekebishe kwamba nilisema *CMA actually* zile hela shilingi bilioni 1.7 zinakwenda TAESA. Naomba nirekebishe hapo kwa kuunganisha na jibu hilo.

**MWENYEKITI:** Sasa mnaona tofauti ya swali aliloanzisha Mheshimiwa Mdee? Mheshimiwa Mdee ilikuwa ni sera na Mheshimiwa Lyimo anauliza hizi hela zimepungua, je, zile kazi nilizokuwa nategemea zitafanyika kutokana na kupungua kwa hizi hela, *its a direct question* kwa kifungu kile. Ndio maana tunaruhusu mshahara wa Waziri siyo kutoa tu, ni kwenye sera, ndio mnajimwaga mnavyoweza lakini hapa ni *specific.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 - Registration *of Trade Unions...* Shs.134, 503,000/=
Kif. 5001 - Youth Development... ... ... .Shs. 976, 732, 700/=

**MWENYEKITI:** Tulipewa *additional paper* pale, nadhani wote mnayo.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

Kif. 1001 - *Administation and General...* ... ... ... ... ... ... ...Shs. 1,124,500,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 – Wizara ya Kazi Ajira na Maendeleo ya Vijana**

Kif. 1001 - *Administation and General...* ... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 278,845,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning...* ... ... ...Shs. 2,680,900,000/=

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 6380 ambacho kinahusu ukarabati wa Ofisi za Kazi yaani *rehabilitation of Labour Offices and Youth Centers,* nikiangalia, kwa miaka mitatu mfululizo wamekuwa wakipewa shilingi milioni moja. Nataka kujua kwa mwaka huu wanategemea kukarabati vituo vingapi na vipi?

**MWENYEKITI:** Umeipata Mheshimiwa Waziri? Safari hii mna shilingi bilioni moja, milioni mia sita.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa tumezipata lakini orodha ya ofisi ambazo tunategemea kuzikarabati mwaka huu ziko katika hotuba, tumeziorodhesha kama anataka tutampatia kwa wakati wake lakini tumeziorodhesha.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi katika kifungu hiki kidogo ambacho kimeandikwa ni HIV/AIDS katika masuala ya …

**MWENYEKITI:** Kitaje namba yake!

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu kidogo cha 5492, HIV/AIDS, niko chini ya *policy and planning.* Katika maeneo ya Ukanda wa Maziwa, yanaonekana kwamba yameathirika zaidi kwa ugonjwa huo hasa kwa sababu ya kuwa na ajira duni kutokana na suala la uvuvi. Je, katika mpango huu, kutakuwa na uangalizi zaidi katika maeneo hayo kwa mfano ukiangalia maeneo ya Ukerewe, kule Musoma maeneo ya Kata ya Nyanja na kuna Mkoa wa Ruvuma na maeneo mengine yote ya pwani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ukifika katika kifungu, unauliza hizi fedha zitafanya kazi gani. Maana ukianza kupanua wewe, wenyewe kazi yao inayotakiwa kufanywa inajulikana, Mheshimiwa Waziri hizi fedha ni za kazi gani siyo za Ukerewe, siyo za wapi, yeye anajua kabisa.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha zinazohusu wafanyakazi wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Sasa tunakwendaje Ukerewe tena?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, unaona hapa kwa mfano hawezi kuzungumzia hizi hela ziko *specific* kwa eneo fulani. Unaweza kuuliza, je, zitakwenda Ukerewe? Watakwambia sivyo kama alivyojibu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - Labour... ... ... ... ... ... ... ... Shs. 1,237,305,000/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata maelezo kwenye kifungu cha 5415 ambacho kinasomeka kama *Combat Hazardious Child Labour in Urambo*. Nilitaka kujua kama maeneo mengine hayana matatizo hayo ya watoto ambao wanafanya kazi katika mazingira hatarishi, kwa tafsiri yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mwaka jana zilikuwa zimetengwa Urambo, mwaka huu zimetengwa Urambo, maeneo mengine ni vifungu vipi vya pesa ambavyo vinafanya kazi hiyo ambayo pesa hizi zimepangiwa kufanya Urambo.

**MWENYEKITI:** Ungeniuliza kazi gani zinafanyika Urambo, ningekuelewa sasa ukisema vingine vimewekwa wapi, havijaonekana, hapa vipo, ni hivi vya Urambo tu basi, Mheshimiwa Waziri Urambo mnafanya kazi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba *ILO* walipoamua kusaidia katika suala hili la ku-*combat* au kupambana na ajira mbaya ya watoto, kuna maeneo ambayo yalionekana kwamba ni *pilot project*. Kuna Ilemela na Urambo. Sasa *specifically* hela hizi zitafanya nini Urambo ambayo ndio tumeanza nayo nadhani katika hapa tunaweza tukachambua baadaye tukamueleza tunafanya nini, lakini *pilot project* ya mpango wa *ILO* ni kusaidia maeneo hayo na baadaye watakwenda kwenye maeneo mengine.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - Employment *Division*... ... ... Shs. 3,425,741,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Youth Development*... ... ... ... ... ..300,000,000/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi. Ukiangalia kifungu hiki cha 5001 kinahusu maendeleo ya vijana. S*ub*vote 5492 kinahusu masuala ya Ukimwi, ni wazi kwamba janga la Ukimwi hapa nchini ni kubwa na asilimia kubwa ya wanaoathirika ni vijana. Ukiangalia katika fedha walizotengewa zote zinatoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kifungu hicho hicho ambacho Mheshimiwa Stella Manyanya aliuliza ambacho Waziri amejibu kwamba ni kwa ajili ya Wizara na mimi nakubaliana naye, mtaona fedha zilizotengwa ni za ndani. Sasa nilikuwa nauliza ni kwa nini Wizara haikuona umuhimu walau wa kuwapatia vijana hawa fedha za ndani kidogo ili waanzie wakati tunasubiri fedha za nje?

**MWENYEKITI:** Sasa maana yake atoe zile shilingi milioni 100 kule aweke huku? Angefanya hivyo? Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Katika kumgawa sungura huyu mdogo, sisi tulimua kwamba tupange kama tulivyopanga na tuna matumaini makubwa kwamba hizo fedha ambazo wafadhili wamesema watatupa, tuna hakika zitapatikana kutokana na historia, huwa hawatuangushi hawa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia makadirio ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2009- 2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii, kuipongeza Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na kuwatakia heri katika utekelezaji wa shughuli zao katika mwaka unaofuata.

Waheshimiwa Wabunge, kama walivyoeleza hapa, mmeona tatizo la vijana, ni kubwa. Nadhani nguvu zenu nyingi zitaenda katika sehemu hiyo.

Kesho tunaingia Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tukiangalia ratiba yetu ya nyuma ilikuwa ni Wizara ya Mambo ya Nje. Sasa kwa sababu Randama yao wamewasilisha asubuhi, kwa hiyo, tutaingia Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Suala lingine ambalo nilikuwa napenda kulitolea ufafanuzi kesho ni kuhusu uamuzi ambao Mheshimiwa Spika aliutoa kuhusu ripoti ya *CAG*. Lakini wakati huo huo, masharti ya Kanuni hii ya Kamati na ninaomba hili lizingatiwe kwa sababu labda watu hawafahamu. Kanuni ya 114(10), (11) na (12), zinatoa masharti kwa Kamati zote na mara nyingi imekuwa ikivunjwa. Kanuni ya 114(1), inasema hivi:-

*"Masharti ya Kanuni hii yatatumika kwa Kamati zote za Kudumu."*

Kanuni ya 114(10), inasema:-

*"Bila ya kujali masharti ya fasili ya (9) ya kanuni hii…*

Kanuni ya 114(9) inasema:-

*"Shughuli za kawaida za Kamati zitaendeshwa kwa uwazi ambapo Kamati itaalika wadau ili kupata maoni na ushauri wao kwa ajili ya kuboresha Muswada au jambo ambalo litakuwa linashughulikiwa na Kamati hiyo."*

Sasa Kanuni ya 114(10) inasema:-

*“Bila ya kujali masharti ya fasili ya (9) ya Kanuni hii, shughuli zote za Kamati zinazohusu kuandaa na kutoa mapendekezo ya kuwasilisha Bungeni zitafanywa kwa faragha.”* Hiyo ni Kanuni ya 114(10).

Kanuni ya 114(11) inasema:-

*“Maoni ya Kamati yatakuwa ni yale yaliyokubaliwa na wajumbe walio wengi na kuwasilishwa Bungeni na Mwenyekiti au Mjumbe mwingine.”*

Kanuni ya 114(12) inasema:-

*“Mjumbe yeyote wa Kamati hataruhusiwa kuzungumzia hadharani maoni ya Kamati kuhusu Muswada au jambo lolote litakalokuwa linashughulikiwa na Kamati kabla maoni hayo hayajawasilishwa rasmi Bungeni.” (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi vifungu, kuna watu wengine wamekuwa wanaanza kuzungumzia habari za Kamati wakati Mwenyekiti wa Kamati hajawasilisha na mara nyingi taarifa zile zinakuwa zina upotoshaji wa aina yake. Mwenyekiti anasema yeye amepewa *mandate,* wakati ukiwafuata Wajumbe wanasema hakuna *mandate* aliyopewa na Wajumbe wanaohusika. Kwa hiyo, hili limekuwa likiendelea kutokea hasa kwenye Kamati ya Mashirika ya Umma, Kamati za *Local Government*, kwenye Kamati ya *PAC,* naona wamejifunza siku hizi. Sasa haya sio utaratibu, tutaleta *information* ambazo hazihusiki.

Sasa uamuzi wa Spika kuhusu aliyozungumza Mheshimiwa Waziri, tutaangalia kwenye *Hansard* na tutatoa maelezo kesho.

Halafu lingine, mnapowataja watu au taasisi ambazo hazikai humu ndani, Kanuni ya 71(1), inawapa uwezo wale watu kukata rufaa kwa Spika. Wakikata rufaa kwa Spika, Kamati yetu ya Haki na Maadili, itapitia uchunguzi wote na ikija kufahamika kwamba Mheshimiwa hukusema kwa usahihi kuhusu kampuni hiyo watakusema hapa kwamba hukusema sahihi pia kama maneno yako ni sahihi pia yatasemwa hapa hapa. Kwa hiyo, hivi ni vitu vya ku-*note* na wananchi wanaotusikiliza pia wana haki zao ndani ya Bunge hili kama watasemwa visivyo. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, basi kesho tutakuwa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka Kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 17 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*